Uhifadhi wa Utamaduni kupitia Tafsiri ya Riwaya za *Kaburi Bila Msalaba* na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali*

Na

Georginah Nyatichi Makini

Tasnifu Hii Imewasilishwa Katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii, Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika ili Kutimiza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu

Chuo Kikuu cha Moi

2025

IKIRARI

MTAHINIWA

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa ili kutosheleza mahitaji ya digrii katika Chuo Kikuu chochote. Hakuna ruhusa ya kutolesha sehemu yoyote bila idhini yangu au ya Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: ______________________________________ Tarehe:____________________

Georginah Nyatichi Makini
SASS/DPHIL/KIS/6015/22

WASIMAMIZI

Tasnifu hii imeidhinishwa kuwasilishwa ili itahiniwe kwa kibali chetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: ______________________________________ Tarehe:____________________

Prof. Nathan Oyori Ogechi

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Kitivo cha Fani na Sayansi za Jamii

Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi: ______________________________________ Tarehe:____________________

Prof. Mosol Mark Kandagor

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika

Kitivo cha Fani na Sayansi za Jamii

Chuo Kikuu cha Moi

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa familia yangu: mume wangu mpendwa, Caleb Nyangaresi na watoto wetu: Esther, Elias na Elsie.

SHUKRANI

Ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kufanikisha kazi hii. Shukrani za mwanzo namtunukia Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siha nilipokuwa nikishughulikia kazi hii.

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu, Profesa Ogechi Nathan na Profesa Mosol Kandagor, wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu Cha Moi. Pongezi za dhati kwa kunielekeza, kunishauri na kunisajiisha kila wakati nilipoelekea kukata tamaa. Nawashukuru kwa msaada wa makala na vitabu vilivyochangia kufanikisha usomi wangu. Mungu awabariki na kuwazidishia zaidi. Aidha, Profesa Zaja Omboga wa Chuo kikuu cha Nairobi pia alikuwa wa msaada kwangu kwa kunishauri kuhusu uandishi wa tasnifu na kuniazima vitabu nilivyohitaji kukamilishia kazi yangu. Mwenyezi Mungu akujalie zaidi kwa ukarimu wako.

Sitawasahau kuwashukuru wasomi na wanafunzi wenzangu katika darasa la uzamifu: Mkundane, Abrahamu, Masinde, Jackline, Naom na Catherine. Asante kwa msaada wenu. Mlinifaa kwa makala na ushauri wenu wakati wa kushughulikia kazi yangu.

Aidha, sitawasahau wazazi wangu wapendwa, marehemu mzee Michael Makini na mama Teresia Makini pamoja na ndugu zangu wapendwa: Thomas, Ann, Cosmas, Elizabeth, Irine, Bivon na mpendwa Edina. Hakika mlinitia moyo na kunichochea nitie bidii zaidi katika kazi yangu. Familia yangu pia mumenifaa si haba. Mume wangu Caleb Nyangaresi, watoto wetu: Esther, Elias na Elsie. Ufanisi wa utafiti huu umechangiwa pakubwa na juhudi na uvumilivu wenu. Asante sana.

Mwisho, nachukua fursa hii kushukuru Chuo kikuu cha Moi na Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa kunipa fursa ya kusomea shahada ya digri ya uzamifu. Kwenu nyote shukrani za dhati kwa kuwa wa msaada nilipokuwa nikifanya utafiti. Asante na Mungu awabariki.

IKISIRI

Taaluma ya tafsiri inajumuisha si tu kubadilisha maneno kutoka lugha moja hadi nyingine, bali pia kuhamisha na kutafsiri maadili, desturi na mitazamo mbalimbali ya kitamaduni. Utafiti huu ulikusudia kueleza na kuchanganua jinsi uhifadhi wa utamaduni umeendelezwa kupitia tafsiri ya riwaya za *Kaburi Bila Msalaba (*Kareithi) na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* (Kitereza*)*. Utafiti uliongozwa na madhumuni matatu: kubaini vipengele vya kitamaduni katika matini teule, kutoa maelezo yanayothibitisha kwamba riwaya hizi mbili ni hazina ya hifadhi ya utamaduni wa maisha ya jamii mahususi za Kiafrika; kujadili na kuitathimini michakato na mikakati iliyotumiwa kutafsiri kazi chanzi kama mikakati ya uhifadhi wa utamaduni katika riwaya hizi mbili; kuonyesha jinsi udumishwaji wa baadhi ya vipengele vya lugha chanzi (Kiswahili na Kikerewe) unavyoweza kufasiriwa kama ithibati ya uhifadhi wa utamaduni katika tungo asilia na katika tafsiri. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: nadharia ya anthropolojia na nadharia ya *Skopos.* Nadharia ya anthropolojia ilizingatia tapo la isimu anthropolojia ambalo linachunguza tabia na mienendo ya watu na jinsi wanavyotumia lugha kwa lengo la kuonyesha ukweli na uhalisia wa mambo katika jamii. Nadharia ya *Skopos* huchukulia shughuli ya kutafsiri kama kitendo kilicho na malengo. Yaani, kabla mtafsiri hajaanza kazi yake ni sharti aelewe lengo la tafsiri yake. Utafiti ulikuwa wa maktabani. Mtafiti alijikita katika riwaya za Kareithi na Kitereza na tafsiri zao katika lugha ya Kiingereza. Matini teule zilisomwa na data msingi kurekodiwa. Data ilipangwa na ilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti na matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Kuhusu lengo la kwanza, utafiti uligundua kwamba fasihi haiumbwi katika ombwe tupu bali hufungamanishwa na maisha ya binadamu na mazingira yake. Dhana za kitamaduni zinapotafsiriwa huwa ni njia moja ya kuhifadhi utamaduni kwa hadhira lengwa. Mintarafu ya lengo la pili, utafiti ulibaini kwamba mikakati maalum ilitumiwa ili kuhawilisha vipengele vya kitamaduni kutoka matini chanzi hadi hadhira lengwa jinsi nadharia ya *Skopos* inavyoweka. Vipengele vingi vya kitamaduni katika matini asilia viliweza kudumishwa kupitia mikakati mbalimbali ya tafsiri. Kulingana na lengo la tatu, utafiti ulionyesha kwamba mbinu nyingi za ujielezaji hufungamana na utamaduni na miktadha ya kila siku ya jamii husika. Mbinu hizi zinapohawilishwa mikakati maalum hushirikishwa na hii huwa ni njia moja ya kuhifadhi utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Utafiti ulihitimisha kwamba uhifadhi wa utamaduni unawezeshwa kupitia mchakato wa tafsiri. Utafiti huu unapendekeza kuwe na tafiti zingine zinazozingatia maandishi ambayo hayakushughulikiwa katika utafiti huu kama vile tamthilia na hadithi fupi. Aidha, utafiti unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia tofauti kando na nadharia ya anthropolojia na nadharia ya *Skopos*.

ABSTRACT

Translation encompasses not only changing words but also transferring and interpreting the morals, customs, and various cultural perspectives of a specific language into another language. The study endeavors to investigate how culture has been preserved through the translation of the two novels: *Unmarked Grave* (Kareithi*)* and *Mr. Myombekere and His Wife Bugonoka and their son Ntulanalwo and Daughter Bulihwali* (Kitereza*)*. The study was guided by three objectives: to give an explanation and examples depicting Kareithi's and Kitereza's novels that they are a rich treasure in traditional culture of the life of the Kikuyu and Kikerewe communities; to discuss the processes and strategies used in translating the original text as a way of culture preservation in the two novels; to investigated how maintenance of language features in Kiswahili and Kikerewe are evidence of culture preservation in the original and in translated texts. This research was guided by two theories: anthropological and *Scopos* theory. The anthropological theory took a linguistic anthropological perspective on how language is used to 'hear' culture happening. It contends that human beings create meaning and bring about new experiences through the language they use. *Scopos* theory focused on the purpose of translation which determines the translation methods and strategies that are to be employed in order to produce a functionally adequate result. This was a library based study with a case study design. The four texts were read and examples of traditional culture were recorded as primary data in our study. Collected data was recorded and analyzed according to research objectives and the tenets of the theories. Research findings were presented in descriptive form. On objective one, the study established that literature is not created in a vacuum but rather it is bound in people's experiences and their environment. When aspects of culture are translated they contribute to culture preservation from one community to another. In light of objective two, the study established that specific strategies were used to translate traditional culture from original text to translated text as *Scopos* theory states. Fragments of culture were retained through different translation strategies. In respect to objective three, literary devices are bound in people's culture and in their day to day contexts in any given society. When literary devices are translated they contribute in culture preservation through translation. The study concludes that there is culture preservation through translation. The study recommends future researches to be conducted by using other genres like the play and short stories. Either, a study can be done on the same topic but using different theories other than anthropological and *Scopos* theories.

YALIYOMO

IKIRARI ii
TABARUKU iii
SHUKRANI..iv
IKISIRI v
ABSTRACT..vi
YALIYOMO..vii
ORODHA YA MAJEDWALI..xi
MAELEZO YA ISTILAHI..xii
MAELEZO YA AKRONIMU..xiii
SURA YA KWANZA 1
MISINGI YA UTAFITI 1
1.0 Utangulizi..1
1.1 Usuli wa Mada 1
1.2 Suala la Utafiti 11
1.3 Malengo ya Utafiti 12
1.4 Maswali ya Utafiti..13
1.5 Umuhimu wa Utafiti 13
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti..17
1.7 Mhutasari wa Sura 18
SURA YA PILI..19
MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA............................19
2.0 Utangulizi..19
2.1 Dhana ya Tafsiri..19
2.2 Historia ya Tafsiri 20
2.3 Fasihi Tafsiri 22
2.4 Tafsiri na Utamaduni 23
2.5 Fasihi Tafsiriwa 25
2.5.1 Tafsiri za fasihi kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili............28
2.5.2 Tafsiri za fasihi ya Kiafrika hadi lugha ya Kiingereza..................................37
2.5.3 Tafsiri za fasihi zilizotumia nadharia ya Skopos na Anthropolojia 41
2.6 Kiunzi cha Nadharia 45
2.6.1 Nadharia ya Anthropolojia..45

2.6.1.1 Mtazamo wa kijamii au kiutamaduni 48
2.6.1.2 Mtazamo wa upekee wa kihistoria 49
2.6.1.3 Mtazamo wa Kimuundo 50
2.6.1.4 Mtazamo wa Kiuchumi na Kisiasa 51
2.6.2 Nadharia ya Skopos...52
2.7 Mhutasari wa Sura 57
SURA YA TATU 58
MBINU ZA KUENDESHEA UTAFITI...58
3.0 Utangulizi..58
3.1 Msuko wa Utafiti 58
3.2 Eneo la Utafiti 59
3.3 Uteuzi wa Sampuli 59
3.4 Ukusanyaji Data 60
3.5 Vifaa vya Utafiti 61
3.6 Uchambuzi wa Data 61
3.7 Uwasilishaji wa Data 62
3.8 Masuala ya Maadili katika utafiti huu 62
3.9 Mhutasari wa Sura 63
SURA YA NNE 64
HISTORIA NA UTAMADUNI WA WAKIKUYU NA WAKEREWE................64
4.0 Utangulizi..64
4.1 Historia na Utamaduni wa Wakikuyu...64
4.1.1 Mapambano dhidi ya ukoloni...65
4.1.2 Maisha ya P.M. Kareithi 67
4.1.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba* 67
4.2 Historia na Utamaduni wa Wakerebe 69
4.2.1 Maisha ya Aniceti Kitereza 70
4.2.2 MC2 Muhtasari wa riwaya ya *Bwana Myombekere Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali* 71
4.3 Mhutasari wa Sura 73
SURA YA TANO 74
UHIFADHI WA UTAMADUNI KUPITIA MCHAKATO WA TAFSIRI 74
5.0 Utangulizi..74
5.1 Usawiri wa Vipengele vya Kitamaduni katika Riwaya Teule 74

5.1.1 Utamaduni wa mazingira ya kiekolojia....77
5.1.1.1 Ekolojia ya wanyama....79
5.1.1.2 Ekolojia ya samaki....81
5.1.1.3 Ekolojia ya ndege....83
5.1.1.4 Ekolojia ya Miti na Majani....86
5.1.2 Utamaduni wa Kijamii....90
5.1.2.1 Mila na Desturi....91
5.1.2.2 Imani ya Dini....101
5.1.2.3 Shughuli za Kazi....103
5.1.2.4 Asasi za Kijamii....106
5.1.2.5 Burudani na Starehe....107
5.1.3 Utamaduni Nyenzo....111
5.1.3.1 Vyakula na Vinywaji....112
5.1.3.2 Vifaa vya Kazi....115
5.1.3.3 Mavazi....121
5.1.3.4 Makazi na Viwanda....123
5.2 Hitimisho....124
SURA YA SITA....125
UHIFADHI WA VIPENGELE VYA KITAMADUNI KUPITIA MIKAKATI YA TAFSIRI....125
6.0 Utangulizi....125
6.1 Mikakati ya Kutafsiri....125
6.1.1 Ufafanuzi au upanuzi maana....129
6.1.2 Ujumuishaji wa Dhana....136
6.1.2.1 Uhawilishaji....137
6.1.2.2 Majina ya watu....138
6.1.2.3 Maneno katika Nyimbo....141
6.1.3 Muungano wa Mbinu za Tafsiri....142
6.2 Mhutasari wa Sura....143
SURA YA SABA....144
UDUMISHWAJI WA VIPENGELE VYA UJIELEZAJI UNAVYOFASIRIWA KAMA ITHIBATI YA UHIFADHI WA UTAMADUNI....144
7.0 Utangulizi....144
7.1 Vipengele vya Ujielezaji....144

7.1.1 Matumizi ya Methali 146
7.1.2 Matumizi ya Tashbihi 153
7.1.3 Matumizi ya Jazanda 158
7.1.4 Matumizi ya Tashihisi 160
7.1.5 Matumizi ya Tanakali za Sauti 163
7.1.6 Majina ya Kimajazi 167
7.1.6.1 Myombekere 167
7.1.6.2 Bugonoka 168
7.1.6.3 Ntulanalwo 169
7.1.6.4 Bulihwali 169
7.2 Muhtasari wa Sura 170
SURA YA NANE 171
MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI 171
8.0 Utangulizi 171
8.1 Muhtasari wa Utafiti 171
8.1.1 Uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri 172
8.1.2 Uhifadhi wa vipengele vya kitamaduni kupitia mikakati ya tafsiri 173
8.1.3 Udumishwaji wa vipengele vya ujielezaji unavyofasiriwa kama ithibati ya uhifadhi wa utamaduni 174
8.2 Mchango wa Utafiti 175
8.3 Mapendekezo ya Utafitii 176
MAREJELEO 178
KIAMBATISHO 186

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 5.1: Utamaduni wa mazingira ya kiekolojia 78
Jedwali 5.2: Vielelezo vya Utamaduni wa Kijamii 91
Jedwali 5.3: Vielelezo vya Utamaduni Nyenzo 111
Jedwali 6.1: Mikakati ya kutafsiri kama njia ya kuhifadhi utamaduni 128
Jedwali 7.1: Vipengele vya Ujielezaji 145

MAELEZO YA ISTILAHI

Mchakato	Mfuatano wa hatua katika utekelezaji wa jambo.
Uhawilishaji	Uhamishaji wa maana ya ujumbe katika tafsiri.
Uhifadhi	Ni mchakato wa kulinda, kutunza, kunusuru na kusalimisha kwa makini habari fulani muhimu isiyotumika mara kwa mara katika kipindi cha sasa lakini ambayo inaweza kuwekwa kwa marejeleo katika siku za usoni.
Ujumbe	Masuala yoyote muhimu katika kazi ya fasihi.
Utamaduni	Ni mkusanyiko wa mila na desturi zote za jamii inayotumia lugha moja mahsusi kama njia ya mawasiliano.

MAELEZO YA AKRONIMU

HA	Hadhira Asilia
HL	Hadhira Lengwa
HP	Hadhira pokezi
LC	Lugha Chanzi
LL	Lugha Lengwa
MC	Matini Chanzi
MC1	Riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba*
MC2	Riwaya ya *Bwana Myombekere Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali*
MT	Matini Tafsiri

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii ya kwanza imepambanua msingi wa utafiti. Hapa, vipengee mbalimbali vimeangaziwa. Vipengee vyenyewe ni pamoja na: usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na upeo na mipaka ya utafiti.

1.1 Usuli wa Mada

Tafsiri ni taaluma katika tasnia ya mawasiliano ambayo imetumiwa kwa miaka mingi na katika taaluma nyingi kutekeleza au kufikia matakwa au malengo mbalimbali ya kimawasiliano. Newmark (1988) anahoji kwamba tafsiri ni taaluma inayotumia lugha kwa uelewa kwamba katika tafsiri lugha hukita kuwili - katika lugha na utamaduni chanzi kwa upande mmoja, na katika lugha na utamaduni lengwa kwa upande mwingine. Kwa kuwa tafsiri inatumia lugha kama mbinu na chombo cha kuwezesha mawasiliano inaishia kueleweka kama uhalisia wa uashiriaji wa mipangilio na taratibu mnapoweza kudhihirishwa thamani, maadili na desturi za kitamaduni na jamii. Kwa mintarafu hii, kutafsiri kwa aina yoyote ile kunaashiria uasisi wa mawasiliano tata yanayoashiria ukaribu na umbali ulioko kati ya lugha na tamaduni za jamii mbalimbali. Kwa misingi hii, kutafsiri kutoka lugha moja hadi lugha nyingine ni shughuli inayohitaji uelewa, tajriba na stadi zinazowezesha kubaini upatanifu, ulinganifu na upekee wa lugha na utamaduni miongoni mwa lugha zinazohusika.

Bassnett (2002) anasema kwamba taaluma ya tafsiri haishirikishi ubadilishanaji wa vipengele vya kileksia na sarufi kati ya lugha mbili bali huhitaji uwasilishaji wa miktadha ya kitamaduni. Katika hali ambapo masuala yanayotafsiriwa yanahusu masuala ya kitamaduni kama vile kutafsiri fasihi, kutafsiri kunashurutisha udhibiti wa

maarifa changamano sio tu maarifa ya lugha, bali pia maarifa ya kimawasiliano, kitamaduni na kiutekelezi. Kwa mfano, katika tafsiri za kifasihi, mtafsiri anawajibika kutekeleza wajibu wake changamano kama daraja, wakala na mpatanishi wa kitamaduni. Hii ni kwa kuwa matini chanzi ya kifasihi inayotafsiriwa mara nyingi inaweza kuangaliwa kihalisi kama zao halisi la utamaduni mahususi mnamokitwa ishara na taswira anuwai za kitamaduni. Katika hali hizi, mtafsiri anatarajiwa kuwa mtu au mtaalamu aliye na uwezo wa kuzibaini ishara na taswira za kitamaduni. Inafaa awe aliyetaalamika katika mawasiliano ya kitamaduni na awezaye: kujenga upatanifu wa kitamaduni; awezaye kubaini ilipo miktadha ya kitamaduni; kuzitambua na kuzifasiri maana za kitamaduni na kubaini jinsi ya kupunguza au kuziba mapengo na masafa ya kitamaduni. Ni sharti mtafsiri awajibike kubaini na kuzieleza kaida na desturi za kitamaduni, utambulisho anuwai wa kitamaduni na kijamii, taratibu za mahusiano ya kijamii.

Kutafsiri fasihi kunaweza kuangaliwa kihalisi kama shughuli inayotekelezwa katika miktadha ya wingi-utamaduni kwa upande mmoja na inatekelezwa pia katika misingi na miktadha ya wingi-lugha kwa upande mwingine. Zaidi ya hayo, tafsiri za kifasihi ni sharti ziangaliwe kama uhalisi wa kiutekelezi kwa jinsi zinazoonyesha na jinsi zinazowakilisha mahusiano ya ubadilishanaji na uhawilishaji wa kitamaduni, jinsi zinazodhihirisha upekee na ulinganifu wa lugha, ulinganifu wa utamaduni na maaana. Ni muhimu kutaja kuwa kipengele cha utamaduni huathiri pa kubwa tafsiri.

Jilala (2014) anasema suala la utamaduni katika tafsiri haliwezi kuelezeka kwa urahisi bila kuhusisha utamaduni wa jamii husika kwa sababu lugha ni kipengele cha utamaduni. Jamii huwasilisha maarifa na utamaduni wao kupitia lugha. Ugumu hutokana na shida ya kupata neno mwafaka katika lugha lengwa kwa kuzingatia utamaduni wa dhana hiyo kwa lugha chasili. Matokeo ya kweli ni kuwa lugha mbili

huwa na maana tofauti kidesturi na kitamaduni. Kwa kuwa fasihi ni zao la utamaduni mahususi, kutafsiri fasihi kutoka lugha moja hadi nyingine kunashurutisha kwamba mtafsiri awe na tajriba ya kina ya utamaduni wa lugha ya fasihi husika, tajriba inayomwezesha kubaini na kudhihirisha upekee wa lugha chanzi na upekee wa lugha lengwa. Tafsiri kama hizi zinamwajibisha mtafsiri wa fasihi kuwa mpatanishi wa kitamaduni kwa sababu utamaduni wa kila lugha inayohusika katika mchakato wa tafsiri unashawishi sio tu ujenzi wa maana bali pia ufasiri wa maana hiyo. Tafsiri za kifasihi ni njia madhubuti zinazowezesha usemezano katika miktadha ya wingi-utamaduni ambao mtafsiri anawajibika kuwa mjenzi wa daraja za mabadilishano kati ya tamaduni, mitagusano kati ya watu wa asili tofauti na makutano kati ya lugha tofauti na kati ya vipindi na awamu tofauti za kihistoria. Tafsiri za kifasihi zinaweza kuangaliwa kama ujenzi wa daraja na misingi inayotetea uanuwai wa kitamaduni pia zinaweza kutazamwa kama mkakati unaotetea kustawika kwa upekee wa kila utamaduni, kuimarika kwa utamaduni na zaidi kuonyesha umuhimu wa tofauti na ugeni wa kila utamaduni. Kwa mintarafu hii, tafsiri inawezesha kuondoa lugha, fasihi na utamaduni : ubanifu na ufunge wa mipaka ya lugha moja, ujinga na kutojua kulikoathirika kwa njia hasi na ubanifu wa kutokuelewa na hata woga na kuogopa ‘wengine’.

Kwa kutilia maanani ukweli na madai yanayobainishwa, basi tafsiri za fasihi katika fasihi ya Kiswahili ni uhalisia ambao umekuwepo kwa siku nyingi tangia fasihi hii ilipoanza kutagusana na fasihi nyingine za kilimwengu. Huu ni uhalisia unaojibainisha kwa uwazi hasa inapozingatiwa kwamba wasifu wa sasa wa fasihi ya Kiswahili unasheheni tafsiri za aina nyingi zilizo na mianzo yake katika anuwai za kiulimwengu. Kwa mfano, uanuwai huu wa mianzo ya kifasihi kupitia kwa tafsiri unatokana na mitagusano kupitia kwa tafsiri za fasihi za kilimwengu. Zaja (2006)

anahoji kwamba fasihi ya Kiswahili imewahi kupokea tafsiri kutoka utamaduni wa Kigiriki kutokana na tafsiri kama vile *Mfalme Edipode*, kutoka Kirusi kupitia tafsiri ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, kutoka Kijapani katika tafsiri ya *Chagua Maisha* na mianzo mingine mingi kutoka utamaduni wa Kiingereza kupitia tafsiri za *Mapebari wa Venisi, Julius Kaizari, Kisiwa Chenye Hazina, Kuizunguka Dunia kwa Siku Themanini, Safari za Guliva, Elisi katika Nchi ya Ajabu na Mshimo ya Mfalme Suleimani* miongoni mwa tafsiri zitokazo kwa lugha ya Kiingereza.

Kwa mujibu wa Ngugi wa Thiong'o (1986:56), lugha hubeba utamaduni na utamaduni hubeba amali zote ambazo hutufanya tujitambue na kupata mahali petu halisi ulimwenguni. Aidha, anasisitiza kuwa tajriba za Kiafrika haziwezi kamwe kufafanuliwa kwa lugha zingine isipokuwa zile za Kiafrika. Jambo hili linazipa lugha kipaumbele kama chombo cha kujiendeleza katika sekta mbalimbali na kama chombo cha kuhifadhi utamaduni. Licha ya fasihi ya Kiswahili kupokea tafsiri kutoka lugha ya Kiingereza, fasihi ya Kiswahili pia imeweza kupokea tafsiri kutoka kwa lugha za Kiafrika kama vile: *Wimbo wa Lawino* (tafsiri kutoka lugha ya Kiacholi) na *Shetani Msalabani* kutoka lugha ya Gikuyu. Kuna pia tafsiri za fasihi za Kiafrika zilizoandikwa kwa lugha za kigeni kama vile - *Barua Ndefu Kama Hii, Shujaa Okonkwo, Mshale wa Mungu, Mchimba Madini, Usilie Mpenzi Wangu.*

Uhalisia huu wa kutafsiri kazi za fasihi na bunilizi za aina nyingi kutoka mianzo ya lugha mbalimbali za ulimwengu, ni mchakato uliowezesha fasihi ya Kiswahili kutagusana na tajriba pana za kifasihi. Isitoshe, uhalisia huu kuhusu kutafsiri fasihi umewahi kushawishi na kuchochea usomaji pamoja na tafiti za aina nyingi ambapo kumeangaziwa kwa masuala ya aina nyingi. Kuna tafiti ambazo zimeangalia tafsiri kama: mkakati wa kutajirisha fasihi, mchakato wa kuhawilisha utamaduni na mkakati wa kupanua hadhira na upokezi wa fasihi za kilimwengu. Hata hivyo, tafsiri hizi

zimekuwa na mwelekeo wa aina moja, yaani kuangalia jinsi tafsiri hizi zilivyoingia katika fasihi ya Kiswahili na kuiathiri kwa njia chanya au njia hasi. Kadri ya ufahamu wetu, hakuna ithibati kwamba tafsiri kama fasihi ya Kiswahili imewahi kuangaliwa na kutafitiwa kama mchakato wa uhifadhi, mchakato wa kujenga hifadhi ya tamaduni, desturi na mienendo ya kitamaduni ya tamaduni za Kiswahili au tamaduni zinazoshabihiana na Kiswahili. Hii ni licha ya kwamba tafsiri za kifasihi zinaweza kuangaliwa kama mchakato wa kuanzisha na kudumisha mahusiano ya kitamaduni, umoja na utangamano miongoni mwa wanajamii wa mataifa tofauti tofauti ulimwenguni (Mutuli, 2009; Maitaria, 2016).

Dai hili linachochea swali: Je, tafsiri inaweza kuangaliwa, kuchanganuliwa na kutafitiwa kwa misingi ya kutaka kuonyesha jinsi tafsiri ilivyo na mkakati wa uhifadhi na mkakati wa uteteaji wa haki za kitamaduni? Ili kuweza kuonyesha ufaafu wa utafiti wa aina hii, ni muhimu kwanza ielezwe na ifafanuliwe dhana ya uhifadhi, hususan uhifadhi wa kitamaduni unaowezeshwa na tafsiri.

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2004), uhifadhi katika muktadha huu unaweza kufafanuliwa kuwa ni mchakato wa kulinda, kutunza, kunusuru na kusalimisha kwa makini habari fulani muhimu isiyotumika mara kwa mara katika kipindi cha sasa lakini ambayo inaweza kuwekwa hifadhi kwa marejeleo katika siku za usoni. Hii ni dhana inayohusiana na uhifadhi wa habari unaodhamiria kuzuia kupotea, kusahaulika na kudhalilishwa kwa habari iliyo na umuhimu mkubwa. Habari ya aina hii inaweza kuangaliwa kama hazina, hifadhi, bohari, ghala la makumbusho la maarifa na ufahamu unaotokana na tajriba za mitagusano ya watu. Hii ni habari ambayo watu huirejelea ili kuthibitisha uwepo wao duniani. Hifadhi hii ya maarifa inaweza kufafanuliwa kuwa ni taasisi ya maarifa iliyokitwa kihistoria - kwa mfano, kupitia tungo za kisanaa kama vile ngano, nyimbo masimulizi ya kiasilia, tungo za

kifasihi na hata tafsiri za sanaa hizo. Hifadhi ni taasisi inayosajili, inayohodhi, inayochuja, kuchanganua na kuwezesha upatikanaji wa data kuhusiana na wasifu wa maisha ya watu, tamaduni, desturi na kaida za maisha yao. Mifano hapa ni tamaduni za maisha ya watu wa jamii za wachache, mawanda na upeo wa tajriba za kiujumui za watu, kama inavyodhihirika katika riwaya za Munuhe Kareithi na Aniceti Kitereza na zinazotafitiwa katika tasnifu hii.

Kulingana na Ngesu (2020) anasema, kumekuwa na mwamko wa hivi karibuni wa kutafsiri kazi za Kiswahili kwenda Kiingereza na lugha nyinginezo, kinyume na ilivyokuwa awali ambapo kazi mbalimbali zilikuwa zikitafsiriwa kwa wingi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Kazi kama hizi zinahitajika kwa sababu zitatuwezesha kuangazia na kuchanganua maandishi na tungo asilia, maandishi na tungo zilizodhihirisha ubora, upekee na tunu za kiutunzi kiasi cha kushawishi kutafsiriwa kwa lugha za kigeni. Tungo hizo tunu ni matokeo ya taarifa na maarifa yaliyotafsiriwa kutokana na ufahamu asilia, ushuhudiaji wa kibinafsi na stakabadhi azizi za aina mbalimbali. La muhimu kuhusiana na maandishi na tungo za aina hii, ni kwamba zina wasifu wa kuhifadhi uhalisi hai, ni ithibati ya viwakilishi vya uhalisi au hata uhalisi wa kiubunifu na kiujumi. Kwa kuangalia na kutathimini michakato na taratibu hizi za uhifadhi, inawezekana mtazamo mmoja wa kufanya hivyo ukawa ni kupitia tathmini ya tafsiri, ziwe tafsiri za nyaraka rasmi, mawasiliano ya batini za kibinafsi na zaidi au kama inavyonuiwa katika utafiti huu, tafsiri za tungo adimu za kifasihi.

Tafiti za aina hii zinaweza kuangazia uibukaji wa taswira, ishara, viashiria na vidokezi vyovyote vile vya kutafsiriwa - hasa kutafsiriwa kwa tungo asilia za fasihi kwa lugha za kigeni. Utafiti huu unaweza kuangaliwa kama utafiti wa matini za kifasihi kama nyaraka za kifasihi. Swali ni: Je, tafsiri ina nafasi na inatekeleza majukumu gani katika uwekaji wa hifadhi ya ujumla wa maisha ya watu katika jamii

mahsusi katika kipindi fulani cha historia? Hifadhi za maarifa sawia na tafsiri za kifasihi zinaweza kuangaliwa kama “eneo la mtagusano” mahali ambapo lugha, matini na tungo za kifasihi na kumbukizi za jamii kwa jumla hutagusana. Hapana shaka kwamba hifadhi za maarifa ya jadi zina uwezo mkubwa kuathiri, kushawishi, kuelewa na kufahamu mambo ya sasa. Vile vile hifadhi hizi zinaweza kuonyesha majukumu yanayotekelezwa na tafsiri katika vipindi mbalimbali vya historia.

El- Dali (2011) aliwahi kusisitiza kwamba utamaduni wa lugha lengwa usilazimishwe kwa matini asilia. Anashikilia kwamba kila matini itazamwe kwa kuzingatia utamaduni wa matini na lugha asilia. Kwa kujikita katika misingi na uelewa wa uhifadhi wa maarifa, utafiti wa tafsiri za kifasihi unaaangazia masuala mahususi ya kitamaduni na kihistoria ya jamii fulani maalum hasa kwa kadri masuala hayo yalivyosawiriwa na kujitokeza katika matini na tungo chanzi za kifasihi: *Kaburi Bila Msalaba* na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali.* Vile vile, msisitizo unawekwa katika kuangazia dhana nzima ya uhifadhi na upitishaji wa ujumla wa utamaduni na jamii husika kwa kuchanganua mchakato wa kutafsiri, kuchanganua uhalisia wa kiisimu na uhusika wao katika kujenga utambulisho wa jamii husika, uashiriaji na uakisisaji wa uchangamano wa utamaduni kwa kadri ulivyowasilishwa kama kazi timilifu ya kisanaa kama ilivyo katika kazi hii. Hali kadhalika, katika utafiti wa aina hii, ni jambo la kimsingi kuchanganua uhalisia wa kihistoria na kitamaduni uliohawilishwa kupitia kwa tafsiri, hususan udhahiri wa uhawilishaji wa masuala hayo. Utafiti huu unaazimia pia kuangazia na kuyapa msisitizo masuala ya “uhalisia wa uwili” uhalisia wa historia na tafsiri katika tungo zinazoweza kuangaliwa na kuchukuliwa kama viashiria vya hifadhi na kanzi ya maarifa. Kulingana na mtazamo wa mwandishi wa riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali* alikuwa anatamani kuwasilisha kisanifu

na kisanaa mitazamo ya kizamani, uhalisia wa kale na maisha ya jamii yake kama yalivyokuwa katika vipindi maalum vya kihistoria. Gerald & Charlotte Hartwing (1976) (katika ukurasa wa nyuma wa tafsiri) wanasisitiza kauli hii kwa kuhoji kwamba:

> *"Completely unaffected by post-world War II influence, Kitereza does not write in the genre of most contemporary African Writers. He is not seeking identification: he fights no battles. Voices no protest… His goal is to preserve tradition before it is erased by time. His intended audience; the Kerebe.*
>
> *Pasina kuathiriwa au kushawishiwa kwa njia yoyote ile na vishawishi vya tajriba ya baada ya Vita Vikuu vya II vya Dunia. Kitereza haandiki kwa kuafiki kaida na desturi za kitanzu kama walivyofanya waandishi wengine wa kisasa wa Kiafrika. Hatafuti kutambuliwa, hapigani vita vyovyote, hapati sauti yoyote ya upinzani… bali lengo lake ni kuhifadhi utamaduni kabla haujafutwa na wakati. Hadhira yake ni Wakerebe.*

Lengo lake kuu lilikuwa ni kuwasilisha habari na historia ya jamii yake jinsi ilivyokuwa hapo zamani. Hii ilikuwa ni njia moja ya kuweka hifadhi ya amali za jamii kabla hazijafutwa na wakati.

Licha ya kwamba uwezekano huu wa kiutafiti wa aina hii umekuwepo katika fasihi ya Kiswahili kwa muda mrefu, tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu fasihi tafsiri katika fasihi ya Kiswahili hazijaushirikisha mwelekeo huu wa kiutafiti, badala yake tafiti nyingi zimeshughulikia tafsiri zilizotolewa kutoka lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni hadi lugha ya Kiswahili. Kuhusiana na suala hili, Ruhumbika (2002) anahoji kwamba, katika awamu za awali za fasihi andishi ya Kiswahili, tafsiri za aina hii zilihitajika ili kuchangia kuimarisha maandishi machache ya fasihi na lugha yaliyokuwepo katika awamu hizo za mwanzo za tungo za fasihi ya Kiswahili. Michakato yote ya kutafsiri fasihi za kigeni katika kipindi hicho, ilikuwa ni kipindi cha kipragmatiki iliyokuza na kuipa sura mpya fasihi ya Kiswahili. Kadri muda ulivyosonga na kuibua mitazamo mipya katika fasihi hii, ndivyo fasihi tafsiri

ilivyozidi kupokelewa na kuibua mijadala changamano ya kiusomi. Hadhira ya fasihi ya Kiswahili ilikuwa radhi kupokea fasihi asilia sawia na ilivyopokea tafsiri za fasihi zilizoingia katika fasihi na kwa njia hizo kukumbatia mabadiliko yaliyoshuhudiwa katika ulimwengu wa usomaji wa kazi bunilizi kuongezeka. Kuendelea kuhitajika kwa tafsiri za fasihi kulichochewa na sababu nyingi kama vile: sababu za kisiasa zilizochochea kutafsiriwa kwa kazi za kifasihi- *Mafukara wa Ulimwengu (Wretched of the Earth).* Hali kadhalika kulikuwa na sababu za kitamaduni na za kielimu lakini katika kipindi hicho hicho, baadhi ya tungo asilia za kiafrika zilianza kutafsiriwa moja kwa moja na kuanza kusambazwa ulimwenguni kupitia lugha za kigeni. Mchakato wa tafsiri uliwajibishwa kutumika kama njia na mkakati wa kimsingi wa kuendeleza na kuhifadhi utamaduni wa jamii kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine.

Utafiti wetu ulipania kuuchanganua ukweli uliokwishatajwa kwa kadri unavyojitokeza katika riwaya ya Munuhe Kareithi- *Kaburi Bila Msalaba* na riwaya ya Kitereza- *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali*. Kuhusiana na tukio hili la kiutunzi, Ruhumbika (2002), akinukuu stakabadhi za Kitereza anasema.

> *"I finished writing this book on February 13th, 1946, a book I wrote out of my deeply felt desire to preserve the customs and the way of life of our ancestors, such as they actually lived them in the days of yore, when our people dressed in skins of cows and goats and slept on beddings of hides of cows, goats and sheep, all expertly treated and turned into soft clothing materials which folded nicely and were comfortable to wear and to sleep on…"*
>
> *(Nilimaliza kuandika kitabu hiki tarehe 13 mwezi wa Februari 1945, kitabu nilichoandika kutokana na hamasa na ari niliyokuwa nayo ya kutaka kuhifadhi tamaduni, desturi na njia za maisha za mababu zetu, kwa kadri walivyoishi katika siku hizo za kale, wakati watu wetu walipovaa mavazi yaliyotengenezwa kwa ngozi za ng'ombe na mbuzi na walilalia malalio ya ngozi za ng'ombe na kondoo, yaliyotengenezwa kwa ustadi wa kufanywa laini kuwa mavazi yaliyokunjika kwa urahisi na yaliyokuwa mororo kuvaa na kulalia…).*

Hamasa na ari hiyo ya kuhifadhi utamaduni vilimsukuma mtunzi kuitafsiri kazi hii kwa Kiswahili, tafsiri iliyohitimishwa katika mwaka wa 1969 na kukawia kupata mchapishaji hadi mwaka wa 1981. Tafsiri ya riwaya hii kutoka mianzo ya Kikerewe na Kiswahili, kwa kiasi Kifaransa na Kijerumani, na hatimaye tafsiri timilifu kwa lugha ya Kiingereza iliyotokea mwaka wa 2002 kupitia kwa juhudi za jamaa wake, Gabriel Ruhumbika, ni ithibati ya mchakato mzima wa uhifadhi. Kuhusiana na suala hili la uhifadhi, Mulokozi (1985) alikuwa amehoji kuwa riwaya hii ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihali*, ilikuwa ni tunu iliyosanifiwa kwa ufasaha wa kipekee, ufasaha uliotokea tu kwa mara moja katika fasihi ya Kiswahili. Mulokozi 1985:45 alihoji kwamba:

> *The story, that is; Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Tulanalwo na Bulihwali of course, much richer than the above skeleton may lead one to believe. It is not confined to the lives of Myombekere and Bugonoka and their children, but deals rather with the life of the Kerebe society of the time, seen through the life, actions, problems and aspirations of this family. Myombekere represents Kerebe manhood just as Bugonoka represents Kerebe womanhood. Their quest is the perennial quest of their society, for they are expressing and enacting the dominant value of that society. As their lives unfold before us, we are gradually introduced to the whole tapestry of the Kerebe world: the culture, customs, beliefs, practices, human relations and productive activities; the geographical environment, flora and fauna, months and seasons; and the sciences, oral literature, art and craft.*
>
> *(Hadithi hii, yaani hadithi ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Tulanalwo na Bulihwali, ni hadithi yenye ukwasi na utajiri wa kimawazo kuliko ambavyo muhtarasri huu hapa juu unavyoweza kutushawishi kuamini. Hadithi hii haifungiki katika maisha ya Myombekere na Bugonoka na Watoto wao, ni hadithi inayosawiri na kusimulia maisha ya jamii ya Kerebe ya wakati huo kwa kadri inavyowasilishwa na kuonekana kupitia maisha, matendo, matukio, matatizo na matamanio ya familia hii. Myombekere anawasilisha dhana ya uanaume wa Kikerebe kama Bugonoka anavyowasilisha dhana ya uanauke wa Kikerebe. Matamani yao, utafutaji wao ni utafutaji wa kila siku wa jamii yao, kwa sababu kupitia matendo yao wanaeleza na kutekeleza thamani tawala za jamii hiyo. Kadri Maisha yao yanavyojikunjua na kujidhihirisha mbele yetu, tunaingizwa pole pole na hatua kwa hatua katika mfumo mzima wa ulimwengu wa Kerebe:utamaduni, mila, desturi, Imani, mahusiano*

> *ya kibinadamu na taratibu za uzalishaji; tunaingizwa katika mazingira ya kijiografia, mimea na wanyama wake, miezi na misimu, mifumo yake ya kisayansi, fasihi yake, sanaa yake,ufundi na kazi mikono. (178))*

Kwa mintarafu ya uhalisi huu wa kihistoria, kimaeneo na kiutunzi, tuliona haja ya kuchanganua riwaya hizi mbili - *Kaburi Bila Msalaba* na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali.* Tuliangazia ujitokezaji wao kwa Kiingereza sio tu kama kazi ya fasihi ya Kiafrika iliyohawilishwa hadi lugha ya Kiingereza bali pia kuutathmini mchakato wote wa kuitafsiri kama mchakato na mkakati wa kuhifadhi utamaduni wa Kiafrika kupitia taaluma ya tafsiri.

1.2 Suala la Utafiti

Tungo za kifasihi kwa kawaida huwa zinasanifiwa kiubunifu hivi kwamba zinawezeshwa kubeba habari na maarifa muhimu ya jamii kuhusiana na historia na utamaduni wa jamii husika. Yaani, mienendo na desturi za maisha ya jamii hiyo, mifumo ya uwazaji na miono - ulimwengu ya jamii mahususi pamoja na imani na itikadi zao. Kwa mintarafu hii, katika utafiti huu tulipania kuangazia na kutathmini jinsi uhalisia wa kitamaduni na kihistoria unavyosawiriwa makusudi ili kuhifadhiwa kupitia mchakato wa tafsiri.

Utafiti huu, hali kadhalika, ulichanganua sampuli teule ya msamiati, istilahi zinazoashiria masuala ya kitamaduni na kihistoria, ujielezaji wa kisanifu na maelezo ya moja kwa moja ya mwandishi au mtafsiri yanayojitokeza katika MC1 (*Kaburi Bila Msalaba)* na MC2 (*Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali*) pamoja na tafsiri zao. Kwa kujikita katika uchanganuzi wa elementi za kiisimu, matumizi mahususi ya msamiati na istilahi teule, utafiti huu uliangazia vipengele vilivyo na uwezo wa kubaini maarifa na habari za kitamaduni na kihistoria. Vivyo hivyo, tuliangazia mitindo ya ujielezaji inayojibainisha katika kazi hizi mahususi

kutoka Kenya na Tanzania. Utafiti huu ulibaini viashiria vya uhalisi wa kihistoria na vipengele vya kitamaduni vinavyoshirikishwa katika uhifadhi wa tungo za kifasihi.

Mbali na utafiti huu kuwa na umuhimu wa kiubunifu na kisanaa, utafiti huu hali kadhalika uliwasilisha uwezo wa kubainisha uhalisia wa kitamaduni, kihistoria na kianthropolojia.

Kadri ya ufahamu wetu, ingawa tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu fasihi tafsiri ya Kiswahili, hakuna utafiti uliochanganua suala la uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Utafiti huu ulibaini pengo hili na ulijaribu kuliziba kwa kutumia vielelezo vya riwaya mbili - *Kaburi Bila Msalaba na Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali.* Riwaya hizi zilisomwa huku vipengele vya kitamaduni vikiteuliwa na kuchanganuliwa.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulipania kufikia malengo yafuatayo:

i. Kubaini na kueleza, kwa njia ya mifano kwamba riwaya za *Kaburi Bila Msalaba* na riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* ni hazina ya hifadhi na utajiri tunu wa utamaduni wa kijadi na ukale wa maisha ya jamii mahususi ya Kiafrika.

ii. Kuijadili na kuitathmini michakato na mikakati iliyotumiwa kutafsiri kazi chanzi kama mikakati ya uhifadhi na uhawilishaji wa kitamaduni wa riwaya za *Kaburi Bila Msalaba* na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali.*

iii. Kufasili jinsi udumishwaji wa vipengele anuwai vya ujielezaji katika lugha chanzi unavyoweza kufasiriwa kama ithibati ya wazi ya uhifadhi wa utamaduni wa moja kwa moja katika tungo asilia na katika tafsiri.

1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali ya utafiti yafuatayo:

i. Ni vipi riwaya za *Kaburi Bila Msalaba* na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* zinaweza kuangaliwa na kutathminiwa kuwa ni hazina na hifadhi ya utajiri wa utamaduni wa jamii mahususi za Kiafrika?

ii. Mtafsiri ametumia mikakati na michakato gani ili kutafsiri kazi chanzi kama njia ya uhifadhi na uhawilishaji wa kitamaduni katika MC1 na MC2?

iii. Je, ni kwa njia gani udumishwaji wa vipengele anuwai vya ujielezaji vya lugha chanzi unaweza kufasiriwa kama ithibati wazi ya uhifadhi wa utamaduni wa moja kwa moja katika tungo asilia na katika tafsiri?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Kuna sababu nyingi zinazoweza kutolewa kuhalalisha umuhimu wa kuhifadhi utamaduni. Utamaduni ni nguzo na kielelezo cha uhifadhi wa uadilifu, ukamilifu na uzima wetu kama watu katika jamii mahususi. Umuhimu wa urithi wa vipengele vya utamaduni usiodhibitika haujitokezi katika viashiria vya wazi bali ni utajiri na ukwasi wa maarifa na stadi za maisha zinazopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Urithi na utamaduni asilia wa taifa, jamii au kundi la watu, ni uhalisia wenye tunu na upekee, urithi unaojibainisha kwa mifumo ya uwazaji, urithi wa maeneo ya kitamaduni, majengo, madhabahu na vipengele vingine vyenye umuhimu wa kitamaduni.

Utamaduni na historia yake hujumuisha amali za uadilifu, imani na madhumuni ya kitamaduni. Hizi ndizo nguzo za utaifa wa watu. Kwa hivyo, uhifadhi wa utamaduni ni uhifadhi wa utaifa wa watu. Uhifadhi wa utamaduni wa watu ni suala fungamani na

tata. Hii ni kwa sababu hili ni suala linalohitaji usawazishaji wa vipengele vingi. Kwa mfano, katika kutambua upekee wetu kama watu, ni sharti watu wawe radhi kutambua tamaduni zinazowapa nguvu na tamaduni zinazowadhalilisha. Urithi wa kitamaduni unajumuisha miundo mbalimbali ya kitamaduni, sanaa na vifaa anuwai vya kitamaduni katika jamii mahususi. Urithi huu hali kadhalika, unajumuisha vipengele visivyodhihirika kama vile lugha, desturi, imani, mila na jadi. Utamaduni wa kundi lolote la kijamii huwa tofauti, wenye upekee na hauwezi kubadilishwa na utamaduni mbadala. Hii ni mojawapo ya sababu za kuhifadhi utamaduni kwa ajili ya vizazi vya baadaye kama njia ya kuhakikisha mstakabali wa jamii mahususi.

Ni sharti kizazi kichanga kidumishe utambulisho wake kama watu, kuwatambua na kuwaenzi watangulizi wao. Hivyo hivyo, ni sharti kizazi hiki kifuate desturi, amali na tamaduni hizo ili kuzuia mabadiliko na mageuzi yaliyo na athari hasi. Kudumisha historia, desturi na jadi ya watu kwa jumla ni hatua inayoimarisha mazingira ya kizazi kilichoko, hususan udumishwaji wa mirathi ya mahali na sehemu zilizo na umuhimu wa kitamaduni. Kuna manufaa ya kiikolojia kuhifadhi na kudumisha majengo ya makazi na kibiashara pamoja na miundo ya jadi ya ujenzi, hii ni kwa kuwa uhifadhi na udumishwaji wa mambo ya kihistoria ni namna udumishwaji wa maendeleo ya makazi, uhifadhi huu unazidisha thamani ya majengo, miundo mbinu na ardhi kwa jumla.

Uhifadhi na udumishaji wa mirathi ya kitamaduni unapunguza utegemezi wa nyenzo na vifaa vipya. Unapunguza uchafuzi wa nyenzo na matumizi mengi ya kawi. Mbali na kutunza, kuhifadhi na kuendeleza mirathi ya kitamaduni, kuna manufaa ya kuhifadhi lugha na mitazamo ya jadi ya upekee wa njia za maisha za makundi mahsusi ya jamii. Pamoja na kwamba kunaibuka mitazamo ya kisasa ya kuangalia maisha, ni sharti itambuliwe kuwa usasa una gharama, na wakati mwingine maarifa

ya jadi yanasaidia kutatua matatizo ya usasa. Hii ndio maana kuna haja na msisitizo wa kutetea kuhifadhi lugha, tamaduni, mila, desturi na jadi za makundi ya wachache na makundi ya waliotengwa.

Kauli zinazotolewa kuhusiana na manufaa ya kujifunza lugha za kisasa zinachangia kufisha lugha za kiasili ilhali kuna manufaa mengi yanayoweza kupatikana katika lugha hizo. Lugha za kiasili zisipohifadhiwa, mara nyingi lugha hizi huwa katika hatari ya kuangamia na kupotea kabisa. Hii ndio maana kunatolewa hamasisho kuhusu uhifadhi wa kitamaduni. Ili kuzuia au hata kudhibiti upoteaji wa lugha na hatimaye upoteaji wa utamaduni, kuna haja ya kuhifadhi utamaduni unaohimiliwa na lugha hizo. Hili linaweza kufanywa kwa njia mbili: kuhifadhi lugha kunahifadhi utamaduni na kuhifadhi utamaduni kunahifadhi lugha.

Ni kosa kubwa kutowajibika kuhifadhi lugha na tamaduni za watu, kwa sababu kuziacha lugha hizi kupotea ni sawa na kupoteza uanuwai na upekee wa miono - ulimwengu ya jamii nyingi duniani. Lo Liyong (1972) anafafanua utamaduni kama jumla ya shughuli, kumbukumbu, matumaini na mipango ya baadaye ya jamii fulani zikiwemo pia ndoto na maono ya jamii hizo. Udumishaji wa utambulisho wa makundi ya kijamii unashawishi haja na dharura iliyopo ya uhifadhi wa kitamaduni. Kadri utelekezi wowote wa uhifadhi wa kitamaduni unavyozidi ndivyo ukunjufu wa ulimwengu wetu unavyoendelea kudidimia. Watu wanapokuwa hawana ufahamu wa umuhimu wa kitamaduni, uwezo wao wa fikira huwa katika mbano. Majaribio yoyote ya kutaka kufanya uanuwai wa utamaduni kuwa na jinsi moja, yanasababisha thamani ya kuwa na mitazamo anuwai ya kujifunza. Vilevile, juhudi kama hizo za kubana uanuwai wa kitamaduni zinafilisha uwezo wetu wa kusuluhisha matatizo katika hali fulani. Juhudi hizo ni hatari katika mitagusano ya binadamu na mazingira yake.

Mbinu na njia moja madhubuti ya uhifadhi wa utamaduni ni kupitia mifumo ya elimu, hususan pale mifumo ya elimu inapokuwa na mikakati fumbati inayoshirikisha ufahamu wa utamaduni katika mitaala yake, kwa mfano, ufundishaji wa fasihi ya jadi. Elimu kama hiyo inaweza kuangaliwa kama mkakati wa kuhifadhi mirathi ya kitamaduni inayoonekana na ile isiyoonekana. Ni sharti kizazi cha sasa kielewe umuhimu wa kutambua thamani iliyoko ya uhifadhi wa utamaduni. Kila mara jamii inaheshimiwa wakati inapotambua na kujitambulisha na utamaduni wake. Utamaduni na mirathi ya kitamaduni ambayo hujitambulisha nayo, ni kitu cha kuonewa fahari. Uhifadhi wa uanuwai wa utamaduni na mirathi ya kitamaduni husaidia na kuwanufaisha sio tu wale wanaotetea tamaduni zao, bali pia huchangia kuhifadhi falsafa za maisha na mifumo ya fikira na uwazaji katika ulimwengu tunamoishi.

Uhifadhi wa kitamaduni ni muhimu hata katika nyakati za kizazi kinachojiangalia na kujitambulisha kama kizazi cha kidijitali na kiteknolojia. Uhifadhi wa utamaduni hujenga hisia za umoja na utambulisho kwa kuwa sehemu ya kundi au jamii mahususi ya watu. Hii ndio maana mababu walipitisha mirathi mingi ya kitamaduni kwa vizazi vya baadaye. Uhifadhi wa utamaduni unawezekana hata katika kizazi cha maisha ya kisasa yaliyo na kasi, mivutano na shinikizo za aina nyingi. Uhifadhi wa kitamaduni unahitaji pia ulinzi na utunzaji wa mirathi ya kitamaduni. Muhimu zaidi ni kwamba, usambazaji na uenezaji wa mafao na manufaaa mengine ya kitamaduni ni moja ya njia za hakika za uhifadhi wa utamaduni.

Katika baadhi ya jamii na nchi mirathi ya urithi wa kitamaduni ni haki ya kibinadamu na ni haki ya kikatiba. Katiba ya Jamhuri ya Kenya (2010) inatambua utamaduni kama nguzo muhimu ya kuimarisha jamii inayoweza kujitambulisha kikamilifu. Jambo hili limesisitizwa katika sura ya 4 kifungu cha 44 kinachosema: kila mwanajamii ana haki ya kutumia lugha na kushiriki katika maisha ya kitamaduni kwa

chaguo lake. Raia anayetoka katika jamii ya utamaduni au lugha fulani ana haki pamoja na wanajamii wenzake. Aidha, ana haki ya kufurahia utamaduni wake na kutumia lugha yake. Vile vile ana haki ya kuunda, kujiunga na kudumisha vyama vya kitamaduni na kilugha katika jamii. Katiba inatambua utamaduni kama msingi wa taifa na mkusanyiko wa ustaarabu wa watu wa taifa moja. Katiba ya Kenya imebaini kwa uwazi kuwa serikali itakuza aina zote za kujieleza za kitaifa na za kitamaduni kupitia fasihi, sanaa, sherehe za kitamaduni, sayansi, mawasiliano, vyombo vya habari, machapisho na njia zingine za mawasiliano. Kwa mintarafu hii, ni wajibu wa kila raia kulinda, kukuza, kueneza, na kuhifadhi utamaduni wao.

Aidha, utafiti huu utakuwa kama rejea ya baadaye kwa wasomi na wataalamu wa masuala ya fasihi na tafsiri. Marifaa haya yatawafaa kwa kubaini viashiaria vya utamaduni katika matini za fasihi na kuzuka na mikakati ifaayo katika mchakato wa tafsiri.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza suala la uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Kazi hii ilijikita katika riwaya mbili kutoka Kenya na Tanzania mtawalia: *Kaburi Bila Msalaba* na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* na tafsiri zao – *Unmarked Grave* na *Mr. Myombekere and His Wife Bugonoka, Their Son Ntulanalwo and Their Daughter Bulihwali.* Utafiti huu ulichunguza namna uhifadhi wa utamaduni unawezeshwa kupitia mchakato wa tafsiri.

Kuna muumano thabiti kati ya lugha na utamaduni wa watu. Uhusiano huu umebainishwa kupitia viashiria vya kitamaduni, dhana na msamiati wa kitamaduni. Mifano ya utamaduni wa kiekolojia, utamaduni wa kijamii na utamaduni nyenzo, yaani vifaa vya kijamii iliorodheshwa na kulinganishwa katika matini chanzi na

matini lengwa pekee ili kubaini namna vielelezo hivyo vinavyotumika kuhifadhi utamaduni kwa hadhira lengwa. Kwa kutumia maelezo na mifano ya matini zilizoteuliwa tumeeleza jinsi riwaya hizi ni hazina kuu ya maisha ya kijadi katika jamii mahsusi ya Kiafrika. Aidha, mikakati ya upanuzi maana, ujumuishaji wa dhana, uhawilishaji na muungano wa mbinu za tafsiri iliyotumiwa kutafsiri vielelezo vya utamaduni kama njia ya kuhifadhi utamaduni katika matini lengwa pekee ndiyo imejadiliwa. Utafiti huu haukudhamiria kuonyesha makosa katika fasihi tafsiri bali umeonyesha nafasi ya lugha kama mkakati wa uhifadhi na uhawilishaji wa utamaduni na uhalisi wa kihistoria.

1.7 Mhutasari wa Sura

Sura hii imeshughulikia masuala ya kimsingi katika utafiti huu kwa kuonyesha usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti na pia sababu za kuchagua mada. Imeangazia pia upeo na mipaka ya utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulikia mambo yafuatayo: usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za utafiti na kuweka wazi upeo na mipaka ya utafiti huu. Sura hii imeangazia yaliyoandikwa kuhusu mada na kueleza kwa undani nadharia zinazoongoza utafiti huu.

2.1 Dhana ya Tafsiri

Tafsiri ni utaratibu muhimu katika mawasiliano ya binadamu. Taaluma hii huchangia kwa kuwasilisha habari kutoka LC hadi LL. Kulingana na Kamusi ya TUKI (2002), tafsiri ni mchakato wa kutoa mawazo kutoka lugha moja kwenda kwa lugha nyingine bila kubadilisha maana. Ujumbe na mawazo ya matini chanzi hudumishwa ila kinachobadilika ni lugha. Maarifa haya yanahusu umilikaji wa mali ya jamii, mila, dhana na mienendo ya binadamu kwa jumla. Mazingira ndiyo malighafi ya lugha kwani jamii huchota kutoka kwa vitu vinavyoizunguka. Kila jamii inafasiri maana kwa mujibu wa utamaduni wake.

Wolf (2007) anasema mchakato wa tafsiri kama utaratibu na matokeo ni muhimu ushirikishwe katika miktadha ya kijamii. Kwa misingi hii mchakato wa tafsiri huwa unafanywa na binadamu katika utaratibu wa kijamii na kwa njia nyingine zoezi la tafsiri haliepuki mifumo ya kijamii ambayo hutegemea matokeo na mikakati ya kufanikisha mchakato wa tafsiri. Zoezi la tafsiri halipatikani kwenye ombwe tupu bali katika mazingira na miktadha maalum ya kitamaduni.

Tafsiri ni uga muhimu kwa sababu hurahisisha mawasiliano baina ya watu wanaozungumza lugha tofauti (Ezika 2012 na Bustani, 2014). Mawazo mbalimbali

katika sekta tofauti ulimwenguni husafirishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kupitia tafsiri. Katika muktadha wa utafiti huu, tafsiri ni nyenzo ya kueneza utamaduni na ni mbinu ya kujifunza na kufundisha lugha ya pili au ya kigeni. Mchakato wa tafsiri umepitia hatua mbalimbali katika historia.

2.2 Historia ya Tafsiri

Maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisayansi duniani yalitokana na juhudi za ugunduzi za watu wa kale, na yametufikia kwa njia ya tafsiri. Zakhir (2010) akielezea historia ya tafsiri anasema kuwa tafsiri inaaminiwa kuanza pale wanadamu walipoanza kuwa na lugha tofauti. Taaluma ya tafsiri ina historia ndefu kutoka pale mwanzo binadamu alipozuka na lugha mabalimbali katika mawasiliano yao. Wanjala (2011) anaeleza kuwa historia ina taarifa, maelezo na uchambuzi wa matukio, watu na nyakati teule zinazoathiri maisha ya wanajamiii husika, sasa na hata siku za usoni. Mwansoko na wenzake (2015) wanaeleza historia ya tafsiri kuwa mchakato wa tafsiri ulianza Afrika huko Misri miaka elfu tatu (3000) na zaidi kabla ya Kristo, ugunduzi wa ustaarabu uliokuwa Misri uliigwa na Wayunani, hatimaye kuufanya kuwa chumbuko la ustarrabu katika karne ya 19. Ustaarabu huu wa Wamisri ulikuzwa na kuendelezwa kupitia mchakato wa tafsiri. Mambo waliyojifunza waliyafasiri kwa Kiyunani na kuyasambaza huko Ulaya. Miongoni mwa kumbukumbu za awali kabisa katika taaluma ya tafsiri ni Bibilia ya Kiyunani iliyotafsiriwa kutoka Kiyaudi.

Baada ya Ukirsto kuenea Ulaya, elimu ya zamani ilianza kupigwa vita vikali kwa kudaiwa kuwa ilikuwa ya ‘kipagani’. Hali hii ilisababisha kipindi kijulikanacho katika historia kama ‘zama za giza’ ambapo maandishi yote ya kidini na ya kisayansi yalisitishwa. Hatua hii ilikwamiza zoezi la tafsiri kwa sababu hakukuwa na maandishi ya vitabu. Baada ya muda hali hii ilibadilika kuanzia karne ya kumi na mbili hadi kumi na sita kulikuwa na mvuvumko wa Kikrito ambapo tafsiri za Bibilia zilizidishwa

mno kwa sababu watu wengi walihitaji kusoma kutoka makabila mbalimbali ulimwenguni. Wataalamu wa tafsiri walilazimika kutoa tafsiri nyingi za Biblilia ili kukidhia haja na mahitaji ya waumini.

Karne ya kumi na tisa ni kipindi muhimu katika historia ya tafsiri. Wataalamu wengi waliishughulikia tafsiri kwa kuihusisha na masuala ya fasihi andishi. Mtazamo huu ulizua upungufu mkubwa ulioifanya tafsiri kukosa msingi imara wa kinadhari ambao ungehusisha vipengele vyake mbalimbali. Licha ya majaribio mengi kufanywa na wataalamu wengi kuna ufa mkubwa baina ya nadhari za tafsiri na utekelezaji halisi wa tafsiri. Nadharia nyingi za tafsiri sio toshelezi kwa hivyo uwezo wa kutoa miongozo kamilifu kwa zoezi zima la tafsiri ni lazima itolewe. Aidha, kuna changamoto nyingine inayosababishwa na tofauti za kitamaduni baina ya matini chanzi na matini lengwa. Tofauti hizi za kitamaduni zinaweza kuwa dini, mavazi, mila na desturi zingine za kijamii.

Karne ya ishirini imeshuhudia maendeleo na ujenzi mkubwa katika taaluma ya tafsiri. Hatua za maendeleo katika sayansi na teknolojia zimechangia pakubwa ongezeko la kazi za tafsiri. Viwango vya tafsiri vinazidi kupanda kwa sababu kuna program mbalimbali za tafsiri kwenye mtandao. Mkondo wa kisasa katika tafsiri umejikita zaidi katika vipengele vya maana na mawasiliano ambavyo vinachukuliwa na wataalamu wengi kuwa vya kimsingi zaidi katika kufanikisha mchakato wa tafsiri. Katika mchakato wa kufanya tafsiri ya kazi za fasihi kutoka LC hadi LL ni sharti lugha fulani itambuliwe na utamaduni wake husika. Mfasiri hufanya maamuzi muhimu ili kufikisha ujumbe wa mwandishi katika mfumo wa LL ambayo ina mfumo wa kitamaduni ulio tofauti na mfumo wa LC. Shughuli ya tafsiri kwa hakika inahitaji urazini wa utamaduni wa Makala Chanzi ili kutekeleza tafsiri iliyo bora. Utamaduni wa jamii moja huathiri moja kwa moja matumizi ya maneno na utunzi wa sentensi.

2.3 Fasihi Tafsiri

Fasihi tafsiri huwa ni ufunguo wa kujenga daraja la ushirika kwa kuzifahamu jamii zingine. Hadhira lengwa inaweza kujifunza kwa urahisi yanayotokea katika sehemu nyingine ulimwenguni kutokana na kazi za fasihi zilizotafsiriwa. Kwa hivyo, watu wanaotokana na utamaduni tofauti wanaweza kustahikiana na kuvumiliana ili kuimarisha maelewano katika ngazi za kimataifa. Kwa mantiki hii, viashiria asilia vya utamaduni wa kiafrika hufafanuliwa kwa tajriba ya wageni ili kujenga ufahamu kwa urahisi. Fasihi tafsiriwa inaweza kuwa chombo mwafaka cha kujenga na kudumisha mahusiano ya kitamaduni, umoja na utangamano maalum miongoni mwa wanajamii wanaotokana na jamii au mataifa tofauti ulimwenguni (Maitaria, 2016 na Mutui, 2009). Umataifa huu unawezeshwa kupitia fasihi tafsiriwa. Uhalisia huu wa maisha unaweza kuwanasua wenyeji kutokana na 'ufinyu' wa mawazo kuhusu mwonoulimwengu wao.

Fasihi tafsiriwa ni fasihi inayojibainisha kwa kuhusishwa na uhalisi wa mifumo ya lugha na utamaduni wa jamii husika. Kimsingi tungo za kifasihi hutungwa kutokana na mazingira halisi ya jamii na lugha hutumika kama chombo cha kusafirisha uhalisia huu wa kijamii. Fasihi tafsiriwa huwa ni njia ya kusambaza na kuhifadhi utamaduni kutoka jamii moja hadi nyingine. Aina hii ya fasihi huchukua na kudhibiti nafasi dhahiri na kutekeleza majukumu mahsusi katika hadhira lengwa. Fasihi hii haikosi kutekeleza uamili mahususi katika fasihi na lugha lengwa. Ni muhimu kuelewa kwamba kutafsiri fasihi si unakili wa kikasuku bali ni uhalisi wa kiubunifu unaojibanisha katika miktadha na mifumo ya lugha, fasihi na utamaduni lengwa. Basi kwa mintarafu hii, hali hii huipa hadhi fasihi ya Kiswahili pamoja na lugha katika muktadha wa kimataifa, kimaeneo barani Afrika na katika mataifa mengine ulimwenguni.

2.4 Tafsiri na Utamaduni

Tafsiri na utamaduni ni masuala yaliyo na uhusiano wa karibu na yanahitaji umakini wa hali ya juu. Tafsiri bila kuzingatia utamaduni husika hupotosha ujumbe hata kuathiri lengo la tafsiri. Utamaduni ni hali ya maisha ya watu wa jamii fulani ikiwa ni pamoja na itikadi na imani zao (King'ei 2010, Al- Hassan 2013; Mwansoko na wenzake, 2015). Katika zoezi la tafsiri ni lazima mtafsiri azingatie vipengele vyote vya kitamaduni hasa vya LC na LL kwa sababu kila lugha ina utamaduni wake mahususi.

Ei- Dali (2011) aliwahi kusisitiza kwamba utamaduni wa LL usilazimishwe kwa matini asilia. Anashikilia kwamba kila matini itazamwe kwa kuzingatia utamaduni wa matini na lugha asilia. Utamaduni wa kijamii unarejelea mawazo yasiyo dhahiri waliyo nayo binadamu kuhusu mazingira yao zikiwemo imani, desturi, amali, busara, sheria, kanuni, lugha, mashirika na asasi za kijamii. Yapo maneno ambayo ni ya kipekee na mara nyingi huwa ni viwakilishi vya utamaduni katika jamii husika. Mengi ya maneno haya huwa ni ya kitamaduni na ni rahisi kuyatambua kwa kuwa yanahusishwa na lugha maalum na hayawezi kutafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja. Kawaida desturi nyingi za kitamaduni huelezwa kwa lugha ya kawaida ambapo tafsiri ya moja kwa moja huweza kupotosha maana.

Baker (1992) anaeleza kuwa neno katika hadhira asilia huweza kuwasilisha dhana iliyo tofauti kabisa katika utamaduni wa hadhira pokezi. Maneno yanayohusu dini na imani, itikadi na aina ya vyakula, mazingira na mengine mengi hukosa visawe katika lugha nyingine. Kila lugha kama kiwakilishi cha utamaduni mahususi huwa na dhana zilizo na upekee na umahususi maalum ambao unatambulika tu katika lugha hiyo. Ni kweli kwamba utamaduni huipa jamii upekee na kuifanya kutambuliwa kwa njia ya

kipekee. Upekee huu ni chanzo cha changamoto za kutafsiri vielelezo mbalimbali vya kitamaduni.

Jilala (2006) anasema tafsiri ni mchakato wa uhawilishaji wa mawazo ama ujumbe ulio katika utamaduni wa lugha chanzi na kuweka mawazo ama ujumbe huo katika utamaduni wa lugha lengwa. Mtaalamu huyu anaongeza suala la utamaduni katika tafsiri na kuona kuwa hauwezi kuielezea dhana ya tafsiri bila kuhusisha utamaduni kwa sababu lugha ni kipengele cha utamaduni. Tamaduni hutofautiana baina ya jamii mbalimbali ulimwenguni. Tamaduni huwa zimejengwa na jamii katika mifumo bainifu inayodhihirika kupitia mila, desturi, kaida, miiko, na mafundisho yanayopitishwa kimapokezi tangu jadi. Mwansoko na wenzake (2006) wanavyouita ‘uhawilishaji’ unamanisha usafirishaji wa maudhui na maana sio tu kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine, bali pia wa utamaduni, mawazo na miundo tofauti ya lugha. Tofauti hizi za kitamaduni humlazimisha mtafsiri wakati mwingine kutumia maneno yanayoakisi mahitaji ya kimaana na kuwasiliana kwa hadhira lengwa. Gouadec (2007) anaeleza kuwa, licha ya kuwa au kujua lugha zaidi ya moja ni jambo muhimu katika tafsiri lakini halitoshi. Badala yake mtafsiri anahitaji kuwa na weledi wa lugha na uelewa mpana wa utamaduni, historia, mitazamo ya jamii ambazo lugha zake zinahusika kwenye kazi zinazofasiriwa na pia weledi kwa mada inayoshughulikiwa kwa mchakato wa tafsiri.

House (2009) anasema kuwa tafsiri sio tu tendo la kiisimu bali pia ni la kitamaduni; ni kitendo cha kuwasiliana baina ya tamaduni. Tafsiri kila wakati inahusu lugha na utamaduni na haviwezi kutenganishwa kamwe. Tamaduni zote za kila jamii huwa ni hazina kuu ya mikusanyiko mikubwa ya maarifa, tajriba, busara na hekima katika harakati za kila siku za jamii mahususi. Lugha huwa ndani ya utamaduni kwa kuwa

hueleweka zaidi inapoelezwa ndani ya utamaduni. Kwa misingi hiyo lugha hueneza, hukuza na kuimarisha vipengele mbalimbali vya kitamaduni.

Aidha, Mshindo (2010) anasema kutafsiri ni kufafanua maana ya matini moja na kutayarisha baadaye matini nyingine inayowiana nayo ambayo huitwa tafsiri na ambayo inawakilisha ujumbe ule ule uliomo katika matini ya awali kwa kutumia lugha nyingine. Mawazo ya matini asilia hudumishwa ila lugha ndiyo hubadilika.

Salehi (2012) anadai kuwa matini hufasiriwa sio kwenye ombwe tu bali kwa kuegemea kaida za jamii husika ambamo wanajamii huzifafanulia tabia zao na za wenzao. Kaida za jamii huwa ni tamaduni zinazoelezea tajriba za watu katika jamii husika. Utamaduni huwa ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao na mambo na taratibu zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha na jamii nyingine. Jamii huwa na jumla ya mambo yanayobuniwa ili kukidhi utashi na maendeleo yao.

Kulingana na mawazo yaliyonukuliwa ya wataalamu mbalimbali tunapata kuwa tafsiri ni mchakato unaohusisha uhamishaji wa ujumbe ulio katika utamaduni wa lugha chanzi na kuuweka ujumbe huo katika utamaduni wa lugha nyingine. Kuna vipengele mbalimbali vya kitamaduni katika fasihi tafsiriwa.

2.5 Fasihi Tafsiriwa

Fasihi tafsiriwa ni kauli ya kijumla inayoashiria tafsiri katika tanzu zote za fasihi ambazo zinaweza kujumuisha maandishi ya kinathari, tamthilia, ushairi, fasihi ya watoto na miongoni mwa migao mingine ya fasihi. Johnson (1991:1), anaeleza fasihi kuwa ni musanyiko wa maarifa katika mifumo ya kiusimulizi au kimaandishi, kuwa ni mwigo wa maisha halisi ambayo yanaakisi ustaarabu na utamaduni. Aidha, anaendelea kuhoji kwamba fasihi ni mwigo wa maisha ya watu katika jamii unaoangazia kila kipengele cha shughuli za kibinadamu. Shughuli hizi zinajumuisha

tamaduni zao, burudani, maarifa yao na mifumo ya mahusiano mengine. Katika maelezo yake hakubainisha maarifa haya yanajibainisha katika utanzu upi. Basi inaweza kuchukuliwa kwa kijumla kwamba maarifa haya hujitokeza katika tanzu zote za fasihi. Masuala haya yanapoangaliwa katika mkabala wa tafsiri za fasihi, yana maana kwamba tafsiri za fasihi zinajishughulisha na tafsiri za matini zilizojaa na kusheheni vipengele tata vya kitamaduni vinavyojifunga katika miktadha maalum ya kijamii.

Aidha, fasihi tafsiriwa ni tafsiri ambayo hufanikishwa na uhawilishaji wa maana hasa yenye wasifu wa kifasihi kutoka lugha chanzi kwenda kwa lugha lengwa (Yegon, 2016). Fasihi tafsiriwa ni pana kwa misingi kwamba hujumuisha mambo mengine ambayo ni ufafanuzi wa maana ya matini, unukuzi na uandishi mpya. Kuna sababu mbalimbali zinazofanya fasihi kutafsiriwa miongoni mwa sababu hizo ni pamoja na: kupanua hadhira, kuwafikia walengwa mahsusi wa bunilizi husika, kupanua soko kwa wasomaji na kuhifadhi utamaduni wa matini chanzi. Kutoka mwanzo wa mchakato wa tafsiri, mtafsiri wa fasihi ni muhimu ajishughulishe kuelewa na kuthibiti sio tu upekee wa lugha bali pia miundo ya lugha pamoja na yaliyomo katika kazi husika. Katika zoezi la tafsiri, mtafsiri anashurutishwa kushiriki katika ubunifu wa mwandishi wa kazi chanzi katika miktadha ya jamii husika na fasihi lengwa.

Tafsiri nyingi za kifasihi zinazofanya katika fasihi za kiulimwengu zinahusisha kazi za kiubunifu, hususan nathari kazi za riwaya na haditi fupi. Utanzu wa riwaya unafafanuliwa kama ni kazi ya fasihi ya kubuni inayojikita katika mambo ya kweli na yasiyo ya ukweli na huwa na muundo wa nathari. Huwa na msuko mpana unaosheheni vitushi vingi pamoja na wahusika wa kutosha wanaendeleza dhamira na maudhui ya mwandishi. Ufahamu wa sifa hizi kuhusiana na riwaya na kazi zote katika tafsiri za fasihi una maana kwamba, ni sharti mtafsiri aelewe ufundi na

muonoulimwengu wa mwandishi ili aweze kufanikisha shughuli nzima ya tafsiri. Mtafsiri anafaa kuelewa maana za maneno zinazorejelea dhana mbalimbali kwa sababu dhana hizi zinaweza kuwa na athari pana katika miktadha fulani ya kiusomi na katika taaluma ya tafsiri. Ili kufanikisha zoezi la tafsiri mtafsiri anashurutika kuangalia na kubaini mitindo ya kiuandishi kwa kuangazia mifumo yake ya kifani, usawiri wa wahusika, ujenzi wa mandhari, uwasilishaji wa dhamira na maudhui katika kazi yake.

Kuna ithibati za aina mbalimbali kwamba suala la tafsiri na uhusika wake wa kibunilizi katika fasihi ya Kiswahili limewahi kujitokeza katika tafiti mbalimbali, na limewahi kujadiliwa kwa njia anuwai katika fasihi ya Kiswahili na katika fasihi nyingi za kilimwengu. Tafiti nyingi za fasihi tafsiri zimechangia kutolewa kwa mahitimisho mengi juu ya masuala kama; udhaifu wa kutafsiri fasihi, ukosefu wa ulinganifu katika tafsiri, maamuzi ya mtafsiri katika tafsiri za fasihi, michango ya tafsiri katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili na mengine mengi. Baadhi ya kauli na mahitimisho ambayo yametolewa ni ya kijumla na baadhi zikiwa kauli kuhusiana na kazi mahususi.

Ufahamu huu unatuchochea kuhoji kwamba mapitio ya maandishi na machapisho yaliyodhamiriwa katika utafiti huu umelenga kubaini masuala ibuka katika kazi ambazo zimetafitiwa na kuliangazia suala la fasihi tafsiri na uhusika wake katika fasihi ya Kiswahili kwa jumla na mitagusano ya fasihi za kigeni kupitia kwa mchakato wa tafsiri. Hii ni kwa kuwa kazi za aina hiyo zilizopo kwa kiasi zitakuwa zinaoana na mada ya utafiti huu na kwa hivyo zinachangia kukuza hoja na kauli zitakazokuwa zinaoana na mada ya utafiti zitatuelekeza katika mahitimisho ya jumla juu ya tafsiri za fasihi kama mkakati wa uhifadhi wa tamaduni za Kiafrika. Kwa hivyo, mapitio ya maandishi na machapisho yanayojumuishwa hapa ni yale yaliyo na

mlandano wa masuala ya tafsiri za fasihi, uhusika wa mitindo ya kiutunzi na matumizi lugha katika tafsiri. Mapitio hayo yatajifunga katika utunzi, utafiti na uhawilishaji wa fasihi kutoka kwa kazi chanzi hadi kwa hadhira lengwa na kuweka kipaumbele katika mwelekeo wa mabadilishano- tafsiri hadi lugha ya Kiswahili na tafsiri kutoka Kiswahili hadi kwa fasihi na hadhira ya kigeni. Mapitio ya maandishi yanayoangazia dhana ya uhusika wa fasihi kama mkakati wa uhifadhi wa utamaduni yatajumulishwa pia, maandishi yanayoangazia athari za kiuamili za tafsiri za fasihi kwa kadri zinavyochangia ufanisi wa kiutunzi na uimarikaji wa fasihi ya Kiswahili yatashirikishwa pia. Maandishi yanayoangazia udhihirikaji, ugeukaji na udumishwaji wa mitazamo mahususi juu ya tafsiri na uhusika katika fasihi kwa jumla yatakuwa muhimu. Aidha, mapitio yanayohusu nadharia ya Skopos na anthropolojia yalishirikishwa. Mapitio haya yanalenga vilevile kuonyesha ufaafu na umuhimu wa kuzingatia maendeleo ya kiutunzi yanayojitokeza katika tasnia nzima ya tafsiri yaliangaziwa hasa kubaini yalichochea aina gani ya tafiti za kiusomi.

2.5.1 Tafsiri za fasihi kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili

Tafsiri nyingi zilifanywa kutoka lugha ya Kiingereza hadi kwa lugha ya Kiswahili. Wakati wa enzi hizi au kwa kipindi hiki lugha ya Kiswahili ilikuwa imependelewa na ilikuwa inatumiwa katika mawasiliano ya kijamii. Kwa kuwa hakukuwa na kazi zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili kulikuwa na msukumo wa kutafsiri kazi kutoka lugha ya Kiingereza hadi kwa lugha ya Kiswahili ili kuzibia pengo la uhaba wa maandishi katika lugha ya Kiswahili. Katika muktadha huu hakika fasihi ya Kiswahili iliweza kupigwa jeki kimsamiati, kimuundo, kimtindo na kimaudhui kupitia kwa kunga za uwasilishaji wa fasihi tafsiri. Hadhira ya Afrika iliweza kupata upenyu na kuona uhalisia wa maovu katika mazingira yao kwa kupitia 'jicho la ugenini' basi, fasihi hii ya ugenini iliinua na kuimarisha fasihi ya Kiafrika. Kadri muda ulivyosonga

ndivyo tulipata wataalamu na watafiti wengi wa masuala ya tafsiri za fasihi wakiwa wanazichunguza na kutathmini kazi hizi wakizingatia mada mbali mbali.

Tafsiri ya mawasiliano huwa ni nyenzo kuu katika mchakato mzima wa tafsiri. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uzalishaji wa tafsiri bora na sadifu yenye mshikamano wa maana ya ujumbe wa matini chanzi katika matini lengwa. Beaton na wenziwe (2002) wanapendekeza hatua tatu za kufanikisha kutafsiri matini za kitamaduni nazo ni: kutambua uhusiano au muktadha wa lugha, kupima maana ya tafsiri ya neno katika lugha zote na kurudia matini zote ili kupata ulinganifu maana katika tafsiri. Kulingana na Omboga (1986) yeye anapendekeza tafsiri ya mawasiliano kuwa ni mwafaka zaidi kwa kuwa ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na matatizo ya tafsiri. Alikusudia kuangazia matatizo na athari za tafsiri kutokana na udhaifu na hali duni ya kazi tafsiri kwa kuangazia riwaya ya Ayi Kwei Armah – *The Beautiful Ones Are Not Yet Born* (1968) na tafsiri yake *Wema Hawajazaliwa.* Katika tafsiri ya fasihi mtafsiri kuzuka na kazi isiyo kamilifu ni kutokuwa na uelewa wa tamaduni za lugha mbili zilizohusika. Hali hii inapotokea mtafsiri amehawilisha lugha pekee na kupuuza vipengele vingine muhimu ambavyo ni muktadha na utamaduni. Osano (1997) ameshadidia madai ya Omboga kwa kusema kuwa baadhi ya kazi zilizowahi kutafsiriwa vyema zaidi na kufikia upeo wa juu ziliegemea nadharia ya mawasiliano kuliko nadharia zingine za tafsiri. Kulingana na utaratibu wake, mawasiliano hufuma vigezo vitano vya kimsingi ambavyo ni; mwasilishi, mpokezi, ujumbe, chombo na vikwazo (muktadha wa mawasiliano na utamaduni). Vigezo hivi hutoa mwongozo thabiti kwa taaluma ya tafsiri. Kwa sababu mawasiliano ya kifasihi yanapitishwa kwa njia ya maandishi, maandishi katika tafsiri ni sharti yapokelewe kwa njia ya kusomwa na ni kupitia kwa usomaji ndipo maana huibuka. Utafiti huu utatuwezesha kutoa

mwanga kwa kazi yetu kwa sababu imebaini kiwango kipi mawasiliano yanaweza kuafikiwa licha ya tofauti za lugha zilizoko kati ya matini chanzi na matini lengwa.

Mchakato wa kuhawilisha mawazo kutoka lugha moja hadi nyingine hukumbwa na changamoto mbalimbali kwa sababu ya upekee wa lugha katika kila jamii. Newmark (1988) anaeleza kuwa; utamaduni ni mkusanyiko wa mila na desturi zote za jamii inayotumia lugha mahsusi kama njia yake ya mawasiliano. Upekee huu wa kiisimu huwa ni changamoto katika shughuli ya kutafsiri ambayo hujidhihirisha katika vipengele vinne vikuu yaani maumbo ya sauti, maumbo ya maneno, miundo ya sentensi pamoja na maana. Aidha, vipengele vya kitamaduni kama vile; ekolojia, mila na desturi pamoja na dini huwa ni changamoto katika tafsiri. Mutie (1997) alitafiti changamoto zilizojitokeza katika mchakato wa kutafsiri tamthilia ya Kiingereza hadi kwa Kiswahili. Utafiti wake ulijikita katika tamthilia *Mizigo* iliyotafsiriwa kwa Kiswahili na Bi. Muro, alilinganisha matini chanzi iitwayo *The Burdens* iliyotungwa na John Ruganda. Katika utafiti wake Mutie aligundua kwamba mitindo tofauti ya lugha mbili husababisha tofauti katika tafsiri. Alieleza matatizo yanayomkumba mtafsiri na namna matatizo hayo yanavyoathiri sanaa katika lugha pokezi. Ni dhahiri kwamba licha ya watafsiri kujitahidi kuteua visawe katika lugha pokezi, ni nadra sana kuweza kupata visawe vya lugha ya Sanaa kwani kila lugha huwa na upekee wake katika matumizi yake ya sanaa. Hali hii inapotokea humshurutisha mtafsiri kukiuka uaminifu wake kwa shughuli nzima ya tafsiri. Kazi yake imeonyesha nafasi na uamili wa tafsiri katika ukuaji wa fasihi lengwa na vile vile ameonyesha nafasi ya lugha na utamaduni katika mchakato wa tafsiri. Japo Mutie alichunguza tamthilia na kazi yetu inajikita katika riwaya, hizi zote ni kazi bunilizi ambapo moja ya malengo yetu yanazungumzia namna ya kukabiliana na changamoto hizi katika mchakato wa tafsiri.

Kazi hii itatoa mchango katika utafiti wetu kwa sababu moja ya malengo yetu hujikita katika mikakati ya kutafsiri vipengele vya kitamaduni.

Mahusiano mapana na uelewa wa utamaduni yanadhamiria kuonyesha kwamba kila kitu na kila hali ya maisha ya watu katika jamii inachangia kuibuka kwa desturi, itikadi na maadili ya jamii husika. Uhalisia huu huangazia mazingira na maumbile yanayoonekena na yasiyoonekana katika miktadha maalum. Al- Zahran (2003) anasema tafsiri sio tu mchakato unaoziba pengo linaloletwa na tofauti za lugha bali kwa kiwango kikubwa huwa kama daraja kati ya tamaduni tofauti. Changamoto za kitamaduni huzuka kutokana na matini lengwa kukosa usawa wa moja kwa moja kwa neno lililojitokeza katika matini chanzi. Hivyo mfasiri hulazimika kuweka maneno yanayokidhi ujumbe katika mawasiliano kwa hadhira pokezi ijapokuwa maneno hayo si msamiati halisi uliotumika katika matini chanzi. Aidha, Nida (1964) anashikilia kwamba lugha haiwezi kueleweka nje ya mfumo wa utamaduni ambao lugha yenyewe ni sehemu muhimu. Kwake mtafsiri hajishughulishi tu na maneno bali pia na muktadha ambamo maneno hayo yanatumika na usawe wowote unafaa kuzingatia miktadha yote miwili; ya makala asilia na makala pokezi. Omondi (1997) anajadili masuala mbalimbali ambayo huzuka kama matatizo kwa mtafsiri anapojihusisha na vipengele vya maana katika tafsiri ya diwani ya *Risasi Zianzapo kuchanua* (1975) na kuhusisha na matini chanzi iitwayo *When Bullets begin to Flower* (1972). Omondi anahoji kwamba si jambo rahisi kutafsiri au kuweza kupitisha ujumbe na maana ya matini asilia kama alivyolenga mwandishi katika hadhira lengwa; wakati mwingine maana hutatizika kwa sababu za kitamaduni. Ni wazi kwamba kwa sababu mtafsiri hukumbana na tofauti za lugha chanzi na lugha lengwa basi ni sharti awe na kaida au taratibu maalum za kuwasilisha maana asilia inavyokusudiwa. Kaida hizi zinamwezesha mtafiti kufanikiwa katika shughuli yake ya tafsiri. Kazi ya Omondi

inaweza kusemwa kuwa ni kazi ya kinadhari na kiutekelezi. Kwa misingi hiyo inaonyesha, uhalisi wa kutafsiri, kanuni na hatua zinazoweza kufuatwa katika kutafsiri kazi ya fasihi. Mawazo haya yataongoza mjadala katika tasnifu yetu.

Kuhusiana na uhakiki wa kazi za tafsiri za kifasihi; kazi ya Malangwa (2005) ina mahusiko ya moja kwa moja na malengo ya utafiti wetu. Utafiti wake ulihusu namna ya kutafsiri matini za kiufundi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili kwa kutumia mifano ya programu za kompyuta. Katika utafiti huo aligundua kuwa moja ya changamoto zinazowakabili watafsiri wa matini za kiufundi kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili ni Pamoja na tofauti za lugha, utamaduni na ukosefu wa visawe linganifu. Matini za kiufundi huwa na istilahi maalumu ambazo huwa vigumu kuhawilishwa kwa lugha tofauti kwa sababu ya upekee wa lugha katika kila jamii. Miongoni mwa mikakati anayopendelea zaidi ni ugenishaji yaani kuswahilisha maneno kutoka utamaduni wa kigeni kwenda kwa lugha ya Kiswahili. Suala la mikakati ni miongoni mwa malengo yetu katika utafiti huu. Basi kazi hii itaijenga kazi yetu kwa njia ya kipekee.

Nafasi ya utamaduni katika tafsiri ni kipengele muhimu kwa kufanikisha shughuli nzima ya uhawilishaji wa ujumbe kutoka matini chanzi hadi matini lengwa. Uwepo wa lugha nyingi zinazowakilisha tamaduni tofauti na umuhimu wa mawasiliano hufanya tafsiri kuwa shughuli muhimu. Mawasiliano kwa njia hii hufanikisha ubadilishanaji wa utamaduni na ni muhimu kuzingatiwa katika mchakato wa tafsiri. Tafsiri imefanikisha mwingiliano baina ya mienendo, mila na desturi, maadili na itikadi za kidini kati ya jamii tofauti tofauti. Kuna muumano dhabiti kati ya lugha na utamaduni wa watu wanaotumia lugha hiyo. Osore (2011) alichunguza jinsi utamaduni wa Kiingereza ulivyokutanishwa na utamaduni wa Waswahili kupitia mchakato wa tafsiri. Alichanganua habari na tafsiri zinazofanyika katika bunge la

Afrika. Uchanganuzi wake ulibaini mbinu zinazotumika kutafsiri msamiati wa serikali na bunge. Aidha, aliangazia jinsi tafsiri hizi ni njia mwafaka ya kuhifadhi utamaduni asilia. Utafiti wake umesisitiza umuhimu wa kuhifadhi utamaduni kupitia tafsiri. Ili kufanikisha mchakato wowote wa tafsiri ni muhimu mtafsiri aelewe tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Aina hizi za tafsiri ni muhimu kwa sababu zinasabihiana na mawazo ya Guo (2012) ambaye anapendekeza mbinu za usawe wa kisemantiki na usawe wa kipragmatiki kuwa mwafaka kwa kutafsiri matini zilizo na masuala ya kitamaduni. Usawe wa kisemantiki ukiwa na maana husishi ya neno ilhali usawe wa kipragmatiki ukizalisha maana kutokana na muktadha. Muktadha huu ukihusu tajriba ya mzungumzaji na msikilizaji. Mkakati wa ugenishaji pia ni muhimu kwa mtafsiri kuamua kuvunja kaida za lugha na kuhifadhi ugeni katika makala tafsiri. Ili kufanikisha mchakato wa tafsiri ni sharti mbinu hizi zishirikishwe kwa matokeo bora. Kuna mengi yanayoweza kutoka kwa kazi ya Osore ili kufanikisha mahitimisho ya kazi yetu.

Ili kufaulisha zoezi la tafsiri, ni muhimu mtafsiri kuelewa hatua mbalimbali zitakazoshirikishwa katika mchakato wa tafsiri. Utaratibu huu huzingatiwa kwa sababu kila matini hufumwa kwa njia tofauti huku ikijikita katika mazingira na miktadha maalum. Jilala (2014) anadai kuwa, hatua za tafsiri mbalimbali hutegemea aina ya matini, na utamaduni wa lugha anazozishughulikia mfasiri wa matini. Anajadili kuwa, mfasiri matini za kitamaduni hufuata hatua mahusussi za tafsiri. Katika kielelezo chake cha mawasiliano ya Kitamaduni (MMK) Jalala anapendekeza hatua tano ambazo zinafaa kutumika katika mchakato wa tafsiri ili kufikia ufanisi wa mawasiliano katika matini za kitamaduni nazo ni: maandalizi, utafutaji wa visawe vya kitamaduni, mchakato wa tafsiri, uhusiano na uzalishaji wa matini lengwa. Hatua hizi ni muhimu kwa mfasiri ili kufanikisha zoezi la tafsiri. Mfasiri anapopata kazi ya

kutafsiri anapaswa kujianda kisaikolojia na kujua wajibu wake katika matini anazotafsiri. Aidha, lazima afahamu aina ya matini anayoikabili na pia ajue ni lugha zipi anazozifanyia kazi. Muhimu zaidi mfasiri sharti ajue na atambue mazingira yanayomzunguka katika mchakato wa tafsiri.

Mchakato wowote wa kutafsiri tamathali za semi hauna budi kubaini kwa uwazi tamathali zinazotafsiriwa zimetumika katika miktadha gani na zinatekeleza wajibu gani katika jamii hiyo. Tamathali hizo zinaweza kujitokeza kama viwakilishi vya utamaduni katika miktadha ya kawaidha au katika mazungumzo ya kawaida ya wanajamii. Katika hali kama hii haiwakilishi tamathali za semi tu bali huwakilisha vikoa vya utamaduni katika jamii hiyo. Kwa hivyo, zinashurutisha mtafsiri kutafsiriwa katika utamaduni uliokitwa katika tamathali hizo. Kuna maafikiano ya kijumla kwamba kila tamathali katika upekee wake wa kimatumizi, huwasilisha maana mahususi katika miktadha mahususi. Ni muhimu mtafsiri atafsiri dhana hizi kwa uangalifu ili asitafsiri tu maana bali pia ahawilishe hali na fahiwa za kitamaduni kama zinavyojidhihirisha katika matini chanzi. Nzyoka (2014) amechunguza mikakati ya kutafsiri tamathali za semi katika tamthilia. Alichanganua tamthilia iliyotafsiriwa na Wafula *Antigoni* (2009) na tamthilia ya Kiingereza iliyotafsiriwa na Townsend: *Antigone* (1962). Kazi yake ilichunguza mikakati iliyotumiwa kutafsiri jazanda, tashbihi na misemo katika matini tafsiri. Mikakati saba iliafikiwa kutokana na kazi yake: tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, kutafsiri kwa kuondoa msemo, kutafsiri kwa kufasiri, kutafsiri kwa kudumisha visawe na kuongeza ufafanuzi kwa kutumia vipengele vinavyofanana na kubadilisha tashbihi kama nia ya kinahau na kuwa dhana. Mikakati hii yote inachangiana na kukamilishana wakati wa tafsiri. Suala la mikakati ni dhana msingi katika malengo ya utafiti wetu. Kazi hii itatoa mchango wa kipekee kwa tasnifu yetu.

Wakati wa kutafsiri pana haja kwa mtafsiri kufahamu matatizo yanayojitokeza wakati wa kutafsiri fasihi kwa ujumla. Mtafsiri aelewe mandhari ya kiwakati, kijiografia, kijamii, kisaikolojia na kimuktadha ili afanikishe mchakato wa tafsiri. Utafiti wa Nyangeri (2014) umeonyesha ulinganifu maana katika tafsiri ya vitendo na semi katika kazi ya kifasihi. Katika utafiti wake amerejelea vitabu viwili *Musa na Shamba la shule Pamoja na Musa na Wateka Nyara.* Nyangeri aligundua kuwa vitendo vya usemi ambavyo hufungamana na utamaduni wa Kiingereza ndivyo huibua changamoto katika tafsiri. Vitendo na usemi vya utamaduni wa Kiingereza visivyojitokeza kwenye utamaduni wa Kiswahili vinaweza kufafanuliwa lakini haviwezi kuibuliwa kwenye utamaduni huo. Iwapo vitaibuliwa basi ujumbe utatatiza kwa hadhira lengwa. Katika fasihi tafsiri tatizo la ulinganifu maana lipo na haliwezi kupuuzwa ila tu ni mtafsiri azuke na mbinu au mikakati ya kukabiliana na tatizo hili. Kutokana na utafiti huu kuna mengi yanayoweza kuhawilishwa ili kuongoza mijadala katika kazi yetu.

Miktadha na mazingira yanayojidhihirisha katika matini za fasihi huzua tofauti na matatizo katika tafsiri. Tofauti hizi huzuka kutokana na uhalisia wa maisha na upekee wa utamaduni katika jamii mbalimbali. Hemed (2018) ametafiti juu ya changamoto za kutafsiri riwaya kutoka Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia mfano wa riwaya ya Robinson Crusoe. Utafiti wake ulibaini kuwa changamoto za kutafsiri riwaya ni pamoja na changamoto za kiisimu, utamaduni na uteuzi mbaya wa visawe. Tofauti za kitamaduni na mambo kama dini, mavazi, mila na desturi za jamii mbali mbali huwa na ujumbe mahsusi na hivyo yanapotafsiriwa kwa Kiswahili hupoteza ile maana halisi na kupotosha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira lengwa na kwa hivyo hutatiza mawasiliano. Ili kufanikisha shughuli nzima ya tafsiri, mtafsiri ni sharti awe mweledi kwa mada anayotafsiri, awe na ujuzi wa lugha anazozitafsiri, ajue

utamaduni, historia na mitazamo ya jamii anazotafsiri kazi zao. Kwa kushirikisha kielelezo cha mawasiliano ya kitamaduni kilichopendekezwa na Jalala (2014) basi atakuwa amefanisha mchakato wa tafsiri.

Kulingana na lengo la tafsiri matumizi ya mikakati mbalimbali ni sehemu muhimu katika zoezi zima la tafsiri. Dhamira ya mtafsiri ndio itakayompa mikakati ambayo atatumia kuhawilisha ujumbe kutoka hadhira asilia hadi hadhira lengwa. Kamundi (2019) ametafiti juu ya mikakati ya kuafikia ulinganifu wa maana katika tafsiri ya kifasihi. Alitathmini tafsiri za kazi mbili za Barbara Kimenye (1968) *Moses in Trouble, Moses and the Ghost.* Katika kazi yake alijibu maswali kuhusu mikakati iliyotumiwa kutafsiri tamathali mbalimbali ili kuafikia ulinganifu katika tafsiri za Matundura (2013) *Musa Mshakani na Musa na Pepo.* Kazi hii imetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi kwa lugha ya Kiswahili ambapo alibaini kuwa mikakati hutumiwa kimwingiliano ili kuweza kuhamisha ujumbe usio na dosari. Aidha, alibaini kuwa mikakati inayotumiwa kutafsiri nomino za pekee kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili hutegemea mchango wa nomino husika katika matini. Majina ya kwanza ya watu yanaweza kuhamishwa moja kwa moja na kwa hivyo huweza kuhifadhi uraia na utamaduni wa jamii husika. Hili hufanyika pale ambapo inakisiwa kuwa majina yale hayadokezi maana yoyote katika matini. Vilevile ni muhimu kuhifadhiwa kwa jina lile kwa kulitumia kama lilivyo ili kutoa mwongozo au kulitumia jina lile na kisha kutoa ufafanuzi baadaye kwa utondoti. Muhimu zaidi ni kuwa, taratibu za kutafsiri ambazo zinazingatia maana za kimuktadha zinahawilisha ujumbe ulivyokusudiwa ipasavyo. Maoni ya Kamundi ni muhimu kwa utafiti wetu kwa kuwa yanatupa mwongozo wa kuendeleza mjadala wetu.

Kuna mengi yamezungumziwa na watafiti wengi hasa wakiangazia tafsiri kutoka lugha ya Kiingereza hadi kwa lugha ya Kiswahili kutoka changamoto, ubora na

udhaifu wa kazi tafsiri, tararibu Pamoja na mikakati ya kufanikisha shughuli nzima ya tafsiri. Yaliyoorodheshwa katika utafiti wetu yataendeleza mjadala na kusaidia kuafikia malengo yetu.

2.5.2 Tafsiri za fasihi ya Kiafrika hadi lugha ya Kiingereza

Ni dhahiri kwamba fasihi tafsiriwa haiwezi kuchukua nafasi sawia na kuwa na uamili sawia na ule wa matini tafsiriwa inapopokelewa katika miktadha lengwa. Tofauti hizi husababishwa na tofauti za kimazingira maana kila eneo huwa na upekee wake. Changamoto kubwa iliyotokana na fasihi za kigeni zilizotafsiriwa kwa Kiswahili ni kuwa fasihi hii ilikuwa na nafasi finyu katika muktadha wa utamaduni wa wenyeji wa Afrika. Hii inatokana na sababu kwamba kazi za kigeni zilizotafsiriwa zilikuwa zimezingatia mazingira na utamaduni wa kigeni na maudhui yaliyohawilishwa hufasiriwa kwa misingi hiyo. Fasihi kwa ujumla hutokana na mazingira ya wenyeji ili kufumbata hali halisi ya utamaduni wao. Aidha, baada ya fasihi za kigeni kuingia katika mazingira ya Afrika, wenyeji walijengewa imani kwamba fasihi iliyobuniwa na kuwasilishwa kwa mazingira yao ni ya kiwango cha chini au ubora wao ni wa kutiliwa shaka. Kizazi baada ya kizazi wakaupendelea utamaduni wa kigeni huku wakidhalilisha utamaduni wao wa Kiafrika. Watetezi wa lugha za kiafrika wakawa na mwamuko kwamba ni sharti wabuni kazi za fasihi katika lugha zao na waanze kutafsiri kwa lugha ya Kiingereza ili kuhifadhi utamaduni wao uliotishia kuangamizwa na kizazi kichanga. Wasanii wa fasihi walianza kuaandika kwa lugha ya Kiswahili, Kiacholi, Kikerebe na Gikuyu ili kukabiliana na haja na matakwa ya wanajamii. Wataalamu na watafiti wa fasihi iliyotafsiriwa kutoka lugha za Kiafrika hadi kwa lugha ya Kiingereza si wengi kwa sababu kazi zenyewe ni chache.

Katika kazi yoyote ya fasihi kwa sababu ya kushirikisha wahusika na mandhari yanayotofautiana, kuna uwezekano wa kutumia mbinu mbalimbali za lugha. Uhalisia

huu lazima uzingatiwe wakati wa kutafsiri kwa sababu mbinu za lugha hushawishi na kuathiri mawasiliano katika fasihi. Murithi (2018) amefanya utafiti juu ya tamthilia *Kifo Kismani* ya Kithaka wa Mberia iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili na kutafsiriwa katika lugha ya Kiingereza – *Death at the well.* Katika utafiti wake alichunguza maudhui, mbinu za lugha na wahusika jinsi yamewasilishwa kwa matini chanzi hadi kwa matini lengwa. Uhawilishaji wa maudhui katika fasihi tafsiri hautatizi kama uhawilishaji wa mbinu za kisanaa katika kazi ya kifasihi. Kazi ya Sanaa mara nyingi hufungamanishwa na masuala ya kitamaduni na kwa hivyo huwa ni vigumu kuhawilisha ujumbe huo moja kwa moja kwa hadhira lengwa. Guerra (2012) alihoji kwamba wakati wowote ambapo tamaduni mbili zinapokaribiana, inakuwa vigumu kwa mtafsiri kufanikisha uhamisho wa maana ili kufaulu katika jukumu lake la kuwasiliana na hadhira pokezi. Basi kwa misingi hiyo amezuka na mikakati mbalimbali itakayotusaidia kutoa mwanga kwa utafiti wetu.

Matini za kishairi ni miongoni mwa matini ambazo zimesemekana kuwa tata kufasiriwa kwa ufasaha. Adongo (2019) alichunguza changamoto za kutafsiri ushairi kwa kutumia *Wimbo wa Lawino* wa Paul Sozigwa (1975) na kubaini changamoto zinazomtatiza mtafsiri ni pamoja na zile zinazofungamana na masuala ya kiisimu na ya kitamaduni. Sozigwa alitafsiri ushairi kutoka lugha ya Ki-Acholi hadi lugha ya Kiingereza- *Song of Lawino* cha Okoth P' Bitek ambapo masuala mengi ya kitamaduni yalimtatiza kuyatafsiri kwa hadhira lengwa. Aidha, amewasilisha na kujadili jinsi changamoto za kiisimu zinavyoathiri matumizi ya lugha katika kutafsiri ushairi. Adongo amefafanua jinsi matumizi ya lugha yaliathiri ujumi katika ushairi wa Lawino. Kufanikisha mawasiliano ya kifasihi kwa shughuli ya tafsiri mtafsiri sharti aelewe masuala ya utamaduni, changamoto za kiisimu kwa lugha chanzi na lugha lengwa Pamoja na masuala ya kiujumi. Kazi hii inaonyesha uhalisi wa kutafsiri,

utaratibu na hatua za kuzingatiwa ili kufanikisha mchakato wa tafsiri. Madhali ushairi na riwaya ni tanzu za fasihi kuna mengi yanaweza kuhawilishwa kutoka kwa kazi hii ili kujenga tasnifu yetu. Maswala mengi yamejadiliwa yana mshabaha mkubwa na kazi yetu.

Kuingiza matini chanzi katika fasihi lengwa kupitia mchakato wa tafsiri hushurutisha kuwepo kwa mabadiliko, yaani hulazimisha matini chanzi kufanyiwa mabadiliko anuai ili kuiwezesha matini hiyo kutambulika na kukubalika katika miktadha ya hadhira lengwa. Uhalisia huu unatuwezesha kuhoji kwamba kuna matatizo mbalimbali yanayotokana au yanayoandamana na zoezi la tafsiri. Newmark (1982) amefanya mijadala mirefu ambapo amewasilisha aina mbalimbali za matatizo ya kutafsiri, nadharia za kuelezea matatizo hayo Pamoja na kanuni za kufanikisha shughuli ya kutafsiri. Mtaalamu huyu amewasilisha kanuni na mapendekezo jinsi ya kutafsiri lugha ya kitamathali, kutafsiri kisemantiki, kutafsiri kimawasilano na vilevile jinsi ya kutafsiri mambo kama sitiari, jazanda na tashbiha. Maoni ya Newmark ni kazi za kiutekelezi, ambazo hata kama zinatambua umuhimu wa nadharia, zinaweka kipaumbele katika sehemu ya utekelezi. Anasisitiza kwamba mtafsiri huzingatia maana na ujumbe uliokusudiwa na matini chanzi. Lengo la tafsiri huru huwa ni kusababisha athari sawa na ile ya matini lengwa. Hatua za tafsiri zilizopendekezwa haziwezi kutumika kutafsiri matini za kitamaduni, matini za kitamaduni zinahitaji hatua mahsusi ili kuhawilisha maana na ujumbe linganifu kwa hadhira lengwa. Kila jamii huwa na namna ambayo huitazama jamii yake. Katika juhudi za kuunganisha thamani ya lugha na utamaduni, mtafsiri wakati wote hujaribu kusawazisha tamaduni tofauti ili kufikia kiwango kinachoeleweka kwa msomaji wa tafsiri (Lefever 1999).

Fasihi tafsiriwa hufafanuliwa na kutafsiriwa katika utamaduni mahsusi. Katika hali zote za ubainikaji wake kuanzia utekelezaji wake na usomaji wake fasihi tafsiriwa

hujibainisha katika miktadha yake ya kitamaduni. Kazi yoyote iliyotafsiriwa huchukua nafasi dhahiri katika utamaduni lengwa, usomaji na ufasiri wake unashawishiwa na mitazamo ya fasihi lengwa katika matini zilizotafsiriwa. Munday (2001) anasema mitazamo ya nadharia za awali za tafsiri ziliegemea isimu lakini kuanzia miaka ya 1970 wataalamu walianza kuzungumzia nafasi ya utamaduni katika tafsiri ambapo masuala ya kijamii, kitamaduni na kihistoria yanachukuliwa kuwa muhimu katika tafsiri. Hii ni kwa sababu tafsiri ni mchakato unaofanywa kati ya lugha na kati ya tamaduni. Tofauti kati ya lugha na tamaduni huathiri mchakato wa tafsiri. Kuna uhusiano wa karibu kati ya lugha na utamaduni wa watu wanaotumia lugha hiyo kama lugha ya kwanza. Uhusianao huu hubainika wazi kupitia viambajengo, dhana na maneno ya kitamaduni. Hali kama hii hutatiza watafsiri na hasa wakalimani wanapojaribu kutafsiri kwa kuzingatia uamilifu wa makala asilia. Kutokana na hali hii tafsiri sio tu mchakato unaoziba pengo linaloletwa na tofauti za lugha bali kwa kiwango kikubwa huwa kama daraja kati ya tamaduni tofauti (Namy 1978). Kulingana na maoni ya Namy ni kuwa mawasiliano ni mchakato wa tafsiri unahusisha tamaduni. Mitazamo hii ni muhimu kwa kazi yetu kwani kuna uhusiano wa moja kwa moja na malengo yetu.

Zipo hali mbalimbali katika historia za fasihi ikiwemo fasihi ya Kiswahili ambapo fasihi lengwa ililazimishwa kupokea tafsiri za kifasihi hasa katika hali za ukoloni ambapo fasihi kama ya Kiswahili ilichukua tafsiri za fasihi ya Kiingereza. Guo (2012) anaeleza kuwa tofauti za kitamaduni na kihistoria ni mojawapo ya matatizo yanayomkumba mtafsiri. Utamaduni wa kihistoria unahusu mila, desturi, mielekeo, amali na itikadi ya jamii fulani na ambayo jamii hiyo huja kupata katika harakati ya maendeleo ya kihistoria. Maendeleo na mabadiliko ya kihistoria ni mengi na basi utamaduni wa kihistoria ni wa aina mbalimbali. Utamaduni wa kiasili unatokana na

eneo la kijiografia, mazingira ya kiasili na mila za kijamii; mambo haya huchangia kuunda utamaduni wa kiasili na jamii fulani. Guo anasema kuwa tofauti za miktadha ya kitamaduni ya kihistoria husababisha matatizo ya mawasiliano kati ya mataifa na jamii mbalimbali. Maoni yake ni kwamba visawe vya kipragmatiki vinafaa zaidi kwa hali kama hii humwelekeza mtafsiri kutozingatia lugha na kufanya uteuzi utakaofanikisha mawasiliano kwa hadhira lengwa. Guo anataja kuwa kutokana na tofauti hizi maneno ya lugha fulani yanaweza kuwa na maana tofauti katika utamaduni tofauti. Kwa hivyo, mtafsiri anafaa kuelewa mikakati mwafaka ya kutafsiri dhana kama hizi bila kutatiza maana iliyokusudiwa.

2.5.3 Tafsiri za fasihi zilizotumia nadharia ya Skopos na Anthropolojia

Nadharia ya *Skopos* na mbinu ya mawasiliano inapotumika ni vigumu kupata matokeo halisi katika mchakato wa tafsiri. Kiuhalisia kinachosisitizwa ni kwamba si rahisi kutafsiri matini za kitamaduni. Tofauti hizo zinajidhihirisha katika mazingira ya kiekolojia, historia, isimu na utamaduni wa jamii moja hadi nyingine. Mwansoko na wenzake (2005), wanadokeza kuwa tofauti za kijiografia, kihistoria, kifalsafa, kifasihi, kiisimu na kiutamaduni baina ya lugha ambazo mtafsiri anazifanyia kazi zinaweza kusababisha akose kisawe cha lugha chanzi kwa lugha lengwa. Ni dhahiri kwamba tofauti za kitamaduni huwa tatizo kubwa kwa mtafsiri hata kuliko tofauti za kiisimu.

Malangwa (2014) katika makala yake ya changamoto na mbinu za kutathmini tafsiri alibainisha mambo ya kiutamaduni yanaweza kuleta changamoto za tafsiri ikiwa ni maneno yanayohusu vyakula, vinywaji, mahusiano ya koo, shughuli za kitamaduni na mifumo ya kisiasa. Mtaalamu huyu alibaini kuwa maneno yaliyokuwa kwenye matini chanzi ya Kiswahili yametafsiriwa kwa kuhamishwa kama yalivyokuwa katika matini lengwa ya Kiingereza. Kilichomfanya mtafsiri kutumia mkakati huu wa kuhawilisha

dhana za kitamaduni jinsi zilivyo ni kutokana na kukosa visawe mwafaka kwa dhana hizo katika hadhira lengwa. Nadharia ya Skopos inasisitiza ni muhimu mtafsiri aelewe lengo la kutafsiri matini fulani. Baada ya kubainisha lengo inakuwa rahisi kuzuka na mbinu mwafaka za kutafsiri dhana zinazoshirikisha vipengele vya kitamaduni. Ni vigumu kupata tafsiri ambayo haina kabisa vionjo vyovyote vya LC kwenye ML endapo matini husika imejifunga katika miktadha ya kitamaduni.

Kuwepo kwa maneno na dhana za kitamaduni katika fasihi husababisha matatizo ya tafsiri hasa pale mtafsiri anapokuwa hana ufahamu na maarifa ya utamaduni chanzi. Maneno ya kuelezea dhana tofauti tofauti katika jamii hupewa dhima kulingana na utamaduni, muktadha na uzoefu wa jamii husika. Msingi wa nadharia ya Skopos ni kuiona tafsiri kama utekelezaji wa vitendo kwa kuzingatia matini asilia. Nadharia hii ilisababisha na kuleta mabadiliko yaliyokuwepo kwa muda mrefu katika taaluma ya tafsiri kwa kuiona tafsiri kama tendo la kiisimu na kuanza kuiona kama dhana na dhima ya utamaduni wa jamii. Muktadha unaozunguka mchakato wa tafsiri ni kipengele muhimu ili kufanikisha tafsiri. Kwa misingi hii, kila tendo lina matokeo lengo la matini lengwa ndilo linamwezesha mtafsiri kuchagua mikakati na mbinu ya kufanikisha mchakato mzima wa tafsiri. Jilala (2017) katika makala yake ya changamoto za kutafsiri matini za kitalii amebaini kuwa kuna changamoto za kutafsiri matini za kiutamaduni katika jamii ya ulumbi kwa kutumia mifano ya majina katika matini za kitalii nchini Tanzania. Aligundia kuwa kuna changamoto za kutafsiri matini kama vile: changamoto za kisemantiki, ukosefu wa visawe vya Kiswahili, tofauti za dhima ya maneno kutoka jamii moja hadi nyingine. Aidha, alihoji kuwa wakati wa kutafsiri matini za kitamaduni katika jamii ya ulumbi, lugha kuu hubeba mzigo katika kufumbata tamaduni zote.

Aidha, Malangwa na wenzake (2022) wameshughulikia changamoto za mbinu za kutathmini tafsiri na kugundua kuwa kuna mbinu nne za kutathmini tafsiri: tafsiri rejeshi, kupima uelewaji, kupima uasili na kupima ulinganifu. Kwa mbinu zote zilizotumika ilibainika kwamba lengo lilikuwa ni kusaidia hadhira lengwa kupata ujumbe lakini si uzingativu wa uasili wa tafsiri. Wataalamu hawa waligundua kuwa sio faafu zaidi kuitumia tathmini tafsiri za kiutamaduni kutokana na tofauti kubwa za kitamaduni zilizopo baina ya lugha moja na nyingine. Kiuhalisia si rahisi kupata tafsiri ambayo haina vipengele vyovyote vya kitamaduni vya MC kwenye ML. Wanasisitiza kuwa unaweza kuepuka vionjo vya kitahajia na miundo mbalimbali ya sentensi lakini huwezi kuepuka vionjo mbalimbali vya istilahi na msamiati kama tafsiri imehusisha lugha mbili tofauti. Wanapendekeza matumizi ya mbinu za kutathmini tafsiri yaamriwe na mbinu na nadharia iliyotumika wakati wa kutafsiri MC kwenda kwa HL. Nadharia inayosisitiza lengo la tafsiri yaani ya *Skopos* ni mwafaka zaidi kwa tafsiri iliyo na vionjo vya kitamaduni.

Duniani kote binadamu wameweza kuwasiliana na kutangamana kupitia mchakato wa tafsiri. Mchakato huu umetumika kama nyenzo na daraja muhimu la kuwaunganisha watu wa jamii, lugha na utamaduni tofauti kuwasiliana na kuelewana katika maarifa, mila, desturi zilizofungamana na utamaduni huo. Jilala (2023) ameshughulikia mchango wa tafsiri za J.K Nyerere katika maendeleo ya Kiswahili. Alitathmini mchango wa tafsiri za J.K Nyerere katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ili kuona ni kwa kiasi gani kazi za tafsiri zimeweza kukuza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili. Alitumia data kutoka vitabu viwili vya tafsiri ambavyo ni: *Julius Kaizari na Mabepari wa Venisi*. Ametumia nadharia ya *Skopos* ambapo ansema nadharia hii imejikita katika uhawilishaji tafsiri kutoka kwenye ulinganifu wa kiisimu kwenda kwenye ubora wa kiuamilifu au kidhima. Nadharia ya *Skopos* inasisitiza kuwa tafsiri

inachukuliwa kuwa ni mchakato wa mawasiliano ya mwingiliano wa tamaduni ambao matokeo au zao lake ni matini yenye uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi katika mazingira na muktadha mahsusi wa matumizi.

Mkataba wa huduma ni njia moja ya kujitolea kwa shirika ili kuhakikisha kwamba utoaji wao wa huduma unaridhisha kwa umma. Tafsiri za mkataba wa huduma kama lugha nyingi hupanua mawanda ya kufahamika kwa mkataba huo na huduma zinazotolewa na mashirika husika. Michira na wenzake (2020) wamechunguza tafsiri ya mkataba wa huduma na kubaini kuwa mtafsiri anafaa kujua lengo la kutafsiri mkataba wa huduma kabla ya zoezi la tafsiri kuanza. Hali hii imewekwa wazi na nadharia ya *Skopos*. Wataalamu hawa wanasisitiza malengo ya matini na kile kinachotarajiwa na wasomaji au wapokezi wa matini hiyo. Tofauti za kimtazamo baina ya mpokezi na mtoaji wa ujumbe zinaweza kuchangia katika fasili tofauti ya ujumbe ulio katika mkataba wa huduma. Ni muhimu mtafsiri kuzingatia miktadha na mazingira ya kimatumizi katika dhana na istilahi zinazotumika katika mkataba wa huduma. Bila kulizingatia hili na kujua lengo la tafsiri namna linavyowekwa wazi na nadharia ya *Skopos* utata utatokea katika mawasiliano baina ya mtoaji huduma na mpokezi.

Wanaanthropojia hujihusisha na utambulishaji na vipengele vya utamaduni katika mifumo ya kiuchumi, kisiasa, kidini na kadhalika. Huchunguza na kubaini mabadiliko yaliyoipitikia jamii husika. Uchunguzi wao hujikita katika miktadha inayoshirikisha taasisi mabailmbali za kijamii zinazomulika muundo wa ndani wa jamii. Kuchunguza kwa upekee masuala ya kijamii husaidia kuelewa kwamba tamaduni za ulimwenguni ni tofauti na changamano. Mumbua (2019) amechunguza kuwepo au kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika tawasifu ya Mbali na Nyumbani na kugundua uwepo wa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha

mbalimbali ya kimajukumu. Utafiti wake ulionyesha kuwepo kwao finyu katika mazingira na miktadha fulani na kutokuwepo kwao kabisa katika miktadha mingine. Utafiti ulidhihirisha kwamba wanawake wamewasilishwa kwa ufinyu katika miktadha ya kielimu, kidini, kiuchumi na kisiasa. Ucheleweshaji huu umesababishwa na kutoshirikishwa na kutohusishwa katika shughuli na harakati za kijamii. Utafiti wake ulionyesha kuwa katika mzingira na miktadha ya kijeshi wanawake hawapo. Sababu zinazochangia kuwepo na kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika Mbali na Nyumbani ni za Kianthropolojia na za Kihistoria yaani zimesababishwa na mazingira na miktadha maalum. Tofauti za kimazingira zimesababishwa na itikadi kwamba jamii za kiulimwengu zinaamini kwamba, maumbile ya mwanamke pamoja na majukumu yake ya uzazi hayamruhusu kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kijamii. Suala la mazingira na muktadha ni muhimu katika utafiti wetu. Mtafsiri anapotafsiri matini yoyote ni sharti aangalie miktadha maalum ambayo imejikita katika kazi yenyewe. Maoni haya yataendeleza mjadala wa tasnifu yetu kwa sababu yanasahibiana na malengo yetu.

2.6 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili: nadharia ya anthropolojia na nadharia ya Skopos. Nadharia ya anthropolojia ilijikita katika isimu anthropolojia inayochunguza jinsi lugha inavyotumika katika miktadha ya kitamaduni. Aidha, nadharia ya *Skopos* inasisistiza kuwa kila tafsiri lazima itangaze *Skopos* yake, yaani itangaze nia yake ya tafsiri. Misingi na mihimili ya nadharia hizi imeongoza mijadala katika kuhakiki, kufafanua na kutathmini masuala ya tafsiri kama mchakato wa kuhifadhi utamaduni.

2.6.1 Nadharia ya Anthropolojia

Neno anthropolojia lina asili ya Ugiriki. Ugiriki ‘anthropos’ humanisha binadamu na ‘logos’ huwakilisha sayansi ya binadamu (Barnard, 2000). Kulingana na Haviland,

Prins, Walrath and McBride (2011) nadharia ya antropolojia hushughulikia binadamu kwa wakati wote na mahali popote. Nadharia hii inatafiti tabia na mienendo ya watu kwa lengo la kupata ushahidi wa wazi kwa masuala ya kihistoria na kuonyesha ukweli na uhalisia wa mambo katika jamii. Mabadiliko makubwa kuhusu nadharia hii yalitokea kati ya karne ya 19 – 20 japo kule Ufaransa na Ujerumani. Nadharia hii ilishika kasi kati ya karne ya 17 -18 wakitumia majina tofauti. Kule Uingereza jina anthropolojia lilionekana kutumika katika mwaka wa 1805 (McGee na Warms, 2012).

Ahmed (1986) anasema wajibu wa taaluma ya anthropolojia ni kuchunguza tabia ya binadamu. Uchunguzi huu humwezesha binadamu kujielewa na kuelewa utamaduni wa watu wengine. Kwa misingi hii, nadharia ya anthropolojia ni uchunguzi unaomlenga binadamu katika jamii ili umwezeshe binadamu kujielewa kwa wakati wote na mahali popote. Langness (1974) anafafanua anthropolojia kama taaluma ya kisayansi inayolenga kumchunguza binadamu katika jamii na utamaduni wake. Huu ni uchunguzi wa tamaduni za binadamu unaoshirikisha mbinu kama utazamaji na ushiriki kwa kukusanya data na kuitolea maelezo.

Wataalamu mbalimbali wametoa maelezo ya kuchangia nadharia ya anthropolojia. Kulikuwa na shule mbalimbali zilizochangia maendeleo ya nadharia ya anthropolojia. Waasisi wa shule ya mageuzi walikuwa Herbert Spencer and Charles Dawin. Kwa ujumla uchunguzi wao ulisisitiza mchakato wa maendeleo ya taratibu. Huu ni utaratibu ambao unashirikisha vitu vidogo kukua hadi kuchukua umbo changamano. Herbert Spencer ambaye kazi yake ilikuwa na mvuto mkubwa kule Marekani katika taaluma ya Sosholojia alitumia mawazo haya ili kuelezea mageuzi yanayopatikana katika jamii. Jamii hupitia mageuzi mbalimbali kadri muda unavyosonga. Japo mawazo haya ya Spencer yalikuwa na mvuto mkubwa katika jamii ya Marekani baada ya kifo chake mawazo hayo yalikosolewa na wataalamu kama Rrazer na Tylor (Tylor

1903). Kulingana na Tylor jamii hupitia hatua tofauti tofauti: ushenzi, ukosaji wa utambulisho na ustaarabu (Scupin De Corse 2012). Tylor aliamini wasasi na wasaka matunda mwitu na jamii nyingi za Kiafrika zilikuwa katika kitengo cha chini kuliko jamii nyingi za kule Marekani zilizokuwa zimestaarabika.

Franz Boas ambaye anafahamika kama mwasisi wa nadharia ya anthropolojia aliamini katika mawazo ya upekee wa kihistoria. Yaani kila jamii na utamaduni wake unafaa kuchunguzwa kwa upekee wao. Boas alisisitiza umuhimu wa utafiti wa nyanjani na kwa utafiti wake alizuru jamii mbalimbali. Kulingana na wataalamu wa mageuzi walionyesha kwamba kuna tamaduni nyingine ambazo ni bora zaidi kuliko nyingine. Mawazo yao yaliegemea jamii za Marekani kuwa na utamaduni uliostaarabika kuliko utamaduni wa Kiafrika. Boas aligundua kwamba kila jamii ina upekee wao wa kitamaduni na hakuna utamaduni ulio bora kuliko mwingine (Stoking, 1965). Alisisitiza kuwa kila jamii huwa na upekee wao wa utamaduni na yeyote asidunishe utamaduni wa watu wengine. Kulingana na maoni ya Boas jamii haifai kuwekwa katika vitengo vya ushenzi na ustaarabu. Mtazamo huu hudunisha tamaduni za watu wengine. Mtaalamu huyu alisisitiza uchunguzi wa utamaduni kwa upekee wao (Langness, 1974).

Ember and Peregrine (2011) walisema, kulingana na Malinowski sifa za kitamaduni husaidia kutosheleza mahitaji ya wanajamii. Yaani hutosheleza mahitaji ya kimsingi au mahitaji mengine ya wanajamii. Alifanya uchunguzi wake na kugundua kwamba wanajamii wana imani kwa miujiza na iwapo wanataka suluhisho kwa mambo haya wasiyoweza kuzuia hutumia mbinu za kitamaduni ili kupata msaada wa kisaikolojia (Scupin and De Corse, 2012). Malinowski alihitimisha kwamba kila jamii huwa na mahitaji ya kimwili na kisaikolojia na mashirika ya kitamaduni, mila na itikadi za kijamii hutumiwa kutosheleza mahitaji yao (Scupin and De Corse, 2012).

Kwa ujumla wanaanthropolojia hawa walijitokeza na mitazamo mbalimbali ya kitamaduni iliyodai kwamba, tamaduni katika jamii hukua sambamba kupitia hatua fulani za kimsingi na maendeleo. Walidai pia kuwa utamaduni ulienea kwa njia ya msambao kutokana na maingiliano ya watu. Wataalamu hawa walipendekeza utathmini wa masuala ya kitamaduni kwa upekeee na kuzingatia kwamba tamaduni mbalimbali hutofautiana na kufanana. Kulingana na Cara (1976), nadharia ya anthropolojia ina matapo manne; anthropolojia ya kitamaduni, akiolojia, isimu anthropolojia na anthropolojia ya mazingira. Utafiti huu uliongozwa na tapo la isimu anthropolojia ambalo linajihusisha na matumizi ya lugha katika jamii. Tapo hili la anthropolojia lina mitazamo ifuatayo:

2.6.1.1 Mtazamo wa kijamii au kiutamaduni

Utamaduni kwa mujibu wa Newmark (1988:94) ni mkusanyiko wa mila na desturi zote za jamii inayotumia lugha moja mahsusi kama njia moja ya mawasiliano. Uwepo wa jamii nyingi huwakilisha tamaduni tofauti tofauti. Taaluma ya tafsiri hufanikisha ubadilishanaji wa utamaduni na maarifa. Mtazamo huu unatambua kwamba kuna tamaduni nyingi ulimwenguni na tamaduni hizo ni changamano. Jamii nyingi ulimwenguni hufanana na kutofautiana kutokana na tamaduni mbalimbali ulimwenguni. Ponera (2014) anadai kuwa utamaduni ni jumla ya matendo, fikra, mifumo ya maisha na kiashiria kingine chochote ambacho kinaweza kutumiwa kumwongoza na kumtambulisha mtu mmoja kwa jamii nyingine.

Utamaduni ni suala msingi katika isimu anthropolojia kwa kuwa unahusisha yale yote yanayopokezwa katika jamii fulani. Utamaduni huwa ni mila, asili, jadi na desturi za kundi fulani la jamii. Kila jamii ulimwenguni huwa na mambo fulani ya kitamaduni ambayo jamii hiyo inaweza kujitambulisha nayo. Kwa hivyo, utamaduni wa

kianthropolojia katika utafiti huu utazingatia jamii ya Wakerebe kutoka Tanzania na jamii ya Wakikuyu kutoka Kenya.

Namy (1978) anasema ufasiri sio tu ni kubadilisha maneno kutoka lugha moja hadi nyingine bali ni kuweka daraja la kisemantiki kati ya tamaduni mbili na miono - ulimwengu tofauti. Msamiati wa lugha yoyote ile duniani, maana za maneno hujengeka kutokana na utamaduni wa jamii husika. Mzawa wa lugha yeyote ile huwa na uwezo mkubwa wa kutumia msamiati mpana katika lugha yake. Iribemwangi na Mukhwana (2011:154) wanadai kuwa msamiati ni hazina ya maneno ambayo mzungumzaji wa lugha humiliki. Yaani, msamiati hutokana na mazingira ya jamii ile na utamaduni ukiwa ndani mwake. Maana ya maneno ni kiungo muhimu katika lugha kwani ndicho kitovu cha tafsiri. Katika utafiti huu, madai ya nadharia hii yatasaidia kuonyesha ni kwa namna gani utamaduni utakuwa umehifadhiwa kwa lugha tatu kupitia mchakato wa tafsiri: Kikerewe, Kiswahili na Kiingereza. Hifadhi yake itawekwa kwa lugha mbalimbali itakayokuwa inasambazwa kutoka lugha moja hadi nyingine kupitia kwa taaluma ya tafsiri.

2.6.1.2 Mtazamo wa upekee wa kihistoria

Chanzo cha fasihi ni katika maisha ya binadamu. Madumulla (1988) anaeleza kuwa katika kipindi cha maisha kuna matukio fulani ambayo hujitokeza zaidi kuliko mengine. Baadhi ya matukio haya yanaweza kuathiri jamii kwa njia mbalimbali kulingana na kipindi maalum cha kihistoria. Matukio haya huwa na athari kwa jamii husika na huwa katika kumbukumbu za jamii hiyo miaka mingi baadaye. Mtazamo wa upekee wa kihistoria una madai yake katika kuchunguza ukweli wa mambo ya kihistoria na kusisitiza matokeo yake kuliko uchunguzi wa kisayansi. Historia inaeleza matukio ya wakati uliopita.

Mlacha (1984) anahoji kuwa historia ya kipindi fulani cha utunzi ina umuhimu katika utunzi wa kazi ya fasihi. Fasihi huzaliwa katika jamii kwa wakati na kipindi fulani cha kihistoria. Masuala ya kihistoria huathiri mtunzi kimaudhui, kifani na kidhamira. Ukweli hujibainisha jambo linapochunguzwa kihistoria. Upekee huu wa kihistoria haupatikani katika ombwe tupu bali katika jamii inayobeba maisha na mienendo ya watu. Mhimili huu ulituwezesha kuchunguza muktadha uliochangia kutungwa kwa riwaya ya Kareithi na riwaya ya Kitereza na namna riwaya hizo zilivyopokelewa katika jamii yao. Mtazamo huu ulitusaidia pia kuchunguza matukio riwayani kihistoria na kutathmini maisha ya wanajamii ili kujiepusha na hisia na chukizi fulani kutoka kwa hadhira. Fasihi huathiriwa na masuala ya kihistoria basi msomaji wa kazi ya fasihi anahitaji kuelewa wakati wa kihistoria ambapo kazi hiyo ilitungwa ili kuitathmini na kielewa kazi hiyo ipasavyo.

2.6.1.3 Mtazamo wa Kimuundo

Kazi ya fasihi inapaswa kuchukuliwa kama muundo, yaani, iliyo na mpangilio maalum. Viungo vyake vinategemeana hivi kwamba kazi kamilifu huwa ni mwafaka zaidi kuliko kiungo kimoja. Kazi ya fasihi huwa ni muundo wa vipande vinavyopatana kuhusiana ili kujenga kazi kamilifu; kisa kimoja hutokea ili kusababisha kingine. Haya yote yanawezekana kupitia kwa lugha inayotumika. Buliba (2001) anasema kuwa, lugha husaidia kudhibiti uhusiano wa kijamii. Lugha ndio huwaleta watu hao pamoja kwa kujenga uhusiano wa kibinafsi katika kiwango cha mtu kwa mtu, mtu na jamii yake, mtu na taifa lake na mtu na ulimwengu wake. Ufanisi wa mawasiliano baina ya binadamu hutegemea lugha inayotumika. Binadamu wanapowasiliana ndipo wanapojenga uhusiano wao.

Katika kila jamii lugha hutumika kama chombo cha kusuka utamaduni wao. Utamaduni ni suala msingi katika nadharia ya anthropolojia kwa sababu linahusisha

yale yote yanapokezwa katika jamii fulani. Kinachowezesha na kufanikisha upokezi huu ni matumizi ya lugha kwa upekee wake. Lugha hufungamanisha watu wanaohusika nayo. Mtazamo huu umechunguza jinsi lugha ilivyotumiwa katika riwaya ya Kareithi na Kitereza ili kuwasilisha kazi kisanaa. Lugha ni chombo cha wanajamii wanachokitumia kutathminia mifumo ya mawasiliano kati ya binadamu na huwawezesha kuelezea uhalisia wao wa jamii. Fasihi hukuzwa na kuimarishwa kupitia lugha. Utamaduni wa jamii husika uhifadhiwa kupitia lugha. Mtazamo huu ulikuwa mwafaka kwa kazi yetu kwa kuwa uliangazia jinsi jamii ya Wakerebe na Wakikuyu wanavyotumia lugha kuhifadhi utamaduni wao kupitia mchakato wa tafsiri.

2.6.1.4 Mtazamo wa Kiuchumi na Kisiasa

Mifumo ya kiuchumi na kisiasa ni uti wa mgongo wa kila jamii. Mifumo hii hubadilika kadri muda unavyosonga. Mabadiliko yanaposhuhudiwa mifumo ya kijamii pia hubadilika. Miller (1990) anahoji kwamba ni vigumu kutenga utamaduni na athari zinazotokana na misukumo kama vile ukoloni na ubeberu. Mabadiliko haya huangaliwa kihistoria, yaani, hali ilivyokuwa na hali ilivyo sasa. Mahusiano kati ya mtazamo wa kiuchumi na kisiasa ni masuala ya kimsingi katika utafiti huu. Matukio ya jamii ya Wakikuyu na Wakerebe ni uhalisia wa maisha yalivyokuwa katika wakati huo, na utaratibu wa maisha yao unaweza kubadilika kulingana na mpito wa wakati. Foucault (1980) anasema kwamba fasihi haiwezi kutengwa na historia hurejelea uwezo wa kijamii na kisiasa. Mtazamo huu utaonyesha namna masuala ya siasa na kiuchumi huathiri maisha ya binadamu katika jamii. Huathiri jamii kwa njia chanya au hasi na mwandishi hupata fursa ya kuzungumzia uhalisia huu kupitia fasihi.

Nadharia ya isimu anthropolojia ni mwafaka kwa kazi yetu kwa kuwa lengo kuu la Kareithi na Kitereza ni kuhifadhi utamaduni wa Kiafrika kabla haujafutwa na wakati.

Matukio ya Wakikuyu na Wakerebe yanawasilishwa kwa uhalisia wao pasina athari zozote za utamaduni wa kigeni. Nadharia hii iliongoza mijadala kwa kujadili uhalisia wa maisha ya Wakikuyu na Wakerebe ili kuweka wazi tatizo linalotafitiwa.

2.6.2 Nadharia ya Skopos

Nadharia hii iliasisiwa na Hans J. Vermeer kule Ujerumani mnamo miaka ya 1970. Asili ya neno "*Skopos"* ni Kigriki lenye maana 'nia ya kutafsiri.' Linatumika kama istilahi ili kurejelea lengo la tafsiri. Msingi wa nadharia ya *Skopos* ni kuiona tafsiri kama utekelezaji wa kitendo mahususi kwa kuzingatia uamili wa tafsiri katika miktadha lengwa pasina kuipotosha matini asilia. Nadharia hii inasisitiza kuwa kila tafsiri hufanywa kwa lengo fulani na lazima lengo hilo litimizwe kwa kadri iwezekanavyo katika miktadha lengwa. Nadharia ya *Skopos* huchukulia shughuli ya kutafsiri kama kitendo kilicho na malengo. Kitendo hicho kinafaa kumlenga mpokeaji katika mazingira ya msomaji. Kwa mujibu wa nadharia hii, kutafsiri ni kuzalisha matini lengwa, kwa kuzingatia lengo, mpokezi na mazingira lengwa (Schaffner, 1978).

Vermeer (1989) anasema kwamba hakuna matini chanzi iliyo na tafsiri moja tu ambayo ni sahihi na inayokubalika. Hivyo basi, kila tafsiri ni lazima itangaze skopos yake, yaani ieleze nia yake. Lengo la tafsiri ndilo linachagua njia, mbinu na mikakati ya tafsiri ili kufanikisha shughuli nzima ya tafsiri. *Skopos* ya matini lengwa si lazima ifanane na skopos ya matini chanzi. Kwa hivyo, inabidi skopos ya matini lengwa ifafanuliwe ili mchakato wa tafsiri ufanikiwe inavyotarajiwa. Mtafsiri sharti kwanza aelewe nia ya tafsiri ni gani, kama ni ya kufahamisha ili aweze kujua jinsi ya kuendeleza shughuli ya tafsiri. Kuelewa nia ya tafsiri huwa kunamsaidia mtafsiri kubainisha rejista atakayotumia katika kufanya tafsiri ile, maneno atakayoteua, urefu wa sentensi atakazotumia na maelezo mengine kuhusu mchakato wa tafsiri.

Matini lengwa huwa haina ujumbe asilimia moja unaofanana na ule katika matini chanzi. Hii ni kwa sababu lugha hutofautiana katika maumbo mengi kama vile kuwepo kwa dhana mahsusi, istilahi za kipekee, miundo ya maneno na hata miundo ya sentensi. Uhalisia huu una maana kwamba wakati mwingine kupata istilahi mwafaka zinazowiana kimaana katika lugha chanzi na lugha lengwa huwa ni vigumu. Hata ujumbe huo utahawilishwa kutoka matini lengwa hadi matini chanzi huenda maana ikawa tofauti na kwa hivyo kutatiza mawasiliano.

Reiss (1990) anaishadidia nadharia hii kwa kusisitiza kuwa, mara tu mtu anapoibaini nia ya tafsiri, basi mikakati mingine kama vile urekebishaji na uundaji mpya wa matini itajitokeza yenyewe wakati wa shughuli ya kutafsiri. Matini tafsiri haibainishwi tu na matini chanzi bali pia hubainishwa na nia ya kutafsiri. Nadharia ya *Skopos* hujikita katika kutathmini matini kwa malengo maalum ambayo yanapelekea kukamilisha dhima sawa katika utamaduni chanzi na utamaduni lengwa. Tafsiri nzuri ni ile inayoiwezesha hadhira lengwa kupata tafsiri yenye ushikamani wa matini chanzi (Lauscher, 2002). Lengo la nadharia hii katika muktadha wa tafsiri ni kuielezea shughuli ya tafsiri katika mtazamo wa lugha lengwa. Nadharia hii imejikita katika malengo ya tafsiri ambayo huzingatia mbinu na mikakati ya tafsiri inayotumika katika kutoa matokeo stahiki ya kidhima (Nord, 2007). Matini za riwaya huandikwa ili kutimiza lengo fulani katika jamii. Vermeer (1984:101) kama anavyonukuliwa na Nord (1979:29) anasema kuwa, kila matini huzalishwa kwa lengo fulani maalum na ni lazima ikidhi lengo hilo. Kwa hivyo, lengo la tafsiri lazima lielezwe na liwekwe wazi kabla shughuli nzima ya tafsiri kuanza.

Kwa mujibu wa nadharia hii, wataalamu wanaitazama tafsiri sio tu kama mchakato wa uhawilishaji wa ujumbe bali kama muundo mahsusi wa tendo la kibinadamu, ambao ni sawa na matendo mengine ya kibinadamu (Jalala, 2014). Vipengele muhimu

vinavyohusu maisha ya binadamu katika jamii ni sharti vishirikishwe katika zoezi la tafsiri. Lerson (1984) anahoji kuwa tafsiri inahusisha uhawilishaji wa maana iliyoko katika maandishi ya lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa. Kwa misingi hii, muktadha ni jambo muhimu linalohitajika kuzingatiwa. Muktadha unaoizunguka tafsiri hauwezi kupuuzwa bali huchukuliwa kama kigezo muhimu cha kufanikisha tafsiri. Muktadha huhusisha mambo kama vile: utamaduni wa hadhira, hadhira, wateja na dhima ya matini iliyokusudiwa na hadhira na utamaduni lengwa (Vermeer, 1989). Nadharia ya *Skopos* ina kanuni sita kuu:

i) Matini lengwa huwa na lengo au madhumuni yake. Kwa mujibu wa nadharia hii, zoezi la tafsiri ni tendo linalotekelezwa kwa nia fulani. Lengo la tafsiri ndilo linalobaini njia, mbinu na kanuni za tafsiri ambazo hutumika kutoa tafsiri yenye usahihi wa kimatumizi kwa hadhira lengwa. Mtafsiri ni sharti aelewe nia ya tafsiri ni gani, kama ni ya kufahamisha, kuelimisha au kufurahisha ili aweze kujua jinsi atakavyofanya tafsiri yake. Hii ni kanuni muhimu katika nadharia ya *Skopos.* Kwa mantiki hiyo, mfasiri anapaswa kufasiri kwa kuzingatia lengo la hadhira inayokusudiwa. Kwa mfano riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba* na riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi yake Bugonoka na watoto wao Ntulanalwo na Bulhawali* zimetafsiriwa kwa misingi ile ya kutaka kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii husika. Kanuni hii inasisitiza kwamba tafsiri lazima itangaze Skopos (nia) yake. Ni muhimu ifahamike kuwa Skopos ya matini lengwa sio lazima ifanane na matini chanzi. Tofauti hizi husababishwa na tofauti za kimazingira, kijamii, kitamaduni na kihistoria.

ii) Matini lengwa hufafanua taarifa za kitamaduni za lugha lengwa. Kwa hivyo, msisitizo wa tafsiri upo katika uzingatiaji wa muktadha

unaozunguka tafsiri kama vile utamaduni, hadhira na dhima inayokusudiwa kwa hadhira lengwa. Tafsiri hutoa msisitizo wa utamaduni wa hadhira lengwa. Mwandishi yeyote anapofuma kazi yake ni sharti ashirikishe miktadha ya kila siku ya jamii husika. Vipengele vya kitamaduni kutoka matini teule vimetolewa kutoka miktadha ya jamii ya Wakikuyu na Wakerewe.

iii) Tatu, matumizi ya matini lengwa, si lazima yafanane na utamaduni chanzi. Tofauti hizi hutokana na muachano wa kitamaduni baina ya lugha chanzi na lugha lengwa. Matini lengwa haina ujumbe asilimia moja unaofanana na ule katika matini chanzi. Hii ina maana kwamba hakuna tafsiri ambayo haina dosari. Hii ni kwa sababu lugha hutofautiana katika mambo mengi kama vile uwepo wa dhana mahususi, msamiati mahususi, istilahi za kipekee, miundo ya maneno na hata miundo ya sentensi. Uhalisia huu una maana kwamba kupata istilahi mwafaka zinazowiana kimaana katika lugha chanzi na katika lugha lengwa wakati mwingine huwa vigumu. Kwa mintarafu hii, MC1 na MC2 kwa namna zimetafsiriwa hazifanani na matini tafsiriwa. Matini hizi hazina ujumbe asilimia moja unoafanana.

iv) Matini lengwa lazima iwe na mshikamano. Matini lengwa ni sharti itafsiriwe kwa namna ambavyo itashikamana na matini chanzi. Kanuni hii ina maana kuwa matini lengwa lazima iwe na maana kwa hadhira lengwa katika muktadha wa mawasiliano yao. Matini lengwa lazima ifuate utaratibu unaofaa na iwiane na matini chanzi ili ujumbe ueleweke vizuri na hadhira lengwa. Katika kutafsiri MC1 na MC2 ni sharti mtafsiri ahakikishe kuwa ujumbe katika MC umewiana na ule katika matini lengwa.

v) Matini lengwa lazima iwe na mshikamano na matini chanzi (kanuni ya uamilifu na usahihi). Uamilifu uzingatiwe hata kama nia ndiyo humwongoza mtafsiri katika kufanya tafsiri yake. Ni muhimu ahakikishe kuwa matini chanzi inashikamana na matini lengwa ili kuwasilisha ujumbe ipasavyo.

Kanuni ya ushikamani inasisitiza kuwa matini lengwa ni sharti iwe na maana kwa hadhira lengwa katika utamaduni wa lugha lengwa na katika muktadha wa kimawasiliano ambao matini lengwa itatumika. Matini lengwa lazima iwe na ushikamani wa kutosha ili kuruhusu watumiaji wa matini lengwa kuielewa kwa kutumia maarifa yao ya awali na hali ya mazingira. Kiini cha tafsiri ni matini kuwa sehemu ya mwendelezo wa ulimwengu iliyoandikwa kwa lugha chanzi. Kuna vipengele muhimu katika nadharia hii ambavyo ni utamaduni na lugha ya mtu binafsi ambavyo ni sababu inayobaini mchakato wa tafsiri.

Kwa kuwa lengo kuu la kazi hii ni kuchunguza jinsi zoezi la tafsiri linavyochangia uhifadhi wa utamaduni wa jamii husika basi nadharia hii imetumika kuchunguza, kujadili na kutathimini jinsi lengo hili limeafikiwa. Kanuni hizi mbili zilitumika katika kazi hii ili kuongoza mijadala na kubaini mikakati inayotumiwa ili kuleta ushikamani wa maana katika matini chanzi na matini lengwa na hatimaye kufikia azma ya kuhifadhi utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri.

Mfasiri anatazamwa kama mwandishi wa matini lengwa na ameondolewa kutoka katika pingamizi na vikwazo vinavyowekwa na mawazo finyu ya dhana ya tafsiri. Kulingana na mihimili ya nadharia ya *Skopos,* ni muhimu kusisitiza kuwa nadharia imejikita katika kuangalia tafsiri kama tendo linalohusisha vipengele vya kiisimu na kiutamaduni pamoja ili kufanikisha shughuli ya tafsiri. Katika shughuli ya tafsiri,

nadharia hii imeshirikisha suala la lengo, dhima, weledi, mbinu na mawasiliano katika shughuli nzima ya tafsiri.

Kulingana na malengo ya utafiti huu, nadharia hii ni muhimu kwa uchunguzi wetu kwa sababu inaitazama tafsiri kama tendo linalohusisha lengo, dhima, isimu, utamaduni na mawasiliano. Kwa hivyo, kwa kutumia mawazo ya nadharia hii malengo ya utafiti wetu yaliafikiwa. Misingi ya nadharia ya *Skopos* ilisaidia kuchunguza mbinu na mikakati ya tafsiri kama njia mojawapo ya kuhifadhi utamaduni. Kwa kutumia nadharia ya *Skopos* tumeonyesha ni jinsi gani ushikamani wa maana na matini umeafikiwa kupitia mchakato wa tafsiri.

2.7 Mhutasari wa Sura

Sura hii imeangazia mapitio ya maandishi kwa kuchambua na kuhakiki yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti huu. Maandishi yaliyopitiwa yalikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mada ya uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Mihimili ya nadharia ya anthropolojia na *Skopos* imeshughulikiwa inavyochukuana na malengo ya utafiti. Aidha, suala la tafsiri limeshughulikiwa ipasavyo pamoja na vipengele mbalimbali vya kitamaduni vinavyotumika katika kazi ya fasihi. Sura inayofuata imeangazia mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

MBINU ZA KUENDESHEA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inahusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli iliyoteuliwa, data ilivyokusanywa na jinsi uchanganuzi wa data ulivyofanywa.

3.1 Msuko wa Utafiti

Muundo wa utafiti ni ramani inayochorwa kuonyesha sura nzima ya utafiti inavyopaswa kuanzia ukusanyaji wa data mpaka uandishi wa tasnifu (Kothari, 2008). Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Muundo huu humpa mtafiti uhuru wa kuteua jambo moja na kulizamia kisha kulitolea mahitimisho mwafaka. Mtafiti huteua eneo lake la utafiti na kulishughulikia kwa kupata data itakayofanikisha utafiti wake. Gay, Mills na Airasian (2006) wanafafanua kuwa utafiti wa aina hii hutoa maelezo au ufafanuzi wa jinsi mambo yalivyo na aghalabu hutumika katika tafiti za lugha na fasihi. Mbinu hii humwezesha mtafiti kupata habari muhimu na sahihi kwa kutumia muda na gharama ndogo ikilinganishwa na mbinu zingine za utafiti.

Mbinu hii ya kimaelezo ilikuwa faafu kwa utafiti wetu kwa sababu ilitusaidia kuchambua maandishi yanayoshirikisha vipengele mbalimbali vya kitamaduni na mikakati iliyotumiwa kutafsiri vipengele hivi kama njia mojawapo ya kuhifadhi utamaduni. Katika utafiti huu, MC1 na MC2 pamoja na tafsiri zao zilisomwa na kudondoa vifungu mahususi kwa kurekodi vipengele vya kitamaduni kwenye daftari maalum. Hatimaye, tulichanganua data kwa kuongozwa na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ni wa maktabani. Kulingana na Ogechi (2024), utafiti wa maktabani ni uchunguzi unaoendeshwa maktabani katika chuo kikuu, chuo cha kati, manispaa au maktaba ya kibinafsi ambapo mtafiti hupekua katalogi, kompyuta, vitabu, magazeti akitafuta habari kuhusu mada yake. Utafiti huu ulihusu ukusanyaji wa data kwa kusoma riwaya teule ambazo ni: *Kaburi Bila Msalaba* na *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali (1981)* na tafsiri zao za Kiingereza*'Unmarked Grave' (2007)* na*'Mr. Myombekere His Wife Bogonoka Ntulanalwo and Bulihwali' (2002).* Majarida, vitabu, tasnifu, makala ya mitandaoni na maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada yetu ya utafiti – tafsiri kama mchakato wa kuhifadhi utamaduni yalisomwa. Maandishi haya yalisomwa kutokana na ukweli kwamba taaluma ya tafsiri inahusu matini zilizoandikwa. Kwa hivyo, vyanzo vya data vinavyotarajiwa kwa kiasi kikubwa ni machapisho.

Katika utafiti huu tulijikita katika mitandao ya kiakademia ili kufanikiwa kupata yanayohusiana na mada yetu ya utafiti. Young (1984) anaafiki upataji wa data mezani bila kuwatafuta watafitiwa na wahojiwa kwa kuwasaili. Usomaji huu ulitusaidia kukusanya data za kimsingi kuhusiana na mifano na vielelezo vya kitamaduni kutoka tungo, matukio na mandhari yanayodhihirika riwayani. Aidha, usomaji wetu ulibainisha mikakati iliyotumika ili kutafsiri vielelezo vya kitamaduni kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza. Maarifa kutoka sehemu hizi mbalimbali yalifaidi utafiti huu kwa kuongoza mijadala iliyotumika hatimaye kutoa mahitimisho ya kazi yetu.

3.3 Uteuzi wa Sampuli

Babbie (1999) anaeleza sampuli kuwa kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka kundi kubwa la watafitiwa linalotoa data ya kuwakilisha kundi zima. Utafiti

huu ulitumia sampuli ya kimakusudi. Oduma (2006) anasema kuwa usampulishaji wa aina hii unahusisha uteuzi wa sehemu fulani kama eneo la utafiti au watu fulani kama wasaili. Riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba* na riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* na tafsiri zao za Kiingereza '*Unmarked Grave'* na *'Mr. Myombekere His Wife Bugonoka Ntulanalwo and Bulihwali'* ziliteuliwa. Riwaya za Kitereza na Kareithi ziliteuliwa kimakusudi kwa sababu zilikuwa na viashiria vya utamaduni na pia ni kazi za kihistoria zilizofungamana na miktadha ya kitamaduni. Aidha, uteuzi huu uliongozwa na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia ya anthropolojia na nadharia ya *Skopos*. Kwa misingi hii, uteuzi huu wa sampuli kimakusudi ulifaa kwa huu utafiti kwa kuonyesha jinsi uhifadhi wa utamaduni ulidumishwa kupitia mchakato wa tafsiri.

3.4 Ukusanyaji Data

Data zilizotumika katika utafiti huu zilikusanywa kutoka matini chanzi za Kiswahili na matini lengwa za Kiingereza. Data kutoka riwaya ya Kareithi na Kitereza ziliteuliwa kutoka sura ya kwanza hadi ya mwisho kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia. Vielelezo vya utamaduni vilivyoteuliwa kama sampuli kutoka matini chanzi na matini lengwa vilirekodiwa katika daftari maalum kisha zikapangwa kulingana na makundi yao. Kategoria hizo zilikuwa kama zifuatazo: utamaduni wa mazingira ya kiekolojia, utamaduni wa kijamii na utamaduni nyenzo, yaani, vifaa vya kijamii. Aidha, mikakati iliyotumiwa kutafsiri vielelezo hivi ilipangwa pamoja na mifano yao. Miongoni mwa mikakati iliyoongoza mijadala yetu ni: mkakati wa upanuzi maana, ujumuishaji wa dhana, uhawilishaji na mkakati wa muungano wa mbinu za tafsiri. Data kutoka MC1 na MC2 zilipangwa sambamba ili ziweze kueleweka kwa urahisi kwa lengo la kubaini jinsi taaluma ya tafsiri ni mchakato wa kuhifadhi utamaduni.

3.5 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti vilivyotumika katika utafiti huu ni pamoja na kalamu na shajara. Shajara ni kitabu cha kuwekea kumbukumbu za kila siku (TUKI 2013). Shajara hii ilitumika kuhifadhi kumbukumbu za taarifa zilizopatikana kutoka kwa mtandao zilizohusiana na mada ya utafiti wetu. Aidha, daftari hili lilitumiwa kuweka rekodi ya data msingi zilizopatikana kutoka MC1 na MC2 kulingana na malengo yetu ya utafiti. Vifaa hivi vilitumiwa na mtafiti ili kurahisisha na kufanikisha kazi yake ya kukusanya data.

3.6 Uchambuzi wa Data

Mbinu ya uchanganuzi matini humwezesha mtafiti kusoma maandishi husika kwa uzingativu wa ndani ili aweze kubaini data zitakazomwezesha kujibu maswali ya utafiti (Leininger 1985). Katika muktadha huu, mtafiti alipopata maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti aliyanukuu katika shajara kwa ajili ya kuyatumia baadaye katika uchambuzi wa data akiongozwa na malengo na mihimili ya nadharia za utafiti. Sehemu hii ya uchanganuzi wa data ilishirikisha nukuu mbalimbali zilizotumiwa na mtafiti katika kujenga au kuthibitisha hoja fulani kwa minajili ya kufanikisha malengo ya utafiti. Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu ya uchanganuzi wa matini ni nzuri na haipotezi muda katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii ni mwafaka hasa mtafiti anapomakinika kusoma maandishi husika huku akiongozwa na malengo ya utafiti. Uchanganuzi ulifanywa kwa kuainisha mifano ya vielelezo vya utamaduni na mikakati iliyotumika kutafsiri mifano hii.

Taylor na Bogdan (1984) wanaeleza kwamba uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itamwezesha mtafiti kujibu maswali ya utafiti. Uchanganuzi humwongoza mtafiti kusoma vitabu na majarida mbalimbali yanayomsaidia kufahamu masuala mbalimbali ya kitamaduni.

Baada ya kusoma kazi husika, mtafiti hutumia njia ya maelezo katika kuzichambua data kwa njia mwafaka inayomsaidia msomaji kuielewa kwa wepesi. Katika utafiti wetu, uchambuzi wa data ulizingatia hatua zifuatazo: hatua ya kwanza ambayo ni ya kupanga data zilizokusanywa kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Baadaye tulitofautisha mada kuu na mada ndogo kulingana na malengo yetu. Sababu kuu ya uundaji wa mada hizi ni kwa ajili ya kurahisisha zoezi la uchanganuzi data. Hatua ya tatu ilikuwa ni kuchambua data kwa kuzidondoa na kuzitolea mifano na maelezo mwafaka kulingana na mada ya utafiti. Hatimaye, uchambuzi wa data ulianza kwa kudondoa vielelezo vya utamaduni kutoka MC1 na MC2 na kuvitolea ufafanuzi faafu wa kimaelezo.

3.7 Uwasilishaji wa Data

Data za utafiti ziliwasilishwa kwa maelezo ya kinathari. Mifano na maelezo yalizingatia vielelezo vya utamaduni pamoja na mikakati ya kutafsiri vielelezo hivyo kutoka matini chanzi hadi kwa lugha lengwa kama njia mojawapo ya kuhifadhi utamaduni. Aidha, vipengele vya ujielezaji vinavyofasiriwa kama ithibati ya uhifadhi wa utamaduni viliwasilishwa. Mifano ilipangwa katika makundi mawili katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Uwasilishaji ulizingatia lugha ya Kiswahili mwanzo kwa italiki kisha kufuatwa kwa lugha ya Kiingereza nayo kwa italiki. Maneno ya Kikerewe yaliyodhihirika katika dondoo la Kiswahili na Kiingereza yamekolezwa rangi. Ufafanuzi wa dhana hizi umetolewa katika matini teule uliomuongoza mtafiti kuendeleza mijadala yake katika utafiti huu. Data hii iliwasilishwa kulingana na malengo ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia.

3.8 Masuala ya Maadili katika utafiti huu

Maadili hurejelea kuheshimu taratibu, miiko, mila na desturi zinazoongoza maisha au shughuli fulani katika jamii (Kumar 1999). Miiko na mila ni jambo la lazima katika

kila jamii kwa sababu ndiyo inaongoza shughuli zote za binadamu. Mtafiti aliongozwa na miiko hii ya utafiti kwa kusoma matini teule za kubuni kulingana na malengo ya utafiti. Aidha, utafiti huu umefanywa kwa kuongozwa na miiko yote ya utafiti. Nukuu zote zinazorejelea kazi hii zimedondolewa kwa usahihi kutoka kwa kazi zilizoteuliwa.

3.9 Mhutasari wa Sura

Sura hii imeangazia msuko wa utafiti ambao ni utafiti wa kimaelezo. Muundo huu unampa mtafiti fursa ya kuliteua jambo na kulizamia kisha kulitolea mahitimisho. Ukusanyaji data umejikita katika matini mbili ambazo ni MC1 na MC2. Baada ya kuzisoma viashiri vya utamaduni viliteuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Aidha, sura hii imeangazia uchambuzi na uwasilishaji wa data.

SURA YA NNE

HISTORIA NA UTAMADUNI WA WAKIKUYU NA WAKEREWE

4.0 Utangulizi

Sura hii imeeleza historia na utamaduni wa Wakikuyu unaongozwa na MC1 na utamaduni wa Wakerewe unaowakilishwa na MC2. Katika uandishi wa fasihi utamaduni hufungamana na matukio ya kila siku ya wanajamii. Historia ya jamii hizi mbili unatupa msingi wa utafiti wetu.

4.1 Historia na Utamaduni wa Wakikuyu

Wakikuyu ni mojawapo ya makabila makubwa zaidi nchini Kenya, wenye historia tajiri ya asili, uhamaji, na utamaduni wa kipekee unaohusiana kwa karibu na Mlima Kenya. Wakikuyu ni sehemu ya jamii ya Wabantu, waliotoka katika eneo la beseni la Mto Kongo na kuhamia mashariki mwa Afrika. Kabila la Wakikuyu lilitokea Mlima Kenya, wakiongozwa na Gikuyu na mkewe Mumbi, waliowekwa na Mungu wao *Ngai* kwenye mlima huo na kupewa ardhi yenye rutuba. Gikuyu na Mumbi walizaa wasichana kumi na mmoja, ambao walikuwa waanzilishi wa koo kuu za Kikuyu. Wanaume wa kuoa mabinti hawa walitoka makabila jirani kama Wakamba, Wameru, na Waembu. Wengi wanaishi hasa katika nyanda za juu za Kenya ya Kati, maeneo yanayozunguka Mlima Kenya kama Kiambu, Murang'a, Nyeri, Kirinyaga, na sehemu za Embu na Meru. Mlima Kenya, unaoitwa *Kĩrĩma kĩrĩ Nyaga* kwa Kikuyu, ni mahali patakatifu ambapo wazee walitolea kafara kwa Ngai. Wao ni wakulima hodari, wakilima mazao kama mahindi, viazi, na kahawa. Katika historia ya kisasa, wamekuwa mstari wa mbele katika biashara, elimu, na siasa nchini Kenya. Walikuwa na mfumo wa koo na wazee wa ukoo waliotoa uongozi wa kijamii na kiroho. Kabila hili lina mila na desturi tajiri, ikiwemo sherehe za tohara, hadithi simulizi, na sanaa ya ufinyanzi, ususi, na muziki wa jadi.

4.1.1 Mapambano dhidi ya ukoloni

Wakikuyu walihusika katika mapambano dhidi ya ukoloni, hasa kupitia harakati za Mau Mau, ambazo zililenga kupigania ardhi na uhuru kutoka kwa Waingereza. Ukoloni wa Waingereza ulileta mabadiliko makubwa kwa Wakikuyu, hasa kupokonywa ardhi yao ya jadi katika maeneo ya nyanda za juu. Ardhi hiyo ilitwaliwa na wakoloni kwa ajili ya mashamba ya kibiashara, na Wakikuyu wengi walilazimika kuwa wafanyakazi wa mashamba au kuishi kama wakulima bila ardhi. Mau Mau ilikuwa harakati ya siri ya kijeshi na kisiasa ya Wakikuyu (na makabila mengine) iliyolenga kupigania uhuru wa Kenya. Ilianza rasmi mwanzoni mwa miaka ya 1950, ikiongozwa na wapigania uhuru kama Dedan Kimathi, General China, Jomo Kenyatta na wengine. Wanamgambo wa Mau Mau walifanya mashambulizi dhidi ya majeshi ya kikoloni, wakitumia mbinu za msituni na ujasusi.

Ili kukabiliana na waafrika, serikali ya kikoloni ilijitokeza na ukandamizaji mkali, ikitangaza hali ya hatari mwaka 1952. Maelfu ya Wakikuyu walikamatwa, wakiwekwa kwenye kambi za mateso, au kufungwa bila mashtaka. Dedan Kimathi alikamatwa mwaka 1956 na baadaye kunyongwa, lakini akabaki kuwa shujaa wa kitaifa. Ingawa Mau Mau haikufanikisha uhuru moja kwa moja, ilichochea msukumo wa kisiasa na kuonyesha uhitaji wa mabadiliko. Wakikuyu walikuwa mstari wa mbele katika siasa za kitaifa, na Jomo Kenyatta, ambaye pia alikuwa Mkikuyu, alikuwa rais wa kwanza wa Kenya mwaka 1963. Wanamgambo wa Mau Mau walikuwa wapigania uhuru wa Kenya waliopambana dhidi ya ukoloni wa Waingereza kati ya 1952 na 1960, wakitumia mbinu za msituni, ujasusi, na mshikamano wa kijamii. Lengo kuu lilikuwa kupigania ardhi na uhuru, baada ya kupokonywa mashamba yao na kutengwa kisiasa na kijamii na wakoloni. Harakati hizi ziliitwa rasmi Kenya Land and Freedom Army (KLFA), lakini jina "Mau Mau" lilibaki maarufu.

Viongozi Mashuhuri walikuwa Dedan Kimathi: Kamanda mkuu wa Mau Mau, aliongoza mapambano ya msituni na kuunda miundo ya kijeshi. Waruhiu Itote (General China): Alikamatwa na baadaye kushirikiana na wakoloni, lakini alikuwa mwanzo mmoja wa wapiganaji hodari. Stanley Mathenge: Alikuwa kiongozi wa kijeshi, lakini baadaye alitoweka na hatima yake haijulikani. Musa Mwariama: Aliongoza vikosi vya Mau Mau katika maeneo ya Meru. Jomo Kenyatta: aliongoza siasa za kitaifa na kuwa rais wa kwanza wa Kenya 1963. Katika harakati ya vita, wanamgambo walijificha msituni, hasa katika milima ya Aberdare na Mlima Kenya. Walitumia silaha za kienyeji, ujasusi wa kijamii, na viapo vya siri (oath) kuimarisha mshikamano. Walishambulia vituo vya polisi, mashamba ya wakoloni, na walioshirikiana na Waingereza. Baada ya mashambulizi haya mateso na ukandamizaji kwa wanamgambo yalifuata. Watu wengi waliuawa katika harakati hii. Dedan Kimathi alikamatwa mwaka 1956 na kunyongwa lakini akabaki kuwa ishara ya ukombozi. Ingawa Mau Mau haikufanikisha uhuru moja kwa moja, ilichochea msukumo wa kisiasa na kuonyesha uhitaji wa mabadiliko. Wanamgambo wa Mau Mau walitambuliwa rasmi kama wapigania uhuru na serikali ya Kenya miaka mingi baadaye.

Historia ya Wakikuyu imejikita katika hadithi za asili, kilimo na uchumi, na mapambano ya Mau Mau yaliyokuwa msingi wa uhuru wa Kenya. Wameendelea kuwa na nafasi kubwa katika siasa na maendeleo ya taifa. Historia ya jamii moja imefungamanishwa na utamaduni wake. Binadamu wanapokuwa na maarifa kuhusu historian a utamaduni wao hupata hisia za umoja na mshikamano katika makundi mbalimbali ya kijamii. Utamaduni wa Wakikuyu ni tajiri, wenye kina na unaoweka thamani kubwa katika familia, imani, kazi, na heshima. Ingawa utandawazi umebadilisha baadhi ya vipengele hivi, msingi wa utamaduni kama heshima kwa

mababu, umuhimu wa jamii, na nguvu ya mila umeendelea kuhifadhi utambulisho wa Agĩkũyũ hadi leo.

4.1.2 Maisha ya P.M. Kareithi

Marehemu Manuhe Kareithi alizaliwa kwenye kijiji cha Mbari ya Hwai katika wilaya ya Nyeri na alifariki 1977 katika ajali ya barabara. Manuhe alisoma katika shule ya Tumutumu na hatimaye akaenda kwenye shule ya Kagumo ambako alihitimu na kupata shahada ya Ualimu. Aliendelea kujielimisha mwenyewe na mwishowe akaingia Chuo Kikuu Cha Makerere. Baadaye aliweza kujiunga na Chuo Cha Kent, Ohio nchini Marekani. Kareithi anaeleza kumbukumbu ya mambo aliyoshuhudia wakati wa hali ya hatari kabla ya Jamhuri ya Kenya haijajinyakulia uhuru. Uandishi wake umefumbata matukio ya Mau Mau kwa njia ya kipekee na kwa lugha ya Kiswahili. Manuhe amefaulu waziwazi kufafanua vita vya uhuru wa Kenya na gharama walipitia wazalendo. Kareithi ni mzaliwa wa Nyeri na uandishi wa riwaya hii umezunguka miktadha ya utamaduni wa Wakikuyu.

4.1.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Kaburi Bila Msalaba*

MC1 ni riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** iliyoandikwa na Munuhe Kareithi aliyezaliwa katika kijiji cha Mbari - ya - Hwai katika Wilaya ya Nyeri (1969) kisha kutafsiriwa na Chege Githiora mwaka wa (2007). Hii ni riwaya ya kihistoria ambayo iliandikwa wakati wa vita vya Mau Mau nchini Kenya. Vita vya Mau Mau vilianza mwanzoni mwa miaka ya hamsini miongoni mwa Wakikuyu waliofukuzwa na wazungu kutoka mashamba yao mnamo karne ya 19. Watu waliokuwa wakishukiwa kuwa wanamgambo wa Mau Mau, wake kwa waume waliingizwa katika kambi za mateso bila kufikishwa mahakamani. Wengi wao wamenyongwa katika mapambano hayo.

Mau Mau lilikuwa ni kundi la wapiganiaji wa Kenya waliokuwa wakipinga utawala wa kikoloni wa Waingereza kutoka mwaka wa 1952 hadi 1960. Muuungano wa kundi hili ulionyesha vile watu wanaweza kufanya mengi kupitia umoja na uzalendo wao. Uasi uliokuwa unaendelea kimya kimya hatimaye ulizuka na kuwa vita vya wazi wakati Gavana wa kikoloni alipotangaza hali ya hatari na kuomba majeshi zaidi kutoka Uingereza. Ingawa kundi hili halikuwa na mafanikio makubwa ya kijeshi, upinzani wao dhidi ya mkoloni uliharakisha upatikanaji wa uhuru nchini Kenya. Harakati za wanamgambo hawa zilichangia pakubwa kuikomboa nchi ya Kenya kutoka kwa minyororo ya mkoloni.

Sehemu kubwa ya kundi la Mau Mau iliundwa na watu wa kabila la Gikuyu huku kukiwa na baadhi ya wanachama kutoka Embu na Meru. Wakikuyu wenyewe hawakuwa wakiliita kundi hili Mau Mau bali waliliita "Muingi" yaani vuguvugu. Historia inasema kwamba mtu wa kwanza aliyekamatwa na serikali ya kikoloni alikuwa mzee Jomo Kenyatta, ambaye miaka kumi baadaye alikuwa Rais wa kwanza wa Kenya.

Riwaya hii ina jumla ya kurasa 120. Matukio ya kihistoria yanamzunguka msichana wa Kikuyu Mumbi, ambaye mpenzi wake aliuliwa katika harakati ya kupigania uhuru wa nchi ya Kenya. Naye baadaye akanajisiwa na kufariki akiwa anajifungua. Hadithi yenyewe imeanza mwaka wa 1948 wakati Meja Blue na vijana wenzake walipotoka vita vya pili vya dunia na kurudi hapa Kenya. Riwaya hii ni kumbukumbu ya taabu zilizowapata wazalendo wakiwa katika harakati ya kupigania uhuru wao. Historia hii ya Kenya imefumbatwa kupitia kwa ubunifu wa Kareithi huku akiangazia vipengele mbalimbali vya kitamaduni. Riwaya hii inaangazia historia na utamaduni wa nchi ya Kenya ya jinsi na namna walivyojikomboa mikononi mwa mkoloni.

4.2 Historia na Utamaduni wa Wakerebe

Jamii ya Wakerebe inapatikana katika Mkoa wa Mwanza, hasa Kisiwa cha Ukerewe, ambacho ndicho kisiwa kikubwa zaidi katika Ziwa Victoria na pia kisiwa kikubwa barani Afrika. Utamaduni wa Wakerebe umejengwa juu ya mila, imani na mfumo wa maisha ambao unalingana na mazingira ya kisiwa yaani uvuvi, kilimo cha visiwa, na heshima kwa mababu. Wakerebe ni sehemu ya makabila ya Kibantu ambayo historia inaonyesha walihama kutoka maeneo ya Kongo kwa karne nyingi zilizopita. Waliwasili katika visiwa na pembezoni mwa Ziwa Victoria, wakianzisha makazi yao kutokana na wingi wa maji, rutuba ya udongo, na samaki. Kulingana na simulizi za jadi, Ukerewe ilikaliwa na makabila tofauti yaliyokuja kwa nyakati tofauti, lakini Wakerebe walijenga utawala wao kwa mfumo wa machifu. Chifu maarufu waliotajwa ni pamoja na wale waliotawala maeneo ya Bugorora, Nansio na Nyamkiri.

Ukristo uliingia kupitia wamishonari wa Kijerumani na Wafaransa katika karne ya 19. Ukoloni wa Kijerumani na baadaye wa Kiingereza uliathiri mfumo wa uongozi wa kimila. Kabla ya ukoloni, Wakerebe waliongozwa na machifu (Bakungu) waliokuwa na mamlaka juu ya ardhi, masuala ya ndoa, sheria na matambiko. Chifu alisaidiwa na wazee wa ukoo katika kutoa maamuzi. Wakerebe wanaamini kuwa roho za mababu zinaendelea kulinda ukoo. Mazishi ya Wakerebe yanafanywa kwa heshima kubwa, na mara nyingi kuna tambiko la kuomba mababu wawapokee marehemu. Jamii hii iliamini katika Mungu Muumba, mara nyingi anayetajwa kwa majina yanayobadilika kulingana na ukoo lakini aliyekuwa juu ya miungu midogo na mizimu. Mababu wanachukuliwa kuwa walinzi wa familia. Kabla ya kufanya maamuzi makubwa kama ujenzi, ndoa au safari, familia ilikuwa inatoa tambiko maalumu. Wakerebe huzungumza Kikerebe, lugha ya Kibantu yenye uhusiano wa karibu na Kihaya, Kisukuma na Kijita. Historia na utamaduni wa Wakerebe ni mkusanyiko wa tamaduni

za Kibantu zilizochanganyika na athari za mazingira ya kisiwa. Msingi wa maisha yao umejikita katika uvuvi, kilimo, familia, na heshima kwa mizimu ya mababu. Hata katika zama za kisasa, Wakerebe wanaendelea kuhifadhi utambulisho wao kupitia lugha, muziki, mila na desturi.

4.2.1 Maisha ya Aniceti Kitereza

Aniceti Kitereza alizaliwa mnamo mwaka wa 1896 katika kijiji cha Sukumaland mahali baba yake Bwana Malindima na malikia wa Wakerebe alikuwa amefungwa. Baada ya kifo cha babake mnamo mwaka wa 1901 Kitereza alirudi Ukerewe na mama yake. Kwa muda Kitereza aliishi na mjombake ambaye alikuwa Omokama (mfalme) wa Ukerewe. Mwaka wa 1905 alijiunga na shule ya kanisa Kagunguli Ukerewe. Baada ya kufuzu mwaka wa 1909 alitumwa Bukoba ili ajifunze zaidi kuhusu lugha na theolojia. Mwaka wa 1919 alifuzu kama mwalimu na katekisti pale Kagunguli.

Tangu utotoni Kitereza alikuwa na ari kubwa ya elimu. Alijifunza lugha ya Kiswahili, Kijerumani na Kiingereza. Wajerumani walipoondoka alijifundisha lugha ya Kiingereza kwa kutumia kamusi ya Kiingereza. Kuanzia mwaka wa 1939, Kitereza alijishughulisha na uchunguzi wa mila na historia na ukusanyaji wa ngano na methali za Kikerewe lakini mkusanyiko huu haukuchapishwa.

Kitereza kwa kutoridhika na mshahara aliopewa na shirika la kanisa aliacha kazi hiyo na kujiunga na mfanyi biashara Mgiriki mnamo 1939. Kwa sababu ya vita aliacha kuhudumu katika duka na kurudi kwa shirika la kanisa ambapo alihudumu kama mtafsiri wa vitabu vya dini. Ugonjwa wa mifupa ulimlazimisha kustaafu mapema na kurudi nyumbani Kagunguli ambapo aliishi na mke wake, Ann Katura. Alipompoteza mke wake mwaka wa 1980 ilikuwa wazi kwamba hangeishi muda mrefu kwa sababu alikuwa anamtegemea mke wake kwa mambo mengi. Familia hii ilikuwa na watoto

wanne ambao walifariki mapema kwa hivyo Kitereza hakuwa na mtu yeyote wa karibu. Athari ya kifo cha mke wake ilichangia pakubwa kwa uandishi wa riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhwali.*

Kitereza, kama mhusika wake mkuu Myombekere, alijiona kama mtu ambaye hakufanikiwa maishani kwa kutoacha kizazi chake nyuma cha kuendeleza jina lake na matendo yake. Utamaduni wa Wakerebe ulikuwa unaamini mwanamume asiye na watoto ni mtu maskini ila tu huzuni na aibu humfuata kwa maisha yake. Kitereza hakugundua 'kizazi' alichowaachia binadamu kwa kuandika riwaya ya Bwana Myombekere.

Mnamo mwaka wa 1945 riwaya hii ilikuwa imeandikwa kwa lugha ya Kikerebe lakini ilikosa wachapishaji kwa sababu ilikuwa imeandikwa kwa lugha ya mama. Profesa Gerald Hartwig ambaye ni rafiki yake wa dhati alimshauri kutafsiri mswada huu kutoka lugha ya Kikerebe hadi lugha ya Kiswahili. Bila kukawia aliutafsiri mswada huu na kumkabidhi Profesa Hartwing ambaye alishawishi kampuni ya Heinmann Educational Books ambao walikubali kuchapisha riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhwali.* Mnamo mwaka wa 2002 ilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza na Gabriel Ruhumbika.

4.2.2 MC2 Muhtasari wa riwaya ya *Bwana Myombekere Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali*

Riwaya ya Bwana Myombekere ni mojawapo wa riwaya ambayo imezingatia utamaduni wa mwafrika. Utamaduni ambao umepitia tawala mbalimbali kama vile utawala wa Waarabu, Wajerumani, na Waingereza. Tawala hizi ziliweza kupenyeza tamaduni zao na kuathiri mawazo na matendo ya kiafrika (Mlacha 1987). Elimu na

dini zilitumika kwa muda ili kudunisha na kufifisha utamaduni wa mtu mweusi. Kwao, Sengo na Lucas (1975:6):

> Mila na desturi za kiafrika hazikuwa za kiungwana, mwafrika aliyebaki akifanya kiafrika alionekana mshenzi na mtu asiyeendelea.

Kitereza alionyesha jinsi alivyofanikiwa kuzionyesha mila na desturi za Wakerewe na kuzirithisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali* imegawika katika majuzuu mawili. Madumulla (1988:33) anaeleza kuwa:

> Hii ni riwaya ambayo iko katika majuzuu mawili, ni riwaya ndefu kuliko riwaya iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Anasisitiza kuwa utanzu huu wa riwaya umejikita sio tu katika kueleza hali mbalimbali ya maisha ya Wakerewe bali pia vipengele mbalimbali vya kitamaduni vimejadiliwa kwa undani.

Utafiti huu umejikita katika juzuu la kwanza ambalo lina jumla ya kurasa 296. Kazi hii ilitafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza na Gabriel Ruhumbika mwaka wa 2002. Kitereza huzungumzia mila na desturi mbalimbali ambazo hupatikana katika jamii ya Wakerewe.

Familia ya Bwana Myombekere imetumika kama kiwakilishi cha jamii nzima ya Wakerewe kwa hali mbalimbali; uhusiano wao, maisha ya unyumba, raha na taabu za Wakerewe, sherehe na misiba yao, malezi na majukumu yao, kifo, ibada, ustaarabu na utamaduni wa Wakerewe kabla na baada ya ujio wa wakoloni umejadiliwa. Kwa kuhitimisha maoni haya, Madumulla (1988:34) anasema kuwa riwaya hii ingefaa iitwe “Mila na ada za Wakerewe” kwa sababu riwaya imesheheni utamaduni wa Wakerewe. Riwaya hii imezingatia zaidi mila na desturi za Wakerewe kwa kutumia maisha ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka. Maisha yao yameonyesha mzunguko baina ya mtu, utamaduni na muundo wa jamii husika. Mulokozi (1985:213) anaeleza wazi kwamba:

> Kitereza alikuwa na lengo la kutunza na kuhifadhi lugha, mila, desturi na utamaduni wa Bakerebe.

Kwa kutumia kisa cha kusikitisha, kisa kilichosababishwa na desturi za kabila hilo kwamba mwanamke ambaye hajajaliwa watoto anafaa kuachwa na mumewe, mwandishi ameendeleza ploti ya vitushi vyake kwa kutuonyesha raha na taabu, ubaya na uzuri wa kufuata mila na desturi.

Sehemu ya kwanza ya riwaya hii imeshughulikia hatua za Myombekere kumchukua mke wake kutoka kwao, kulipa dhamana kulingana na utamaduni wa Wakerebe na Bugonoka kutafuta mganga aliyemshughulikia hadi akafanikiwa kupata watoto. Riwaya imezunguka maisha ya Myombekere na Bugonoka ambao wanachukuliwa kama viwakilishi vya jinsia ya kike na ya kiume katika utamaduni wa Wakerebe. Kupitia kwao tunajifunza imani, mila, itikadi, misimu na sanaa ya jamii hii. Maisha na utamaduni wao umejidhihirisha katika kazi yao ya kila siku: uvuvi, usasi na ukulima. Ziwa ni shamba lao la pili ambalo linafidia vyakula vyao vya shambani. Kitereza ametunza na kuhifadhi vipengele vya kitamaduni ili viweze kufaidi kizazi chake na kizazi cha baadaye.

4.3 Mhutasari wa Sura

Sura hii imeangazia historia na utamaduni wa riwaya teule: MC1 utamaduni wa Wakikuyu na MC2 utamaduni wa Wakerebe. Waandishi wameonyesha shughuli zao za kila siku na ndani mwa maisha yao mna vipengele mbalimbali vya kitamaduni. Sura zifuatazo zimesawiri maelezo na mifano ya vipengele vya kitamaduni katika riwaya hizi mbili na tafsiri zao.

SURA YA TANO

UHIFADHI WA UTAMADUNI KUPITIA MCHAKATO WA TAFSIRI

5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeangazia historia na utamaduni wa matini teule. Sura hii imeshughulikia uchanganuzi na uwasilishaji data ambao umeongozwa na lengo la kwanza la utafiti ambalo ni: kubaini kwa njia ya maelezo na mifano kuwa MC1 na MC2 ni riwaya zilizo hazina na hifadhi kuu ya vipengele vya utamaduni wa jadi na ukale wa maisha ya jamii mahsusi ya kiafrika. Sehemu hii imechanganua vipengele mbali mbali vya kitamaduni kutoka kwa riwaya hizi mbili pamoja na tafsiri zao.

5.1 Usawiri wa Vipengele vya Kitamaduni katika Riwaya Teule

Kila jamii huwa na mambo yanayobuniwa ili kukidhi utashi na maendeleo yao kwa ujumla. Mambo hayo huwa ni mwenendo wa maisha ya jamii fulani, mtazamo wao na taratibu zao za maisha zinazotofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Ni wazi kusema kwamba utamaduni huipa jamii upekee na kuifanya itambuliwe kwa njia maalum ulimwenguni. Mila na desturi za jamii husika hujengwa, hukomaa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Iwapo hili halitatekelezwa pana hatari ya kufifia kwa utamaduni wake na kwa hivyo, jamii kupoteza utambulisho wake.

Hakuna utamaduni ulimwenguni ambao hauathiriwi na utamaduni mwingine. Hii ni kwa sababu utamaduni ni kitu kinachopanuka na kubadilika kila wakati kutokana na maingiliano baina ya watu wanaotumia lugha tofauti hasa katika mawasiliano yao ya kila siku. Jamii fulani inapokuwa na kifaa fulani cha kitamaduni huku wengine hawana, njia mojawapo ya kuonyesha mahusiano ni kwa utamaduni mmoja kukopa dhana ya kutajia kifaa husika kutoka kwa utamaduni mwingine. Kimsingi, lugha ambazo zimekuwa na mahusiano ya muda huathiriana na kwa hivyo, hurahisisha shughuli ya kutafsiri kinyume na zile ambazo hazijawa na maingiliano yoyote kwa

vile hakuna kukopa msamiati. Kila jamiii hujiundia msamiati wake kwa namna ya kipekee. Kwa hivyo, uteuzi wa msamiati hujikita kwenye mazingira wanamokulia jamii. Kila jamii ina miundo yake ya kisiasa, uongozi, imani na itikadi mbalimbali ambazo hutofautiana na jamii nyingine.

Maana kwa ujumla wake imefungamanishwa na utamaduni na kwa sababu hii, kila jamii huelewa ujumbe kwa muktadha wa utamaduni wao (Larson 1984). Mona (2000) anaashiria kwamba lugha chanzi inaweza kuwa na neno ambalo linaashiria dhana fulani na neno hilo halipatikani katika utamaduni wa hadhira lengwa. Neno hilo linaweza kuwa dhahania au neno la kawaida linalorejelea imani ya kidini, mila na desturi za jamii husika. Maneno haya ndiyo yanajulikana kama viashiria vya utamaduni (Mona 2000). Hadhira lengwa hufasiri tafsiri yoyote kulingana na utamaduni na tajriba yao na wala sio kulingana na tajriba ya mwandishi wa MC. Basi kwa misingi hii, mtafsiri analazimika asaidie hadhira lengwa kuelewa ujumbe na lengo la MC kwa kutafsiri akizingatia tamaduni zote mbili.

Dare (2008) anasema utamaduni ni ruwaza ya tabia na mawazo ambayo kundi mahususi la kijamii hujifunza, kuumba na vile vile kushiriki. Anasisitiza kuwa utamaduni ni kibainishi na kitambulisho cha lugha, watu, utaifa na uchumi wao. Kwa misingi hii, utamaduni hudhibiti itikadi, desturi, imani, maadili na amali za jamii. Newmark (1988) alianisha vipengele vya kitamaduni katika kategoria tano tofauti. Kategoria hizi ni pamoja na:

i) Ekolojia ambayo hujumuisha wanyama, mimea, upepo unaovuma katika eneo fulani, milima, nchi tambarare miongoni mwa vitu vinginevyo.

ii) Utamaduni nyenzo – hivi ni vitu vya kuonekana na kugusika kama vile vyakula, mavazi, maskani, njia za usafiri na mawasiliano.

iii) Utamaduni wa kijamii ambao hurejelea kazi, burudani na starehe za watu wa jamii husika.

iv) Taasisi za jamii - utamaduni huu hujumuisha mipangilio ya kisiasa, kijamii, kisheria, kidini na ujamii wa jamii fulani.

v) Desturi, mawazo, ishara na tabia – aina hii hujumuisha tabia za watu, imani na falsafa zao katika mazingira wanamoishi.

Katika mchakato wa tafsiri ni lazima vipengele hivi vitiliwe maanani katika shughuli nzima ili kupata matokeo bora. Utafiti usiozingatia haya hutiliwa shaka na hadhira lengwa kwa kuwa ujumbe uliokusudiwa hautawasilishwa kwa ukamilifu. Vipengele hivi vinapodumishwa kwa hadhira lengwa basi utamaduni huhifadhiwa kutoka lugha moja hadi nyingine.

Kuna aina mbili kuu za utamaduni: tamaduni nyenzo (vifaa vya kijamii) na utamaduni usio na nyenzo (Mgbemere 2014). Utamaduni nyenzo hushirikisha vitu vinavyoonekana na vinavyogusika. Huwa ni rasilimali na nafasi ambazo watu hutumia ili kufafanua utamaduni wao. Kwa misingi hii, huwa ni pamoja na makazi, ujirani, miji, shule, makanisa, mahekalu, viwanda, misikiti, vifaa na mbinu za uzalishaji bidhaa na mazao, maghala na kadhalika. Mgbemere pia amebainisha utamaduni usio nyenzo kama mawazo yasiyo dhahiri waliyo nayo watu kuhusu utamaduni wao. Utamaduni usio wa nyenzo ni pamoja na imani kuhusu Mungu, ibada, maadili na adabu. Kulingana na migao hii ya Newmark (1988) na Mgbemere (2014) utafiti huu umezingatia kategoria za utamaduni katika migao mitatu ambayo ni:

i) Utamaduni wa mazingira ya kiekolojia

ii) Utamaduni wa kijamii

iii) Utamaduni wa nyenzo yaani vifaa vya kijamii.

5.1.1 Utamaduni wa mazingira ya kiekolojia

Utamaduni wa mazingira ya kiekolojia umefafanuliwa na Osano (1997), anasema dhana ya mazingira kama hali ya anga na ya kimaumbile inayoizunguka eneo fulani la kijiografia. Kwa njia moja au nyingine mazingira huathiri maisha ya wanadamu katika jamii. Osano ameainisha mazingira katika vitengo mbalimbali kama vile mimea, wanyama na vitu vinginevyo ambavyo hupatikana katika maeneo mbalimbali kwa kutegemea mazingira mahususi. Ni muhimu kutambua kuwa juhudi za binadamu zinaweza kuhifadhi mazingira yake au kuyavuruga na kufanya maisha yake kuwa magumu kuyamudu. Mazingira hurejelea vitu kwa upekee wao. Kwa sababu ya kuwepo kwa hali tofauti za kimazingira, watu hujitokeza na dhana mbalimbali za kutajia vitu vinavyopatikana katika mazingira yao.

Ekolojia kulingana na Newmark (1988) inahusu tofauti inayotokana na mazingira kama mimea, wanyama na hali ya hewa. Ikiwa jamii mbili zinapatikana katika mazingira tofauti kuna uwezekano kwamba kutakuwa na dhana tofauti za kuelezea hali hizi tofauti za kimazingira. Kwa uhalisia huu, mtafsiri atakuwa na kazi ngumu kupata kisawe kitakachoelezea hali hii katika utamaduni tofauti. Hali hii huzua changamoto kwa watafsiri hasa kwa fasihi tafsiriwa kwa sababu tafsiri si zoezi la kubadilisha maana au msimbo bali ni kusafirisha maana kutoka lugha asilia hadi kwa lugha pokezi. Tafsiri ya dhana za kiekolojia huhitaji mikakati mwafaka ili dhana hizo zitafsiriwe ipasavyo kutoka kwa hadhira asilia (HA) hadi hadhira pokezi (HP). Bila weledi huu kwa mtafsiri dhana hizi zinaweza kutafsiriwa kwa njia potoshi na kwa hivyo kukosa kufasiriwa ipasavyo kwa hadhira lengwa.

Ekolojia ni taaluma inayochunguza mifumo na dhima ya maumbile ya kiasili (Oduma, 1971). Kauli hii ya Oduma inaoana na Krebs (1978) anayesema kuwa ekolojia ni taaluma ya kisayansi ambayo inahusu uchunguzi wa mwingiliano na mahusiano kati ya binadamu na binadamu wenzake, wanyama na mimea. Kulingana na wataalamu hawa wawili ni kuwa ekolojia ni taaluma inayochunguza mahusiano na maingiliano baina ya jamii na mazingira yake. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijiografia kama vile: misitu, miti, mabadiliko ya tabia nchi na kadhalika. Kwa vile fasihi hufungamanishwa na maisha ya binadamu, basi msanii hupata msukumo na mshawasha wa kutunga kazi yoyote ya kifasihi, kutokana na matukio na mabadiliko ambayo yanaikumba jamii katika mazingira anamoishi. Tabia ya kijiografia, mazingira, tabia nchi na hali ya hewa huwa tofauti kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine. Kila jamii huzuka na dhana tofauti ili kuelezea na kufafanulia tabia nchi na hali ya anga. Utafiti huu umegawa utamaduni wa mazingira ya kiekolojia katika makundi matano kama yanavyojidhihirisha katika jedwali lifuatalo.

Jedwali 5.1: Utamaduni wa mazingira ya kiekolojia

Mazingira ya kiekolojia	Vielelezo kutoka MC1	Vielelezo kutoka MC2
a) Wanyama	-	14
b) Samaki	-	12
c) Ndege	-	6
d) Misitu, miti, na majani	4	14

Jedwali la 5.1 limetoa muhtasari wa vipengele mbalimbali vya kiekolojia vilivyotumiwa na mwandishi wa MC1 na MC2. Kinachosisitizwa hapa ni mshikamano uliopo kati ya mazingira ya kiekolojia na kazi ya kisanaa. Majina ya mimea, wanyama na mazingira hayapatikani katika utamaduni mwingine kwa sababu majina yao hayahusiani na utamaduni mwingine. Dhana hii inawekwa wazi na

nadharia ya isimu anthropolojia inayosisitiza kuwa kila jamii huwakilisha utamaduni wake tofauti. Hekima na maarifa ya wanajamii huwasilishwa kupitia utamaduni wao. Lugha hutumiwa na jamii kama chombo cha kuhifadhi amali na utamaduni huo. Kwa misingi hii, mtafsiri ametumia mikakati tofauti tofauti ili kufanikisha mawasiliano kwa njia mwafaka.

5.1.1.1 Ekolojia ya wanyama

Kila jamii huwatambulisha wanyama wake kulingana na mifumo yao ya kimazingira. Thamani na mwelekeo wa mnyama fulani hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Waandishi wa sanaa huonyesha jinsi binadamu anavyotangamana na wanyama wanaomzunguka kwa ajili ya kukimu haja na mahitaji yake ya kila siku. Mara nyingi wanyama hawa hutumiwa kwa manufaa yao au hata huwa ni hatari katika mazingira yao. Wanyama mbalimbali hupatikana katika mazingira maalum na ya kipekee. Kutokana na utofauti huu wa kimazingira wanadamu hujitokeza na maneno mbalimbali ya kutajia viumbe hawa wanaowazunguka. Wataalamu na watafsiri mbalimbali wanafaa kuelewa tofauti hizi za kiekolojia wanapoanza zoezi la tafsiri ili kuibuka na mikakati mwafaka ya kufanikisha mchakato wa tafsiri. Ni wazi kwamba kazi hizi za kisanaa zinahusishwa na wanyama wa kufugwa, wanyama wa pori na viumbe wengine wapatikanao katika mazingira na uhalisia wa Wakikuyu na wa Wakerebe. Sehemu hii imeangalia majina mbalimbali ya wanyama kama yalivyotafsiriwa kutoka utamaduni chanzi hadi utamaduni pokezi katika MC2.

Mf 1.

...mwili wake wote ukaishia kuwa tumbo tu kama mdudu mmoja aitwaye ***nalutundubwi.*** *(Uk. 273)*

... all her fresh had deserted wherever else it should normally be and converged on her stomach, which looked like a ball and swollen to bursting like that of the tiny toad ***nalutundubwi.*** *(Pg.333)*

Katika dondoo hili Bugonoka alikuwa na mimba na iliweza kupanuka zaidi na mwili wote ukaishia kuwa tumbo tu, kama mnyama mmoja aitwaye ***nalutundubwi***, tena unene aliokuwa nao machoni mwa watu haukufichika kamwe. Ujauzito wa Bugonoka ulijidhihirisha kwa uwazi maana mwili wake uliongezeka kwa kimo na ukapanuka kiasi kwamba ulilinganishwa na chura huyu. ***Nalutundubwi*** ni aina ya chura wadogo wenye rangi ya kijani kibichi, wana sumu na hupenda sana kukaa kwenye majani mabichi. Mnyama huyu akimuuma ng'ombe, mara hiyo huvimba tumbo na kufa upesi. Maelezo haya yametolewa mwishoni mwa matini teule.

Mf 2

> *...kisha akarudi hima apate kumpa Lweganwa ekisahi na kumshika ndama, sababu ng'ombe Yule alikuwa* ***sina****, yaani alikuwa mweusi sana kwato zake zote. (uk.53)*
>
> *…gave back ekisahi to Lweganwa and then held the cow's calf once more, because the cow being milked was their spotless black cow which had enough milk. (pg.79)*

Mf 3

> *…Lweganwa alipoona nzi waitwao* ***embara*** *wametulia, akamwita Bugonoka, "Lete maji tukamue hawa ng'ombe." (uk.53)*
>
> *…As soon as Lweganwa saw gadflies disappear with the coming of the night, he called aloud Bugonoka in the house and told her, "Please bring water so that we can begin milking cows. (pg.77)*

Aidha, dondoo la pili na la tatu linadhihirisha kuwa Wakerewe walikuwa wafugaji na walitambua mifugo yao kulingana na rangi mbalimbali. Katika dondoo nambari 2 ***sina*** ni ng'ombe mweusi na mara nyingi ng'ombe hawa walikuwa wanasumbuliwa na nzi wa aina ya ***embara***.Wakati mtafsiri alikuwa akihawilisha ujumbe huu kutoka MC2 (Matini Chanzi 2) hadi MT2 (Matini Tafsiriwa 2) yaelekea hakupata kisawe cha kuelezea dhana hizi kwa sababu ya upekee wa kijiografia. Kulingana na nadharia ya *Skopos* zoezi la tafsiri ni sharti litekelezwe kwa nia fulani. Lengo la tafsiri ndilo linabaini njia, mbinu na mikakati itakayotumika ili kuleta usahihi wa kimatumizi

katika hadhira pokezi. Kwa misingi hii, mtafsiri aliweza kudumisha msamiati huu wa Kikerewe kwa hadhira lengwa lakini akautolea maelezo ya ziada yanayoiwezesha hadhira lengwa kuelewa. Kwa jinsi hii, basi vipengele vya kitamaduni vimehawilishwa kutoka lugha ya Kiswahili hadi kwa lugha ya Kiingereza.

5.1.1.2 Ekolojia ya samaki

Wakerewe ni kabila dogo lipatikanalo katika Kisiwa cha Ukerewe, Wilaya ya Ukerewe, Mkoa wa Mwanza. Kabila hili linajihusisha na shughuli ya uvuvi ambayo imewapa umaarufu mkubwa katika eneo hili. Kutokana na kazi hii wana vifaa mbalimbali vya kutekelezea shughuli hii na wameibuka na majina mbali mbali ya kuwatambua aina mbalimbali za samaki. Majina haya yana upekee wao ambao haupatikani katika maeneo mengine.

Mf 4

> *…humu akakuta kuna samaki mmoja aina ya* ***ensato*** *yaani* ***ensendera;*** *akachukua chombo cha kuchotea samaki katika mtego kiitwacho* ***ekisanzo*** *akamchota, akamvua na kumtupa pwani mchangani. Akaendelea kutafuta* ***kitiro*** *cha tatu alipovuruga akakuta kuna samaki mmoja ya* ***ensanto*** *yaani* ***engonogono.*** *(UK.51)*
>
> *… there he found one tilapia of* ***ensendera*** *kind. He took his hand basket and drew the fish out of the water with it; killed it and tossed it into sand on the beach. He went on to the third chamber and likewise stirred the water of the chamber and in that one too he found a single tilapia, this time the big* ***engonogono****. (Pg.75)*

Kulingana na dondoo hili Lweganwa alikuwa ameenda ziwani kuoga na kuchukua samaki. Siku hii alipovuruga maji alipata samaki mmoja anayejulikana ***ensato,*** alichukua chombo akamchota na kumrusha mchangani. ***Engonogono*** kulingana na utamaduni wa Wakerebe ni aina ya samaki anayependwa na huwa mnene aina ya ***ensato.*** Ufafanuzi wa dhana hizi unadhihirisha ***ensendera*** ni aina ya samaki ambaye ni mdogo na mara nyingi huvuliwa wakati wa mvua. Kulingana na ladha ***engonogono*** huwa mtamu kuliko ***ensendera*** na hupendelewa zaidi na Wakerebe. Utamaduni wa

lugha ya Kiingereza ulihifadhi dhana hizi katika matini lengwa ya tafsiri kwa sababu mtafsiri alikosa visawe vyao mahususi vya dhana hizi. Iwapo jamii haiishi karibu na ziwa au bahari inakuwa vigumu kwa mtafsiri kueleza vipengele hivi vya kiekolojia ipasavyo ili hadhira lengwa ifahamu. Kulingana na nadharia ya *Skopos* Reiss (1990) anasisitiza kwamba mara tu mtu anabaini nia ya tafsiri, basi mikakati mwafaka kama vile ufafanuzi, urekebishaji na uundaji mpya wa matini hujitokeza. Kutokana na mawazo haya mtafsiri ameibuka na mikakati ya kufanikisha zoezi zima la tafsiri. Kwa njia hii vipengele mbalimbali vya kitamaduni huhifadhiwa kutoka lugha moja hadi nyingine.

Mf 5

...Lweganwa na Myombekere wakawapa sehemu yao ya ugali na chungu cha kitoweo cha samaki waitwao ***enembe. (****uk.81)*

...Lweganwa na Myombekere ate theirs separately which was Obwita with a relish, ***enembe***. (pg.112)

Lweganwa wakiwa na shemeji yake Myombekere waliletewa chakula na Bugonoka wakafurahia kitoweo cha ugali na samaki. ***Enembe*** ni aina ya samaki mnono asiye na magamba mwilini na huvuliwa kilindini. Mara nyingi Wakerewe wangempikia mgeni mashuhuri aliyefika kwa shughuli maalum kama Myombekere. Mtafsiri ameibuka na mkakati wa ufafanuzi ili kuwezesha hadhira lengwa kuelewa kulingana na nadharia ya *Skopos.*

Mf 6

...samaki waliokuwa wakitegwa na kuuawa kwa wingi hasa ni samaki za ***ebigugu*** *na* ***enkorobondo****. (uk.169)*

...fish traps in the rivers and catch plenty of of the tiny ***ebigugu*** *catfish and* ***enkorobondo. (****pg.217)*

Ebigugu na ***enkorobondono*** ni aina ya samaki wadogo kwa kimo katika utamaduni wa Wakerebe wanaovuliwa katika mito, vidimbwi na hasa wakati wa mvua. Dhana

hizi vile vile zimehawilishwa kutoka utamaduni chanzi hadi kwa utamaduni pokezi kupitia kwa mchakato wa tafsiri. Vermeer (1989) anasisitiza kuwa tafsiri sio tu mchakato wa kuhawilisha ujumbe bali ni muundo mahsusi wa tendo la binadamu ambalo ni sawa na matendo mengine ya kibinadamu. Shughuli zote za binadamu katika jamii ni sharti miktadha yote ishirikishwe katika zoezi la tafsiri ili kupata tafsiri bora. Vipengele vya kitamaduni vimehawilishwa kupitia mikakati ya upanuzi maana ili kuwasiliana na hadhira lengwa.

5.1.1.3 Ekolojia ya ndege

Ni jambo la kawaida kwamba kazi yoyote ya sanaa haikosi kujikita katika wakati maalum, kipindi fulani cha kihistoria, mazingira maalum ya kijiografia pamoja na utamaduni maalum. Ndege pia hupatikana katika maeneo ya kipekee ya kiekolojia. Udhihirikaji wake huwa tofauti kutoka eneo moja hadi lingine kwa sababu za kimazingira. Maeneo mengine ni joto au baridi ambayo si mwafaka kwa makazi ya aina fulani za ndege. Uhalisia huu wa kutafsiri dhana zinazorejea aina mbalimbali za ndege umejidhihirisha katika MC2. Kitereza ameazima vipengele vingi vya kitamaduni kutoka jamii yake ya Kikerewe ili kuisanifu kazi yake ya fasihi na kuipatia utambulisho.

Mf 7.

> *…baada ya kutembea kwa muda, walisikia majogoo yakiwika, baadaye wakaona kumepambazuka, halafu wakasikia ndege wa* ***amabundazi*** *wakiimba kisha wakaanza kujiona viganja vyao. (uk.86)*
>
> *… they had been walking for a fairly long time when they heard cocks from everywhere. Before long, it was the night sky of men's pre-dawn. After a while the* ***amabundazi*** *birds cried out with their thick voices. (pg. 122)*

Wakerebe hawangekuwa na njia ya kujua nyakati zao bila aina mbalimbali za ndege ambao wangetoa sauti zao na binadamu wangejua kwamba kumepambazuka.

Kulingana na dondoo nambari 7, Myombekere na kikundi chake walikuwa wameamka asubuhi ili kupeleka pombe kwa wakwe zake kama adhabu ya kulipia makosa yake. Ndege hawa waliwajulisha kwamba kumepambazuka wakiwa njiani wakienda kutimiza shughuli yao. ***Amabundazi*** ni aina ya ndege anayetoa sauti yake asubuhi na mapema ili kutangazia Wakerebe kwamba kumepambazuka. Aina huyu ya ndege hapatikani katika utamaduni wa lugha ya Kiingereza ndio maana haijakuwa rahisi kutafsiri dhana hii kwa utamaduni lengwa. Kulingana na nadharia ya *Skopos* mtafsiri amelazimika kuibuka na mikakati itakayofanikisha zoezi zima la tafsiri. Mikakati hii hurahisisha dhana hizi kwa utamaduni lengwa kwa kuzitolea ufafanuzi.

Mf 8.

> *Basi hiyo ndiyo hadithi yangu ya kizee! Kuna kidege kidogo sana kiitwacho **enfunzi**; umuonavyo akiwa na manyoya yake mekundu sana, na ukijaribu kumuuliza, atakujibu, "Sisi kwetu tunatumia daima kujipaka rangi nyekundu ya majiwe mekundu!" tena kuna ndege mmoja mdogo pia, huitwa **ensonsoni**; umuonavyo akiwa na mdomo wake mrefu sana kuliko yeye alivyo, muulize upesi, atakujibu, 'Sisi kwetu tumezoea kula katika mti wa msononi ulio na miiba mingi na utomvi ndani yake, ndio sababu tumepata sote mirija ya kujilisha kwa kunyonya utomvu huu!"(uk.209)*
>
> *There you are! That's my elder's little tale for you! When the tiny red bird **enfunzi** is asked why it has red feathers it answers: "Where I come from we smear ourselves with red – earth." When the grain eating **ensonsoni** bird of the long beak is asked why its mouth is so long it answers: "Where I come from we live on sucking juices." So you too make of your tale whatever you will and don't ask me questions I cant answer, lest I too tell you lies. (pg. 259)*

Hiki ni kisa kinachoelezea jinsi wanawake walivyoanza kuishi na wanaume katika himaya zao. Kupitia kwa kisa hiki fanani ametaja ndege wa kiasili kuelezea maumbile yao naye ametamatisha kisa chake kwa kuonyesha kwamba kila hali katika jamii huwa na sababu zake. Jinsi hawa ndege wana sababu ya maumbile yao ndivyo jamii ya binadamu ilivyo na sababu jinsi wanaishi pamoja kama mume na mke. ***Enfunzi*** ni ndege aliye na manyoya mekundu na anapoulizwa kuhusu rangi yake yeye hujibu

kuwa anapotoka wao hujipaka rangi nyekundu. Ndege wa ***ensonsoni*** pia huwa na maelezo yake kwa nini wana midomo mirefu. Wao wanaamini kuwa wanapotoka wao hujilisha kwa miti iliyo na miiba ndio maana wana mirija ya kujilisha kwa kunyonya utomvu wa miti ya msononi. Majina haya yalipohawilishwa kutoka utamaduni lengwa kupitia mikakati mbalimbali ya tafsiri basi utamaduni asilia umehamishwa kutoka hadhira asilia hadi hadhira lengwa. Hii huwa ni njia moja ya kuhifadhi utamaduni kupia taaluma ya tafsiri.

> ***Mf 9***
>
> *... je, ndege hao wanaokula mawele yenu ni ndege wa aina gani? Mimi na mwenzangu Mafwere tukamjibu hivi,* ***ensole*** *na* ***enzeli*** *ndipo naye akasema hivi… (uk.260)*
>
> *…by the way, those birds which are finishing your millet, what species of birds are they? We answered him back quickly my companion Mafwere and I saying together they are mostly* ***ensole*** *and* ***enzeli****. (pg.295)*

Wakerebe wamekuwa wakulima wa aina mbalimbali za nafaka na mara nyingi hukumbana na changamoto ya ndege wanaokula mazao yao. Wanajamii hawangekuwa na njia ya kukabiliana na ndege hawa ila kwenda kwa mganga wa ndege naye angetumia dawa ili kuzuia uharibifu wao. Myombekere na Mfwere walikuwa wamemtembelea mganga ili kumwomba awakinge ndege wanaoharibu nafaka kwa mashamba yao. Ni dhahiri kuwa katika maeneo haya kulikuwa na aina mbalimbali za ndege. ***Ensole*** ni aina ya ndege mwenye rangi ya manjano, ni mdogo na mharibifu kwa nafaka na hutembea kwa kikundi. ***Enzeli*** pia ni aina ya ndege mdogo, hula mawele na hutembea kwa vikundi pia. Ndege hawa hawapatikani katika maeneo mengine ndio maana dhana hizi zimehifadhiwa katika utamaduni lengwa. Kwa mujibu wa nadharia ya *Skopos,* inasisitiza kuwa matini lengwa si lazima ifanane na matini chanzi. Tofauti hizi husababishwa na tofauti za kimazingira, kijamii,

kitamaduni na kihistoria. Uhawilishaji wa vipengele hivi umefanikishwa kwa kuibuka na mikakati mwafaka ya kurahisisha mawasiliano na kudumisha vipengele vya kitamaduni kwa hadhira lengwa.

5.1.1.4 Ekolojia ya Miti na Majani

Katika riwaya zetu teule matumizi mbalimbali ya miti yamechipuka katika miktadha ya utamaduni wa kimazingira ya kiekolojia kwa ujumla. Mahusiano ya binadamu na mazingira yake ni jambo la kawaida kiasi kwamba hakuna msanii atakamilisha utunzi wake bila kuleta mahusiano haya kwa uwazi kwa kazi ya fasihi. Kitereza katika riwaya yake ametaja aina mbalimbali za miti na jinsi inavyotumiwa katika jamii kwa ajili ya matumizi yao.

Mf 10.

> ***….****mtumbi ule wa embeterero ulikuwa umechongwa kutoka katika mti wa* ***muzungute*** *uliokuwa unaivisha pombe haraka sana. (uk.74)*
>
> *…the fermentation dugout in question was of* ***muzungute*** *tree, famours for yielding good beer. (pg. 105)*

Wakerebe walikuwa ni wapenzi wa pombe ya kienyeji iliyokuwa imetengezezwa kutoka kwa ndizi. Kutokana na utamaduni wao walielewa njia mwafaka ya kuivisha pombe haraka na kwa kutumia vifaa vya aina gani. **Muzungute** ni aina ya mti unaotumika kutengeneza mitumbwi ya kukanyagia pombe ya ndizi. Mti ulijulikana kwa umaarufu wake kwa kazi hii. Kwa hivyo, wangechimba shimo kasha vipande mbalimbali vya **muzungute** vingetumika ili kupata matokeo bora. Uhalisia huu wa **muzungute** umemshurutisha mtafsiri kuzuka na mikakati mwafaka ya kutafsiri dhana hii ili kudumisha utamaduni wa MC.

Mf 11.

> ***…****Tulipofika nje ya mji wao, karibu na kichungu pale karibu na mti wa* ***umulinzi*** *pale nikaona mwenzangu amesimama na kusema 'Pokea dawa yako mwenzangu sasa ninarudi nyumbani kwa wageni... (uk.162)*

> *...ones outside the home and on our way, when we came to the big anthill under* **umulinzi** *tree there I saw my sister stand and sha said, 'Receive your medicine sister for now I want to go back home and see other vistors... (pg.210)*

Baada ya Bugonoka kukumbwa na shida ya ugumba kwa muda mrefu alienda kwa mganga ili ampe dawa ya kumwezesha kuzaa. Dondoo hili linadhihirisha wakati Weroba mke wa mganga anamsindikiza na kusimama karibu na mti wa ***umulinzi*** ili kumpa maagizo jinsi ya kutumia dawa. Ni ishara tosha kwamba mti huu ulikuwa unaaminiwa na jamii hii kuwa na nguvu fulani ndio maana Kitereza anasisistiza kuwa Weroba alipofika kwa mti huu alisimama na baadaye akatoa maagizo. Utamaduni huu wa kiekolojia unapofika wakati wa kuutafsiri inamwia vigumu mtafsiri kupata kisawe cha neno kitakachoelezea dhana hii ya mti wa **umulinzi** kwa utamaduni mwingine. Mazingira mengine hayaruhusu kuwa na mti huu au hata ukiwa utakuwa na jina tofauti. Kwa hivyo, mtafsiri anapohawilisha neno hili jinsi lilivyo utamaduni wa Wakerewe unasafirishwa kwa hadhira lengwa kupitia kwa mchakato wa tafsiri. Nadharia ya *Scopos* inasisitiza kwamba lengo la tafsiri ni lazima lieleweke kabla ya mchakato wa tafsiri kuanza. Pindi tu lengo hili limeeleweka mikakati mwafaka ya kudumisha vipengele vya kitamaduni itatumika.

Mf 12.

> *...ndipo akamfungia katikati ya mji wake, penye mti wa* ***omurumba*** *na kumwaacha pale anapiga kelele. (uk.263)*
>
> *...he tethered him at* ***omurumba*** *tree in the compound of his home and left him there crying. (pg.322)*

Mf 13.

> *...walipofika pale mtoni, wakamkuta Nakutuga akipumzika katika kivuli cha mti uitwao* ***umugege****. (uk.102)*
>
> *...when they reached the river, they found their man resting under the shade of* ***omugege*** *tree. (pg.139)*

Tofauti za kiekolojia hujidhihirisha kwa uwazi kutoka lugha chazi hadi kwa lugha lengwa. Dhana hizi zinazoelezea aina mbalimbali za miti katika utamaduni wa

Wakerewe hazipatikani katika lugha ya Kiingereza kwa sababu ya upekee wa mazingira. Kulingana na nadharia ya *Skopos*, mtafsiri anapozichukua dhana hizi kisha kutoa maelezo ya aina hizi za miti atakuwa amehawilisha utamaduni wa Wakerewe hadi kwa hadhira lengwa.

Mf 14.

> *...mgunda ule ulikuwa unajaa majani mengi sana ya kila aina kama haya:* ***amahule,amazuzume*** *na miti mingine hata mimi hapa siwezi kuijua kamwe! Tena kulikuwa na mengine aliyotambaa chini kamamaboga na kukwea juu ya miti zile tulizotaja, yakizifunga funga kama kamba, nayo majani yao ni haya:* ***amasanzwa,ensikesike*** *na* ***amatungamamba*** *na mengine mengi mno. (uk.136)*
>
> *...the fields had become really bushy,overgrown with* ***amahule*** *and* ***amazuzume,*** *mangroves and all sorts of trees, some of whose names even I don't know, which were in turn overran and covered with thickets of vines and tree- climbers like* ***amasanzwa, ensikesike*** *and* ***amatungamamba. (pg. 183)***

Upekee wa mazingira hujidhihirisha kwa njia mahsusi ya kuelezea dhana zinazopatikana katika eneo fulani. Maelezo ya dhana hizi hayapatikani kwingine ila tu sehemu moja. Kauli hizi zimehawilishwa jinsi zilivyo na maelezo kutolewa ili kufanikisha mawasiliano. ***Amahule*** ni aina ya magugu yenye miiba hupatikana sana mtoni na kwenye nchi tambarare. Iwapo eneo halina mto ni nadra kupata aina hii ya magugu katika sehemu hii. Aidha, kuna aina ya ***amazuzume*** ambayo ni aina ya miti ambayo hustawi kwa wingi kwa wingi karibu na mito na mabonde na majani yake hutumika kama sabuni. ***Amatungamamba*** pia ni mmea mtambaaji unaopanda mashina ya miti mingine; hufaa sana kutungia samaki aina ya kambare-mamba, na samaki wengine. Ukaribu wa maji huchangia kumea na kuenea kwa mimea hii. Ni aina ya magugu ambayo hupenda palipo na maji. ***Ensikesike*** ni aina ya mmea wenye kutambaa na kukwea mashina ya miti mingine. Pindi tu binadamau ajipatapo katika mazingira fulani huchukua muda kuelewa manufaa ya kila kitu kilicho katika mazingira yake. Aina hizi za miti na majani huwafaa wakaazi wa maeneo haya

pakubwa. Kutafsiri kwa dhana hizi kunahitaji mikakati mwafaka ili kuhawilisha ujumbe ipasavyo. Kwa njia hii, utamaduni wa lugha asilia hudumizwa kwa lugha pokezi kupitia taaluma ya tafsiri. Kulingana na mtazamo wa kimuundo katika tapo la isimu anthropolojia utamaduni huwa ni uhalisia wa maisha ya binadamu katika jamii. Mahusiano yao, shughuli zao na migogoro yao hudhihirika kupitia matumizi yao ya lugha.

Aidha, katika riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** upekee wa mazingira umeshirikishwa katika kazi ya fasii. Mtunzi huyu pia ameangazia aina mbalimbali za miti na majani katika kazi yake.

Mf 15.

*...Mumbi aliingia hapo shambani kama alivyoamriwa. Majani mengi yaitwayo "**mshika kondoo"** yalishikilia nguo zake na miguu. (uk.11)*

*...when Mumbi got inside the farm plants known as **mshika kondoo** clung to her clothes and legs. (pg.10)*

Mumbi alikuwa ametekwa nyara na askari kwamba yeye alikuwa mmoja wa wana mgambo wa Mau Mau na aliwaibia risasi na siri za mkoloni. Walipoendelea kuwasaka wengine walimuagiza kuingia shambani ambapo majani haya yalishikilia nguo na miguu yake. Aina hii ya mmea huwa na mazoea ya kumea mahali mazao kama mahindi na maharagwe yamepandwa. Iwapo utapata eneo ambalo shughuli ya kilimo haipo basi mmea huu ni nadra kupatikana. Katika mchakato wa tafsiri inamwia vigumu kutafsiri dhana hii kwa lugha ya Kiingereza. Dhana hizi zinapohawilishwa jinsi zilivyo basi inakuwa ni njia moja ya kudumisha utamaduni wa HC hadi kwa HL.

Mf 16.

*...Meja Blue na Wahu walikwenda kwa miguu mpaka karibu na **Mugumo,** yaani mti mkubwa ulio karibu na shule ya Kiamwangi. (uk.19)*

> *...Meja Blue and Wahu walked up to near the huge **Mugumo** tree that was close to Kiamwangi school. (pg.17)*

Mugumo ni aina ya mti uliokuwa mkubwa na kuheshimiwa na wanakijiji kutokana na upekee wake. Chini ya mti huu shughuli za biashara zingeendelea au wazee wangeketi kupumzika au kufuatilia matukio ya siku. Mara nyingi mti huu ungetumika kama njia ya kumwelekeza mtu kwenda mahali fulani. Meja Blue alikuwa anaelekea mjini lakini mpenzi wake alikuwa anamsindikiza. Walipofika maeneo haya walisimama kisha Wahu akamuaga mwenzake. Kisawe cha mugumo kilikosekana ndiposa dhana hii ikatumika jinsi ilivyo ili kuhifadhi utamaduni wa lugha chanzi. Mikakati hii ya tafsiri imeibuka kutokana na *Skopos* ya matini yaani nia ya tafsiri.

Utafiti huu unadhihirisha ukweli kwamba kuna utangamano wa karibu kati ya binadamu na mazingira yake ya kiekolojia. Wanawaelewa wanyama hawa kwa misingi ya manufaa yao, sifa zao na maumbile yao. Aidha, binadamu wanafahamu wanyama waliohatari kwa mazingira yao. Waliohatari wamebuni mbinu za kukabiliana nao na wale walio na manufaa wanajua namna ya kuwashughulikia. Wanyama hawa wamepewa majina kulingana na maeneo wanamopatikana. Ni wazi kwamba mwandishi wa MC2 ameshirikisha dhana za kiekolojia zaidi kuliko mwandishi wa MC1. Dhana hizi zinapotafsiriwa zinamhitaji mtafsiri kuwa macho kwa sababu hazipatikani katika mazingira ya hadhira lengwa.

5.1.2 Utamaduni wa Kijamii

Utamaduni wa kijamii unarejelea mawazo yaliyo dhahiri ambayo wanajamii huwa nayo kuhusu mazingira yao zikiwemo imani, desturi, amali, sheria, lugha na asasi zao za kijamii. Dhana ya utamaduni wa kijamii hushirikisha mawazo na imani kuhusu Miungu, ibada, maadili na adabu pamoja na masuala mengine yasiyo dhahiri. Kupitia kwa migogoro mbalimbali katika matini teule, imani, falsafa zao, desturi na kanuni

zao katika jamii zinaweza kujidhihirisha. Utamaduni wa kijamii huwa na uhusiano wa karibu na fasihi tafsiriwa. Kwa njia moja au nyingine utamaduni wa kijamii huathiri fasihi. Kwa misingi hiyo, utafiti huu umegawa utamaduni wa kijamii katika ruwaza nne kama zinavyojidhihirisha katika Jedwali 5.2:

Jedwali 5.2: Vielelezo vya Utamaduni wa Kijamii

Mifano ya Utamaduni wa Kijamii	Vielelezo kutoka MC1	Vielelezo kutoka MC2
a) Mila na desturi	3	6
b) Imani za dini	2	3
c) Shughuli za kazi	-	2
d) Asasi za kijamii	2	2
e) Burudani na starehe	-	2

Kulingana na Jedwali 5.2 ni dhahiri kwamba utamaduni wa kijamii hujidhihirisha wazi katika kazi za kisanaa. Watunzi wengi hushirikisha shughuli mbalimbali za binadamu katika utunzi wao ili kuleta uhalisia wa kazi yao. Jedwali hili limeonyesha kwamba mtunzi wa MC2 ametumia vipengele vingi vya utamaduni wa kijamii kuliko MC2. Hali hii husababishwa na muktadha pamoja na lengo la mwandishi.

5.1.2.1 Mila na Desturi

Desturi ni jambo la kawaida linalotendwa na jamii fulani mara kwa mara (TUKI 2004). Neno hilo ni sawa na mazoea, ada au kaida. Kwa kawaida, kila jamii huwa na mila na desturi zake ambazo ni nguzo kuu katika jamii yao. Desturi hizi hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kulingana na jamii husika. Baadhi ya mila hizi zinaaminika kuwa za ukweli tangu jadi. Desturi hizi za kijamii huwa na upekee wake mahsusi kutoka jamii moja hadi nyingine. Kutokana na dai hili basi huwa ni tatizo kuhawilisha vipengele hivi vya mila na desturi kutoka matini chanzi hadi matini tafsiri. Kwa mujibu wa Abbas (2015) akimnukuu Robinson (1977), vipengele kama utamaduni na desturi za kitamaduni ni ngumu kutafsirika hasa kama mtafsiri anataka kudumisha muundo na muonjo wa dhana zenyewe. Ili kufanikiwa kutafsiri dhana hizi

sharti mikakati mwafaka ishirikishwe ili kupata tafsiri bora. Riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali* imedhihirisha ukweli huu wa mila na desturi za Wakerebe.

Mf 17.

> *Myombekere alipotupa macho yake mlangoni mwa mji wake, akaona ya kuwa kulikuwa na mkwe wake. Aliponyoosha mguu wake kwenda kumkaribisha mgeni, na alipoangaza macho yake akaona kuwa kulikuwa na mama mkwe pia! Hima! Akarudi nyuma na kugeuka upesi ili wasionane naye uso kwa uso, na mama mkwe naye akasimama pale pale langoni mwa mji.*
>
> *…katika mila za Abakerebe wote wakwe hukimbiana daima: mama mkwe humkimbia mkwe wake, kadhalika mkwe naye humkimbia mama mkwe wake, na hiyo ndiyo heshima katika Ukerewe nzima. (uk. 6)*
>
> *Myombekere looked up towards the gate of his home and saw that the visitor was none other than his father in law and got up and hurried to meet him. However he had made a couple of steps when he saw his mother inlaw too. So he had to withdraw, walking backwards, and likewise his mother in law stood still near the kitchen utensils platform.*
>
> *…Wakerewe customs demanded that parents –in –law and their children-in-law of the opposite sex avoid each other: the mother – in- law avoids her son- in- law and likewise the son- in – law. There is no greater sign of respect than that among the Wakerewe. (pg.6)*

Desturi hii ilikumbatiwa na jamii ya Wakerebe kwa sababu waliona kuwa hakuna njia nyingine ya kuwaonyesha wakwe heshima isipokuwa kupitia njia hii ya kukimbiana. Myombekere mwenyewe amedhihirisha hili alipowatembelea wakwe zake. Bila kutekeleza hili heshima yako kwa wazazi haitajidhihirisha kamwe. Kipengele kama hiki kinapohawilishwa katika utamaduni mwingine huleta hali ya kustahimiliana miongoni mwa makabila kwa sababu ya tofauti hizi za utamaduni wa kijamii. Kila jamii ulimwenguni hukubali na kuheshimu utamaduni wa jamii zingine. Mchakato wa tafsiri husafirisha desturi hizi kutoka lugha moja hadi nyingine. Kwa misingi hii, viashiria vya utamaduni husafirishwa kutoka matini chanzi hadi matini tafsiriwa. Mtasfiri huibuka na mikakati ya kuhawilisha utamaduni wa jamii bila kuzua utata.

Mikakati hii inakubalika na nadharia ya *Skopos* ambayo inasisitiza lengo la tafsiri. Iwapo lengo ni kudumisha utamaduni wa kijamii kwa hivyo mikakati kama udumishwaji na upanuzi maana itatumika ili kuafikia lengo hili.

Mf 18.

> *...msichana alimfuata nyuma na kata ya maji ya kunywa wakati wa kula. Bugonoka alipofika karibu na miguu ya baba yake, akapiga magoti, akashika isabuzyo (chombo cha kunawia vidole, ni kama kimtumbwi hivi kilichotengenezwa kutoka katika mti wa musayu. (uk.6)*
>
> *Following her behind the little girl of their home, carrying a cup of drinking water. When Bugonoka got near to his father's legs, she knelt down, got hold of a washing basin. (pg.8)*

Bugonoka anapomhudumia baba yake na mume wake anapiga magoti mbele yao na hakutatizwa na jambo hilo. Hii iliaminiwa ni njia moja ya kumheshimu mwanamme. Wanawake wote walitii bila kupinga. Desturi hizi zinapotafsiriwa jinsi hii watu wengine wanaweza kushangaa maana hili halitokei kwao. Tofauti hizi za kitamaduni zinayafanya mataifa mengine kukubali na kuheshimu utamaduni wa watu tofauti.

Mf 19.

> **...***mama yake aliporejea alikuta Bugonoka amekwisha kuugawa ugali kutoa sehemu ya mume wake sababu zamani zile baba mkwe alikuwa hawezi kula pamoja na mkwe wake, walikatazwa na mila ya Abakerebe wote. (uk.14)*
>
> *Her mother had prepared two nicely kneaded dishes of obwita, one of her son in-law and the other one for her husband, and also put aside a third cut of food for her daughter and herself. Women normally did not eat with men, and of course, it was unthinkable for Bugonoka's mother to eat with her son-in –law. (pg.22)*

Utamaduni wa Wakerebe ulimuinua mwanaume kiasi kwamba mwanamke alikuwa chini yake kwa kila hali. Mara tu anapomkaribia kumhudumia mila na desturi zilimshurutisha mwanamke kumtii mwanamme. Aidha, mwanamke alikuwa na nafasi yake katika jamii hii. Hangeruhusiwa kutangamana na wanaume, wangetengewa

mahali pao pa kuketi na mahali pao pa kula. Bugonoka na msichana mdogo wanarudi nyumbani ili waweze kula na mama yao.

Mf 20.

> *...wakampa **embete** mmoja bure kwa ukarimu wao. Lweganwa akamtengeneza samaki huyo, akamtoa utumbo na kumkata vipande, kisha akamfunga peke yake kwa sababu ni samaki aliwaye na wanume tu. (uk.51)*
>
> *...then those friends of his gave him a present of one **embete** and he disemboweled the big fish separate parts of his fishing because it's men's fish. (pg.76)*

Baada ya Lweganwa kutembea kidogo kule ufuoni alikutana na wavuvi wa samaki wakubwa. Wavuvi wale walipokwisha kutoa samaki zao katika mtumbwi, wakampa samaki mmoja kwa ukarimu wao. Lweganwa alimtengeneza samaki huyu na kumfunga peke yake kwa sababu ni samaki aliwaye na wanaume tu. Hii ni desturi ya kuwanyima wanawake uhuru wao hadi kwa vyakula wanastahili kula. Desturi hii inapotafsiriwa inaashiria uhifadhi wa utamaduni wa Kikerewe katika lugha ya Kiingereza. Neno **embete** halikupata kisawe chake. Kwa hivyo, lilidumishwa katika utamaduni lengwa.

Vile vile wanawake Wakerewe hawakuruhusiwa kula nyama ya mbuzi, nyama ya pori, kuku hata mayai. Ilikuwa ni miiko kwa yeyote angepatikana akila vyakula hivi.

Mf 21.

> *... alipokuwa tayari akauipua na kugawa sehemu mbalimbali; ule wa wanawake akautia katika kikapu kidogo, na wa baba mji nao akauweka mbali. (uk.55)*
>
> *...she dished it out of the pot and divided it up, putting the woman's share in a separate bowl with the men's bowl. (pg.79)*

Itikadi hizi ziliwashurutisha wanawake kutii pasina kupinga. Walielewa na kukubali nafasi yao katika jamii ya Wakerebe. Tofauti hizi za kitamaduni huwafanya wanawake wengine ulimwenguni kuwakubali wenzao licha ya changamoto hizi wanazopitia. Mchakato wa tafsiri husafirisha na kuhifadhi desturi hizi kwa mataifa

mengine ulimwenguni. Basi ni kusema kuwa utamaduni wa Wakerebe umehifadhiwa kwa mataifa mengine.

Mf 22.

> *...mama yake akafahamu maneno aliyoambiwa na mtoto wake akaona kwamba inawezekana kuwa ni uchungu wa kuzaa, lakini kwa kuwa haitajwi wazi kama ukiwa unamuuma bado mwenye mimba naye pia alimjibu maneno ya kumdanganya Bugonoka hakuyaelewa vizuri. (uk.280)*
>
> *...her mother understood at once that it was labour, but since it is forbidden to mention childbirth pain by name still in travail, she gave her an illusive answer and left her still engulfed in the darkness of her ignorance. (pg. 341)*

Katika jamii ya Wakerewe ni miiko kusema hadharani kwamba unahisi uchungu wa kuzaa. Ukiwa na maumivu ya kujifungua unaficha hadi ujifungue ndio unaanza kuwaeleza wenzako. Wakerewe waliamini ukisema mapema kabla ya kujifungua inawezakuwa bahati mbaya kwako umpoteze mototo. Bugonoka amemficha mama yake lakini mama alijua ni desturi ya jamii hii kutosema ukweli wakati mtu ana uchungu wa kuzaa.

Mf 23.

> *... basi kwa kufuata mila mgao wa kwanza ule wakampa mzee mmoja aliyekuwepo akainywa. Alipobakiza nusu,hapo mtu mmoja aliyekaa karibu na mzee Yule, alikodoa macho yake akamwambia mzee, "Nizawadi mzee, usiuawe na pombe."(uk.29)*
>
> *...and so the first measure of beer was given to an old man in the gathering. The old man drank until near the buttom of the drinking bowl and a man seated beside hime told him, "Don't kill yourself with beer! Leave some for me. (pg.43)*

Dondoo hili linaonyesha unywaji wa pombe katika sherehe za Wakerebe. Baada ya kuamua kesi kati ya Myombekere na Ntama kulikuwa na unywaji wa pombe katika mkutano. Pombe ya Wakerebe ilikuwa imetengenezwa kutokana na ndizi. Kwa mtayarishaji wa pombe ikiwa imeiva na sherehe imeanza ni desturi ya Wakerebe kwamba mzee mmoja hupewa kuonja kabla ya watu wengine kukaribishwa kwa

unywaji wa pombe. Ulikuwa ni utaratibu ulioheshimiwa na kuthaminiwa katika jamii hii. Desturi hii inapohawilishwa kwa utamaduni mwingine hufanya makabila mengine kuuthamini utamaduni wa wenzao.

Mf 24.

…Kunywa kwanza kidogo ndipo unipe au labda unaogopa usife… Lubona alipokwisha kumpa mama yake ile pombe ya ulogo (pombe ya kuondoa uchawi au sumu) kama iliyo desturi na hasa mila ya Abakerebe basi hapo ndipo alianza kugawa pombe. (uk.29)

"…You have to drink a bit first before giving it to me. Unless of course you know it is poisoned and you are afraid od dying." After Luboma gave his mother her "poison" share of the beer as Kikerewe custome dictates, he begun serving people in an orderly manner. (pg.43)

Aidha, desturi za Wakerebe waliamini kwamba mtayarishaji wa pombe alifaa kuonja pombe ili kuondoa sumu yaani wasiwasi wowote kabla ya kuanza kugawa kwa wanywaji pombe. Lubona anampa mamake ili kuonja kabla ya kuwakaribisha wengine kwa unywaji.desturi hii imeweza kuhifadhiwa kwa mataifa wengine kupitia kwa mchakato wa tafsiri.

Mf 25.

…ndiyo wamezidi kumkatalia lakini leo wamenipa maneno ya matumaini kama haya: baba mkweameniambia eti adhabu ya makosa ya jamaa zangu na yangu kwa jumla ni kulipa mitungi sita ya pombe ya ndizi na siku nitakapoipeleka pombe hiyo ndiyo itakuwa siku ya kuja na mke wangu. (uk.66)

…they are still retaining her, except this time I have brought back a good word from them and here it is: it appears my father inlaw wants me to appease him six pots of banana beer and the day I sent the appeasement beer will be the day I will come back with my wife.(pg.95)

Adhabu kwa ugomvi na kufarakana kwa wanandoa ilitolewa na wazazi. Pindi tu mwanamke amekosana na mume wake au familia ya mume wake na kurudi nyumbani kwao ilikuwa ni kazi ngumu kwenda kumchukua. Ilipobainika kwamba mwanume ndiye mkosa alikuwa anatozwa faini ya mitungi kadha ya pombe, mbuzi, ng'ombe au

kurudishiwa mahari aliyotoa kulingana na uzito wa kosa. Myombekere alikuwa ameenda kwao mke wake kumchukua na siku hii baba mke alimwambia alete mitungi sita ya pombe. Ilikuwa ni gharama kwake lakini alijihisi nafuu kwa sababu aliambiwa baada ya kulipa adhabu hii angeruhusiwa kurudi na mke wake. Adhabu hii kwa jamii ya Wakerebe ilisaidia kuwepo kwa nidhamu na heshima kwa wanandoa. Wanaume huopa kukosana na mkewe na kurudi kwao maana ni gharama kumrejesha. Uhawilishaji wa vipengele hivi vya utamaduni vimesaidia uhifadhi wa utamaduni katika hadhira lengwa.

Mf 26.

…nimekuita kukujulisha hivi siku utakaporudi hapa na mke wako, usisahau kuja pamoja na kuni za kabila moja ya mti mmoja, za kuzipikia dawa mtakayokuta nimekwisha kuileta tayari, pamoja na chungu kipya ambacho hakijapika chakula bado. (uk.152)

…I am calling you to tell you the following:when you come here with your wife, don't forget to bring firewood, all of which must be from one and the sama tree, together with a brand new cooking pot for cooking the medicine I will have prepared for you. (pg.199)

Suala la uzazi na ndoa katika jamii ya Wakerebe ni muhimu sana. Jamii husawiri uzazi kama alama ya baraka kwa wanandoa na kukosa kuzaa ni ishara ya laana kwa ndoa yao na jamii kwa ujumla. Kukosa kuzaa husababisha aibu hasa kwa mwanamke. Huweza kusababisha ugomvi na mtafaruku katika familia nzima. Wakati Bugonoka alikosa kuzaa wazazi wake walienda kumchukua kutokana na dhulma walizosikia anapitia katika ndoa yake. Wazazi wake walihisi kwamba alidharauliwa na ndugu na jamaa wa familia ya Myombekere. Siku alipobahatika kurudi nyumbani naye alianza safari ya kutafuta matibabu kwa waganga. Siku hii mganga anamuagiza kufuata mila na desturi za kuleta kuni kutoka kwa mti mmoja na chungu bado hakijapikiwa chochote. Hizi ni jitihada za kusetiri aibu iliyosababishwa na kumkosa mtoto. Dondoo hili linathibitisha jinsi Myombekere alivyoenda kwa waganga ili kuondoa

laana iliyosababishwa kwa kumkosa mtoto. Itikadi hii imesambazwa kwa utamaduni mwingine kupitia zoezi la tafsiri.

Mf 27.

….wakati wa kumkama ng'ombe, Lweganwa alikuwa anapiga mlunzi ili kumtuliza ngombe asifanye ujeuri. (uk.53)

….Lweganwa milked the cow while whisling a song all the time, which now and then breaking off to whisle to the cow a call for calm, to make the cow stand still and let its milk flow freely. (pg. 77)

Hizi zilikuwa ni mila na itikadi zilizoaminiwa na Wakerebe. Pindi tu mtu anapoanza kumkama ng'ombe walikuwa wanaamini kwamba ni sharti ng'ombe atulizwe kwa kupiga mlunzi. Hii ilikuwa njia ya pekee ya kumtuliza ng'ombe na kumfanya aachilie maziwa yake bila kisirani. Kupitia mchakato wa tafsiri imani hii imesambazwa ulimwenguni kote. Imani kama hizi za Wakerebe zimehifadhiwa kwa lugha ya Kiingereza kupitia taaluma ya tafsiri.

Mf 28.

...sasa mke wangu, kwa maana amekwisha kuwa mja mzito hivi anaweza kuwalilia wafu na kukaa matangani? Kibuguma akamjibu na kumwambia hivi, "Sasa kumbe sikuwaambia ya kwamba hawezi kwenda matangani na kulilia wafu mpaka kuzaa kwake; kama sikuwaambia vile, nilipitwa tu, nilikosea." (uk.234)

..,Can indeed my wife, the way she is now, still cry for and bewail aloud her dead relatives and go to her mourning?Kibuguma anwered him, "So I didn't tell you that she can't bewail aloud or attend mournings of her dead until after she has given birth? If that is the case, it was only an oversight on my part.(pg.289)

Jamii ya Wakerebe haingemruhusu mwanamke mja mzito kwenda matanga ya ndugu na jamaa wake. Angeruhusiwa tu kuhudhuria baada ya kujifungua. Pindi tu Myombekere alipopashwa habari kwamba shangazi yao amefariki alikimbia kwa mganga ili amshauri iwapo angeandamana na mkewe kwenda kuwaona waliofikwa na msiba. Ajabu ni kwamba Kibuguma alimkataza naye alitii maana walitaka kumuona mtoto wao. Desturi hii inapatikana tu kwa matini chanzi na inapotafsiriwa kwa lugha

nyingine huwa ni njia moja ya kusambaza na kuhifadhi utamaduni kwa hadhira lengwa.

Mf. 29.

Kibuguna alimwambia Bugonoka kuingia nyumbani na mzigo wake wa kuni na chungu chake, akaleta dawa iliyokatwa na tezo, akaitia katika chungu kipya kile walichokuja nacho, akamwaga maji mabichi ndani yake, dawa ikamezwa. Baadaye akamwambia Bugonoka ainue chungu cha dawa na kukiweka mafigani na kuipika dawa hiyo. (uk.153)

Kibuguna told Bugonoka to follow him inside his house with firewood and her new pot. Once inside, the healer brought medicine chipped with a chisel from a tree and put it in a pot the couple had come with and poured water in the pot until the medicine was completely covered. Then he told Bugonoka to place the pot on the cooking stones and cook the medicine. (pg.200)

Jamii ya Wakerebe ilikuwa na njia ya kusuluhisha magonjwa na matatizo mbalimbali yaliyowasibu. Kwa wakati huu jamii ya Myombekere imemtembelea mganga Kibuguna ili awasaidie kutatua shida ya kukosa watoto. Ilikuwa ni desturi kwamba kabla mganga hajakupa dawa ni sharti mgonjwa angeenda na kuni pamoja na chungu kipya cha kuchemsha dawa yake. Pindi tu mganga anawakaribisha nyumbani anawaomba kuni pamoja na chungu kipya. Baada ya kumpokeza anaweka dawa na kumwaagiza Bugonoka kukiweka chungu kile mafigani.

Aidha, uchemshaji wa dawa ulikuwa na masharti yake. Kibuguna alikuwa na njia ya kujua iwapo mgonjwa wake angeishi muda mrefu au angefariki baada ya kutumia dawa yake. Mila na desturi za uganga wake zilihitaji kwamba baada ya kuchemsha dawa itolewe nje ili nzi waikague.

Mf. 30.

Sababu yenyewe iliyompa Kibuguna kuleta sebuleni dawa hiyo iliyopikwa ni hii: dawa kama hiyo ikiangukiwa na nzi ndani yake akafa, hapo mganga anatambua kweli; mtu huyu mwenye kutibiwa hazitapita siku nyingi bila kufa! Tena kama dawa ya namna hiyo ilikuwa haikuangukiwa na nzi ndani yake akafa, hapo mganga

> *alikuwa anajua wazi tu mtu huyo mwenye kuaguliwa, ana bado siku nyingi za kuishi duniani. (uk.153)*
>
> *He ordered the pot of medicine to be brought outside the door so that should a fly fall into the medicine and die he would know that the person seeking cure from him does not have long to live and if no fly fell into the medicine and died he would know that his patient still had very long to live on this earth. (pg. 201)*

Siku hii mgonjwa wake wa kwanza ambaye ni Bwana Myombekere na bibi yake Bugonoka walikuwa na heri njema maana nzi hakufia ndani ya dawa yao. Kwa hivyo, walikuwa na siku nyingi za kuishi duniani. Hii ni mila na desturi ya jamii hii kuhusu masuala ya uganga.

Sheria za kuchuna dawa na kunyweshwa dawa ya miti shamba ingefanywa na mtoto msichana ambaye bado hajavunja ungo. Kibuguna ana mtoto msichana anayemsaidia kuchukua dawa kutoka msituni. Aidha, anamshauri Bugonoka amtafute mtoto msichana ili amnyeshe dawa.

Mf. 31.

> *Kibuguna akaeleza tena, Mtoto wa kike kama huyo ndiye anafaa kabisa kukunywesha dawa hii. Mtoto huyo utamfahamisha kuwa wakati anapopenda kukunywesha dawa hii, yeye pia inamlazimu uso wake uelekee upande wa magharibi, kwa hiyo mgongo wako na wa mtoto zielekeane na kugusana karibu karibu. (uk. 159)*
>
> *Such a child is the one who should hold this medicine for you to drink. And tell the young child that before making you to drink the medicine she should turn her back on you so that you are back to back. You will be sitting at the door of your house facing East and that child will be close to your back and holding in her hands the calabash of medicine for you to drink. (pg. 205)*

Desturi hizi zilikuwa ni hatua muhimu kwa shughuli nzima ya matibabu. Mgonjwa angetii sheria hizi ili kutatua matatizo yake.

Aidha, riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** imeshirikisha mila na desturi katika utunzi wake. Mila ni sehemu kuu ya maisha katika jamii ya Kiafrika.

Mf 32.

> ***…****hata ikiwa ni pombe ya kupeleka wakati wa kuoa, hakuna mtu yeyote angekubalika kutengeneza. Hiyo ilikuwa shida sana kwa wazee ambao katika mila za Wakikuyu ni lazima wapewe pombe wakati wa kuposa. (uk.32)*
>
> *…it was not even allowed for traditional purposes such as weddings. Anyone caught committing such an offence was taken to prison or slapped with a fine. This created a problem for the elders because in Gikuyu traditions, alcohol was an important part of the marriage negotiations and many other ceremonies. (pg.30)*

Si jamii zote zinazopenda na kuthamini pombe kama jamii ya Wakikuyu. Ilikuwa ni lazima kwa kila sherehe wazee wapewe pombe ya kienyeji. Katika muktadha huu ilikuwa ni desturi kuwa sherehe haingekamilika bila unywaji wa pombe na si kwa kila mtu bali ni wazee tu. Uhawilishaji wa mila kama hizi husambaza na kuhifadhi utamaduni huu kwa mataifa mengine.

Mf 33.

> *…lakini ilikuwa desturi mbaya kwa msichana kusema ana njaa na hasa mbele ya wanume. (uk.83)*
>
> *… but it was bad manners for a lady to say she was hungry, especially to a man. (pg.74)*

Utamaduni wa Kiafrika ulimruhusu mwanaume kutamalaki katika jamii. Mwanamke hakupewa uhuru wa kutawala nafsi yake na ya mume wake katika jamii. Mila na desturi nyingi zilimnyanyasa mwanamke. Utamaduni huu unahifadhiwa kwa mataifa mengine ili vizazi vijavyo vitakaposoma ukweli kama huu wataelewa na kufahamu hatua za ukombozi mwanamke wa Kiafrika amepitia. Haya yote yanawezeshwa kupitia mchakato wa tafsiri.

5.1.2.2 Imani ya Dini

Imani ya dini inaaminika kuwa njia mojawapo ya kuwaelekeza binadamu katika jamii. Kutafsiri dhana zinazohusiana na dini si rahisi kwa sababu dini ina uhusiano wa moja kwa moja na utamaduni. Newmark (1988) anasema kuwa utamaduni ni njia ya

maisha ya jamii fulani itumiayo lugha kama kifaa cha mawasiliano. Changamoto hii ya tafsiri hutokea kwa sababu kuna dhana zinazopatikana katika utamaduni chanzi na dhana hizo hazipatikani katika utamaduni lengwa. Kutafuta kisawe kinachoafiki hali hii inakuwa ni vigumu kwa hivyo mtafsiri analazimika kudumisha vipengele vingi vya imani ya dini katika mchakato wa tafsiri. Mwandishi wa MC2 ameshirikisha vipengele vingi vya imani ya dini.

Mf 34.

> *...sisi maskini makimbilio na maponeo yetu daima huwa ziwani. Kama* ***mugasa,*** *muungu wa bahari, akikupa Baraka zake, unaweza kupata faida ya kufariji kazi yako. (uk.81)*
>
> *...the succorer and last resort of the poor man is always the sea. When* ***mugasa*** *decides to smile on you, you get a catch enough to get you through your needs at the moment.* ***Mogasa*** *gave the catch. (pg.113)*

Kulingana na dondoo hili Wakerebe walikuwa na miungu mbalimbali ambao walishirikishwa katika mahusiano ya binadamu katika jamii. Maisha yako yakienda salama ukiwa mvuvi basi huyo huchukuliwa kuwa ni ***mugasa*** ambaye anaaminiwa kuwa Mungu wa bahari anayewabariki watu wake. Wakerebe waliamini kuwa ukikosa kuvua samaki wengi tena wakubwa bila shaka ***mugasa*** hajakubariki.

Aidha, riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** imetumia vipengele vya imani ya dini. Wahusika wanaamini kwa uwezo wa imani hii ya kidini.

Mf 35.

> *"...Uuui! Ngai. Ni kosa gani tumefanya hata ikatubidi kuadhibiwa hivi? Uuui uui uiuiui." Akajisemea mwenyewe baada ya Mumbi na askari kutoka nyumbani. (uk.77)*
>
> *"...Uui Ngai! What have we done to deserve all these suffering?"she said to herself, watching Mumbi and the Home Guardsas they left the compound...(pg. 68)*

Mama yake Mumbi anamtambua Mungu kwa jina la lugha yake ya kwanza Ngai. Wakikuyu walikuwa na njia ya kumtambua Mungu ambalo mara nyingi huwa vigumu

kulitafsiri. Askari wa miji walikuwa wamekimbizana na familia ya Mumbi hadi walikuwa wamekosa utulivu. Mama anamwita Mungu ili awaondelee mashaka haya. Jinsi Newmark amekili ni vigumu kutafsiri dhana hizi kwa lugha tofauti kwa sababu dhana hizi huwa na upekee wao. Imani ya dini hujikita katika muktadha na mazingira maalum.

5.1.2.3 Shughuli za Kazi

Kila jamii kulingana na mazingira wanamoishi hujishughulisha na kazi fulani. Walio na ardhi iliyo na rotuba hufuga wanyama na kulima aina mbalimbali za vyakula. Walio karibu na ziwa au bahari huvua samaki ili kukimu mahitaji yao ya kila siku. Jamii ya Wakerewe ni wavuvi kwa sababu wanaishi karibu na ziwa. Kwa misingi hii huwa na dhana mbalimbali kurejelea shughuli zao za kazi. Katika riwaya ya ***Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali*** mtunzi amejumlisha shughuli za wanakijiji katika utunzi wake.

Mf 36.

> *...Leganwa alikuwa hayuko, alikuwa amekwenda safari ya mbali pamoja na* ***abanyaga*** *(wawindaji wa viboko) akiwa nahodha wao wakati wa kuwinda. (uk.13)*
>
> *...Bugonoka's brother was not at home Leganwa, who was away from home on a hippopotamus hunting expendition as a rower for the hippopotamus hunters. (pg.21)*

Jamii ya Wakerebe ilienzi na kuthamini kazi kwa sababu ndio iliwapa mahitaji yao ya kila siku. Wanaume kwa mwanawake walitia bidii katika shughuli mbalimbali zilizowapa chakula. Nduguye Bugonoka Leganwa alikuwa ametoka nyumbani kwenda kwa shughuli ya kuwinda viboko wakati wageni walipoingia. Kazi hii ya ***abanyaga*** yaani wawindaji wa viboko ilifanywa na wanaume. Baada ya kulikamata windo wangegawa nyama ya kiboko na kuileta nyumbani ili iwe kitoweo. Dhana hii

inapotafsiriwa kwa utamaduni tofauti na kutolewa maelezo basi utamaduni huu uhifadhiwa kwa hadhira lengwa.

Mf 37.

> *…tulipofika kwa* ***omofumu*** *(mganga) akatuagua kweli. Wake wenzangu ramli hiyo iliwapiga mweleka chini, nyuso zao zikaiva kwa kuona haya. (uk.21)*
>
> *…when we all went to* ***omofumu*** *(diviner) together to know the truth, my husband's other wives were indeed revealed to be the culprits. (pg.28)*

Kila jamii huwa na njia mwafaka ya kutatua na kusuluhisha matatizo yao. Wakerebe walipokumbwa na shida ya magonjwa au changamoto mbalimbali maishani wangeenda kwa ***omofumu*** yaani mganga ili kuwagangua. Mganga aliheshimiwa kwa kazi aliyofanya. Walioenda kwake walipona kupitia kwa ganga ganga zake. Myombekere na mkewe walienda kwa mganga na shida yao ya ugumba kutatuliwa. Baada ya kujifungua watoto walipokumbwa na magonjwa mitishamba ya ***omofumu*** iliwaponya. Katika mazingira ya watu kuenda hospitalini kwa ajili ya matibabu inawawia vigumu kuelewa lakini baada ya dhana kutolewa maelezo inaeleweka kwa hadhira lengwa.

Mf 38.

> *….kumbe mji ule alimokwenda Myombekere kujikinga mvua, ulikuwa ni mji wa* ***omogimba*** *yaani mtengenezaji mvua. (uk.41)*
>
> *…as it happened, the home that Myombekere went was a home of omogimba a rain –maker.(pg.60)*

Omogimba ni mtengenezaji mvua. Wakerebe walitafuta suluhu kwa changamoto yoyote walikumbana nayo. ***Omogimba*** hutengeneza mvua baada ya kukabiliwa na kiangazi. Walikuwa wanaamini nguvu na uwezo wake. Siku hii Myombekere alikuwa njiani kuelekea kwa wakwe wake, akiwa njiani akakabiliwa na mvua na kuingia nyumba iliyokuwa hapo karibu. Alipoingia alishashangaa alijipata kwa nyumba ya

omogimba na kumpata anaendelea na shughuli yake**.** Mchakato wa tafsiri umesafirisha dhana hii kwa mataifa mengine na hii huwa ni njia mwafaka ya kuhifadhi utamaduni asilia kwa hadhira lengwa.

Mf 39.

...baada ya kutembea kidogo hapo pwani akaona mtumbwi wa ***abagonzo*** *(wavuvi wa samaki wakubwa) akawafua, na pale akawakuta watu wanaomjua. (uk.51)*

...he had walked only for a little while and was still by the lake shore when he saw a boat of ***abagonzo*** *fishermen landing and went to them. He found some acquaintances of his among the fishermen just landed. (pg.75)*

Abakerebe walizungukwa na Ziwa Victoria iliyowapa hifadhi na chakula chao cha kila siku. Kwa kawaida watu wanaishi karibu na bahari au ziwa hujishughulisha na uvuvi. Kutokana na mazingira yao wanaume Wakerebe walikuwa ***abagonzo*** yaani wavuvi wa samaki. Mlo wao uliandamana na kitoweo cha samaki. Uvuvi uliwapa aina mbalimbali za samaki. Nduguye Bugonoka alikuwa mvuvi hodari. Alijulikana kwa kuwakamata samaki wengi tena wakubwa.

Mazingira ya mtunzi yanaweza kukudokezea kazi ambayo wanajamii hujihusisha nayo. Kulingana na mifano iliyotolewa kutoka kwa riwaya, jamii ina taaluma mbalimbali. Kuna wale wanaoshughulika na uvuvi nao ni ***abagonzo***, kuna yule anayetengeneza mvua wakati wa kiangazi naye pia anaitwa ***omogimba.*** Aidha, kuna wanaowaeleza sababu za changamoto zao nao hujulikana kama ***omofumu.*** Shughuli hizi za kazi huwezesha wanajamii kuridhika na namna matatizo yao yanatatuliwa. Mtafsiri anapokumbana na dhana hizi za shughuli za kikazi humshurutisha atafute mikakati itakayomwezesha kutafsiri dhana hizo ipasavyo. Jinsi jamii zilivyo tofauti ndivyo dhana zinazoelezea shughuli za kazi zilivyo tofauti pia. Kwa kuhawilisha dhana hizi kasha maelezo kutolewa ni njia moja ya kuhifadhi utamaduni katika jamii tofauti.

5.1.2.4 Asasi za Kijamii

Asasi za kijamii kama vile elimu, ndoa mamlaka hudhihirisha utamaduni wa jamii husika. Asasi hizi hudhihirisha uhalisia unaotuwezesha kuona kwa undani na kuzielewa taratibu na mifumo tata ya makuzi ya watu katika jamii mahususi. Mashirika mbalimbali yanayotoa huduma kwa raia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Tofauti hizi vilevile huzua tofauti za kitamaduni. Katika riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** viwango mbalimbali vya mamlaka vimeonekana.

Mf 40.

***…**na kila mwenye asili ya kizungu, hata akiwa mtoto aliitwa na waafrika **'Bwana'** watoto wachanga waliitwa 'Bwana mdogo' na watu wazima waitwa 'Bwana Mkubwa'. (uk.61)*

*…anyone of white origin, even a child was addressed as **'Bwana'** by all Africans. Small children were addressed as 'Bwana Mdogo' (small Bwana) and adult whites as 'Bwana Mkubwa' (Big Bwana). (pg.64)*

Sehemu hii inaonyesha kuwa asasi ya jamii inayoshirikisha mamlaka wakati mwingine dhana zinazotumiwa katika jamii moja huwa ni ngumu kuitafsiri katika jamii nyingine. Mtafsiri katika dondoo hili amelidumisha neno Bwana ili kuleta wazi dhana ile inayowasilishwa na jamii husika.

Mf 41.

*…tumekataa kabisa kuwa chini ya serikali ya **mzungu.** (uk.51)*

*…we totally refuse to be under a **mzungu** government. (pg.44)*

Mzungu ni neno linalotumika kurejelea mkoloni alipokuwa katika nchi za Afrika. Wazungu wangewadhulumu Waafrika kiasi kwamba walifikia hatima ya kupinga na kukataa uongozi wao. Dhana hizi huwasilisha historia na utamaduni wa jamii husika ambazo mara nyingi si rahisi kutafsirika.

5.1.2.5 Burudani na Starehe

Kila jamii ina shughuli mbalimbali za kikazi za kujiendeleza kimaisha lakini pia wanatenga wakati kwa ajili ya starehe, mapumziko na burudani. Mikutano yao mbalimbali inandamana na nyimbo na sherehe. Shughuli hizi za starehe na burudani zinawaleta wanajamii pamoja na kukuza na kuendeleza historia yao. Watunzi wengi huwa wanashirikisha burudani hizi kwa kazi zao za kisanaa. Kitereza ni miongoni wa watunzi ambao wanaipatia kazi yao uhai kwa kuonyesha jinsi wanajamii wanavyoendeleza shughuli zao za burudani.

Mf 42.

> *...shemeji yako Lweganwa amekwisha kuoa, leo ndio tutakwenda kwao pamoja na ndugu yangu na vijana wote hawa* ***kuhika mu ka*** *na kesho asubuhi ndipo watahimiza kawaida zote za* ***kwich omwoyo*** *(uk.80)*
>
> *...your brother in law Lweganwa is already married. Today is the day for taking the bride to her parents' home for the bridal home coming and tomorrow morning she will be taken there again for their newlyweds* ***kwich omwoyo. (pg.111)***

Jamii ya Wakerewe ilikuwa na utaratibu wa kuanza na kukamilisha sherehe ya arusi basi ***kuhika mu ka*** ni sherehe ya kukamilisha kawaida za arusi; Bwana na Bibi arusi huenda kuwaona wazazi wa Bi. arusi. Mikutano hii inaandamana na sherehe na ushauri kwa wanaojitayarisha kuanza maisha ya ndoa. Aidha, baada ya shughuli zote kukamilika wanaarusi hupewa muda wa kutulizana baada ya taabu zote walizopitia katika maandalizi ya arusi yao. Muda huu ndio unajulikana kama ***kwich'omwoyo*** yaani kutuliza moyo baada ya taabu fulani. Dhana hizi huwa vigumu kutafsirika kwa sababu sherehe hizi hazipatikani katika utamaduni lengwa. Kwa njia hii basi utamaduni asilia unahifadhiwa kwa hadhira lengwa baada ya dhana hizi kutolewa maelezo ya kuwezesha hadhira lengwa kuelewa.

Aidha, wakati Myombekere aliporudi nyumbani na mkewe kulikuwa na burudani na sherehe zilizowasisimua wanakijiji wakaingia kupiga densi.

Mf 43.

…na alipotua sauti yak echini na kuimba chini chini kwa mkato hivi; Zenze, ***Zenze, Zenze Zenze, wee****, mara wakawaona wale vijana watatu wanavunja maungo yao sawa sawa pamoja kama kwamba angekuwa mtu mmoja mle mchezoni. Miili yao ilinyambuka kana kwamba hawana mifupa kabisa. Wanyaji pombe wote walianza kuwapigia makofi iliyotoa mlio kama huu:* ***pwapwa, pwa, kabatu, pwa****! (uk.114)*

…when Myombekere finally leveled off his voice and limited his song to snatches of: ***Zenze, Zenze, Zenze, Zenze, yee****, at once the three little males, together as if of one body, moved and danced as if they did not have a single bone in their bodies! Their audience rewarded them them with the clapping of their hands, the good neighbor of dancing, everyone clapping in rhythm:* ***pwapwa, pwa kabatu, pwa****! (pg.153)*

Baada ya Myombekere kupokezwa mke wake na kurudi nyumbani naye, walipata ndugu na jamaa, marafiki na majirani wakiwa wanawasubiri. Mapokezi yao yalikuwa ya kipekee. Myombekere alikuwa na raha moyoni kwamba amepokezwa mwenzi wake wa moyoni. Wimbo wa ***Zenze*** ulipendwa na wengi. Wote kwa jumla walianza kunyambua miili yao kana kwamba hawakuwa na mifupa. Usiku huu watu walicheza wakiwakaribisha Myombekere na Bugonoka nyumbani. Kwa kukosa kisawe cha kutafsiri wimbo huu, dhana yenyewe imetafsiriwa jinsi ilivyo kasha maelezo yametolewa ili kuwezesha mawasiliano katika hadhira lengwa.

Mf 44.

… ndipo akageuza wimbo akaanza kuimba wimbo mwingine uitwao ***Amalende.*** *Na wimbo huo aliuendesha akiimba na kucharaza kamba za zeze akifuatisha sawasawa na sauti yake nzuri iliyopendeza watu sana. Basi alifuatisha sauti ya kinanda na kuwataja wanawake wote waliokuwa warembo, wenye sura na umbo zuri waliokuwa wanaheshimiwa wakiwa hai hadi kifo chao.(uk.110)*

…and when Myombekere ended that piece he played the tune called ***Amalende****, the tune of a beautiful woman, and sang he song of the tune and emulated the beautiful woman of this earth, all the women whose beuty is sung from the first to the last. (pg.149)*

Jamii ya Wakerebe walikuwa na njia ya kipekee ya kufurahia na kuwa na sherehe. Wakati Myombekere alifanikiwa kumrudisha mkewe lilikuwa ni jambo la kufurahisha. Wote walikuja pamoja kwa ajili ya kumshukuru Myombekere na kumkaribisha Bugonoka nyumbani. ***Amalende*** ni aina ya wimbo uimbwao pamoja na zeze au ngoma wakati wa kutembea. Wimbo huu ulimhusu mwanamke mmoja aliyependeza kwa sura na kwa umbo.Wimbo huu ulipendwa na kufurahikiwa na wanawake na wanaume. Wachezaji waliposimama wenzao walianza kuwapongeza kwa kuwapigia makofi.

Mf 45.

….Nakazenze *wangu, wee, Nakazenze wangu mwenye sifa!*
Kutembea kwako: kwa ajabu, Nakazenze mwenye sifa!
Kuoga kwako: kwa ajabu, wee, Nakazenze mwenye sifa!
Nakazenze wangu,wee, Nakazenze na wageni!
Anapita njia ya bahari, Nakazenze mwenye sifa! (uk.113)

Nakazenzemy woman, yee! Nakazenze the good one!
When she walks people stop to admire her, Nakazenze the noble one.
Nakazenze my woman, yee! Hospitable to visitors.
She is arriving by sea, yee! Nakazenze the noble one. (pg.153)

Huu ni wimbo unaozungumzia sifa za mwanamke mrembo aitwaye ***Nakazenze***. Urembo wake umesifiwa ajabu kwa wimbo. Sifa zake za kuwapokea wageni zimebainisha. Kwa mpenzi wake ***Nakazenze*** alikuwa ni mwanamke wa ajabu. Wakerebe walimlazimisha Myombekere kuuimba wimbo huu maana hata wao uligusa hisia zao za ndani. Mazingira ya mtunzi humwezesha kutumia lugha kwa upekee wake ndio maana kazi ya eneo moja ni sharti itafsiriwa kwa lengo fulani jinsi nadharia ya Skopos inapoweka wazi. Mtafsiri anapojua lengo basi inamuwia rahisi kuteua mikakati ya kutumia ili kufanikisha zoezi la tafsiri.

Mf 46.

…Mukingira mla ulafi, mtoto wa ziwa Lyamonde
Mukingira wa Lyeboga, mtoto wa ziwa lyamonde
Mnywa pombe zote za nchi ya ziwa, Mkingira mla ulafi!

Samaki: mbete, samaki :mbozu, Mkingira mla ulafi!
Ulafi: nyama, samaki:nfuru, Mkingira mla ulafi! (uk.118)

Mkingira it is wrong to eat that way, child of lake Lyamonde
Mukingira, son of Lyegoba, child of lake Lyamonde!
For you the beer pot, for you the beer calabash,
For you embete, for you embozu,
For you the meat,for you enfuru!
Mukingira it is wrong to eat that way! (pg.158)

Wakerebe wangepitisha hekima na maarifa ya jamii yao kupitia kwa nyimbo zilizoimbwa katika sherehe mbalimbali. Bugonoka alianza kuimba wimbo huu wa Mkingira ili kuwashauri wanawake wachanga walionekana kubugia kila kitu bila kujali matumbo yao. Ndani mwa wimbo huu kuna ushauri unaowatahadharisha dhidi ya kula chochote. Japo wengi walipumbazika na wimbo huu, mama mzee mmoja aliwaeleza asili ya wimbo huu. Aliwaambia kwamba zamani kulikuwa na Mkingira aliyekula kila kitu bila kushiba. Maskani ya Mkingira yalikuwa katika kisiwa kiitwacho Lyegoba. Licha ya mtu huyu kula chakula kingi hangeshiba kamwe. Mwandishi amezungumzia uhalisia wa jamii hii kwa kueleza maisha jinsi yalivyo bila kuficha chochote. Sherehe za Abakerebe zinasambazwa ulimwenguni kupitia mchakato wa tafsiri.

Midundo kama hii ya nyimbo na densi haipatikani katika utamaduni mwingine kwa sababu wana njia zao mbadala za kuendesha shughuli kama hizi. Mchakato wa tafsiri umesambaza utamaduni huu kutoka utamaduni asilia hadi utamaduni wa kigeni kwa kuhawilisha dhana hizi jinsi zilivyo katika utamaduni wa Kikerewe.

Ili msanii kufanikisha ubunifu wake wa kazi ya fasihi amefuma kazi yake kwa kushirikisha utamaduni huu katika miktadha mbalimbali kwa kazi yake. Miktadha hii ndio huleta upekee katika utamaduni wa jamii husika. Ni wazi kwamba utamaduni wa kijamii unaoshirikisha mila na desturi, burudani na starehe na imani za dini hudhihirisha uhalisia wa kijamii katika miktadha yao ya kila siku. Uhawilishaji wa

vipengele hivi hufuata mikakati maalum ili kufanikisha mawasiliano kwa hadhira lengwa. Utaratibu huu huwezesha uhifadhi wa utamaduni kupitia zoezi la tafsiri.

5.1.3 Utamaduni Nyenzo

Kazi ya sanaa huwa ni kiwakilishi cha utamaduni mahususi ulio na dhana zilizo na upekee wake katika jamii husika. Ni jambo la kawaida kwamba kazi yoyote ya kifasihi haikosi kukitwa katika utamaduni nyenzo yaani, vifaa vinavyotumika na wanajamii. Vipengele vya kitamaduni katika jamii yoyote hufumbatwa kwa njia na kwa vitu tofauti kama vile vyakula, mavazi na vifaa vya kazi (Brisset, et, al 2012). Vifaa hivi huwa ni vitambulisho asilia vya maisha ya binadamu katika jamii. Aidha, Mgbemere (2014) anaeleza kwamba utamaduni wa nyenzo hurejelea vitu vinavyoonekana, raslimali na nafasi ambazo watu hutumia ili kufafanua utamaduni wao. Hivi ni pamoja na makazi, mavazi, viwanda, vyakula na vifaa vya kuzalisha mazao yao mbalimbali. Newmark (1988) amebainisha makundi matano ya utamaduni nyenzo: vyakula, mavazi, makazi na miji pamoja na taratibu za usafiri. Kulingana na migao ya Newmark utaratibu huu utajifunga katika kategoria nne za utamaduni nyenzo.

Jedwali 5.3: Vielelezo vya Utamaduni Nyenzo

Utamaduni Nyenzo	MC1	MC2
a) Vyakula na vinywaji	2	16
b) Vifaa vya kazi	4	25
c) Mavazi	2	6
d) Makazi na viwanda	2	6

Jedwali hili linaonyesha kuwa kuna matumizi ya utamaduni nyenzo matika matini zetu teule. MC2 imetumia tamaduni nyenzo kwa wingi kuliko MC1. Vyakula na vinywaji vimechukua takwimu za juu kuliko makazi na mavazi. Kategoria inayochukua sehemu kubwa hudhihirisha matumizi yao mapana katika jamii.

5.1.3.1 Vyakula na Vinywaji

Vyakula na vinywaji ni muhimu katika kudumisha uhai wa wanadamu katika jamii. Lugha, kama sehemu ya utamaduni, hutofautiana katika kusawiri vyakula na vinywaji kutoka jamii moja hadi nyingine. Kila jamii huwa na mifumo yao ya vyakula kutoka uandaaji, upishi wa vyakula, na vifaa vya kuandaa ulaji na unywaji wa vyakula hivi. Kulingana na Newmark (1988) vyakula na vinywaji ndio njia mojawapo ya kueleza utamaduni wa jamii fulani. Hii ni sehemu moja ya kutambulisha bara au nchi. Baker (1992) anahoji kwamba kauli zinazorejelea vyakula na vinywaji hazitafsiriki moja kwa moja kila wakati. Hii ina maana kwamba dhana za lugha chanzi hazijulikani katika lugha lengwa na kwa hivyo, zinamlazimisha mtafsiri kuzuka na mikakati maalum itakayofanikisha mchakato wa tafsiri. Riwaya ya ***Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali*** imesawiri maneno yanayohusiana na maandalizi ya vyakula na vinywaji katika jamii ya Wakerewe.

Mf 47.

> ***….****kwa wepesi Bugonoka akaingia nyumbani kuleta* ***Obwita*** *na chungu cha kitoweo. Chungu cha kitoweo kilikuwa kimefunikwa juu yake na* ***ekibo****, yaani kikapu kidogo kitumiwacho kuweka ugali. (uk.7)*
>
> *..In no time she was back in the house and out again with a dish of obwita too was covered by* ***ekibo****, just as the bowl of* ***obwita*** *was covered. (pg.9)*

Obwita ni aina ya chakula miongoni mwa wakazi wa Afrika Mashariki. ***Obwita*** ni chakula kinachoheshimiwa kwa thamani yake kwa wanajamii. Wakerewe pia wanatumia ***Obwita*** kama chakula kikuu. Myombekere alikuwa amewatembelea wakwe wake na kwa heshima na taadhima kuu walimtengenezea ***obwita.*** Kutafsiri dhana ya ***obwita*** katika utamaduni wa kigeni si rahisi kwa hivyo mtafsiri amedumisha dhana hii katika tafsiri yake. Uhawilishaji wa dhana hii katika utamaduni wa kigeni ni njia moja ya kuhamisha utamaduni kutoka hadhira chanzi hadi hadhira lengwa.

Mf 48.

> ***….****Bugonoka kwanza alitabasamu, halafu ndipo akasema, "Ee! Walinilisha nini maskini, ndiyo mchicha na mwata* ***(omusaga****) tu; labda ni mwili ndio umependa wenyewe." (uk.24)*
>
> *…Bugonoka smiled and said, "What could they slaughter for me, the poor people! I was eating nothing but* ***Omusaga*** *greens.(pg.167)*

Jamii ya Abakerebe walipenda kutumia mboga za majani kama chakula chao. Mboga hizi zingetayarishwa na kitoweo cha nyama au samaki ili kutumika pamoja na ugali. Majina haya ya aina mbalimbali za mboga yametolewa ufafanuzi ili kuwezesha hadhira lengwa kuelewa maana ya mboga hizi za kiasili.

Mf 49.

> *Basi mvua ya mwezi wa* ***Ekimezo*** *(Oktoba) ilipoanza kunyesha, Bugonoka, kwa kuwa alikuwa hodari sana wa kilimo, akaanza kulima kando kando ya nyumba yake, apate kupanda mle mbegu za vibuyu au maboga yaitwayo hivi:* ***mpwani, omusasa na omugobe*** *na mbegu zingine za kuzaa vitu kama hivi: kata, vibuyu na vinginevyo, walivyokuwa wakivipanda siku zile.(uk. 218)*
>
> *When the rains of the month of Oktober, the month of* ***Ekimezo,*** *germination begun pouring down from heaven, Bugonoka, the woman who loved farm work she was, turned to tilling close to her home a field for planting greens like* ***mpwani, omusasa na omugobe*** *and othe vegetables which bear gourds for making household calabash utensils. (pg.272)*

Bugonoka alipochukua mimba alianza kupanda aina mbalimbali za mboga za majani karibu na nyumba yake. Hali yake ya kiafya haikumruhusu kuandamana na Myombekere pale mbali kwenda kufanya kazi za shambani. Kwa hivyo, aliamua kupanda mboga kama: ***mpwani, omusasa,na omugobe.*** Hizi ni aina za mboga za majina zilizotumiwa na Abakerebe. Kwa sababu mazingira ya kiekolojia ni tofauti kutoka eneo moja hadi lingine, majina haya yamehawilishwa jinsi yalivyo kisha kutolewa maelezo. Hii ni njia moja ya kuhifadhi utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri.

Mf 50.

> *Bugonoka aliyaona mashamba yale ya viazi, akashangaa sana na akasema, "Viazi hivi mbona umevilima kwa moyo mmoja, kama kwa kusema, 'Jambo la nguvu za mwili wangu, litakalokuwa liwe tu!" Hapo aliinama, akachimba kwa kidole chake juu ya tuta penye shina la tembele liitwalo* ***kandoya*** *akakuta kiazi kimekomaa. (uk. 223)*
>
> *Bugonoka looked at the potatoes and exclaimed in wonder, "You really threw yourself into planting these sweet potatoes and said, 'Lets see what will happen!' Bugonoka bent down and dug at the roots of* ***kandoya*** *sweet potatoe vine with a finger and found underneath a mature sweet potatoe. (pg. 276)*

Abakerebe walikuwa wakulima wa aina mbalimbali za viazi. Bugonoka alipofika shambani alipendezwa na namna viazi vilikuwa vimenawiri kisha akapeleka vidole vyake na kuchimba. Aligundua kuwa viazi aina ya **kandoya** vilikuwa vimekomaa. Akajua kwamba basi vilikuwa tayari kwa mavuno. **Kandoya** ni aina mojawapo ya viazi vitamu vyenye ladha nzuri. Kupitia mchakato wa tafsiri aina mbalimbali za vyakula vimehamishwa kwa utamaduni lengwa. Kupitia njia hii utamaduni asilia umehifadhiwa.

Mf 51.

> *…Lweganwa na Myombekere wakawapa sehemu yao ya ugali na chungu cha kitoweo cha samaki waitwao* ***enembe.*** *(uk.81)*
>
> *…Lweganwa and Myombekere ate their separately which was obwita with a relish,* ***enemba****. (pg.112)*

Mf 52.

> *…baba yake akamjibu, "wacha mwanangu, kwetu usiku wa leo karibu tumeukesha tukinywa pombe ya* ***mpahe*** *(ndizi);labda na umande umetuingilia mwilini.*

Dhana zilizokolezwa ni aina mbalimbali za vyakula na vinyaji katika jamii ya Wakerewe. Katika mchakato wa tafsiri mara nyingi huwa vigumu kupata kisawe kinachodhihirisha uhalisia wa dhana inayotumiwa katika hadhira lengwa. Nadharia ya *Skopos* inasisitiza umuhimu wa mtafsiri kuelewa lengo la tafsiri. Kwa misingi hiyo, mtafsiri hushurutishwa kutumia neno lile lile na kulitolea maelezo baadaye au kutoa

ufafanuzi unaokaribia dhana yenyewe. Uwezekano huu husambaza utamaduni ulimwenguni na kuuhifadhi katika lugha mbalimbali kupitia mchakato wa tafsiri

Aidha, katika riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** kuna matumizi ya dhana zinazorejelea uhalisia wa vyakula na vinywaji katika jamii hii. Upekee wa mazingira hutumia dhana kwa umahususi wake ambazo si rahisi kupatikana katika muktadha mwingine.

Mf **53.**

*…. Kagwe alipika **ugali** wakala na kunywa kwa chai. (uk.21)*

…Kagwe cooked some ugali which they had with tea. (pg.20)

Ugali ni aina ya mlo unaotumiwa na kupendelewa na Wakenya. Makabila mengi nchini Kenya huthamini ugali kama chakula chao kikuu. Kagwe alikuwa ametembelewa na Meja Blue na chakula cha thamani ambacho angepikiwa na rafiki yake ni ugali. Inakuwa vigumu kutafsiri dhana hii kwa utamaduni wa kigeni kwa sababu hawana mlo huu katika mazingira yao. Mtafsiri anahawilisha kipengele hiki jinsi kilivyo na kisha kukitolea maelezo kulingana na nadharia ya *Skopos.*

5.1.3.2 Vifaa vya Kazi

Ili kuendesha shughuli zao za kijamii ipasavyo binadamu huzuka na mbinu pamoja na vifaa vya kufanikisha kazi zao. Vifaa hivi huwasaidia kutekeleza majukumu mbalimbali yanayofanikisha maendeleo yao. Watunzi wa kazi za kifasihi husawiri uhalisia huu wa vifaa vinavyotumika katika jamii kwa njia ya kipekee. Kitereza ameelezea uhalisia huu katika riwaya yake ya ***Bwana Myombekere Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali.***

Mf 54.

*…bugonoka alipofika karibu a miguu ya babake, akapiga magoti, akashika **isabuzyo** (chombo cha kunawia vidole, ni kama kimtumbwi hivi kilichotengenezwa kutoka katika mti wa **musayu.(uk.**7)*

> *... when Bugonoka got near his fathers legs, she knelt down got hold of a washbasin, dusted and wiped it clean and then welcomed her husband and her father to eat. (pg.8)*

Wakati Myombekere alienda kumchukua mke wake, wakwe zake walimuandalia chakula. Vifaa vinavyotumika katika maeneo haya ya Wakerebe vimefungamanishwa na mazingira na Muktadha wa Wakerebe. Kabla hawajala Bugonoka alipiga magoti ili kuwanavya wageni. Katika muktadha huu analazimika kutumia ***isabuzyo*** yaani chombo cha kunawia mkono kilichotengenezwa kutoka kwa mti. Ufafanuzi na maana yametolewa kuhusu chombo hiki ili hadhira lengwa ielewe.

Mf 55.

> *Kulipokucha, Bugonoka akaamka mapema, jinsi alivyozoea kusekua maziwa alfajiri sana. Alipotoka pahali pa kusekua maziwa, akaenda nje na* ***empiki*** *(chombo cha kuwekea moto). Alipotazama nyuma katika zizi la ng'ombe, akasikia sauti kama la ng'ombe aliyezaa akililia ndama wake, akasogea karibu aone ni nini, akakuta kumbe ni ng'ombe amezaa ndama wake wakti ule ule. (uk.167)*
>
> *Early in the morning the following day Bugonoka was up as usual, since it was the custome to churn milk very early in the morning. While still churning her milk, she got up from the churn with her* ***empiki*** *for scenting milk containers to fetch fire for putting in it from the courtyard fireplace. As she came out of the house and looked towards the kraal, she heard the cry of a mother cow calling for its calf and went near and found it was a cow which had just calved. (pg.216)*

Utamaduni wa Wakerebe ulikuwa na vifaa mbalimbali vya kutumika katika shughuli zao za kila siku. Ikiwa jamii ya wafugaji walikuwa na njia mbalimbali za kutayarisha maziwa yao. **Empiki** ni chombo cha kuchukulia moto na vijiti wa kufukizia vyombo vya kuwekea maziwa yawe na ladha nzuri.kifaa hiki kiliwasaidia kuandaa vifaa vya kuwekea maziwa yaliyo na ladha. Kupitia mikakati mbalimbali ya tafsiri dhana hii imeweza kuhawilishwa katika utamaduni lengwa.

Mf 56.

> *...kwa wepesi Bogonoka akaingia nyumbani kuleta ugali na chungu cha kitoweo. Chungu cha kitoweo kilikuja kimefunikwa juu yake na* ***ekibo*** *yaani kikapu kidogo watumiwacho kuweka ugali. (uk.7)*
>
> *... in no time she was back in the house and out again with a dish of obwita and a pot of relish, covered by a bowl, just as a bowl of obwita. (pg.9)*

Ekibo ni kikapu kidogo kilichotengenezwa kwa ajili ya kupakulia obwita (ugali). Enzi hizi Wakerebe hawakuwa na vifaa kama sahani lakini walikuwa na vifaa vilivyotumika katika mazingira yao. Uhalisia wa maisha ya Wakerebe umejidhihirisha namna mwandishi alivyofuma kazi yake kwa kushirikisha vifaa vya maisha ya kawaida ya wanajamii.

Mf 57.

> *...halafu akainua ekibo kilichosheheni ugali mpaka juu, akafuatisha chungu cha kitoweo na* ***olunanga*** *(chombo cha kupakulia kitoweo. (uk.7)*
>
> *...a nicely kneaded and rounded dish wth a well pointed head, and followed that by placing in front of them a pot of relish and a plate. (pg.9)*

Kulingana na madondoo haya kuna majina ya vifaa ambayo yamewasilishwa kwa njia ya kipekee. Maneno haya yanayotajia vifaa vinavyotumika katika mazingira ya Wakerewe, hayapatikani katika mazingira mengine. Kwa mintarafu hii, mtafsiri ameyatumia maneno haya jinsi yalivyo katika utamaduni chanzi na baadaye kuyatolea maelezo ya kijumla ili kumwezesha msomaji wa hadhira lengwa kufahamu kinachowasilishwa. Nadharia ya *Skopos* inasisitiza mtafsiri kutafuta mikakati mwafaka ya kuhawilisha vipengele vya kitamaduni. Katika muktadha huu, Mtafsiri amelazimika kutumia mikakati hii itakayomwezesha kudumisha na kuhifadhi utamaduni wa kiafrika katika mataifa ya kigeni.

Jamii ya Wakerebe walikuwa wavuvi hodari kwa hivyo hawangekosa vifaa mbalimbali vya kufanikisha uvuvi wao.

Mf 58.

> ***….****baadaye Leganwa akaenda baharini kuoga na kuchukua samaki katika* ***olubigo****. Alipofika kwenye mtego ule, akavua nguo yake, akachukua mkuki wa kuvulia samaki katika* ***olubigo*** *uitwao* ***omugera****, akateremkia kwenye ekitiro cha kwanza. (uk.51)*
>
> *…later on that day Lweganwa went to the lake to bathe and to see whether there was any catch in their* ***olubigo*** *fish trap. At the lake he took off his clothes and went into the water with his fishing spear to look for fish in* ***olobigo's*** *catch chambers. (pg.75)*

Jamii hii ilikuwa na mbinu na vifaa vya kuwasaidia kuwateka samaki. ***Olubigo*** ni kifaa cha kitamaduni kinachotumiwa kama mtego wa kuvulia samaki. Yalikuwa ni matete yaliyosimikwa majini karibu na ufuko kwa mviringo au mraba, samaki wakiingia hawatoki mpaka aliyewatega amewapata mle ndani. Kulingana na muktadha huu Lweganwa alikuwa amegatega na alienda kuangalia ni wangapi wameweza kunaswa. Kulingana na mchakato wa tafsiri vifaa hivi huwa ni vigumu kutafsirika kwa sababu katika utamaduni lengwa hamna kazi ya uvuvi na bila shaka hawana dhana kama hizi. Basi mtafsiri amehawilisha dhana hizi kwa utamaduni lengwa na kutoa maelezo ili kuzifafanua zieleweke na hadhira lengwa. Ufahamu huu mpana wa utamaduni wa watu wengine hufanya mataifa mengine kuthamini na kuheshimu utamaduni wa jamii nyingine.

Mf 59.

> *…ndugu yake alipokuwa akinawa vidole, Bugonoka alifungua ndama chapuchapu, kasha akaenda kuchukua* ***ekisahi.*** *Katika harakati hizo, Bugonoka alipotoka nyumbani tu, akakutana na Lweganwa akiangua* ***embohera*** *(kamba ya kufungia miguu ya ng'ombe wakati wa kuwakamua maziwa) (uk.53)*
>
> *…while his brother was washing his hands, Bugonoka quickly untethered a calf and then returned to the house to fetch* ***ekisahi****, coming back in no time with the wooden milk container and rejoining her brother, as he on his part got hold of* ***a cow leg tether****. (pg.77)*

Mf 60.

... mimi nilikuona unafanana kama umeuweka pale juu ya ***ekitwaro.*** *(uk.97)*

...I saw you putting it on top of that ***ekitwaro****. (pg.134)*

Jamii ya wafugaji huwa na dhana za kuelezea shughuli zao mbalimbali pamoja na vifaa vya kufanikisha shughuli hizi. Wakerewe ni wafugaji kwa hivyo hawakosi msamiati wa kuwafunga na kuwakama ng'ombe. ***Ekisahi*** ni chombo cha mbao kinachotumika kuwakama ng'ombe. Aidha, kamba ya kumfunga ng'ombe wanapomkama ni ***embohera***. ***Ekitwaro*** ni sanduku la gome au ganda la mti ambalo hutumika hasa na wanawake kwa kuweka ngozi za kuvaa na mapambo yao. Dhana hizi hazina visawe katika utamaduni lengwa. Mtafsiri amehawilisha utamaduni huu wa matini chanzi kwa hadhira lengwa na kutoa ufafanuzi wa kufanikisha mawasiliano.

Mwandishi wa ***Kaburi Bila Msalaba*** naye amesawiri vifaa vya kazi katika mazingira yake. Kwa sababu kilikuwa ni kipindi cha vita katika historia ya jamii hii basi alisawiri vifaa vya kupambambana na vita vya Mau mau dhidi ya mkoloni.

Mf 61.

….*serikali nayo ilikuwa yeyote kutoka Gavana mpaka walinzi wa nyumbani ambao walikubaliwa kuchukua mikuki tu. Kwa sababu hii waliitwa* ***'kamatimu'*** *yaani watu wa mikuki. (uk.92)*

Wakati wa MauMau Waafrika walijitahidi kupigania uhuru wao. Kwa kutumia silaha kama mkuki walipigana ili kurejesha ardhi ya mababu yao. Dhulma walizoshuhudia chini ya uongozi wa mzungu ziliwatimua kuishi msituni ili kumfukuza mzungu. Kila kuchao wangekula kiapo wakiongozwa na viongozi kama Meja Blue na kufunzwa jinsi ya kutumia mikuki yao. Dhana hii imechukuliwa moja kwa moja kisha maelezo yake kutolewa.

Mf 62

...Government meant anyone from the governor down to the home guards, who were only allowed to carry bows and arrows. This was why there were derisively known as ***'kamatimu'*** *that is 'spear-carriers'. (pg.93)*

...Kinaro aliwasha moto na mara oja akaweka karai *yenye maji moto. (uk.27)*

...Kinaro lit the stove and immediately placed a ***karai*** *with hot water on it. (pg. 28)*

Silaha za kivita ni anuai kulingana na utamaduni husika. Jamii hii ilikuwa inatumia mikuki kwa kupambana na adui wao. Neno ***'kamatimu'*** limepewa tafsiri ya moja kwa moja katika lugha ya Kiingereza kwa sababu halingepata kisawe chake katika utamaduni lengwa kwa sababu ya upekee wa silaha hizi za kivita. Ufahamu wa vifaa mbalimbali vya kazi katika jamii moja huwezesha jamii nyingine kuthamini na kuheshimu utamaduni wa ulimwengu wote. Kulingana na nadharia ya *Skopos* ni sharti kuwe na ushikamani katika lugha lengwa na katika muktadha wa kimawasiliano ambao matini lengwa itatumika.

Mf 63

....Kinaro aliwasha moto na mara moja akaweka ***karai*** *yenye maji moto. Yalipochemka, alitoa unga kutoka ndani ya* ***debe*** *alililoliweka mvunguni mwa kitanda chake, alitoa* ***buyu*** *la maziwa alililolitundika juu ya mti uliokuwa karibu na kichwa cha kitanda. Alitoa vilevile* ***vikebe*** *viwili ambavyo hapo zamani ilitumiwa kwa kutia kahawa au nyama za mikebe na mahabusu wa Kitaliano walioishi hapo Kiganjo. (uk.31)*

...Kinaro lit the stove and immediately placed ***a karai*** *with hot water in it. As soon as it started to boil, he got some maize flour from a container stored under his bed and started to make their meal of ugali. When the meal wasready, he brought out* ***a gourd*** *of milk from anather corner of the bed. He also brought out two old* ***tins*** *which once contained coffee or meat for Italian prisoners of war who had lived there at Kiganjo. (pg.29)*

Kinaro alikuwa ni rafikiye Meja Blue. Urafiki wao ulikuwa wa muda mrefu. Meja Blue alipotoka kijiji kuingi mjini alienda kwa nyumba ya Kinaro. Kinaro

alimkaribisha na akaanza kuandaa chakula. Vifaa vilivyotajwa katika dondoo hili ni vile vifaa vilivyotumika katika nyakati hizi ili kuleta uhalisia wa maisha. ***Karai*** ni chombo kilichotumika kupika ugali badala ya sufuri. Kwa kukosa kisawe mwafaka katika utamaduni lengwa mwandishi amehawilisha dhana hii jinsi ilivyo na baadaye kuitolea maelezo yake. Aidha, kuna ***buyu*** la maziwa linaliozungumziwa. Baada ya kupika Kinaro alileta ***buyu*** lililokuwa limebeba maziwa. Aidha, **mikebe** pia imetumika kumimina maziwa badala ya vikombe. Muktadha huu unaleta uhalisia wa maisha jinsi yalivyokuwa kwa wakati huo.

5.1.3.3 Mavazi

Kulingana na kipindi katika historia kila jamii huwa na mavazi yao maalum. Mavazi haya huwa na malengo maalum: mengine huvaliwa kujisetiri, mengine kuonyesha heshima, mengine katika sherehe maalum au kuonyesha utambulisho wa jamii yao. P. M. Kareithi katika riwaya yake ya ***Kaburi Bila Msalaba*** amefanikiwa kufumbata mambo aliyoyashuhudia wakati wa Mau Mau na utamaduni wa jamii yake katika kipindi hiki. Wakati wa ukoloni nchi nyingi za Bara la Afrika hazikuwa zimestaarabika kwa mavazi yao.

Mf 64.

*…watu wengi kwa kujua wangenyakuliwa vile, walianza kuvaa **'mahuthu'** yaani kabuti ndefu ambazo mtu angetumia kama nguo na blanketi pamoja.(uk.78)*

*…others wore long coats known as **'mahuthu'** in readiness for their inevitable arrest, because they would use them as blankets inside the prison cell. (pg.69)*

Mumbi anaeleza hali ilivyokuwa pale gerezani baada ya kujiunga na mahabusu wengine. Anasema kule ndani vyumba walimolala mahabusu vilikuwa vidogo sana ukilinganisha na hesabu ya watu walioishi humo. Kila kimoja kilikuwa kama futi nne kwa urefu. Katika kila chumba palilala watu zaidi ya kumi, wote wakilala sakafuni na

kujifunika nguo zao. Kutokana na hali hii waliofumaniwa ghafla na askari walivaa **'mahuthu'** wakijua kwamba aina hii ya nguo tena itatumika kama blanketi gerezani. Mtafsiri hakupata msamiati mwafaka kwa hadhira lengwa ndiposa akahawilisha neno hili jinsi lilivyo ili kuwasilisha maana ya utamaduni chanzi. Mavazi huwa na upekee wake katika utamaduni husika. Kila jamii huvaa kulingana na lengo fulani na kila jamii huwa na lengo tofauti. Huu ndio upekee wa utamaduni nyenzo kutoka jamii moja hadi nyingine.

Aidha, Kitereza katika riwaya ya ***Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali*** amesawiri mavazi yao kwa upekee wake. Wakerewe walikuwa wanatumia ngozi za ng'ombe kama mavazi yao.

Mf 65.

> *...Myombekere akavua vazi lake akampa mke wake, akapanda juu ya kitanda akalala. Bugonoka akalitandika vazi la mume wake kwenye lusika (kiambaza) halafu akaja upesi akalikung'uta vazi lake liitwalo* ***enkanda*** *(yaani ngozi ya ng'ombe iliyotengenezwa na kulainishwa kwa ufundi kabisa). Akamfunika mume wake, yeye kwa kuwa alikuwa amevaa obunelele (madodi) miguuni mwake. (uk.56)*
>
> *...Myombekere took off his cow skin robe he was wearing and gave it to his wife and she hung it on the house bulkhead as hiself climbed into the bed and lay down quickly. Bugonoka came and unfolded* ***enkanda*** *and covered her husband on her part she was wearing a lot of obunerere on herlegs. (pg.83)*

Katika enzi hizo kazi hii ilitungwa, jamii ya Wakerewe haikuwa na nguo bali wangetumia ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo kama mavazi yao rasmi. Kulikuwa na mavazi ya wanaume na wanawake. ***Enkada*** ni ngozi ya ng'ombe iliyolainishwa sana ili ivaliwe na watu hasa wanawake. Kupata msamiati huu katika lugha ya Kiingereza ni vigumu ndio maana neno hilo limedumishwa na maelezo kutolewa ili kurahisisha mawasiliano.

5.1.3.4 Makazi na Viwanda

Sehemu mbalimbali za makazi zinadhihirika kutoka jamii moja hadi nyingine. Makazi haya hutofautiana kwa namna yamejengwa, vifaa vilivyotumika na uamilifu wake katika jamii. Watunzi wengi wanapoandika kazi zao hawakosi kushirikisha mazingira ya makazi katika jamii zao. Kitereza ni miongoni mwa watunzi wanaosawiri hali hii katika ubunifu wao.

Mf 66.

> ***…****alipofika mjini tu, na baada ya kusalimiana na baba mkwe na mama mkwe na mke wake Bugonoka, mara akamwona shemejiye, Lweganwa akitoka katika* ***endaro*** *(kijumba chake) akaja kumwamkia (uk.42)*
>
> *…as soon as he arrived and finished exchanging greetings with his father in law and mother in law and his wife Bugonoka, his brother in law Lweganwa also came out of his bachelor house to meet and the two exchanged greetings. (pg.60)*

Katika muktadha huu Wakerewe walikuwa na vyumba mbalimbali na kila mmoja alikuwa amepewa chumba chake. ***Endaro*** ni nyumba ya kijana ambaye bado hajaoa kama Lweganwa. Utamaduni wao ulionyesha vijana ambao bado hawajaoa wanaishi kando na wazazi kwa ajili ya maandalizi ya maisha ya baadaye. Mchakato wa tafsiri umehawilisha utamaduni wa Wakerewe hadi kwa hadhira lengwa kwa kufafanua maana ya ***endaro.*** Kwa misingi hii utamaduni wa Wakerebe utakuwa umehifadhiwa kwa hadhira lengwa. Kwa mujibu wa kanuni ya Skopos, tafsiri ni tendo lililo na lengo au nia. Lengo la tafsiri ndilo linamwezesha mtafsiri kuchagua njia, mbinu na kanuni za kutafsiri ambazo hutumiwa ili kutoa tafsiri isiyo tata kwa HP. Kwa mantiki hiyo, mtafsiri amehifadhi vipengele vya kitamaduni kwa kutumia mbinu kama upanuzi maana au udumishaji wa dhana zinazopatikana katika mazingira tofauti kisha kufafanua maana yao.

Usawiri wa utamaduni katika kazi za kiubunifu hudhihirisha uhalisia wa maisha ya binadamu katika jamii. Maisha yao yanazungukwa na shughuli zao mbalimbali na vifaa vyao vya kufanya kazi. Hakuna fasihi itakamilika pasina kushirikisha vifaa hivi katika shughuli zao za kila siku. Utamaduni wa kijamii huwa na upekee wake kutoka jamii moja hadi nyingine. Wakati wa kutafsiri vipengele hivi ni muhimu mtafsiri kuangazia lengo la tafsiri kabla ya kuanza zoezi lenyewe.

5.2 Hitimisho

Sura hii imeangalia vipengele mbalimbali vya kitamaduni katika MC1 na MC2 na jinsi vinavyotumiwa kuhifadhi utamaduni katika jamii husika. Vipengele hivyo vilizungumziwa katika kategoria tatu ambazo ni: utamaduni wa mazingira ya kiekolojia, utamaduni wa kijamii na utamaduni nyenzo yaani, vifaa vya kijamii. Maneno yanayowakilisha dhana za kitamaduni hayatafsiriki kwa urahisi na hivyo basi humshurutisha mtafsiri kutafuta mikakati itakayomsaidia kuhawilisha utamaduni wa matini chanzi hadi kwa hadhira lengwa. Dhana hizi nyingi zilidumishwa katika matini tafsiriwa kisha maana na ufafanuzi wa maneno hayo kutolewa kwa hadhira lengwa. Nadharia ya *Skopos* ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu imeonyesha ni jinsi gani ushikamani wa maana katika MC umeafikiwa katika matini tafsiri. Ushikamani maana umeafikiwa kwa kumsaidia mtafsiri kuibuka na mikakati ya kutafsiri vipengele vya kitamaduni kwa njia isiyotatiza maana. Kupitia kwa mikakati hii utamaduni utakuwa umehifadhiwa kupitia kwa mchakato wa tafsiri.

SURA YA SITA

UHIFADHI WA VIPENGELE VYA KITAMADUNI KUPITIA MIKAKATI YA TAFSIRI

6.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia tumeeleza na kufafanua vipengele vya kitamaduni na namna vimeweza kuhawilishwa kutoka matini chanzi hadi kwa hadhira lengwa kwa nia ya kuhifadhi utamaduni asilia. Mikakati mbalimbali ilitumika ili kuafikia lengo hili. Katika sura hii mikakati mbalimbali imejadiliwa ilivyotumika kutafsiri vipengele hivi lakini ile tu ilivyochangia uhifadhi wa utamaduni kwa hadhira lengwa.

6.1 Mikakati ya Kutafsiri

Maendeleo katika tasnia ya tafsiri katika miaka ya awali, yalibadilisha mtazamo kuhusu dhana ya tafsiri na kutambua upana na mabadiliko yake. Kupanuka kwa taaluma ya tafsiri kumefanya mchakato wa tafsiri kujiegemeza zaidi kwa vipengele vya kitamaduni kuliko vipengele vya kiisimu. Katika mchakato wa tafsiri, maamuzi kuhusiana na uteuzi wa mbinu na mikakati ya kutafsiri yanaweza kushawishiwa na majukumu yanayokusudiwa kutekelezwa na tafsiri husika. Hali hii ni dhahiri tunapochunguza uamili wa tafsiri kama njia ya kuhifadhi utamaduni wa jamii husika. Wataalamu na wasomi mbalimbali wameandika na kutafiti mengi kuhusu mikakati ya tafsiri katika mchakato wa kutafsiri matini za fasihi. Kulingana na Pjuastuti (2004) anasema mikakati ya tafsiri ni njia au taratibu anazotumia mtafsiri katika kutafsiri maneno, vishazi na sentensi kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa. Ufafanuzi huu umejikita tu katika kuhawilisha ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine na wala si vipengele vya kitamaduni.

Newmark (2003) akitumia jina la taratibu za tafsiri, anaeleza kwamba taratibu za tafsiri ni mchakato wa kuhamisha sentensi na vipashio vingine vidogo kutoka lugha

chanzi kwenda kwa lugha lengwa. Anatumia dhana ya ‘taratibu’ kwa maana ya mikakati na kutoa mifano ifuatayo; utumiaji wa visawe vya kitamaduni, matumizi ya visawe vya kiuamilifu, tafsiri ya dhana, tafsiri ya kiutohozi, uhamishaji, unukuzi, upunguzaji na upanuzi. Molina na Albir (2002) wanaeleza kwamba mikakati ni taratibu (kwa kujua au kutojua, ya kusemwa au ya ishara) inayotumiwa na mtafsiri kutatua matatizo yanayotokea anaposhughulika na mchakato wa tafsiri akiwa na lengo mahsusi. Mikakati hii inaweza kuwa seti zilizopangwa kwa uangalifu mkuu na mtafsiri kwa ajili ya kuhawilisha ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine.

Mikakati ya tafsiri ni namna ya kufikia suluhu ya changamoto katika tafsiri (Fernandez 2012). Tafsiri ya vipengele vya kitamaduni ni jambo linalowasumbua watafsiri kwa matini zozote zile. Miongoni mwa changamoto wanazokumbana nazo ni ile miktadha ya kitamaduni ambayo inapatikana kwa MC lakini inakuwa vigumu kuihawilisha kwa ML. Hali hii hutokea hivi kwa sababu dhana hii haijulikani kwa hadhira lengwa au hamna kisawe mwafaka cha kukamilisha maana kwa hadhira lengwa. Kulingana na Nida (1964) tofauti za kitamaduni huzua changamoto zaidi katika mchakato wa tafsiri kuliko tofauti za mifumo ya lugha. Tofauti hizi za kitamaduni humshurutisha mtafsiri kuibuka na mikakati maalum ya tafsiri. Firoozkoohi (2010) anasema kuwa mtafsiri wa kazi ya fasihi anahitaji kusuluhisha mvutano baina ya usahihi na uzuri wa kazi tafsiri kwa kulinganisha mtindo wa kibinafsi wa lugha ya mwandishi wa LC na matumizi ya kawaida ya vipengele husika vya lugha katika LL. Dhana ya mikakati inaashiria kutoa suluhu hasa kwa vipengele vinavyofungamana na utamaduni wa jamii husika.

Aidha, Wafula (2007) anasema kwamba uteuzi wa mikakati hutegemea matini, lengo la tafsiri na hadhira lengwa. Uteuzi wa mikakati ya tafsiri kwa mujibu wa kaida za tafsiri, hufanyika kabla ya kuanza zoezi la tafsiri. Mtafsiri ni sharti afanye maamuzi ni

mikakati ipi itakuwa mwafaka kwa kazi yake. Uteuzi wa mikakati mwafaka katika mchakato wa tafsiri ni suala muhimu katika mchakato wa tafsiri hasa katika vipengele vya kitamaduni. Baada ya mtafsiri kuamua mwelekeo au lengo la kutafsiri matini, basi huwa anachukua hatua nyingine ya kuchagua mikakati ya tafsiri itakayofanikisha shughuli nzima ya tafsiri.

Baker (1992) anaeleza mikakati ya kutafsiri kama mbinu inayotumika kutafsiri kutokana na sababu kuwa lugha mbili tofauti hukosa visawe vyenye kuleta ulinganifu katika tafsiri. Ili kukabiliana na changamoto hii, Baker anapendekeza mikakati ifuatayo wakati wa mchakato wa tafsiri.

i) Kutafsiri kwa kutumia maneno yenye maana jumuishi. Badala ya kutumia neno ‘chamcha’ mtafsiri anaweza kutumia ‘chakula’ kwa kuwa ni neno jumulishi wala halibainishi wakati maalum wa kula chakula hicho.

ii) Kutafsiri kwa kutumia neno lisilo na dhana jumuishi (bila maelezo mengi). Iwapo mtafsiri angependa kutoa maelezo kuhusu dhana fulani basi maelezo yawekwe kwenye tanbihi.

iii) Kutafsiri kwa kutumia vibadala vya kitamaduni. Mtafsiri anatumia neno lingine katika utamaduni pokezi lenye athari sawa anapokosa neno linalofaa kutafsiri dhana fulani katika utamaduni asilia.

iv) Kutafsiri kwa kukopesha maneno, ambapo neno linaporudiwa rudiwa, maelezo yake hutolewa kisha mtafsiri atakuwa na uhuru wa kulirudia rudia neno hilo kwa kuwa tayari linaeleweka kwa hadhira pokezi.

v) Kutafsiri kwa kutumia fasiri ya neno linalohusiana kimaana.

vi) Kutafsiri kwa kutoa fasili; kwa kutumia maneno yasiyohusiana. Kutafsiri kwa kuacha maneno au sehemu ya matini asilia iwapo kile kinachofafanuliwa si muhimu sana kwa ujenzi wa matini au labda

kuchosha msomaji kutokana na maelezo mengi basi mtafsiri anaweza kupuuza maneno au maelezo na kufupisha sehemu hiyo.

vii) Kutafsiri kwa kutumia kielelezo. Kielelezo ni muhimu iwapo neno limekosa kisawe mwafaka katika hadhira lengwa.

Kwa ujumla, mikakati ya tafsiri ni njia, mbinu, taratibu zinazotumiwa na watafsiri ili kukabiliana na changamoto za kutafsiri matini kutoka LC hadi LL. Guerra (2012) alidai kuwa matatizo na changamoto za kutafsiri ni nyingi ila tu mtafsiri anapotumia mikakati mbalimbali humwezesha kukabiliana nazo. Utafiti huu umebaini kuchunguza mikakati iliyotumika kutafsiri matini teule kama njia ya kuhifadhi utamaduni kupitia kwa mchakato wa tafsiri. Ingawa mikakati mingi imebainishwa hapo juu, utafiti huu umeazimia kutumia mikakati minne kwa lengo la kudumisha na kuhifadhi vipengele vya kitamaduni katika hadhira lengwa. Jedwali lifuatalo linabainisha mikakati hii:

Jedwali 6.1: Mikakati ya kutafsiri kama njia ya kuhifadhi utamaduni

Mikakati ya kutafsiri	MC1	MC2
a) Ufafanuzu au upanuzi maana	10	150
b) Ujumuishaji wa dhana	0	12
c) Uhawilishaji	6	18
d) Muungano wa mbinu za tafsiri	0	14

Jedwali 6.1 limetoa mikakati ya kutafsiri ilivyotumiwa na wasanii wa MC1 na MC2 kama mbinu za kuhifadhi utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Kulingana na jedwali hili mkakati wa upanuzi maana umetumiwa zaidi kuliko mikakati mingine mitatu. Mbinu hii hupendelewa na watafsiri wengi wakati hakuna kisawe cha utamaduni katika utamaduni mwingine na pia huwa mwafaka wakati mtafsiri amebainisha lengo lake la tafsiri. Iwapo lengo ni kuhifadhi na kudumisha vipengele vya kitamaduni basi mkakati huu huwa mwafaka. Mikakati hii imefafanuliwa huku mifano yao ikitolewa kutoka matini teule.

6.1.1 Ufafanuzi au upanuzi maana

Mkakati huu huhakikisha istilahi au dhana inatafsiriwa kwa kutumia ufafanuzi wa umbo au uamilifu wake. Ufafanuzi maana ni kitendo cha kueleza kitu au jambo waziwazi kwa muundo wa maelezo mafupi ili kuiwezesha hadhira husika kuelewa kwa urahisi jambo linalozungumziwa. Kwa hivyo, mkakati huu unaweza kuchukuliwa kama njia ya kufafanua dhana kwa kuitolea maelezo ili ipate kueleweka zaidi kwa hadhira pokezi. Mtafsiri hutafsiri neno bila kutumia kisawe bali hutumia maelezo katika mabano au katika tanbihi. Ordudari (2007) anasema kwamba mkakati wa kutumia tanbihi huipa HP nafasi nzuri ya kuelewa matini tafsiri kama ilivyokusudiwa na mwandishi wa matini chanzi. Lengo la ufafanuzi maana ni kueleza maana ya dhana katika MC kuliko kuitafsiri. Hali hii huwa mwafaka wakati hakuna kisawe kitakachofidia maana katika matini tafsiri. Upanuzi maana husaidia kujiepusha na kupotosha maana au tafsiri pungufu. Aidha, mkakati huu umesaidia kukabiliana na tatizo ambapo hakuna visawe kwa vipengele vya kitamaduni. Mkakati huu wa upanuzi maana utaziba pengo la tofauti za kitamaduni baina ya lugha mbili na utasaidia kusambaza utamaduni kutoka lugha moja hadi nyingine.

Kwa mujibu wa Pembe (2010) dhana ya upanuzi maana katika mchakato wa tafsiri baina ya lugha mbili au zaidi hauepukiki. Hali hii hutokea kwa sababu ya tofauti kisarufi, kitamaduni, kimazingira na historia ya lugha husika. Kusudi kubwa la upanuzi maana katika tafsiri ni kuleta ushikamani wa maana katika matini chanzi na matini tafsiri. Maneno au ufafanuzi unaoingizwa haufai kuwa tofauti kabisa kidhana na habari asilia. Aidha, Chang (2012) anasema kuwa upanuzi maana ni mojawapo wa mbinu inayotakiwa kutumiwa na mtafsiri pale ambapo kuna uhitaji wa kuelezea jambo fulani. Mojawapo wa sababu za upanuzi maana ni kwamba kila lugha huwa na sarufi na tamaduni zake. Kwa hivyo, kuna uwezekano mkubwa kwamba jambo fulani

haliwezi kueleweka vyema baada ya kutafsiriwa bila ya kuongeza maneno ya ziada ya kulifafanua ili lieleweke vyema na HP. Watafsiri wa MC1 na MC2 wametumia mkakati huu ili kuafiki lengo la kuhifadhi utamaduni katika matini husika. Ifuatayo ni mifano kutoka MC2 na tafsiri yake.

Mf 67.

...baba yake akamjibu, wacha mwanangu, kwetu usiku wa leo karibu tumekesha tukinywa pombe ya ***mpahe (ndizi).*** *(uk.4)*

...to which her father responded, what indeed my child! We were drinking ***banana beer*** *almost the whole night. (pg.7)*

Katika utamaduni wa Kikerewe kulikuwa na unywaji wa pombe ya kiasili iliyotengenezwa kutoka kwa ndizi. Babake Bugonoka anamjulisha Myombekere kuwa wameshinda usiku wote kunywa pombe ya ndizi na ndio maana alihitaji kunywa maji ili kukata kiu yake. Dhana ya ***mpahe*** imetolewa ufafanuzi katika mabano na ilipotafsiriwa ilipata ufafanuzi kuwa si pombe nyingine bali ni ile itengenezwayo kutoka kwa ndizi. Kipengele hiki cha kitamaduni kimefafanuliwa ili HP ipate maana iliyokusudiwa katika MC.

Mf 68.

...katika chungu kile palikuwamo kitoweo kiitwacho ***obusanzage*** *(yaani nyama iliyokaushwa kisha ikapondwa sana kwa jiwe la kusagia mtama, ikawa laini. (uk.7)*

...on which to serve the relish, which was ***minced meat seasoned the Kikerewe way. (pg.9)***

Utamaduni wa Kikerewe umejidhihirisha kwa uwazi kupitia vyakula vyao na vifaa vinavyotumika katika maandalizi ya vyakula hivi. ***Obusanzage*** ni aina ya nyama iliyotumiwa katika mazingira ya Kikerewe ndio maana mwandishi amatoa maelezo yake kwa mabano ili kumsaidia msomaji wa utamaduni mwingine. Hii nyama ingetayarishwa kwa njia ya kipekee kwa wakazi wake ndio maana mtafsiri ametoa maelezo kuwa iliyotayarishwa kwa njia ya Kikerewe. Njia ya Kikerewe ni gani?

Ikaushwe, ipondwe kwa jiwe la kusiagia mtama ili iwe laini. Mkakati huu wa ufafanuzi maana umehawilisha maandalizi haya hadi utamaduni mwingine.

Mf 69.

...Bugonoka akaja amefuatana na mama yake, wakafikia kukaa katika kivuli cha ***kitara (****yaani kikapu cha kuweka mawele, mtama mwekundu, ulezi, mahindi n.k). (uk.7)*

...she came accompanied by her mother and the two of them sat down under the ***shade of a grain****. (pg.9)*

Si kawaida ya Wakerewe kuketi nyumbani na kufanya mazungumzo yao pale. Mara nyingi wangeketi chini ya mti au kama siku hii waliketi katika kivuli cha ***kitara.*** Kupitia kwa ufafanuzi wa uamilifu wa ***kitara*** mtafsiri alipata maana asilia naye akalitafsiri kutokana na maelezo yaliyotolewa katika mabano. Ufafanuzi maana huwezesha HP kuelewa mazingira ya hadhira chanzi na vifaa vyao vya kazi. Utamaduni huu wa Kierewe umehifdhiwa kupitia mchakato wa tafsiri.

Mf 70.

... yalipokwisha hayo, wakamwambia Bugonoka na kumhimiza "Ingia ndani upesi, ***ukatoe pembe lako la mzimu na ungo wako,*** *twende zetu tusifike usiku." (uk.8)*

That settled, Bugonoka's parents told her, "Go into the house and take out your ***tiny tray without*** *loss of time, so that we can be on our way back home, for we don't want to travel in the night." (pg.10)*

Ndoa ya Myombekere na Bugonoka ilipoingia doa wazazi wake walienda kwake kumchukua. Kawaida ya Wakerewe msichana anapoolewa hupewa **pembe na mzimu wa ungo** kama njia ya kubariki kizazi chake. Sasa Bugonoka anapochukuliwa wazazi wanamuagiza avichukue vifaa hivi aende navyo. Dondoo hili halijamdokezea msomaji ufafanuzi huu lakini katika tanbihi maelezo haya yametolewa kwa uwazi ili HP waelewe umuhimu wa vifaa hivi katika jamii husika.

Mf 71.

...hasa kabisa mawazo hayo yalimjia wakati aliposhika ***echachi*** *(ngozi ya ng'ombe ya kulalia). (uk.11)*

> *….he was tormented by thoughts throughtout the night thoughts which had started when he took his **cow skin bed**. (pg.18)*

Mchakato wa tafsiri kupitia mkakati wa ufafanuzi na upanuzi maana utakuwa umehawilisha kipengele hiki cha ***echachi*** kutoka Ukerewe hadi kule Magharibi watakapopata nafasi ya kusoma riwaya ya Kitereza. Watashangaa ni vipi ngozi ya ng'ombe itatumika kulalia lakini watajua na kuanza kuthamini utamaduni wa watu wengine ulimwenguni.

Mf 72.

> *…..palikuwapo nyumba nyingine hivi iitwayo **ndaro** (yaani nyumba ya kijana asiyeoa bado) ya ndugu mdogo wa Bugonoka, jina lake Lweganwa. Lweganwa alikuwa hayuko; alikuwa amekwenda safari ya mbali pamoja na **abanyaga** (wawindaji wa viboko). Uk.13)*

> *…in Namwero's home there was, besides his own house, another house of sorts, **the bachelors hut** of Bugonoka's brother Lweganwa, who was **hippopotamus hunters.** (pg.14)*

Kutokana na upanuzi maana ya ndaro na abanyaga HP imeweza kuelewa kwa uwazi maana ya msamiati huu. Msamiati huu haupatikani kwingine isipokuwa kule Ukerewe mahali kuna uwindaji wa viboko na nyumba ya mtu ambaye bado hajaoa nyumba yake huwa kando nay a wazazi. Utamaduni huu umesambazwa kutokana na mkakati huu wa upanuzi maana kutoka jamii moja hadi nyingine.

Mf 73.

> *…baada ya kula Myombekere alimwambia Nkwesi ampe **ekilangi** (tumbako iliyotiwa katika kibuyu. (uk.71)*

> *…after that he asked Nkwesi for some **ekilangi tobacco** and it was brought and given to him. (pg.101)*

Mf 74.

> *…toa nje buyu hilo, tulimimine katika **engunda** (kibuyu kidogo). (uk.85)*

> *…bring that big calabash of beer outside; I want to put some of the beer in this **engunda.** (pg.121)*

Mf 75.

….Bugonoka akaleta ***ekitwaro*** *(yaani chombo cha maganda ya magome cha kuwekea ngozi ya kuvaa)*

..Bugonoka fetched their **ekitwaro** *and took out both her clothes.(pg. 123)*

Mf 76.

….mama yake akamletea **enku** *na mafuta ya samli, akajipaka. (uk.98)*

….her mother then brought her daughter **enku** *and she anointed herself. (pg.135)*

Kulingana na madondoo haya bila upanuzi maana habari hii haingeeleweka na hadhira pokezi. Ufafanuzi huu umeweka dhana hizi kwa uwazi na japo hazipatikani katika mazingira yao hadhira inaweza kuwazia zinamaanisha nini. ***Ekilangi*** ni aina ya tumbaku iliyotiwa katika kibuyu inayochanganywa pamoja na maji na magadi inayotiwa puani. Wakerewe wanaume walikuwa wanatumia tumbaku hii wakati wa starehe na mapumziko baada ya kazi zao. Aidha, ***engunda*** ni kibuyu kidogo chenye mdomo mrefu cha kuweka pombe ya ndizi mtu huweza kusafiri nacho. Myombekere alikuwa anataka kutia pombe kwa ***engunda*** ili waweze kusafiri nayo hadi kwa wakwe zake. Bila maelezo haya katika mabano na mengine katika tanbihi bila shaka dhana hizi hazingeeleweka na HP. Mkakati huu umekuwa wa manufaa kwa kuhawilisha vipengele vya kitamaduni kutoka LC hadi kwa LL. Uhifadhi wa utamaduni umewezeshwa kupitia mbinu hii ya upanuzi maana.

Mf 77.

….mama yake akamletea **enku** *na mafuta ya samli, akajipaka. (uk.98)*

….her mother then brought her daughter **enku** *and she anointed herself. (pg.135)*

Bugonoka anapojiandaa kuenda kwake na mumewe Myombekere mamake alimtayarisha kwa kumletea vifaa muhimu kama ***enku*** aina ya ngozi ya ngombe iliyovaliwa kama nguo ya wanawake. Mtafsiri amehawilisha dhana hii jinsi ilivyo na

kuitolea maelezo baadaye. Inawezekana hii ndiyo tafsiri mwafaka hasa inapozingatiwa kwamba mazingira na miktadha mipya ya matumizi yake ni tofauti.

Sherehe za mziki na vyombo vya mziki huwa na upekee wake kutoka jamii moja hadi nyingine. Upekee huu huambatana na shughuli za binadamu. Wasanii wanapoandika kazi zao hawakosi kushirikisha sherehe za mziki katika kazi zao za ubunifu. Mara nyingi wasanii hudhihirisha uhalisia huu kupitia kazi zao bunilizi. Katika riwaya ya ***Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali*** uhalisia huu wa miziki na vyombo vya miziki umejidhihirisha kwa uwazi.

Mf 78

...mpe pombe nyingi ili aendele kutuchezea ***enanga*** *kwa kuwa tunataka kucheza. (uk.107)*

...give him more beer, so that he can keep on playing ***enanga;*** *we want to dance. (pg.150.)*

Myombekere alipomfikisha Bugonoka kwake ilikuwa ni sherehe ya kufana na kufurahikiwa na kila mtu. Wanakijiji walikuja kwa wingi ili kumkaribisha Bugonoka kwake ndiposa wanataka **enanga** ipigwe ili wacheze. ***Enanga*** ni aina ya zeze yenye umbo la kimtumbwi, huwa na kamba saba na huchezwa na Wakerewe wakati wa sherehe. Katika harakati ya kuhawilisha chombo hiki ya mziki mtafsiri ni sharti atafute mkakati mwafaka ili wakati anatafsiri maana ieleweke kwa hadhira lengwa. La sivyo ujumbe wake utapotoka. Mkakati huu wa upanuzi maana ni mwafaka kwa sababu ***enanga*** limehawilishwa jinsi lilivyo lakini ufafanuzi zaidi umetolewa katika tanbihi. Maelezo haya huwezesha mawasiliano na husaidia kuhifadhi utamaduni wa LC. Katika riwaya hii ya kitereza lengo lake la kuandika likiwa ni kuhifadhi utamaduni na historia ya Wakerewe dhana nyingi zilizotafsiriwa zimehawilishwa jinsi zilivyo kisha kutolewa maana katika mabano au katika tanbihi. Mkakati huu umetumiwa kwa wingi kama njia mojawapo ya kuhifadhi utamaduni wa jamii husika.

Aidha riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** nayo imetumia mkakati huu kwa njia ya kipekee ili kudumisha vipengele vya kitamaduni.

Mf 79.

> ***…****watu wengi, kwa kujua wangenyakuliwa vile, walianza kuvaa* **'mahuthu'** *yaani kabuti ndefu ambazo angetumia kama nguo na blanketi pamoja. (uk.78)*
>
> *…most had no blankets as they had been arrested at short notice and brought there. Others wore long coats known as '****mahuthu****' in readiness for their inevitable arrest, because they would use them as blankets inside the prison cell. (pg.69)*

Muktadha huu unadhihirisha hali ngumu ya wapiganaji wa mau mau. Mara nyingi wangechukuliwa kwa ghafla bila kupanga au kutarajia. Ili kukabilia na hali ngumu iliyokuwa gerezani wangejihami na ***mahuthu*** ili kujikinga dhidi ya baridi gerezani. Ili kuwasilisha maana ya dhana ya ***mahuthu*** maelezo ya ziada yametolewa ili kusaidia hadhira lengwa kutafakari uhalisia huu. Upanuzi au ufafanuzi maana huhawilisha vipengele vya kitamaduni kwa njia faafu kutoka hadira chanzi hadi kwa hadhira lengwa.

Mf 80.

> *…serikali nayo ilikuwa yeyote kutoka gavana mpaka walinzi wa nyumbani ambao wwalikubaliwa kuchukua mikuki tu kwa sababu hii waliita* ***'kamatimu*** *yaani watu wa mikuki. (uk.92)*
>
> *…government meant anyone from the governor down to the home gurds, who were only allowed to carry bows and arrows. This was why they were derisively known as* ***'kamatimu'*** *that is spear-carriers.*

Ufafanuzi maana umehawilisha dhana ya ***kamatimu*** kutoka utamaduni chanzi hadi utamaduni lengwa. Dhana hii imedumishwa kwa utamaduni lengwa kupitia kwa mkakati wa ufafanuzi maana. Vipengele vingi vya kitamaduni katika matini teule vimedumishwa kisha ufafanuzi maana kutolewa ili kurahisisha mawasiliano. Kulingana na mkabala wa nadharia ya *Skopos* tafsiri nzuri ni ile inayoruhusu hadhira lengwa kupata tafsiri yenye ushikamani na matini chanzi (Lauscher, 2000).

Ushikamani maana hufanikiwa kwa kuibuka na mikakati inayohawilisha vipengele vya kitamaduni kwa hadhira pokezi bila kutatiza mawasiliano.

6.1.2 Ujumuishaji wa Dhana

Mkakati huu hutumiwa wakati mtafsiri hutumia maneno ya kijumla zaidi au istilahi isiyo na mahusiano ili kutafsiri dhana za MC. Hali hii husababishwa na tofauti za kimtindo na kitamaduni katika HC na HP. Mkakati huu husaidia kuhifadhi vipengele vinavyofungamanishwa na utamaduni husika. Riwaya ya Kitereza imejumuisha dhana nyingi katika utamaduni wa hadhira pokezi.

Mf 81.

…*alipokwisha kukaa akaomba mtoto wake amletee maji ya kunywa. Bugonoka alipofika nyumbani akatwaa* **kata** *akaipangusa vumbi. Akafunua mtungi, akateka maji upesi akampelekea. (uk.4)*

…his daughter went inside the house and opened the drinking pot took ***a cup*** *for drinking water and beat his mouth agaist her hand to make sure it was free of dirt. (pg.9)*

Mf 82.

…Bugonoka alipofika karibu na miguu ya babake, akapiga magoti akashika ***isabuzyo****. (uk.6)*

…when Bugonoka got near his father's legs, she knelt down, got hold of a ***washing basin. (pg.8)***

Vyombo vya Wakerewe vilikuwa vimetengenezwa kutoka kwa udongo na kwa vipande vya mti lakini mtafsiri anapohawilisha dhana hizi kwa utamaduni lengwa anazingatia uamilifu wa vyombo hivi na kuvipa maana ya kijumla ili kurahisisha mawasiliano. ***Kata*** katika muktadha huu imepewa maana ya kijumla ya ***kikombe*** ilhali ile ya ***isabuzyo*** imetafsiriwa kama ***baseni*** ya kunawia mikono. Mkakati huu ni muhimu kwa kuhifadhi vipengele mbalimbali vya kitamaduni.

Mf 83.

*...kwa wepesi Bugonoka akaingia nyumbani kuleta ughali na chungu cha kitoweo kilikuja kimefunikwa juu yake na **ekibo** yaani kikapu kidogo watuacho kuwekea ugali. (uk.7)*

*...in no time she was back in the house, out again with a dish of obwita and a pot of relish covered by **a bowl**. (pg.9)*

Mf 84.

*...halafu akainua ekibo kilichosheheni ugali mpaka juu, akafuatisha chungu cha kitoweo na **olunanga.** (uk.7)*

*...a nicely kneaded and rounded dish with awell pointed head, and followed that by placing infront of them a pot of relish and **a plate**. (pg.9)*

Katika utamaduni wa Kikerewe ***ekibo*** ni kikapu kidogo cha kuwekea ugali lakini mtafsiri ameipatia dhana hii maana ya kijumla kwa kutumia maana ya ***'bowl'***. Bakuli kubwa la kubeba vyakula mbalimbali. Kwa misingi hii utamaduni wa Kikerewe umehifadhiwa katika lugha ya Kiingereza kwa kutumia mkakati huu wa kujumuisha.

6.1.2.1 Uhawilishaji

Mbinu hii kimsingi ni sawa na ukopaji ambayo hutumika pale ambapo neno au kundi la maneno kutoka LC huchukuliwa bila kubadilishwa kwa njia yoyote ile na kuingizwa katika LL. Mkakati huu pia umetambuliwa na watalamu wengine ambao wametumia istilahi tofauti tofauti ili kuurejelea. Petrulione (2012) anataja 'udumishaji' na 'urudiaji' kama baadhi ya majina yanayotumika ili kurejelea mkakati huu. Aidha, Pedersen (2005) anauita mkakati huu 'ubakizaji'. Kulingana na Newmark, mkakati huu ni mwafaka kwa majina halisi ya watu, mahali, maneno katika nyimbo, majina ya anwani za kazi zisizotafsiriwa miongoni mwa maneno mengine.

6.1.2.2 Majina ya watu

Majina ya watu katika fasihi huwa ni malighafi ya mwandishi anayoyatumia kuwaumbia wahusika wake kwa namna ya kuwafanya viumbe wa kuaminika katika ulimwengu wa fasihi. Uteuzi wa majina ya wahusika katika kazi bunilizi una maana kwamba majina yanatekeleza majukumu mengi kutegemea jinsi mwandishi alivyoyatumia katika kufanikisha kazi yake. Majina ya wahusika yanachangia uhalisia wa kazi ya fasihi, yanaweza kubeba umuhimu fulani wa kimaudhui au kijiografia au yanaweza kuwa kiungo cha kimsingi katika kazi ya sanaa. Ili kutafsiri majina ya wahusika katika kazi za fasihi ni lazima pawepo na uangalifu mkubwa. Mara nyingi majina haya hudokeza habari kuhusu jinsia, umri, asili ya mtu, maana mahususi, utajiri wa lugha na wa kitamaduni. Wahusika wanatumika katika kukuza maudhui na kudhihirisha dhamira ya mwandishi. Kwa hivyo, katika kutafsiri majina kunahitaji uangalifu wa makini ili kufaulu kuwasilisha ujumbe wa mwandishi ipasavyo. Kutafsiri majina ya wahusika kwa njia zinazotofautiana na jinsi yanavyokusudiwa katika kazi chanzi huweza kuchangia kazi potoshi katika kazi ya fasihi. Kuna hatari ya kutafsiri majina hasa pale majina hayo hayajafanyiwa utafiti wa kina kuonyesha kama ni majazi au yanabeba maana fulani.

Hervey na Higgins (1992) wanasema jina linaweza kuhamishwa moja kwa moja kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa bila kufanyiwa mabadiliko yoyote. Mtaalamu huyu anasisitiza kuwa inafaa majina haya yahawilishwe jinsi yalivyo bila kuyatafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine. Aidha, Newmark (1988) anasema kuwa majina ya kwanza ya watu yanahamishwa moja kwa moja na kwa hivyo, huweza kuhifadhi uraia. Hii hufanyika pale ambapo jamii huamini nomino za pekee huwa ni mwatiko wa utamaduni katika jamii mahususi. Riwaya teule katika utafiti huu zimehawilisha majina ya wahusika bila kuyabadilisha. Hii ni njia moja ya kudumisha utamaduni na

uraia wa jamii fulani. Katika riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** mwatiko huu wa utamaduni umejidhihirisha katika majina ya wahusika.

Mf 85.

*...**Mumbi** alipokuwa akiota jua, huku akiwatazama nzi na kufikiria vile alivyokuwa na njaa, chifu na askari wake walifika. (uk.1)*

*...As **Mumbi** basked in the sun, watching the flies and thinking about the hunger, the chief and his **askari** came along.(uk.2)*

Mf 86.

*…ama sivyo utaona wanchopata **Mau Mau** wengine. (uk.2)*

*…otherwise you shall see what other **Mau Mua** get! (pg.3)*

Mf 87.

*...**Meja Blue** na **Wahu** walikwenda kwa miguu mpaka karibu na Mugumo, yaani mti Mkubwa ulio karibu na shule ya Kiamwangi. (uk.19)*

*...**Meja Blue** and **Wahu** walked up to near the huge Mugumo tree that was close to Kiamwangi school. (pg.17)*

Katika muktadha huu mtafsiri alijua kuwa majina ya wahusika si majina tu bali ni majina yaliyofungamanishwa na maana katika muktadha maalum kwa hivyo hakuweza kuyabadili bali akayadumisha jinsi yalivyotumika katika matini chanzi. Kwa misingi hii utamaduni asilia umehawilishwa moja kwa moja kutoka HA hadi HP. Mkakati huu unawasaidia watu ulimwenguni kuelewa na kuthamini utamaduni wa jamii nyingine bila kupinga.

Kitereza pia katika riwaya yake amedumisha majina ya wahusika vivyo hivyo katika matini tafsiri bila kuyabadilisha hata kidogo. Udumishwaji huu huwasilisha uhalisia wa jamii fulani kama umesawiriwa na mwandishi wa kazi ya sanaa.

Mf 88.

*… **Myombekere** akaenda kwa **Kanwaketa** jirani yake… (uk.85)*

*...**Myombekere** went to the home of his neighbor **Kanwaketa**… (pg.89)*

Mf 89.

*...punde wakasikia **Namwero** akimuuliza mke wake, "Je, **Bugonoka** hajarudi bado? (uk.89)*

*...shortly after that they heard **Namwero** calling aloud his wife in the house and asking her, "Has **Bugonoka** not come back in that house? (pg.91)*

Mf 90..

*..Kesi ya **Myombekere** na **Ntamba** kwa Omokungu (Jumbe)…(uk.31)*

*…**Myombekere** is sued in the village court by **Ntamba**. (pg.34)*

*…**Ntamba**, anza wewe, sababu ndiwe ulikuja kumshtaki **Bwana Myombekere** kwa kulisha na kuharibu kabisa mtama wako. (uk.32)*

*…**Ntamba** go first, because you are the one who lodged acomplain against **Myombekere** for having grazed his cows in your millet crop. (pg.48)*

Kitereza aliamua kuwapa wahusika wake majina yaliyofungamana na maana ya jamii yao. Uhasisia huu umejidhihirisha katika jina ***Myombekere*** ambalo linamanisha uwezo wa mwanaume kuitafutia na kuikimu familia yake. Hili ni jina la kimajazi kwa kuwa ***Myombekere*** mwenyewe anajitahidi ili kufanikiwa katika familia yake licha ya changamoto wanazokabiliwa nazo. Aidha, ***Bugonoka*** ni jina la kimajazi linalomanisha mikosi au kisirani. Bugonoka alitaabika sana katika ndoa yake kwa kuchukua muda mrefu bila kujaliwa watoto. Majina ya watoto wao pia hudhihirisha ukweli fulani uliowazunguka kwa wakati huo. ***Ntulanalwo*** linamaanisha kifo ndiye rafiki yangu wa milele. Hili linatokea kwa sababu kulikuwa na mimba nyingi zilizotoka baada ya wao kufanikiwa kuwa na mtoto. ***Bulhawali*** pia huamaanisha ni lini taabu hizi zitakwisha kwa kuwa walikumbwa na mkuroro wa masaibu. Vivyo hivyo ndivyo majina mengi yametumika riwayani. Ukweli huu wa familia ya Myombekere ne Bugonoka hufumbatwa kwa matumizi ya majina ya majazi. Mtafsiri angeyatafsiri basi ujumbe wake asilia ungepotoka bila kuwasilisha maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Kwa kuyadumisha jinsi yalivyo katika matini asilia yamesaidia kuhifadhi ule upekee wa utamaduni katika jamii ya Wakerewe.

Mkakati huu wa uhawilishaji usaidia kudumisha vipengele vya kitamaduni kupitia mchakato wa tafsiri.

6.1.2.3 Maneno katika Nyimbo

Hakuna jamii ulimwenguni isiyokuwa na shughuli ya sherehe na burudani. Sawia na shughuli nyingine za kiuchumi vilevile za sherehe huwa na umuhimu na upekee wao. Wasanii wanapoandika hawakosi kushirikisha utaratibu huu katika kazi zao. Katika riwaya ya Kitereza shughuli hizi zimedhihirisha uhalisia wa maisha ya Wakerewe kwa njia mbalimbali kupitia kwa nyimbo. Sherehe zao nyingi ziliandamana na upigaji mziki na watu kucheza. Vipengele hivi vya nyimbo vikiwa na upekee wao basi mchakato wa tafsiri huwa si rahisi. Kwa hivyo, mtafsiri huzua mkakati wa kuhawilisha nyimbo jinsi zilivyo. Maneno yametafsiriwa moja kwa moja bila kubadilisha maana ya muktadha wa nyimbo kama yanavyodhihirika katika MC2.

Mf 91.

…Nakazenze wangu, wee, Nakazenze wangu mwenye sifa,
Nakazenzewangu wee, ***Nakazenze*** *na wageni,*
Anapita njia ya bahari, Nakazenze mwenye sifa,
(uk.13)

Nakazenze my woman yee, Nakazenze the good one,
Nakazenze my woman yee, hospitable to visitors,
She's arriving by see yee, Nakazenze the noble one
(pg.153)

Nakazenze ni mwanamke aliyependwa na kuenziwa katika jamii ya Wakerewe hadi akaimbwa katika miziki yao. Palipotokea sherehe hasa sherehe ya arusi jamii iliomba wimbo huu uchezwe ili waufurahikie. Pindi tu Myombekere alipomfikisha Bugonoka kwake ndipo sherehe ikaanza na watu waliomba wimbo wa Nakazenze. Mtafsiri hajabadilisha chochote katika wimbo bali hii ni tafsiri ya moja kwa moja kutoka lugha ya Kiswahili hadi lugha ya Kiingereza. Utamaduni wa Wakerewe umehifadhiwa katika wimbo huu na unaposambaza ulimwenguni kupitia mchakato wa tafsiri basi

wimbo huu huzifanya jamii nyingine kukubali na kuheshimu utamaduni wa watu wengine. Leppihalme (1997) anapendekeza kuhifadhiwa kwa jina lile kwa kulitumia jinsi lilivyo au kulitumia jina lile jinsi lilivyo na kisha kutoa mwongozo au kulitumia jina lile na halafu kutoa ufafanuzi wa utondoti.

6.1.3 Muungano wa Mbinu za Tafsiri

Kutafsiri vipengele vya kitamaduni mara nyingi huwatatiza watafsiri na wakati mwingine wanalazimika kutumia mikakati zaidi ya moja ili kuafikia malengo yao. Muungano wa mbinu za tafsiri hushirikisha matumizi ya zaidi ya mbinu moja ili kutafsiri dhana za kitamaduni. Ili kuwasilisha ujumbe vilivyo mtafsiri hulazimika kutumia mbinu zaidi ya moja katika tafsiri yake. Newmark (1988) anapendekeza kuwa mtafsiri anaweza kutumia mbinu mbili au muungano wa mbinu tatu katika kutafsiri kazi fulani. Ruhumbika (2002) ameshirikisha mbinu hizi katika tafsiri ya MC2. Matumizi ya mbinu mbili yamedhihirika katika tafsiri ya riwaya ya ***Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali.***

Mf 92.

"… baba aliondoka asubuhi kwenda baharini kuvua samaki katika mtego uitwao ***olubigo****, lakini kule amekwisha rejea, ati anataka amchonge mtumbwi. Tena mama, huyo amepeleka udaga wake katika* ***lukiri*** *kuanika; nadhani pia yeye yuko karibu kurudi!" (uk.13)*

"My father when he woke up this morning, went to look for fish in his ***olubigo*** *fish trap,but he has finished with that and has already come back. Now he has gone to work on the trunk of a tree he fell yesterday in his farm-lands yonder. I hear he wants to make a boat from it. As to my mother, she has gone to* **sun cassava** *on our* ***drying rock*** *and should be back any minute now." (Pg.19)*

Kutokana na dondoo hili mtafsiri ametumia mikakati miwili ili kutafsiri dhana hizi za kitamaduni. Ametumia mkakati wa uhawilishaji na upanuzi maana. Baadhi ya dhana zilizokolezwa zimehawilishwa jinsi zilivyo na kisha zingine zikatolewa ufafanuzi katika tanbihi. Maelezo na ufafanuzi husaidia hadhira lengwa kuelewa dhana ngeni

katika mazingira yake. Muungano wa mbinu za tafsiri umechangia kuhawilisha utamaduni wa Kikerewe hadi utamaduni mwingine. Mhimili mmoja wa nadharia ya *Skopos* unasisitiza kuwa sio lazima MC ifanane na ML. Utofauti huu wa *Skopos* husababishwa na tofauti za kimazingira, kijamii, kitamaduni na kihistoria. Kwa hivyo, msisitizo wa mchakato wa tafsiri upo katika uzingativu wa muktadha unaozunguka zoezi zima la tafsiri.

Ni dhahiri kwamba mikakati mbalimbali imetumika kutafsiri matini teulie. Kulingana na uchanganuzi huu mkakati uliotumika zaidi ni ule wa upanuzi maana. Dhana zilizotatiza mtafsiri alizitolea maana kwa njia ya ufafanuzi ili kusaidia hadhira lengwa kuelewa kinachozungumziwa. Mikakati hii ilitumiwa kwa lengo la kuhifadhi na kudumisha utamaduni asilia kwa hadhira lengwa.

6.2 Mhutasari wa Sura

Sura hii imeshughulikia mikakati ya tafsiri iliyochangia uhifadhi wa vipengele vya utamaduni katika MC1 na MC2. Kuna mikakati mbalimbali ya tafsiri lakini sura imejikita kwa ile mikakati tu iliyochangia uhifadhi wa utamaduni. Mikakati hiyo ni pamoja na: ufafanuzi au upanuzi maana, ujumuishaji wa dhana, uhawilishaji na muungano wa mbinu za tafsiri. Sehemu hii ilibainisha kuwa mikakati ya ufafanuzi maana na ujumuishaji imetumika zaidi kuliko mikakati mingine. Aidha, sura hii imebaini kuwa uteuzi wa nadharia ya *Skopos* iliafiki mahitaji ya lengo la pili katika utafiti wetu. Nadharia hii hudai kuwa ni lazima mtafsiri ajue na kuelewa lengo la tafsiri yake kabla ya zoezi la tafsiri. Baada ya kuelewa lengo atalazimika kuteua mikakati mwafaka itakayofanikisha zoezi zima la tafsiri. Kulingana na lengo letu la pili mikakati hii ilichangia kuhawilisha utamaduni asilia hadi hadhira lengwa.

SURA YA SABA

UDUMISHWAJI WA VIPENGELE VYA UJIELEZAJI UNAVYOFASIRIWA KAMA ITHIBATI YA UHIFADHI WA UTAMADUNI

7.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia iliangazia mikakati mbalimbali iliyotumika kuhawilisha matini asilia hadi matini tafsiri. Mikakati iliyojadiliwa ilikuwa ile tu iliyodumisha na kuhifadhi vipengele vya kitamaduni. Sura hii, inaangazia jinsi matumizi ya vipengele mbalimbali vya lugha yanavyochangia uhifadhi wa utamaduni katika matini teule.

7.1 Vipengele vya Ujielezaji

Wasanii wa kazi ya fasihi hutumia lugha ili kubeba dhamira, migogoro na ujumbe tofauti kulingana na kazi yao. Kipengele cha lugha ni muhimu kwani ndicho kinatofautisha fasihi na sanaa nyingine. Wamitila (2003) anasema kuwa mwandishi hawezi kusema analotaka kusema bila kutumia lugha. Lugha ni chombo cha kusafirisha mawazo ya mwandishi hadi kwa hadhira yake. Wasanii hawawezi kuwasilisha dhamira na maudhui yao bila kutegemea lugha. Wasanii wanajua kuteka na kuathiri hisia za wasomaji wao kwa kutumia lugha kiubunifu. Upekee wa masimulizi ya mwandishi hujitokeza kwa namna anavyotumia vipengele vya ujielezaji. Senkoro (2011) anasema kwamba tunapoangalia matumizi ya lugha tunazingatia vipengele vifuatavyo: misemo, methali, tamathali za semi na lugha ya wahusika hasa lahaja zao. Matumizi ya vipengele vya ujielezaji katika fasihi hulifanya wazo kutokea kwa udhahiri wenye mnato na usahihi.

Tamaduni zote za kila jamii ulimwenguni huwa ni hazina kuu ya mikusanyiko mikubwa ya mbinu za ujielezaji zinazotumika katika harakati za kila siku kama mbinu za kuwasilisha maarifa, tajriba, busara na hekima. Methali huwa ni mbinu mojawapo ambayo hutumika katika mazungumzo, mijadala na mitagusano mbalimbali katika

jamii. Mieder (2004) amehoji kwamba japo methali zinapatikana kote ulimwenguni kuna pia ukweli kwamba baadhi ya sehemu za ulimwengu zina ukwasi mkubwa wa methali kuliko nyingine. Mieder (2004) amethibitisha kwamba jamii za Afrika Magharibi zina ukwasi mkubwa wa methali zinazolinganishwa na jamii za sehemu za Marekani. Vipengele hivi vilivyotumika kutoka matini teule katika utafiti huu ni pamoja na: methali, tashbihi, jazanda, tashihisi, tanakali za sauti na majina ya majazi.

Jedwali 7.1: Vipengele vya Ujielezaji

	MC1	**MC2**
Methali	12	45
Tashbihi	6	22
Jazanda	4	12
Tashihisi	2	16
Tanakali za sauti	4	10
Majina ya majazi	2	6
Takriri	2	7

Kulingana na jedwali la 7.1 ni wazi kwamba waandishi wa fasihi hufuma kazi zao kwa kutumia vipengele mbalimbali vya ujielezaji. Kulingana na Miles (1971), vipengele vya ujielezaji ni kama uteuzi wa kisanii wa kibinafsi wa kila mtunzi. Kwa kijumla, matumizi ya vipengele vya ujielezaji huwa ni jinsi wasanii wanavyotumia lugha katika kazi za kiubunifu. Vipengele hivi huwa ni mbinu ambazo hutumiwa na mwandishi ili kuyaibua mawazo yake katika matini za kifasihi. Vipengele vya ujielezaji vinaweza kuhusisha mazoea ya mtu binafsi au lengo na azma yake. Hii ndio maana ambayo huwajia watu akilini wanapozungumza kuhusu vipengele vya ujielezaji vya mtu fulani au namna ya kuzungumza kwa kutoa hotuba hadharani. Wingi wa vipengele hivi vya lugha huongeza ladha kwa kazi fulani na hufafanua maudhui na dhamira kwa uwazi. Utafiti wetu ulichunguza vipengele vya ujielezaji katika matini teule lakini vile vipengele tu vinavyofungamanishwa na utamaduni husika.

Vipengele vya ujielezaji huwa na umuhimu mkubwa katika utunzi wa kazi ya fasihi. Vipengele hivi huchangia urembeshaji wa kinachozungumziwa au kurejelewa kwa lugha hiyo na kukifanya kiwe na mvuto mkubwa wa kisanaa. Aidha, vipengele vya ujielezaji hutekeleza jukumu la ufafanuaji na uelezaji wa kinachozungumziwa na kukifanya kieleweke kwa uwazi na wasomaji. Vipengele hivi vinapotumia huleta uthibati fulani wa jambo linalorejelewa katika miktadha husika. Kwa hivyo, vipengele hivi hushadidia maana, hupamba na kuongeza utamu wa lugha.

7.1.1 Matumizi ya Methali

Kila jamii husawiri mazingira yao kwa kutumia hekima na maarifa yapatikanayo katika methali. Katika tamaduni zote zinazotumia methali, kuna kauli zinazokubalika kwamba methali inapotumiwa kwa njia ya mvuto, lugha wazi yenye mnato huweza kupitisha maadili, imani na tamaduni za jamii husika. Methali huwa ni sentensi fupi ya jadi katika jamii mahsusi inayobeba busara, ukweli, maadili na mitazamo ya kijadi ambayo inawasilishwa kwa njia ya kistiari, kwa muundo dumifu unaoweza kukaririwa kutoka kumbukizi na unaopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Mieder 1993). Kulingana na mawazo haya methali hufumbata maarifa ya kawaida, tajriba, busara, hekima na ukweli wa maisha katika jamii. Methali hushawishi wanajamii kuangalia na kutilia maanani kanuni za kimsingi zinazokubalika na kutambulika katika tamaduni mahsusi.

Methali hubuniwa na kukuzwa kutoka kwa tajriba na miktadha ya kitamaduni. Mbinu hii ya ujielezaji hutumiwa na wanajamii ili kuonyesha busara yao na kukuza migogoro yao katika kazi za fasihi. Methali inapotumiwa katika kazi ya fasihi huwa inahawilisha tajriba pana ya maisha ya binadamu, huonyesha kipaji cha uelewa wa dhana mbalimbali za maisha na husisimua upokezanaji wa maarifa miongoni mwa wanajamii. Migogoro inadhihirika kwa uwazi katika methali kwa kuwa ni kupitia fani

hii ambapo imani, mila, desturi na itikadi za kijamii hujitokeza. Kwa kawaida kubuniwa kwa methali huchochewa na utamaduni wa jamii husika na vichochezi hivi hujidhihirisha katika methali. Hakuna kazi ya fasihi inayokamilika bila kushirikishwa aina mbalimbali za methali. Kwa kawaida methali hainyunyuziwi tu kwenye riwaya bali kwa ubunifu mkubwa. Methali hufinyangwa na kushirikishwa katika usimulizi kwa kiasi kwamba inaishia kuwa sehemu ya usimulizi. Aidha, Norrick (1985) anadai kuwa methali ni utanzu wa kijadi wa maongezi na ufunzaji maadili ulio na maana ya jumla, ulio na uwezo wa kutumiwa katika maongezi ya kupokezana na mara nyingi hupokezanwa kisitiari na kijazanda.

Kwa mujibu wa Abbas (2015), ni vigumu vipengele kama utamaduni na desturi za kitamaduni kutafsirika hasa kama mtafsiri anataka kudumisha muundo na muonjo wa methali asili. Muundo na muonjo wa methali hufungamana katika miktadha ya kitamaduni ya jamii fulani. Kila wakati ni muhimu mtafsiri aangazia utamaduni wakati wote kuliko kuangazia sifa za lugha nje ya muktadha. Methali zilizofungamanishwa na imani za kidini na desturi za watu haziwezi kutafsirika moja kwa moja kwa sababu maana ya kitamaduni huweza kupotoka. Inabidi kutumia methali katika lugha lengwa yenye uwezo sawa na ule unaotolewa katika lugha asilia.

Kutafsiri methali katika kazi za kifasihi ni uhalisia unaojibainisha katika hali changamano ambamo mtafsiri anakuta kwamba methali husika haiwezi kutafsiriwa nje ya miktadha ilimotungiwa wala kupuuza uamili uliokusudiwa na jamii asilia. Tafsiri zote za methali zinazopuuza ukweli huu zinaweza kuibua makosa ya aina mbalimbali yanayoweza kuishia kupotosha maana na mawasiliano ya kifasihi na vile vile kuibua uwezekano wa kudhoofisha usanifu wa kazi lengwa. Ghazala (1995) anadai kwamba methali ni vipashio vya kipekee vya kaida za lugha visivyobadilika na ambavyo vina maana zisizobadilika. Sifa hii ya methali hudhihirisha sifa dumifu

yaani inayomshurutisha mtafsiri kuidondosha methali husika jinsi ilivyo au kufafanua maana iliyofichika ndani ya methali yenyewe. Sehemu inayofuata imejadili matumizi ya methali inayodhihirisha udumishwaji wa vipengele vya kitamaduni kutoka MC1 na MC2.

Mf 93.

...*Mwenye chake havunjwi mkono. (uk.19)*

When what you have is really yours and you didn't steal it you run no danger of having your arm broken for it. (pg. 27)

Katika dondoo hili Myombekere amekutana na mwanamke mrembo baada ya mke wake Bugonoka kurudi kwao. Katika safari yake ya kurejea nyumbani amekutana na mwanamke mwingine na kuanza kumposa. Methali hii inamtoka anaporejelea kauli anazotaka kuzitoa ili kumshawishi mwanamke huyu ampende na kumkubali. Katika utamaduni wa Wakerewe humshurutishi mtu kukupenda bali kupitia kwa ushawishi wako anashawishika ndio maana anasema kwamba, ***mwenye chake havunjwi mkono.*** Ili kusisistiza uhuru alio nao mwanamke kukubali au kukataa mwanaume anapotoa posa.

Mf 94.

Mwanamke ni kama ***enamba****, mwanamke haanzi kumposa mwanamume shuruti mwanamme amwanze. (uk.19)*

A woman is like the men's fish ***enamba*** *in the sea, to be got only by he who plunges his fishing spear in the waters. (pg. 27)*

Dondoo la 95 linathibitisha kwa uwazi kwamba methali hufumbata mazingira na itikadi za wanajamii. Kawaida ya Wakerebe katika harakati ya kumposa mwanamke si eti ni mwanamke anaanza bali ni mwanamume anaanza kumposa mwanamke. Ni miiko wakati mwanamke atanzisha shughuli hii. Ukwehi huu umeletwa wazi kupitia kwa matumizi ya methali. Adha, mazingira yao yamesawiriwa, kwa upande mwingine tunajifunza kuwa hii ni jamii ya wavuvi kwa sababu ndani ya methali samaki aina ya

enamba imetumika kwa kumlinganisha mwanamke. Ili kupata muktadha wa methali methali yenyewe imetafsiriwa kwa kutolewa maelezo.

Mf 95.

> *Yule mwanamke akavunja mbavu kwa kucheka (maana ya maneno hayo ya Kikerebe ni: pahali akutapo Omukama amekaa, ndipo hapo atamuamkia kwa heshima na adabu. (uk.19)*
>
> *...where you meet a woman you should court her for as our ancestors put it, "You pay homage to the throne wherever the king happens to be."*

Methali hutumika katika miktadha ya kila siku jiinsi ambavyo Myombekere anavyoitumia katika mawasiliano yake na ya mwanamke aliyekutana naye njiani. Kupitia kwa methali hii tunaelewa mifumo ya kiutawala katika jamii hii. ***Omukami*** ni mfalme aliyetawala himaya ya Wakerewe. Jamii ilimheshimu kama raisi wao. Utamaduni wa Kikerewe umehawilishwa kwa hadhira lengwa kwa matumizi ya methali hii iliyo na vipengele vya kitamaduni.

Mf 96.

> *...Kumbe! Ndiyo maana wajuzi walisema, Jitambulisheni mapema koo zenu, kabla ya kuuana. (uk.29)*
>
> *.....Now I see our people said, before you kill each other know each others clans and relatives. (pg.39)*

Methali hii inasisitiza umuhimu wa kujuana vizuri na ndugu na jamaa. Wakerewe walithamini ukoo wao ndio maana wakiwa katika vikao walitaka kujua watu waliokuwa wamehudhuria mkutano. Baada ya ng'ombe wa Myombekere kula mtama wa Ntama waliingia kwa baraza la wazee ili wajue ni nani alikuwa na hatia. Katika vikao kama hivi mjumbe angetumia methali iliyosheheni hekima na maarifa ya jamii yao. Methali inaonyesha umuhimu wa jamii ya Wakerebe kuthamini umoja na ushirikiano wao katika shughuli wanazotekeleza. Mtafsiri naye amehawilisha maana kwa njia ya moja kwa moja ili kurahisisha mawasiliano kwa hadhira lengwa.

Mf 97.

... Sikillizeni mabwana! Abakerebe walisema, mahali walipo na pombe ya ndizi, hapafichi siri. (uk.31)

...ladies and gentlemen the pot of banana beer is the boom companion of conversation. (pg.36)

Kupitia kwa methali hii tunafahamu kuwa Wakerebe ni wakulima wa ndizi na utengenezaji wa pombe yao hutegemea kilimo cha ndizi. Methali imefumbata utamaduni wa kiekolojia kwamba Wakerewe walithamini pombe ya ndizi. Kesi ya Myombekere na Ntama ilikuwa inasikizwa kwa mjumbe na itikadi yao ilihitaji kwamba sharti watu wawe na pombe. Jamii iliamini kuwa baada ya mtu kunywa pombe ya ndizi siri zote hufichuliwa na mgogoro baina yao husuluhishwa kwa urahisi. Wakerebe wanakuja pamoja kunywa pombe katika vikao vyao kama njia mojawapo ya kupalilia umoja na ushirikiano wao.

Mf 98.

...Wewe husikii daima watu wakisema methali hii; Sote tunalingana lakini kupitana maarifa huwa tunapitana? (uk.43)

...Have you never heard the proverb; we are all equal is only a manner of speaking?

Baada ya Myombekere kujikinga mvua katika nyumba ya mtengenezaji mvua aliweza kushuhudia mkasa uliomshtua. Aliponusurika na wengine waliokuwepo anasimulia kisa chenyewe kwa baba mkwe ndipo naye anamtolea methali hii akimweleza kuwa sote tunalingana lakini kimaarifa tunatofautiana. Baba mkwe alikuwa anadhihirisha tofauti za watengenezaji mvua. Kusema tu watu wanaweza kusema wanapatana lakini wakitofautiana kimaarifa kamwe hawapatani. Wakerewe wanatahadharisha wanakijiji kuwa macho na wenzao. Methali imetumika kuwasilisha umuhimu wa mahusiano miongoni mwa wanakijiji. Baba mkwe anamtahadharisha Myombekere kuwa kuna watengenezaji mvua hodari na wengine hawafanyi kazi yao ipasavyo.

Mf 99.

…Sababu wahenga walisema, "Mzazi hatapiki ila huchukizwa tu."(uk.49)

…because our ancestors said, "The parent never vomits, however disgusting the child is." (pg. 53)

Dondoo hili linaonyesha Myombekere alipofika kwa baba na mama mkwe ili kuomba msamaha kwa makosa yaliyompata akiwa anaishi na mke wake Bugonoka. Anakiri kwamba alifanya kosa na sasa anaomba msamaha. Anamuomba baba mkwe amsamehe na amhurumie kwa kupa mke wake ili waendelee kuishi pamoja jinsi walivyokuwa wakiishi tangu walipofunga ndoa. Myombekere anatumia methali hii ili kusisitiza umuhimu wa msamaha kati ya watoto na wazazi. Jamii ya Wakerewe walienzi na kuthamini maisha ya watoto wao katika ndoa. Walielewa kwamba hii ndio njia moja ya kuendeleza kizazi chao. Wazazi wa Bugonoka walikubali kumsamehe mtoto wao lakini wakamwambia alipe adhabu ya miyungi sita ya pombe ya ndizi. Kupitia kwa maelezo na ufafanuzi wa methali hii, utamaduni huu wa itikadi ya Wakerewe kuhusu malezi ya watoto wao umehawilishwa kutoka hadhira asilia hadi hadhira lengwa.

Mf 100.

….Wakerebe husema, mfanya kazi ndiye mpata chakula. (uk.74)

…..Abakerebe says, the one that works is the one who gets food. (pg.97)

Methali inasisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa vizazi vyoe ili kupata chakula. Jamii ya Wakerebe iliamini kazi kama njia ya kupata riziki. Kazi ya ukulima, ufugaji na uwindaji ingewapa mapato yao ya kila siku. Hekima na maarifa yao yangepitishwa kwa methali kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Wangemheshimu na kumthamini yeyote aliyefanya kazi yake kwa badii. Hali hii ingeondoa uzembe miongoni mwa

wanajamii. Ukweli na uhalisia wa wanajamii hufumbambwa kupitia vipengele mbalimbali vya lugha vinavyotumiwa na waandishi wa fasihi.

Mf 101.

...maskini hachinji huokota (uk.85)

...the poor does not slaughter he collects. (pg.96)

Dondoo hili linadhihirisha matabaka mbalimbali katika jamii; tabaka la wanyonge na tabaka la walivyonavyo. Ukweli ni kwamba maskini hana uwezo wa kuchinja bali yeye husubiri tajiri achinje kisha aokote vilivyoachwa na matajiri. Maneno haya yanasemwa na Myombekere anaporejelea usemi wa Bugonoka kurejelea ngozi aliyoacha kwake kwamba siku moja itamfaa maskini asiyekuwa na hiari ya kuchagua atakacho. Ukweli huu unasambazwa ulimwenguni kupitia mchakato wa tafsiri.

Riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** pia imedhihirisha matumizi ya methali katika usimulizi wake japo si kwa wingi. Matumizi ya methali huwa ni kielelezo cha historia na uhalisia wa tajriba za binadamu na mazingira wanamoishi kwa kipindi fulani. Ujielezi huu huwa ni nguvu na falsafa zinazoiongoza jamii katika miktadha mbalimbali ya maisha yao. Kutafsiri methali katika kazi ya fasihi ni uhalisia unaojibainisha katika hali tata ambapo mtafsiri hawezi kuitafsiri methali nje ya miktadha ilimotungiwa. Aidha, ni muhimu kuzingatia uamili uliokusudiwa kutekelezwa na methali hiyo katika miktadha yake maalum. Tafsiri zozote za fasihi zinazopuuza uhalisia huu zinaweza kuibua makosa yanayoweza kuishia kupotosha maana na mawasiliano ya kifasihi au kudhoofisha usanifu wa kazi lengwa. Baker (1992) anapendekeza kutafsiri methali kwa njia ya maelezo pale ambapo hakuna methali katika lugha lengwa ambayo inalingana na methali hiyo katika lugha chanzi kiuamilifu na kimaana. Kupitia kwa mbinu hii basi ubora wa kazi utaonekana kupitia

mchakato wa tafsiri. Kareithi amedhihirisha uhalisia wa matumizi ya methali katika utunzi wake.

Mf 102.

> *….muda si mrefu, kila mmoja alianza kutoka jasho kwa vile chumba kilivyokuwa kidogo na ugali ulivyokuwa moto. Hawakusema maneno mengi kwani kama Waafrika wasemavyo, "Mto hunyamaa unapojaa." (uk.31)*
>
> *... in a short while, both men bugun to sweat because of the tiny room and the hot ugali. They did not say much because as Africans say, the river is still when it is full. (pg. 29)*

Dondoo hili linarejelea jinsi Kinaro anamkaribisha mgeni wake Meja Blue. Alimpikia ugali akampa na maziwa. Kinaro alikuwa anajiamini kwa kupika ugali kuliko mtu yeyote kule vijijini. Kwa pamoja waliufurahikia mlo huu hadi wakaanza kutoa kijasho. Waliposhibisha matumbo yao Meja Blue alitumia methali hii ili kurejelea mazingira ya kiekolojia ya kule kwao kwamba mto hunyaza unapojaa. Yaani mtu akiwa ameshiba ndipo hunyamanza yaani anatulia. Ni dhihirisho la wazi kwamba methali hubuniwa kutokana na mazingira ya kiekolojia. Aidha, inapotafsiriwa maana asilia hudumishwa kwa kuipa tafsiri ya moja kwa moja au kwa kuitolea ufafanuzi unaowezesha hadhira lewa kuelewa bila tatizo. Kwa njia hii utamaduni husika utakuwa umedumishwa.

7.1.2 Matumizi ya Tashbihi

Tashbihi ni kipengele mojawapo cha ujielezaji katika kazi ya fasihi. Wasanii mbalimbali wametoa maelezo tofauti kuhusu dhana hii. Wales (2001), anafafanua tashbihi kama maelezo ya kiufananisho ambayo yanatumiwa kufananisha dhana moja na nyingine kwa kutumia maneno ya ulinganisho wa moja kwa moja. Dhana inayofananishwa huwa na sifa ambazo zinaeleweka kwa urahisi na kwa kufananisha dhana moja na nyingine hadhira lengwa hubashiri maana inayowasilishwa kwa haraka. Msokile (1993) anasema kwamba tashbihi ni tamathali ya usemi inayohusisha

vitu vitatu; kizungumziwa, kifananishi na kiungo. Kifananishi kipo katika mawazo na huzingatia maana iliyo dhahania. Kiungo ni sifa zipatikanazo katika kitu kinachozungumziwa. Kazi muhimu ya kiungo ni kuhusisha viti vyote wiwili katika kuwasilisha maana iliyokusudiwa. Tashbihi hutumia kauli za ulinganisho kama vile; mithili ya, kana kwamba, kama, kama vile, sawa na, na kadhalika.

Aidha, Wamitila (2004), anasema kuwa tashbihi ni misemo ya kilinganishi ambayo hukieleza kitu au sifa zake kwa kukilinganisha na kingine ili kukuza sifa zake. Dhana inayofananishwa huwa na sifa ambazo zinaeleweka kwa urahisi. Kwa kufananisha dhana moja kwa nyingine hadhira pokezi huelewa haraka na kwa urahisi kinachowasilishwa. Ulinganishi huu hutoa sifa za kitu kwa kufumbata maana yake. Matumizi ya tashbihi hutumiwa katika mazungumzo ya kila siku na kwa hivyo hujumuishwa katika kazi ya fasihi. Kutokana na kauli hii basi, matumizi ya tashbihi hutokana na matumizi ya lugha kimuktadha. Pierini (2007) anasema kwamba mkakati wa kuhifadhi tashbihi unaweza kutumiwa kutafsiri tashbihi katika kazi za kifasihi ili kujiepusha na tatizo la kuleta utata katika mawasiliano kwa hadhira lengwa. Baada ya kupata visawe hivyo, mtafsiri huongeza maelezo yanayoeleza jinsi visawe vilivyotumiwa vinavyofanana ili maana iweze kueleweka kwa uwazi. Lengo la mtafsiri kufanya hivi ni kuondoa utata kwa sababu maneno mengi yaliyotumiwa katika vipengele vya ujielezi huwa na maana ya kimuktadha. Mtafsiri ni sharti awe mwangalifu ili kuteua visawe linganifu vya tashbihi hasa kwa kuzingatia muktadha husika. Katika utafiti huu tutajikita kwa tashibihi zinazofungamanishwa na utamaduni wa matini teule.

Riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* imetumia aina mbalimbali za tashbihi ili kukuza na kuendeleza dhamira na maudhui yake.

Mf 103.

> *…Ehe, si nyinyi Bakerebe mlisema kwamba wanawake ni* ***sawa na samaki****,* ***hunaswa katika amasanzo****! Wakacheka wote kwa furaha. (uk.65)*
>
> *…Aa! Isnt that exactly what Wakerebe men of yore said****, that women are like fish, to be caught by the basketfuls?*** *(pg.91)*

Dondoo hili ladhihirisha shughuli muhimu ya jamii hii ni uvuvi ndio maana msanii anachota ubunifu wake kutoka muktadha wa kawaida wa wanajamii. Jamii inamlinganisha mwanmke na aina ya samaki anayevuliwa haraka na wanaume jinsi samaki wanadanganyika kwa wepesi kupitia mitego ya wavuvi. Sifa za samaki zinalinganishwa na sifa za wanawake ili hadhira lengwa iwe na hiyo taswira. Mkutadha huu unamshirikisha Myombekere akimfanyia mzaha shemejiye Brongo kuhusu suala la kumpata mke. Naye anamwambia kuwa kumpata mwanamke ni rahisi kwa kuwa wanavuliwa kama samaki. Uhawilishaji wa tashibihi umefanywa kwa njia ya moja kwa moja ili kudumisha maana iliyokusudiwa.

Mf 104.

> *... Mbona umenawiri sana na mwili wako umekuwa mnene? Kwenu huko* ***walikuwa wanakulisha nini ukawa kama kiboko…*** *(uk.124)*
>
> *…Ans how plump you have become since going back to your parents! What were they slaughtering for you all the time* ***to make you so fat as a hippo…*** *(pg.167)*

Gwaleba rafikiye Myombekere alikuwa amewatembelea nyumbani mwao na alipomuona Bugonoka baada ya kukaa kwao kwa muda anashangaa jinsi Bugonoka alivyokuwa amenenepa ndivyo anamuuliza alikuwa analishwa nini na wazazi wake. Kupitia kwa Gwaleba matumizi ya tashibihi yanadhihirisha mazingira ya kiekolojia ya viboko maana Wakerebe walikuwa wawindaji hodari wa viboko. Sifa za kiboko zinafananishwa na sifa za Bugonoka kwa jinsi alivyokuwa ameongeza kimo. Hii ni ishara tosha ya kulishwa vizuri na wazazi wake. Kipengele hiki cha ujielezaji

kinadhihirika muktadha na mazingira ya jamii ya Wakerebe. Utamaduni huu umedumishwa kwa kutoa tafsiri ya moja kwa moja.

Mf 105.

...Siku hizo Bugonoka akaanza kunenepa, mwili wake wote ukapata afya. Usoni pake pakaanza kuonyesha dalili ya mwanamke mja mzito yeye umbo lake ***alikuwa mweusi kama mgomba wa kabila ya entundu****. (uk.218)*

...In the meanwhile she became plumper, all her body filled out and she became almost light coloured in the face and really glowing, though she was normally of the smooth and beautiful deep black complexion of ***the black stem of entundu banana.*** *(pg.272)*

Mwandishi anatumia mfano huu wa tashibihi ili kuibua utamaduni wa jamii ya Wakerewe. Utamaduni wa Wakerewe umesawiriwa kwa kuangazia ekolojia ya mazingira inayoainisha aina mbalimbali za migomba inayotoa ndizi ya kutengeneza pombe. Katika jamii hii ni wazi kwamba kuna aina mbalimbali za ndizi ndio maana mwandishi anazungumzia weusi wa Bugonoka hazungumzii 'mweusi kama makaa' bali anasema 'mweusi kama mgomba wa kabila la entundu.' Yaani kinachowazunguka Wakerewe ni aina ya mgomba wa kabila la entundu. Mtafsiri amedumisha kipengele cha entundu kwa sababu hakupata kisawe cha lugha lengwa. Amefafsiri dhana hii jinsi ilivyo na kisha kuitolea maelezo ili kurahisisha mawasiliano kwa hadhira lengwa.

Mf 106.

....mimi kila mara huwa ninasikia watu wakisema, ***je unataka kula kama mwindaji wa viboko?*** *Katika safari hii ndio nimejionea mwenyewe kwa macho yangu: nyama yote hii niliyopakuliwa katika olunanga haitoshi kuliwa na mwindaji viboko. (uk.44)*

*...all the time I used to hear people say**: do you want to eat food like a hippopotamus hunter?*** *And this time I saw with my own eyes what that means: the meat piled on this plate is nothing to what hippopotamus hunter eats. (pg.65)*

Mbinu hii ya ujielezaji ni njia moja ya kutujulisha mazingira ya kiekolojia katika utamaduni wa Wakerebe. Jamii hii ilizungukwa na viboko na walizuka na mbinu za kuwawinda. Waliohusika kwa shughuli hii ya kuwinda viboko walijulikana hadharani kwamba wao hula chakula kingi. Lweganwa anamsimulia Myombekere kisa alichoshuhudia wawindaji wa viboko wakila. Kila wakati jamii inapotaka kuwafunza wanajamii kuhusu masuala ya mlo wangetumia ulinganisho huu wa lugha. Mbinu hii imewezesha utamaduni asilia kuhifadhiwa kwa hadhira lengwa kupitia taaluma ya tafsiri.

Aidha, mwandishi wa ***Kaburi Bila Msalaba*** ametumia tashbihi ili kuleta wazi maudhui na dhamira yake. Visa na matukio yake yameelezwa kiulinganisho. Ufananisho mwingi umechotwa kutoka miktadha ya kawaida ya wanajamii.

Mf 107.

...Macho ya kila mtu yalielekezwa kwake, naye alizungusha macho yake kutoka upande wa kushoto mpaka wa kulia. Alipokodolea watu macho ***yalionekana kama ya simba na kwa muda hakusema lolote****. (uk.50).*

...everyone looked up to listen to the man, ***whose fierce, and lion like eyes darted left and right staring*** *silently at the gathered men and women. (pg. 52)*

Watu wengi walitoka vijiji mbalimbali ili kuja kula kiapo cha kutetea na kupigania uhuru wao. Kiapo kilikuwa siri ya mtu pekee, siri ambayo mtu hangemwambia hata mkewe. Mzee Olalo pia alikuwa miongoni mwa watu waliokuja kula kiapo usiku ule. Kwa muda mrefu alikuwa anaunga mkono serikali ya mzungu na kusaliti ndugu zake waafrika. Walipompata walimpa fursa ya kula kiapo ili asiwe anawasaliti. Usiku huu wamehutubiwa na kiongozi wa MauMau- Meja Mwangi ambaye alionekana mkali kwa macho. Ukali wake unajidhihirisha jinsi ambavyo mzungu amewanyanganya ardhi yao na kunyakua kila kitu walichoachiwa na mababu yao kisha kuwafanya watumwa. Ukali wake unalinganishwa na ukali wa simba jinsi alivyowaangalia

waliokuwa wanakula kiapo. Kiapo walichokula kilikuwa ni cha ushirikiano wa watu weusi. Alitoa wito kila mmoja aweke mkono kwa mapambano ya kumng'oa mzungu mamlakani. Ulinganisho huu unadhihirisha mazingira ya Afrika ambapo utawapata wanyama pori kama simba. Mtafsiri naye amedumisha maelezo haya kwa hadhira lengwa.

Mf 108.

*…**Tumekataa kabisa kuwa kama kondoo anayewekwa** chumbani akingoja kuliwa. (uk.51)*

*…We **refuse to be like sheep being fattened** for slaughter (pg. 44)*

Katika harakati ya kula kiapo ndipo kiongozi wa MauMau anawamotisha Waafrika wasikate tamaa dhidi ya kutetea uhuru wao. Anaposisitiza ujumbe huu ndipo anawaambia kuwa wamakataa kuwa kama kondoo wanaosubiri kuliwa. Ulaji wa kiapo ungewafanya waendelee na mapambano ya kupigania uhuru wao. Kondoo anayewekwa chumbani kusubiri kuliwa ni Waafrika ilhali anayewaweka ni mzungu. Kwa kawaida kondoo ni myama mpole ambaye anapendwa na watu kutoka Mlima Kenya. Mazingira haya yamesawiriwa kupitia ubunifu wa Kareithi.

7.1.3 Matumizi ya Jazanda

Jazanda ni kipengele muhimu katika kazi ya kiubunifu. Matumizi ya jazanda hutekeleza mambo mawili muhimu katika tafsiri. Jazanda husaidia mwandishi kueleza ujumbe wake kwa njia bora na pia inatekeleza nafasi ya matumizi ya lugha kisanaa kwa mujibu wa (Newmark 1988). Kimsingi jazanda hutumia lugha fiche ambayo wakati mwingine huleta utata kimaana. Jazanda inatumia picha inayotufanya kuona jambo zaidi ya maana yake halisi. Upekee wa jazanda unatufanya kuupatia ulinganifu maana. Msani anapotumia jazanda kwa kazi yake hulenga kuremba kazi yake kwa kuwasilisha mawazo yake kwa njia fiche na maneno yenye ujumi na yanayodhihirisha hisia zake. Aidha, matumizi ya jazanda hufikia maana pana na ya kipekee. Ikiwa

tunazungumza na kuandika kijazanda, tunafanya hivyo ili kuvutia kwa maneno yenye ujumi yanayopendeza au kudhihirisha hisia kubwa (Kovecses 2002). Jazanda zinapotafsiriwa kutoka lugha moja kwenda nyingine humhitaji mtafsiri kuwa macho maana jazanda mara nyingi hufungamana na muktadha husika. Muktadha ndio utamaduni wa jamii fulani. Riwaya ya ***Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali*** imetumia jazanda kwa maelezo ya dhamira na maudhui yake.

Mf 109.

*...**mbwa** huyu aliyetengeneza pombe hii ya ndizi anastahili sifa. (uk.30)*

*...**the dog** who pressed this beer from the banana fruit is a real great dog. (pg. 43)*

Baada ya wazee na watu mashuhuri kuamua kesi kati ya Myombekere na Ntama ilikuwa ni desturi kuwa na pombe katika shughuli kama hii. Maneno haya yanamtoka mzee mmoja baada ya kubugia pombe ile kwa muda ndipo akatoa kauli yake. Waliokuwa wameketi walivunja mbavu kwa kicheko. Hata yule aliyeleta pombe *hakukasirika* kamwe kwa kuitwa "mbwa' kwa sababu ilikuwa ni desturi ya jadi yao Abakerebe walikuwa wakisema hivyo wakitaka kumsifu mtu ambaye ameivisha pombe vizuri. Ulinganisho huu unaleta wazi sifa za mtu aliyeivisha pombe kuwa yeye ni hatari. Mchakato wa tafsiri umehawilisha matumizi haya ya jazanda kwa njia ya moja kwa moja lakini yakatolewa ufafanuzi ili watu wa utamaduni lengwa wapete kuelewa. Uamilifu unadhibiti tafsiri kima cha kuwiana na mawazo ya Hans Vermeer katika nadharia ya *Skopos* kwamba kutafsiri kunafaa kushughulikia jukumu la matini chanzi na matini lengwa kwa kuwa kutafsiri ni kuzalisha matini lengwa. Kulingana na Vermeer (1989) hakuna matini chanzi iliyo na tafsiri moja tu na ambayo ni sahihi na inayokubalika.

Aidha, riwaya ya ***Kaburi Bila Msalaba*** nayo imetumia jazanda katika kazi yake.

Mf 110.

*…Bwana wake **aliponyakuliwa na mwewe**, yaani Mau Mau, mke wa mzee wa Lalo alitaabika sana. (uk.54)*

*…when her **husband was snatched by the "hawks"** that's the Mau Mau, Mzee wa Lalo's wife was left very frightened. (pg.60)*

Haikuwa rahisi kwa Waafrika ambao walikuwa wanashirikiana na mzungu. Waafrika wote waliwaona kama wasaliti. Usiku huu kikundi cha MauMau kilifika nyumbani mwa mzee Lalo ili kumnyakua. Mke wake alibaki akitaabika moyoni baada ya kumnyakua kwa sababu keshoye alijua kuwa angemuona bwanake akiwa amekatwa katwa vipande namna walivyowafanyia Waafrika waliokataa kushirikiana na wenzao. Ulinganisho huu unaleta wazi sifa za mwewe jinsi anavyonyakua vifaranga bila kumtahadharisha kuku kwamba anachukua mtoto wake. Vilevile, kikundi hiki cha Mau Mau pia hakingekua na huruma kwa mtu ambaye hashirikiani nao katika harakati za mapinduzi.

7.1.4 Matumizi ya Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo kitu kisichokuwa na uhai au uwezo wa kuishi (urazini / ung'amuzi) wa kibinadamu kinapewa sifa hiyo (Wamitila 2010). Lugha ya aina hii inapotumiwa katika fasihi hujenga taswira na fahiwa za aina fulani akilini mwa msomaji. Uhakiki wa maana katika tafsiri za fasihi hauwezi kuishia katika kuyachanganua maneno katika upekee wake bali kwa kuangalia namna yanavyojitokeza katika muktadha wa matumizi. Mbinu hizi za ujielezi hazikosi kufungamanishwa katika mazingira ya utamaduni husika. Kitereza ametumia mbinu hii ya ujielezi katika kazi yake.

Mf 111.

*….Migomba zake zilikuwa changa bado ndipo zinaanza **kuvunja ungo** kabla hazijazaa matunda mengi. (uk.145)*

> *….in his banana plantation, the bananas were young they **had not yet attained their maturity**. (pg.193)*

Kuvunja ungo ni kwa binadamu lakini migomba ya ndizi imepewa sifa hizi za urazini za kutenda kama binadamu. Mwandishi anapotumia dhana hii anarejelea jinsi migomba ilikuwa karibu kuanza kutoa ndizi. Matumizi ya tashihisi imeeleza mazingira ya Wakerebe kwa uwazi kwamba migomba ingetumika katika shughuli zao za kila siku. Nadharia ya isimu Anthropolojia inasisitiza kwamba kazi yoyote ya kifasihi inayochukuliwa kuwa tafsiri haielei katika ombwe tupu bali inaibuka na kujibainisha kwa kuhusishwa na kukitwa katika miktadha ya lugha, fasihi na utamaduni husika.

Mf 112.

> *…**jembe nalo, mikononi mwake likawa rafiki mwema** na ndio maana alikuwa anamfukuzilia mbali Yule adui njaa nyumbani mwake. (uk.14)*
>
> ***She was also friends with her hoe**, a real hard worker and as a result, hunger and famine were things unknown to her house. (pg.22)*

Dondoo hili linamrejelea Bugonoka jinsi alivyopenda na kuenzi kazi yake. Dhana ya jembe imepewa nafasi ya kutenda kama binadamu mikononi mwa Bugonoka eti ***jembe lilikuwa na urafiki naye*** yaani lilifanya kazi vizuri. Bugonoka anamiminiwa sifa na mwandishi ishara tosha kwamba alizirithi kutoka kwa mamake. Matumizi ya mbinu hii humfanya msomaji kujenga picha hii akilini inayomwezesha kuelewa vizuri kinachozungumziwa na mwandishi. Kupitia kwa mbinu hii ya ujielezaji tunaelewa kwamba wakaazi wa jamii hii ni wakulima kutokana na vifaa wanavyovitumia katika kazi zao. Jembe hudhihirisha shughuli za uzalishaji mali ambapo tashihisi hii inaonyesha kuwa jamii hii ni ya wakulima na huthamini kilimo kama uti wa mgongo wa jamii yao. Matumizi ya mbinu za ujielezaji hufungamana na utamaduni husika.

Mf 113.

*...yeye kijana yule mle ndani na mama yake ikawa **"duduli" "duduli" hata** kata nazo zikapiga kelele**. Gongoro! Gongoro**! Pite pite wakamuona mtoto anakuja nje pamoja na mtungi wa pombe.(uk.29)*

*...all the other men could hear from outside was: **"duduli!" "duduli!**" between him and his mother, together with the sound of calabashes knocking against each other**. Gongoro! Gongoro!** Before long he emerged straining under the weight of a pot of beer. (pg.41)*

Fasihi ni zao la utamaduni mahususi. Hakuna fasihi bila kuelezea uhalisia wa wanajamii katika miktadha yao ya kawaida. Kila mwandishi hujaribu kushirikisha shughuli na vifaa vya jamii husika kwa kazi yake. Katika jamii ya Wakerebe kata ni kifaa cha kuchotea maji au kunywa maji. Vifaa hivi vinapotumiwa katika kazi ya fasihi humsaidia mwandishi kuafikia lengo lake na kueleza maudhui yake kwa njia inayoeleweka kwa hadhira lengwa. Kutafsiri fasihi kunaweza kufafanuliwa kuwa ni maingiliano ya hadhi maalum ya kitamaduni. Muktadha unawezesha kubainisha mambo mengi.

Mf 114.

*...kabla ya kumaliza mazungumzo hayo, jogoo la kwanza liliwika, "kokoleke" wenyewe wakasema na kujibizana hivi, **"Umetukuta nasi hatujalala, usijitape bure" (uk.116)***

...before Myombekere and his companions knew it they heard the first cockcrow go: Tata wee! "You found us awake, don't you ever brag you woke sus up."

Kila mtu alijishughulisha na nyimbo na kucheza hadi wakasahau kwamba muda ulikuwa umeenda. Waliposikia jogoo akiwika ndipo walipogutuka kwamba kulikuwa kumekucha. Kulipambazuka bado wakiwa wanakunywa pombe na kunengua viungo vya miili yao. Kwa kutumia mbinu ya uhaishaji walianza kuongea na jogoo kwamba asiseme kwamba yeye ndiye aliwaamsha maana tayari aliwika akawapata bado hawajalala. Kupitia mbinu hii ya ujielezaji tunajulishwa kwamba hii ni jamii ya wafugaji na jogoo hutekeleza wajibu wake kwa kuwaamsha.

Mf 115.

...Myombekere akapokea kata, akamwagia mpini maji ukiwa na jembe pamoja ndani yake, maji yakitelemkia katika olusabuzyo. Pale pale chuma kilipomwagiliwa maji mabichi, na mpini ukiwa na joto la moto wa chuma, hapo ***vikaanza kufoka vyote pamoja,*** *ikawa: tokotoko! Na fwofwofwo! (uk.135)*

Myombekere poured water on the hoe in the handle with the water running into the washing basin and leaving behind ***the red hot iron hoe hissing from its contact*** *with the water and making the water boil: tokotoko! Fwofwofwo!(pg.181)*

Dondoo hili linadhihirisha matumizi ya mbinu ya tashihisi. Jembe lisilokuwa na uhai linapewa sifa ya kutenda kama binadamu. Mwandishi anasema kwamba baada ya kumwagilia jembe maji lililokuwa moto ***lilianza kufoka***. Jembe halina uwezo wa kutenda kama binadamu bali ni sifa ya binadamu imechukuliwa na kupewa kitu kisichokuwa na uhai. Kupitia mbinu hii ya ujielezaji utamaduni wa Wakerebe unahifadhiwa kwa hadhira lengwa kupitia mchakato wa tafsiri. Aidha, mbinu hii inatuwezesha kuelewa kwamba hii ni jamii ya wakulima kupitia vifaa vyao vya kazi kama jembe.

7.1.5 Matumizi ya Tanakali za Sauti

Hii ni tamathali ya usemi inayotoa au kuiga mlio wa vitu, watu na wanyama Senkoro (2011). Milio hii humsaidia mwandisi kufafanua ujumbe wake kwa njia ya uwazi na inayoeleweka kwa urahisi na hadhira yake. Wamitila (2010) anasema hii ni mbinu ya uigaji wa sauti fulani. Msingi wa matumizi ya mbinu hii ni kuhakikisha kuwa hali fulani inaelezwa kwa njia kamilifu na kwa ufasaha. Aidha, inatumiwa kujenga aina mbalimbali za taswira akilini mwa msomaji. Sehemu inayofuata inaangazia aina mbalimbali za tanakali za sauti jinsi zimetumiwa na mwandishi wa MC2.

Mf 116.

*....**akamchapa kwa vijiti: pu!pu!pu!** Mtoto akalia wee! Vijiti vile nilivyokatika na Ntama alipotaka kurudia vingine, hapo mtoto akaponyoka mkononi mwa Yule mwanaume, akaanza kupiga mbio. (uk.25)*

> *...**belaboring him with twigs of tree: pu!pu!pu!** The child cried until he could cry no more. When the twigs he had were all used up and he went looking for more, the child managed to tear himself up from the grip of his hand and ran for his life. (pg.37)*

Ntama alimfumania mpwa wa Myombekere akilisha ng'ombe wao mtama wake. Bila kukawia alianza kumpa adhabu ya viboko kwa kutumia vijiti. Alimchapa hadi vijiti alivyokuwa navyo vikaisha. Alipoenda kutafuta vingine Kafugwa alipata nafasi na kuponyoka kutoka mikononi mwake. Japo alikimbia aliondoka na majeraha mabaya yaliyomfanya Myombekere kumkanda mtoto kwa maji moto aliporudi kutoka kwa shughuli zake. Kutokana na adhabu hii, Kafugwa alivimba mwili mzima. Kupitia kwa tanakali hii tunajenga taswira jinsi mtoto alivyochapwa na Ntama. Aidha, tunaelewa utamaduni wa jamii ya Wakerebe kwamba mtoto akikosa anapewa adhabu ya viboko. Vilevile tunajifunza kwamba utamaduni huu unamruhusu yeyote kumadhibu mtoto si lazima awe ni mzazi wake. Utamaduni huu unapotafsiriwa dhana hii inahawilishwa vivyo hivyo kisha maelezo ya dhana kutolewa baadaye. Kupitia mchakato wa tafsiri utamaduni huu umesambwa kutoka utamaduni chanzi hadi utamaduni lengwa.

Mf 117.

> *....walipotoka nje na kusonga karibu na Namwero, ndipo Myombekere akaanza kuwakumbusha maneno ya kuomba radhi na kutaka arudishiwe mke wake Bugonoka. Alianza kufungua koo lake**, akakohoa hivi: koho!koho!** apate kuomba radhi kwa wakwe kwa sauti isiyo na kizuizi. (uk.48)*
>
> *...they went and sat near Namwero and Myombekere once more spoke words of wooing back his wife Bugonoka**. He first coughed very slightly this way: koho!koho!** to clear his throat so that he can speak to his father il law.*

Dondoo hili linadhihirisha matumizi ya tanakali za sauti jinsi Myombekere alivyojitayarisha kuomba radhi wakwe zake. Baada ya mke kukosewa na kurudi kwao haikwa rahisi kwa mwanamume kusimama mbele ya wakwe wake kuomba msamaha. Tanakali hii inaonyesha utamaduni wa Wakerebe kwamba makosa yakitokea kati ya mume na mke wanaweza kukutana na wazazi na kuongea kwa kuomba msamaha.

Tanakali hii ya sauti imehamishwa hivyo kwa kukosa kisawe cha sauti ya kufidia taswira hii.

Mf 118.

> *...yalitoa mvumo mkubwa ajabu yalipodondoka katika chombo kile hata mtu aliyekuwa mbali aliweza kusikia mvumo kama huuu:* ***Vuu! Siyo kama hivi: chorwe, chorwe, au: chororwe!*** *(uk54)*
>
> *...its milk was was zooming in ekisahi so that even from a distance what one heard was**: Vuu! And not chorwe, chorwe! Or even chororwe!*** *(pg.79)*

Mlio huu ni wa maziwa, dhihirisho lililowazi kwamba kupitia mbinu hii ya ujielezaji msomaji anaweza kujifunza utamaduni wa eneo fulani ulimwengini. Mwandishi anapata nafasi nzuri ya kuchora picha ya kile anachokizungumzia. Aidha, kupitia mbinu hii tunajifunza kwamba riwaya hii imebuniwa kwa mazingira ya wakulima na wafugaji. Utamaduni huu umeweza kuhifadhiwa kwa hadhira lengwa kupitia mchakato wa tafsiri.

Mf 119.

> *... Gwaleba naye kwa jinsi alivyokuwa tayari na shoka yake, hakumpa nafasi ya kumshambulia,* ***alimpiga upesi na shoka barabara kichwani paa!*** *Na ng'ombe akaanguka chini alilia* ***boo!*** *(uk.130)*
>
> *...Gwaleba, on his part brought down his axe* ***right on the middle of of his dammed skull: po!*** *The cow fell down while crying* ***boo!*** *(Pg. 172)*

Utamaduni huu ulimuheshimu mwanaume yeyote aliyemwangusha ng'ombe kwa shoka. Gwaleba ameshangiliwa kama shujaa kwa kumuangusha ng'ombe huyu. Kupitia tanakali hizi za sauti tunajifunza mengi kuhusu jamii hii. Tanakali hizi za sauti zinadhihirisha kwamba jamii hii ni ya wafugaji na wanatumia nyama ya ng'ombe kama kitoweo chao. Utamaduni huu umesambazwa na kuhifadhiwa kwa makabila mengine kupitia taaluma ya tafsiri.

Mf 120.

...mara nikasikia nyumbani mle vitu vinagongana na kutoa sauti: ***gunguru!gunguru!bogoto!bogoto:*** *tamati! Kumbe wanagonganisha mangozi, ndiyo yanayopiga kelele kwa kuteremshwa na kuangushwa chini. (uk. 173)*

...I heard noises of: ***gunguru! Gunguru! Bogoto! Bogoto!*** *Without even realizing it was the noise of hides being moved about. (pg.220)*

Myombekere anasimulia kisa walipokuwa na Gwaleba katika nyumba ya Omukama. Kwa hofu ya kumuogopa Omukama, Gwaleba alipoitwa Myombekere alianza kutetemeka. Ghafla alisikia sauti hii iliyomtetemesha zaidi lakini ilikuwa ni sauti ya ngozi zilizoanguka chini zilipokuwa zikihamishwa. Mbinu hii ya ujielezaji inatufunza kuwa jamii hii ni ya wafugaji na huwa wanatayarisha ngozi kwa matumizi yao ya nyumbani. Mbinu hii mbali na kusisitiza ujumbe wa mwandishi husaidia kuhifadhi utamaduni kwa hadhira lengwa kupitia zoezi la tafsiri.

Mf 121.

...Anakazana kupika viazi akavitia katika chungu chake vikiwa vibichi bado na huku anavibebena (anavibumung'unya) vibichi mdomoni mwake vikivumisha sautikama hii: ***pokocho! Pokocho! Au magunu magunu.*** *(uk.180)*

...there's a wife when she is putting sweet potatoes in the cooking pot she is already chewing the raw food without a break so that you hear nothing but: ***pokocho! Pokocho! Magunu! Magunu!*** *(pg.227)*

Pokocho! Pokocho! Ni tanakali za sauti zinazoiga sauti wakati mwanamke anatafuna viazi vibichi. Sauti hizi zinamsaidia msomaji kujenga taswira namna viazi hivi vinapotafunwa vibichi. Kwa misingi hii, maudhui na dhamira huwasilishwa kwa njia bora zaidi. Aidha, sauti hizi zinajenga na kufafanua utamaduni wa mwandishi. Kupitia sauti hizi wasomaji wanaelewa vyakula vinavyoliwa na jamii husika. Kutokana na mbinu hii tunafahamu kwamba Wakerebe ni wakulima wa viazi na huvitumiwa kama chakula vikiwa vibichi na vikiwa vimepikwa. Kupitia mchakato wa tafsiri utamaduni hii utakuwa umehawilishwa kutoka hadhira chanzi hadi hadhira lengwa.

Wakerebe walikuwa wanasumbuliwa na wanyama wa pori kuharibu mimea yao. Baada ya kushauriana na *Omukani* wanakubaliana kwenda kuwawinda hao wanyama. Walikubaliana wachukue mbwa wawaongoze kwa uwindaji huo. *Omukami* anawashauri kwamba watakapoenda na mbwa wake wanawaagiza mara moja na wanatii. Anawaagiza kwa kutumia tanakali za sauti. Anaiga ile sauti mbwa wake wanafahamu. Tanakali hii inapotafsiriwa ilisalia katika lugha asilia kwa sababu si rahisi kupata kisawe cha sauti hiyo kwa lugha lengwa.

7.1.6 Majina ya Kimajazi

Majina haya hutolewa kulingana na mila na desturi za jamii husika. Wametila (2010)

Anaeleza kuwa majina haya yanaweza kuhusiana na tabia, maisha na matukio mbalimbali katika jamii. Jinsi majina haya yanavyotumiwa na mwandishi ni njia moja ya kukuza dhamira na maudhui yake. Aidha, ni njia moja ya kuendeleza utamaduni ambamo kazi yenyewe imebuniwa. Majina hayo ni kama yafuatayo:

7.1.6.1 Myombekere

Jina hili huwakilisha jinsia ya kiume katika jamii ya Wakerewe. Jina Myombekere humaanisha mjenga mji, anayejali na kuitetea familia yake. Aidha, jina hili hupewa mtu mwenye uvumilivu na aliye na uwezo wa kustahili mambo mengi maishani. Wakerewe waliwatarajia wanaume wote kuwa na sifa hizi na wazipokeze kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Myombekere alipitia changamoto nyingi maishani lakini aliweza kuibuka kama mshindi. Katika ndoa yake alianza kwa kuwapoteza watoto wake. Baada ya shinikizo kutoka kwa ndugu na jamii mke wake aliweza kuondoka kwenda kwake. Maisha ya kuishi pekee yake yalimfanya mpweke hadi alianza safari ya kwenda kumtafuta mke wake kutoka kwao. Haikuwa rahisi kwa sababu

iliandamana na gharama ya kulipa kwa wakwe zake. Ilimgharimu kubadilisha beberu wake kwa ndizi ya kutengeneza pombe ya kupeleka kwa wakwe zake kama adhabu.

Mf 122.

...Baba mkwe na mama mkwe, mimi nimekuja kwenu kutaka radhi na kuwaomba mke wangu, nipeni niende naye; sikuja kujitua mzigo na kutaka mali ya mahari, nayo mimi simo kamwe! (uk.16)

...my father- in –lawa and mya mother-in-law, I have come here to woo back my wife, and I have nothing nothing to do with those other matters of escorting her back home and wanting back the pride-price I gave you for her. (pg. 25)

Kupitia kwa maneno haya ni wazi kwamba Myombekere alikuwa mjenga mji hakika namna ambavyo anaomba msamaha na kuwashawishi wazazi wa Bugonoka wamwachilie mke wake aende naye.

7.1.6.2 Bugonoka

Huwakilisha jinsia ya kike katika jamii ya Abakerebe. Bugonoka ni jina la msichana mrembo. Anayewajibika katika boma lake kwa kila shughuli inayomhitaji kama mama na bibi. Alikuwa ni mwanamke wa kujitayarisha mapema; kusiaga unga, kutafuta mboga na kuni na kupikia familia yake kwa wakati unaofaa.

Mf 123.

.....jamani! Kumbe, ufundi ufundi wa kupika wa mwanamke yeyote nchini hutokana katika mafiga ya mama yake. ***Bugonoka*** *naye ufundi wake wake wa kupika kila aina ya chakula na mboga ulitoka kweli kwa mama yake mzazi. Hata aliposaga mtama au mawele siku zote unga wake aliulainisha kwa njia ya kushangaza. Kwake kila wakati unga ulikuwa tayari (sio kama wengine wasiojua utandaji mwema). Ndio maana Bugonoka alikuwa mwepesi sana wa kuwachangamkia wageni na kuwatuliza njaa upesi. (uk.14)*

...no wonder ***Bugonoka*** *was such a great cook! A woman is a great cook or a poor one depending depending on what she learnt ftom her mother's kitchen. And it was from her mother tha Bugonoka learnt to be such a wonderful cook of every kind of relish. It was from her mother too that she leart mastery of grinding grain so that her flour was soft to perfection. And she always had flour in her store. She was not the type of woman who goes to the grinding stone whenever*

> *a visitor calls. And so, in Bugonoka's home a hungry visitor got attended to and given something to eat ata once. (pg.21)*

Sifa za mwanamke wa Kikerewe zimejidhihirisha wazi kupitia mwanamke kielezo Bugonoka. Yeye huwa mwepesi wa mambo mengi. Huwa mpishi hodari na hujua kuandaa na kutayarisha mambo yake mapema. Kila wakati huwakaribisha wageni nyumbani kwake na kuwapa chakula. Wakerebe wanaamini mtoto msichana hujifunza mambo haya yote kutoka kwa mamake mzazi.

7.1.6.3 Ntulanalwo

Ntulanalwo ni mtoto wa Myombekere na Bugonoka. Kwa Wakerewe jina hili lina maana kwamba mauti tunaishi nayo kila siku binadamu ni marehemu. Ni ukumbusho kwamba maisha ya binadamu ni kama maua humea, hukua na hunyauka baada ya muda mfupi. Haya ni maandalizi kwa binadamu aishi akijua kwamba siku moja maisha yake yatakwisha. Myombekere na Bugonoka wamempa mtoto huyu jina kwa misingi kwamba kuna yale walikuwa wamepitia maishani yaliyokuwa machungu sana.

7.1.6.4 Bulihwali

Huyu ni mtoto wa Myombekere na Bugonoka. Jina hili hupewa mtoto baada ya wazazi wake kukumbwa na huzuni kwa muda mrefu. Wazazi hawa waliishi kwa muda bila watoto na wakati tumbo lao la uzazi lilipofunguka wakawapoteza watoto wao wawili. Kwa kuitwa tasa Bugonoka alirejea kwao kwa muda. Myombekere akaja kumchukua kwa wazazi wake na wakaanza maisha yao upya tena. Myombekere na Bugonoka walifunga safari ya kwenda kwa mganga ili kutafuta tiba pale. Wanapomuita mtoto Bulhawali wanalenga kujibu swali huzuni utaisha lini? Hili ni jina lililo na maana ya kipekee. Majina mengi katika riwaya hii yamefungamanishwa na maana kimkutadha. Katika shughuli zao za kila siku utamaduni wao umefumwa

mle ndani. Mtafsiri alipohawilisha maana hakutafsiri maana kwa sababu maana asililia ingepotea na kukosa kuwasilisha maana iliyokusudiwa katika matini asilia.

Jamii nyingi hasa za kiafrika huwa na njia ya kueleza maarifa na hekima ya jamii yao kupitia methali. Kulingana na utafiti huu, vipengele vya ujielezaji vinadhihirisha methali hutumika kwa wingi kwa kazi ya fasihi kuliko mbinu zingine za ujielezaji. Kila jamii hupokeza maarifa na tajriba zao kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine kupitia kwa matumizi ya methali. Mila na itikadi mbalimbali huwasilishwa kwa njia ya methali. Matumizi ya mbinu hizi za ujielezaji hutegemea mazingira na muktadha maalum.

7.2 Muhtasari wa Sura

Sura hii imeshughulikia vipengele mbalimbali vya ujielezaji kama mbinu za kuhifadhi na kudumisha utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Waandishi wengi hutumia mbinu hizi ili kukuza na kuendeleza dhamira na maudhui yao. Katika utafiti huu, mbinu mbalimbali kama vile; methali, tashibihi, jazanda, tashihisi, tanakali za sauti na majina ya majazi zimetumika. Kulingana na lengo letu la tatu matumizi ya vipengele hivi huchangia kudumisha utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Sura inayofuata ni muhtasari, mahitimisho na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA NANE

MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

8.0 Utangulizi

Katika sura hii ya mwisho, tumetoa muhtasari wa utafiti. Sehemu ya tatu imetoa matokeo ya utafiti, sehemu ya nne imetoa mahitimisho ya utafiti huku sehemu ya mwisho ikilainisha malengo ya kazi ya utafiti. Mapendekezo ya utafiti yametolewa katika sehemu ya sita.

8.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulitathimini vipengele mbalimbali vya kitamaduni vinavyochangia uhifadhi wa utamaduni katika matini teule za fasihi. Sura ya kwanza iliweka msingi wa tasnifu ambapo masuala ya kinadharia yaliwasilishwa. Masuala yaliyowasilishwa ni: usuli wa utafiti, suala la utafiti, msingi ya nadharia, upeo na mipaka ya utafiti, umuhimu na sababu za utafiti pia zilifafanuliwa. Sura ya pili iliwasilililisha mapitio ya maandishi na sura ya tatu imejadili mbinu za utafiti zilizotumika kufanikisha kazi hii. Sura ya nne ilitoa muhtasari na historia ya matini teule MC1 Na MC2.

Sura ya tano ilichanganua vipengele vya kitamaduni vinavyochangia uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri katika matini teule. Nilihakiki vipengele vya kitamaduni katika kategoria mbalimbali. Sura ya sita ilishughulikia mikakati mbalimbali iliyotumika ili kutafsiri vipengele vya kitamaduni katika matini chanzi hadi matini tafsiri. Vipengele vilivyojadiliwa ni vile vilivyochangia uhifadhi wa utamaduni. Aidha, sura ya saba ilifafanua mbinu za ujielezaji zilizochangia uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Sura ya nane ni mahitimisho ya tasnifu. Maelezo yametolewa kulingana na malengo yaliyoongoza utafiti. Vilevile, sura hii imetoa matokeo na mapendekezo ya utafiti ambayo yanaweza kushughulikiwa na

watafiti wa baadaye. Sehemu inayofuata inajadili matokeo ya utafiti kwa misingi ya kila lengo.

8.1.1 Uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua namna uhifadhi wa utamaduni umefanikiwa kupitia mchakato wa tafsiri. Usawiri wa vipengele vya kitamaduni umefanywa kutoka matini teule. Usawiri huu umezingatia vipengele vya kitamaduni katika kategoria tatu: utamaduni wa mazingira ya kiekolojia, utamaduni wa kijamii na utamaduni nyenzo, yaani vifaa vya kijamii. Utafiti uligundua kwamba kila jamii huwa na vipengele vyake vya kitamaduni vinavyoitambulisha jamii kwa njia ya kipekee. Aidha, utafiti uligundua kwamba fasihi haiumbwi katika ombwe tupu bali hufungamanishwa na maisha ya binadamu na mazingira yake. Msanii yeyote anapoandika ni sharti afafanue dhamira na maudhui yake na kuyafungamanisha na tabia ya kiekolojia, mazingira, tabia nchi na hali ya hewa. Mazingira ya kiekolojia huwa tofauti kutoka utamaduni mmoja hadi mwingine.

Utafiti ulibaini kwamba majina ya wanyama, samaki, ndege, maeneo ya maji, misitu na majani hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Kulingana na utafiti huu ilionekana kuwa kila jamii huwa na utamaduni unaorejelea mazingira yao zikiwemo imani, desturi, amali, sheria, lugha na asasi za kijamii. Kupitia migogoro ya wanajamii mwandishi husuka kazi yake kwa kudhihirisha imani, falsafa zao na desturi za wanajamii. Watunzi wengi hushirikisha shughuli mbalimbali za binadamu katika utunzi wao ili kuleta uhalisia wa kazi yao. Kulingana na muktadha tofauti kila msanii huzuka na imani, desturi na mawazo tofauti kutoka jamii na kizazi kimoja hadi kingine. Utafiti ulibaini jamii zinatofautiana katika imani na desturi.

Utafiti huu ulionyesha kuwa kila jamii huwa na upekee wake kwa utamaduni nyenzo, yaani vifaa vinavyotumiwa na wanajamii katika shughuli zao za kila siku. Kila jamii ina njia ya kuelezea vyakula vyao, mavazi na vifaa vyao vya kazi. Vifaa hivi katika jamii moja hutofautiana na vifaa vya jamii nyingine na kila mtunzi hufuma kazi yake kulingana na muktadha unaomzunguka kwa wakati anaandika. Utafiti ulibaini kuwa wakati wa uhawilishaji wa vipengele vya kitamaduni ni sharti mtafsiri awe mwangalifu wakati wa tafsiri kwa sababu dhana hizi hazipatikani katika utamaduni mwingine.

Maoni ya mtafiti kulingana na lengo la kwanza ni kuwa vipengele vya kitamaduni huhifadhiwa kupitia mchakato wa tafsiri. Muhimu ni kuwa mtafsiri anafaa aelewe lengo lake la tafsiri kabla ya kuanza zoezi la tafsiri namna ambavyo wazo hili limejikita katika nadharia ya *Skopos*. Baada ya kuelewa lengo la tafsiri ni heri mtafsiri azuke na mikakati mbalimbali ya kuhawilisha vipengele vya kitamaduni. Namna ambavyo vipengele hivi vitahawilishwa itakuwa ni njia mwafaka ya kuhifadhi utamaduni asilia kwa hadhira lengwa.

8.1.2 Uhifadhi wa vipengele vya kitamaduni kupitia mikakati ya tafsiri

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kufafanua vipengele vya kitamaduni na namna vimeweza kuhawilishwa kutoka matini chanzi hadi matini tafsiriwa kwa nia ya kuhifadhi utamaduni asilia. Utafiti uligundua kuwa ili kuhifadhi utamaduni asilia kwa hadhira lengwa mbinu mbalimbali ni sharti zitumiwe na mtafsiri. Kulingana na utafiti wetu mbinu zilizotumiwa ni zile zinazochangia kwa kudumisha na kuhifadhi vipengele vya kitamaduni katika hadhira lengwa. Utafiti ulibaini kuwa mbinu zifuatazo zilitumiwa kuhawilisha dhana za kitamaduni katika matini teule: ufafanuzi au upanuzi maana, ujumuishaji wa dhana, uhawilishaji na muungano wa mbinu nyingine za tafsiri.

Mkakati wa upanuzi maana ulipendelewa zaidi na watafsiri wa matini teule kwa sababu mahali hakungekuwa na kisawe cha vipengele vya kitamaduni katika hadhira lengwa ingekuwa rahisi kutoa maana au kufafanua dhana yenyewe. Nadharia ya *Skopos* ilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu inasisitiza umuhimu wa kubaini lengo la utafiti kabla ya zoezi la utafiti kuanza. Iwapo lengo la kutafsiri lilikuwa ni kudumisha utamaduni basi mikakati mwafaka ni lazima itumike kutafsiri kazi asilia. Vipengele vingi vya kitamaduni vya matini asilia vimeweza kudumishwa kupitia mikakati mbalimbali ya tafsiri.

8.1.3 Udumishwaji wa vipengele vya ujielezaji unavyofasiriwa kama ithibati ya uhifadhi wa utamaduni

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kufafanua vipengele vya ujielezaji kama ithibati ya uhifadhi wa utamaduni. Utafiti huu ulionyesha kuwa kila msanii huwa na tajriba ya kutumia vipengele vyake vya ujielezaji. Aidha, utafiti ulibaini kuwa kila jamii ulimwenguni huwa ni hazina kuu ya mikusanyiko mikubwa ya mbinu za ujielezaji zinazotumika na wanajamii ili kuwasilisha maarifa, tajriba, busara na hekima kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hii husababishwa na tajriba ya mwandishi na urefu wa kazi yake. Aidha, utafiti ulibaini aina mbalimbali za ujielezaji zilizotumika katika matini teule ni: methali, tashbihi, jazanda, semi na tanakali za sauti. Ilidhihirika kwamba methali ni miongoni mwa mbinu zilizotumika zaidi kuliko zingine.

Aidha, utafiti ulibaini kwamba mbinu nyingi za ujielezaji hufungamana na utamaduni husika. Katika harakati ya kuhawilisha tajriba, maarifa na mawazo yao kutoka kizazi kimoja hadi kingine, wanajamii hufungamanisha mbinu za ujielezaji katika miktadha yao ya kila siku. Kulingana na miktadha tofauti utafiti ulielekea kwamba wakati wa kutafsiri vipenge hivi vya ujielezaji mtafiti ni sharti atumie mikakati mahsusi ili kuleta mawasiliano katika hadhira lengwa la sivyo, kutazuka utata katika mawasiliano. Vile

vile utafiti ulibaini kuwa vipengele hivi vinapotafsiriwa kwa kutumia mikakati maalum basi utamaduni asilia huhifadhiwa kwa hadhira pokezi kupitia mchakato wa tafsiri.

Utafiti huu ulionyesha jinsi vipengele vya kitamaduni vinaweza kuhifadhiwa kupitia mchakato wa tafsiri. Utafiti huu ulizingatia riwaya teule: *Kaburi Bila Msalaba na Bwana Myombekere Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulhawali***.** Utafiti umebaini kuwa vipengele vya kitamaduni vinahifadhiwa na kudumishwa kupitia mikakati mbalimbali ya tafsiri na mbinu mbalimbali za ujielezaji. Muhimu zaidi ni kwamba mtafsiri aelewe lengo la tafsiri jinsi nadharia ya *Skopos* inavyoweka wazi. Matokeo ya utafiti huu yatachangia pakubwa katika taaluma ya Kiswahili kwa jumla. Sehemu inayofuata inaeleza mchango wa utafiti.

8.2 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umebaini kuwa fasihi hasa fasihi andishi inaweza kutumika kama njia moja ya kuhifadhi utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri. Utamaduni unaotishiwa na wakati unaweza kudumishwa miongoni mwa wanajamii kupitia taaluma ya tafsiri. Ujumbe unaowasilishwa katika utafiti huu unaweza kuwasaidia wanajamii kujitambulisha na utamaduni wao na hata kuuonea fahari ulimwenguni.

Tafsiri na utamaduni ni masuala yanayohitaji umakini wa hali ya juu. Tafsiri ikifanyika pasipo kuzingatia utamaduni, hupwaya na kupotosha ujumbe hata kuathiri lengo la tafsiri. Nadharia ya anthropolojia na *Skopos* zilikuwa na mchango katika utafiti wetu kwa jinsi zilitusaidia kuchunguza na kujadili udhihirikaji wa vipengele vya kitamaduni katika matumizi ya lugha ya wanajamii na endapo lengo la tafsiri liliafikiwa. Lengo la kutafsiri matini liliafikiwa kwa namna nadharia ilisisitiza mikakati maalum kutumika ili kufanikisha mchakato wa tafsiri. Kupitia mikakati hii

vipengele vya kitamaduni katika matini teule viliweza kuhawilishwa kutoka matini asili hadi matini lengwa bila kutatiza mawasiliano. Uteuzi wa mikakati hii kulingana na mtafsiri uliwezesha udumishwaji wa vipengele mbalimbali vya utamaduni katika hadhira lengwa. Nadharia ya anthropolojia na *Skopos* ilikuwa na mchango kwa kazi yetu kwa kutuwezesha kupata data faafu na kuichanganua data kulingana na malengo ya utafiti.

Uteuzi wa matini teule pia ulikuwa na mchango katika utafiti wetu. Riwaya ya Kareithi na Kitereza zilikuwa ni riwaya za kihistoria na kwa hivyo waandishi walishirikisha vipengele vya kitamaduni ili kuwasilisha dhamira na maudhui yao. Mbinu za utafiti zilikuwa na mchango katika utafiti huu kwa kuwa data faafu iliyofanikisha utafiti, ilipatikana kwa kudondoa vipengele vya kitamaduni, mikakati mbalimbali iliyotumika kutafsiri vipengele hivi pamoja na mbinu za ujielezaji zilizojikita katika utamaduni wa jamii husika. Ili kubaini jinsi uhifadhi wa utamaduni umefanikishwa kupitia mchakato wa tafsiri, data katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza ilitumika na ilikuwa data asilia kutoka matini teule.

Uwanja wa utafiti ni mpana lakini utafiti wetu umeshughulikia sehemu moja tu ikiongozwa na malengo ya utafiti pamoja na upeo na mipaka ya utafiti wetu. Hata hivyo imebainika kwamba katika taaluma ya tafsiri kuna maeneo na sehemu nyingi ambazo bado hazijafanyiwa utafiti. Sehemu inayofuata tumetoa mapendekezo ya baadhi ya sehemu ambazo tumebaini zinaweza kufanyiwa utafiti zaidi ili kuziba baadhi ya mapengo ya kitaaluma ambayo bado hayajazibwa.

8.3 Mapendekezo ya Utafitii

Utafiti huu ulishughulikia uhifadhi wa utamaduni kupitia mchakato wa tafsiri kwa kuzingatia riwaya mbili teule. Tofauti na utanzu wa riwaya, utafiti zaidi unaweza

kufanywa katika sehemu zingine za fasihi andishi kama vile hadithi fupi, tamthilia na ushairi. Utafiti unaweza kufanywa kwa kuzingatia maandishi ambayo hayakushughulikiwa katika utafiti huu.

Utafiti waweza kufanywa kwa kutumia nadharia tofauti kando na nadharia ya anthropolojia na nadharia ya *Skopos*. Vile vile utafiti unaweza kufanywa kwa kulinganisha na kulinganua mikakati mbalimbali ya kutafsiri matini za fasihi.

Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha jinsi uhifadhi wa utamaduni umeshughulikiwa kupitia tafsiri kwa kutumia tanzu za fasihi simulizi. Utafiti unaweza kuzingatia tafsiri ya mashairi simulizi, ngano, tanzu fupi na tanzu zingine za fasihi simulizi. Vilevile, uchunguzi unaweza kufanywa kwa kutumia riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* ili kubaini namna utamaduni umehifadhiwa kupia tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zilizoshirikishwa katika riwaya. Pamoja na hayo, uchunguzi unaweza kufanywa ili kubaini mbinu na mikakati iliyotumika kuhawilisha tanzu hizi za fasihi simulizi hadi kwa lugha ya Kiingereza.

Utafiti wetu umejikita katika juzuu ya kwanza ya riwaya ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka Ntulanalwo na Bulihwali* basi utafiti mwingine wa jinsi hii itaweza kufanya kwa kuzingatia juzuu ya pili ya riwaya hii.

MAREJELEO

Abbas, I. (2015). *Euphemism and (Self-) Censorship: Strategies for translating taboos into Arabic.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Cha Concordia. Haijachapishwa.

Adair, J. (2009). *Effective Communication: The most Important Management Skills of all.* Pan books.

Ahmed, A. S. (1986). *Towards Islamic Anthropology Definition, Dogma and Directions.* USA: New Era Publications.

Al–Hassan, A. (2013). The Importance of Culture: Should Culture be Translated? *International Journal of Applied Linguistics & English Literature*, Juz 2 (2): 96-100

Alvarez, R., & Vidal, M. C. A. (1996). *Translating A Political Act.* Translation Power Subversion Clevedon: Multilingual Matters Ltd.

Al-Zahran, A. (2023). *Translators and culture specific references: A relevance theoretic approach to Arabic- English- Arabic Translation*. Chuo Kikuu Cha Salford: Tasnifu ya Uzamifu. Haijachapishwa.

-------------- (2003). *The consecutive conference interpreter as intercultural mediator: a cognitive-pragmatic approach to the interpreter's role*. Chuo Kikuu Cha Salford: Tasnifu ya Uzamifu. Haijachapishwa.

Arsenteva E., & Kayumova A. (2014). *Translation Possibilities of Occasional Contextual Modification of Phraseological units*. Proverbium 29.

Babbie, E. (1990). *Survey Research Methods.* Belmont, CA: Academic Press.

Baker, M. (1992). *In Other Words: A Coursebook on Translation*. Routledge. London.

------------ (2002). *Encyclopedia of Translation Studies*. London: Tylor & Francis Group

Bakize, L. H. (2018). *Tafsiri na Ukalimani*. Dar es Salaam: Maccony Printers Press.

Bassnett, S. (2002). *Translation Studies.* (3rd ed.). London: Routledge.

------------- (2003). Judging translation. *Wasafiri,* 18(40), 42-44.

Beaton, D. E., Bombardier, C., Guillemin, F., & Ferraz, M. B. (2000). Guidelines for the process of cross-cultural adaptation of self-report measures. *Spine.* Juzuu 25 no. 24 uk. 3186-3191.

Barnard, A. (2000). *History and Theory in Anthropology.* UK: Cambridge University Press.

Bogdan R. C., Biklen S. K. (1992). *Qualitative research for education: An introduction to theory and methods* (2nd ed.). Boston: Allyn 8#x38; Bacon.

Boas, F. (1966). *Race Language and Culture*. Free Press. Government Printing Office.

Brisset, A. (2012). Globalization, translation, and cultural diversity. *Translation and Interpreting Studies*, 12(2), 253-277.

Buliba, A. F. (2001). Lugha, Utamaduni na Jamii, katika maendeleo ya kitaifa na kimataifa Katika N. L. Shitemi na Wenzake (2001) *Kiswahili a tool of Development in Multidisciplinary Approach*. Moi University Press.

Bustani, A. M. K. (2014). *Culture in Arabic to English Literary Translation.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Cha Salford: Tasnifu ya Uzamifu. Haijachapishwa.

Cara, E. (1976). *People in Perspective: An Introduction to Cultural Anthropology*. Randsom House: New York.

Chang, Y. (2012). A Tentative Analysis of English Film Translation Characteristics and Principles. Theory and Practice in Language studies katika *Academic Publisher Manufactured.* Finland. Vol.2 uk. 71-76.

Chege, G. (2017). *Unmarked Grave*. Phoenix Publishers. Nairobi.

Constitution of Kenya, (2010). *Kenya Law Reform Commission*. http://www.klrc.go.ke. Imepakuliwa 06.06.2024

Dare, S.O. (2008). *Theatre and the Celebration of the Material Aspect of Culture in Contemprary Nigeria*. Nigeria.

Ezika, C. G. (2012*). A translation of Oliver Twist by Charles Dickens: Problems and Principles.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nigeria: Nsukka. Haijachapishwa.

El- Dali (2011). Towards an Understanding of the Distinctive Nature of Translation Studies. *Journal of King Sand University- Language and Translation.* Juz. (23): 29-45.

Ember, M. R., & Peregrine, P. N. (2011). *Anthropology.* (13th edition) USA: Pearson.

Firoozkoohi, S. (2010). Culture Specific Items In Literary Translation. *Translation Journal* Vol.14, No.1 Oct.2023. http://translationjournal.net/journal/51 culture.htm

Foucault, M. (1980). *Politics. Philosophy and Culture: Interviews and other writings*. London: Routledge.

Fowler, D. (1987). Katika Giglioli, P. (ed.). *Language and Social Context.* Middlesex: Penguin.

Gay, L. R., Mills, G. E., & Airasian, P. (2006). *Educational Research: Competencies for Analysis and Application*. Columbus: Merrill Greenwood.

Ghazala, H. (1985). *Translation as Problems and Solutions*. (10th ed.) Jeddah: Konooz Elmarefa.

Gerald, W. H. (1973). *A Cultural History of the Kerebe of Tanzania*. African Publishing co.

Gouadec, D. (2007). *Translation as a Profession.* Amsterdam: John Benjamins.

Guerra, A. F. (2012). Translating Culture: Problems, Strategies, and Practical Realities. *Journal of Literature Culture and Literary Translation,* 1(3), 1–27.

Guo, H. (2012). A brief Analysis of Culture and Translation: *Theory and Practice in Language Studies*.Vol.2, Kur. 243-347

Guo, T., Misra, M., Tam, J. W., & Kroll, J. F. (2012). On the time course of accessing meaning in a second language: an electrophysiological and behavioral investigation of translation recognition. *Journal of Experimental Psychology: Learning, Memory, and Cognition,* 38(5), 1165.

Hassan, A. (2013). The Importance of Culture in Translation: Should Culture be Translated?. *International journal of applied linguistics and English literature*, 2(2), 96-100.

Hervey, S., & H. I. (1992) *Thinking Translation: A Course in Translation Method*, London & New York: Routledge.

Haviland, W. A; Walrath, H. E. & McBride, B. (2011). *Athropology The Human Challenge* (13th edition. Australia: Wadsworth Cengage Learning.

House, J. (2009). Translation, interpreting and intercultural communication. In *The Routledge handbook of language and intercultural communication* (pp. 502-516). Routledge.

Jilala, H. (2008). *The artistic uses of metaphors in constructing meanings and messages in new generation songs in Tanzania*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

------------- (2014*). Athari za Kitamaduni katika Tafsiri: Mifano kutoka matini za kitalii katika makumbusho za Tanzania.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Cha Dar- es- Salaam. Haijachapishwa.

Jilala, H. (2023). Mchango wa Tafsiri za JK Nyerere katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili. *Mwanga wa Lugha,* 8(1), 75-88.

Kamundi, H. M. (2023). Bilingualism or Monolingualism? Exploring Possibilities of Using Translation as a Method of Teaching English and Kiswahili in Kenya. *Journal of African Languages & Literary Studies (JoALLS),* 4(3).

Kareithi, P. M. (1969). *Kaburi Bila Msalaba*. Phoenix Publishers. Nairobi.

-------------- (2017). *Unmarked Grave.* Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.

Kimenye, B. (1968). *Moses in Trouble land.* Nairobi: Oxford University Press.

------------- (1968). *Moses and the Ghost*. Nairobi. Oxford University Press.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Kiswahili Isimujamiii*. Institute of Kiswahili Research University of Daresalaam. Tanzania.

-------------- (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar- es- Salaam: TATAKI.

Kitereza A. (1981). *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali.* Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.

------------ (2002). *Mr. Myombekere and His Wife Bugonoka, Their Son Ntulanalwo and Daughter Bulihwali*. Dar es Salaam. Mkuki wa Nyota Publishers.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*: New Delhl: New Age International Publishing Ltd.

Kovecses, Z. (2002). *Metaphor: A practical introduction*. Oxford: Oxford University Press.

Kovecses, Z. (2002). Language, figurative thought, and cross-cultural comparison. *Metaphor and Symbol,* 18, 311–320.

Kumar, R. (1999). *Research Methodology: A step-by-step guide for beginners*. New Delhi: SAGE Publications India Pvt Ltd.

Larson, L. M. (1984). *Meaning Based Translation*. London: University Press of America.

Lauscher, S. (2000). Translation Quality Assessment: where cana Theory and Trasnlator meet? *The Translator,* 6(2) uk. 149-18

Langness, L.l. (1974). *The Study of Culture* (Revised Edition). California: Chandler & Sharp Publishers, Inc.

Lefever A. (1999). Mother Courages Cucumber. Atext System and Refraction in 'A theory of Literature'. Katika Venuti L. *The Translation Studies Reader*. London: Routledge.

Leininger, M. (1985c). *Ethnoscience method and componential analysis. In Qualitative research methods in nursing*. Orlando, FL: Grune & Stratton p. 237-251.

lo Liyong, T. (Ed.). (1972). *Popular culture of East Africa: oral literature*. Longman Publishing Group.

Leppihalme, R. (1997). *Culture Bumps: An empirical Approach to the Translation of Allusions*. Clevedon: Multilingual Matters.

Maitaria, J. N., & Momanyi, C. (2016). Visawe katika Methali Tafsiriwa za Kiswahili katika H. Jilala, *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam. Daudi Publishing Company Ltd kur. 275-293.

Malangwa, P. S. (2012). Overcoming the barriers through Literal and Descriptive Translations: Examples of Kanga names. *Journal for studies in Humanities and Social Sciences*. Juz.1, namba1, 51-62.

Malangwa, S., & Masha, L. (2022). *Changamoto na Mbinu za Kutathmini Tafsiri.* Tasnifu haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Matundura, B. (2013). *Musa Mashakani.* Nairobi. Oxford University Press.

---------- (2013). *Musa na Pepo.* Nairobi. Oxford Univerty Press.

McG EE, R. J., & Warms, R. L. (2012). *Anthropological Theory. An Introductory History* (5th edition). USA: Mc Graw-Hill.

Mgbemere, C. D. (2014). Cues in Igbo Cultural Matrix: Analysis of Achebe's Arrow of God. *Journal of Culture, Society and Development- An open Access International Journal* Vol 4.

Miller, C. (1990). *Theories of Africans*. New York: Routledge.

---------- (1990). Rhetorical community: The cultural basis of genre. *Genre and the new rhetoric,* 6778.

Mieder, W. (2004). *Proverbs- A Handbook*. Westport, CT; Greenwood Press.

---------- (1993). *Proverbs are never out of Season. Popular Wisdom in the modern Age.* New York: Oxford University Press.

Miles, J. (1971). *Language in Social Groups*: California: Stanford University Press.

Mshindo, H. B. (2010). *Kufasiri na Tafsiri.* Zanzibar: Kiwanda cha Uchapaji Chuo Kikuu cha Chukwani.

Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications.* New York: Routledge.

Mutie, E. (1997). *Sanaa katika Tafsiri: Matatizo na Athari zake.* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Mutuli J. A. (2009). *The Adequacy of Translation Theory with Respect to Drama. The case study of Samwel Mushi's Mfalme Edipode*. Tasnifu. (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mumbua, K. R. (2019). *Kuwepo au Kutokuwepo kwa Wahusika wa kike katika Tawasifu ya Mbali na Nyumbani*. Tasnifu haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Msokile, M. (1993). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: DUP.

Mwansoko, H. (mh) (2015). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Toleo la nne. Dar-es- Salaam: TUKI.

Mwansoko, H.J.M., Mekacha, R.D.K., Masoko, D.L.W., & Mtesigwa, P.C.K. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu.* Dar-es-Salaam: TUKI.

Mwansoko, H. J. M. (2016). Ukuzaji wa Kiswahili kupitia Tafsiri: Hatua Moja Mbele, Mbili Nyuma. Katika H. Jilala, (ed.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istihahi.* Dar es Salaam: Daud Publishing Company Limited. pp. 2-18.xv.Newm.

Namy, C. (1978). Reflections on the Training of Simultaneous Interpreters A metalinguistic approach. In *Language interpretation and communication* (pp. 25-33). Boston, MA: Springer US.

Naude, M.C., & Naude, J. A. (2010). The Translator as an a Agent of Change and Transformation: The Case of Translating Biblical Proverbs. *Agent of Change OTE23/10* (2010), 306-321

Newmark, L., Hubbard, P., & Prifti, P. R. (1982). *Standard Albanian: A reference grammar for students.* Stanford University Press.

Newmark, P. (1988). *Approaches to Translation.* Shanghai Foreign Language Education Press.

---------- (1988). Pragmatic translation and literalism. *TTR: traduction, terminologie, rédaction,* 1(2), 133-145.

--------- (1988). *A textbook of translation* (Vol. 66, pp. 1-312). New York: Prentice hall.

Nida, E. A. (1964). *Toward a science of translating: with special reference to principles and procedures involved in Bible translating*. Brill Archive.

---------- (1993). *Language, Culture and Translating*. Shanghai: Foreign Language Education Press.

----------(1996). *The Sociolinguistics of Interlingual Communication*. Bruxelles: Éditions du Hazard (collection Traductologie).

Nida, E. A. (1964). *Language Structure and Translation*, Stanford: Stanford University Press.

Nida, E., & Taber, C. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: Brill.

Nord, C. (2001). *Translating as a Purposeful Activity- Functional Approaches Explained.* Shangai: Foreign Languages Education Press.

Nord, C. (2007). Skopos. Loyalty and Translational Conventions. *Target*, 3(1): 91-109

Norrick, N. R. (1985). *How Proverbs mean. Semantic Studies in English Proverbs*. Berlin: Mouton.

Ngesu, S. N. M. (2020). Nafasi ya Tafsiri katika Ufundishaji wa Kiswahili: Mfano wa Ufundishaji wa Kiswahili katika shule za Upili nchini Uganda. *Jarida la Mwanga wa Lugha. Juz. 7 (1): 71-78*

Nyangeri, P. (2014). *Vitendo usemi na Ulinganifu wa maana katika Tafsiri: Mifano kutoka kazi mbili teule za Barbara Kimenye*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi. Nairobi. Haijachapishwa.

Nzyoka, S. (2014). *Tathmini ya Tafsiri na mikakati ya kutafsiri Tamathali za semi katika tamthilia ya Antigon*: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Kenyatta. Nairobi: Haijachapishwa.

Oduma, R. (2006). *Phonological Adaptation of Loan words in Ateso*. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Moi: Haijachapishwa.

Ogechi, N. O. (2024). *Taratibu za kuendesha Utafiti na Masuala Mengine*. The Jomo Kenyatta Foundation. 51 Enterprise Road, Industrial Area. Kenya.

Omboga, Z. (2006). *Sitting Text, Culture and Pedagogy in Literal Translation: A Theorisation of Translation in Culture Transfer with examples from selected texts in Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu Cha Kenyatta: Nairobi: Haijachapishwa.

Omondi, F. O. (1997*). Dhana na Matatizo ya Tafsiri. Tathmini ya Risasi zianzapo kuchanua;* Tasnifu yay a M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Osore, P. (2011). Nafasi ya Utamaduni katika Tafsiri: Mfano wa Msamiati wa Serikali na Bunge. *Jarida la CHAKITA.*

